# 27 JUNI, 2023

# BUNGE LA TANZANIA

___

# MAJADILIANO YA BUNGE

___

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Hamsini na Sita – Tarehe 27 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Maelezo ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi.

Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa Ruaha.

**MHE. NANCY H. NYALUSI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia mapendekezo ya kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruah ana taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Uchambuzi wa Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa iliyopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Uchambuzi wa Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa iliyopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MHE. FLATEI G. MASSAY K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uchambuzi wa Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa iliyopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 734

**Kupandisha hadhi Mji wa Magugu**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kupandisha hadhi Mji wa Magugu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa Mamlaka za Miji Midogo hufanyika kwa kuzingatia Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007 pamoja na Mwongozo wa Uanzishaji wa Maeneo ya Utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2014 ambapo umeanishwa utaratibu na vigezo vinavyopaswa kufuatwa.

Mheshimiwa Spika, kusudio la kupandisha hadhi Mji wa Magugu lipo katika hatua za upangaji wa Mji ikiwemo uandaaji

wa mpango wa jumla na mpango kina ambapo ikikamilika itatangazwa kupitia gazeti la Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Sina swali la nyongeza lakini niipongeze Serikali kwa hatua hii iliyofikia na ninaomba wakamilishe hatua zilizobaki za mchakato ili kuhakikisha kwamba jambo hili linakamilika na kutangaza mji huu kuwa na Mamlaka ya Mji Mdogo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mamlaka ya Mji mdogo wa Katesh ni ya muda mrefu na Mji wa Katesh umepanuka sana. Je, Serikali lini itachukua hatua ya kuanzisha Mamlaka kamili ya Mji wa Katesh?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hhayuma, Serikali kwa sasa bado inaweka kipaumbele katika kumalizia ujenzi wa miundombinu kwenye maeneo ambayo ni mapya na maeneo yale ambapo Halmashauri zilihamia kwenye maeneo yale ya kiutawala na pale Serikali itakapomaliza ujenzi wa miundombinu hii muhimu, tutaanza kuangalia tena namna ya kuweza kuanza kupandisha hadhi maeneo mengine ya Mamlaka za Miji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri Mji mdogo wa Kibaya na Matui imekuwa ipo kwa muda mrefu sana, sasa imewaacha wale siyo

wenyeviti siyo Wenyeviti wa Mitaa wame-*hang* tu kwa muda mrefu.

Je, ni lini Serikali italeta mpango ili suala hili likae vizuri? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali Serikali kwa sasa imeweka kipaumbele katika umaliziaji wa miundombinu na ujenzi wa miundombinu mingine katika maeneo mapya ya kiutawala ambayo yalianzishwa hivi karibuni na yale maeneo ambapo Halmashauri zilihamia kwenye maeneo hayo ya utawala. Pale ambapo zoezi hili litakamilika la ujenzi wa miundombinu hii tutaanza kuangalia namna gani ya kuanza kupandisha hadhi Miji hii, ikiwemo Kibaya na Matui kule Kiteto.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupandisha hadhi Mji wa Kibaha kuwa Manispaa ya Kibaha umefikia hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma la kupandisha hadhi Mji wa Kibaha kuwa Manispaa. Ombi hili la Manispaa ya Kibaha la kukidhi vigezo, kwanza walipewa vigezo vya kuweza kufikia ili waweze kupandishwa hadhi ikiwemo idadi ya watu. Waliwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI Aprili mwaka huu lile ombi lao la kuweza kupandishwa hadhi na tayari lipo kwenye timu ambayo

wanaiangalia kuona kama vigezo vile vimekidhi kwa ajili ya kupandishwa hadhi na kuwa Manispaa ya Kibaha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 735

**Hitaji la Sekondari Kata ya Mjimwema – Makambako**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa Shule ya Sekondari katika Kata ya Mjimwema Makambako?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatekeleza mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (*SEQUIP)* ambapo ujenzi wa shule mpya unafanyika katika Kata ambazo hazina shule. Katika awamu ya kwanza shule 231 zimejengwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi unaendelea ambapo jumla ya shule 1,000 zitajengwa na mchakato wa kupeleka fedha kwa Halmshauri utakapokamilika fedha hizo zitapelekwa. Hivyo, Halmashauri iweke kipaumbele cha ujenzi wa shule hii kwenye mpango wake kwa awamu zijazo katika Kata ambazo hazina shule ikiwemo Kata ya Mjimwema Makambako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, shule hii ya Mjimwema Makambako ni shule ambayo Mheshimiwa Mbunge aliiweka moja kati ya vipaumbele vya shule zake ambazo tulivileta TAMISEMI ili ziweza kujengwa kutokana na eneo hili kuwa na uhitaji mkubwa wa sekondari.

Je, ni lini Serikali itafanyia kazi mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge ili shule iweze kujengwa pale?

Swali la pili, hata Wilaya ya Makete nilileta kipaumbele kwenye Kata ya Kigala ambayo kwa muda mrefu haina Shule ya Sekondari ya Kata. Ni lini Serikali itajenga Sekondari ya Kata kwenye Kata ya Kigala ili wananchi waweze kupata elimu kwa mazingira ya karibu? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza. Kuhusu swali hili la kwanza la Kata ya Mjimwema kupata shule, kama nilivyokwisha sema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali kwa sasa ipo mbioni kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya katika Kata ambazo hazina shule kwenye Halmashauri mbalimbali nchini na kila Halmashauri kwenye Halmashauri 184 itapata shule moja. Tumetenga kiasi cha shilingi milioni 570 kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo. Awamu ya kwanza ya hizo shule 231 ilienda milioni 470, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeangalia hali ya mabadiliko ya vifaa, bei na kadhalika na kuweka *minimum* kuwa ni milioni 570. Sasa ni wajibu wa Halmashauri ya Mji wa Makambako wenyewe kuhakikisha kwamba fedha hii inapofika waweke kipaumbele Shule ya Mjimwema ili iweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Kata ya Kigala kule Makete vilevile Halmashauri ya Wilaya ya Makete itapokea shilingi

*minimum* milioni 570 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya katika Halmashauri yao, hivyo basi ni wajibu wao kuhakikisha kwamba wanapeleka fedha katika Kata hii ya Kigala kwa ajili ya ujenzi wa sekondari mpya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye ukarabati wa shule ya Sekondari ya *SUA*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Dkt. Ishengoma la Serikali kupeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule ya Sekondari ya SUA. Tutatuma timu pale ya Afisa Elimu wetu wa Sekondari katika Halmashauri ile kuweza kufanya tathmini ya nini kinachohitajika kufanyika katika ukarabai ule na watawasilisha taarifa ile Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa Shule ya Sekondari *SUA*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 736

**Uwiano sawa katika bajeti za Halmashauri**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutenga fedha ili kuweka uwiano sawa kwa bajeti za Halmashauri kwani Halmashauri nyingi haziwezi kujiendesha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua utofauti uliopo wa uwezo wa Halmashauri kujiendesha baina ya Halmashauri moja na nyingine kutokana na uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri. Kwa kutambua hilo, Serikali imeziweka Halmashauri kwenye madaraja manne kwa kuzingatia uwezo wa Halmashauri kukusanya mapato kutokana na fursa za vyanzo vya mapato vilivyopo kwenye eneo husika la utawala.

Mheshimiwa Spika, ili kuziwezesha Halmashauri zisizo na fursa za kukusanya mapato makubwa kujiendesha na kwa kuzingatia madaraja hayo Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuzipunguzia viwango vya upelekaji wa fedha za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo;

(ii) Kuziondolea mchango wa asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa Barabara;

(iii) Kuzisaidia kulipa stahiki za Viongozi hususan Wakurugenzi na Wakuu wa Idara;

(iv) Kuzisaidia kulipa posho za kila mwezi za Waheshimiwa Madiwani; na

(v) Kuziongezea viwango vya ruzuku ya matumizi ya kawaida na ruzuku ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuziwezesha Halmashauri zenye uwezo mdogo wa ukusanyaji wa mapato ili ziweze kujiendesha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri nyingi zinakosa fedha za kujiendesha zenyewe kutokana na Serikali Kuu kuchelewesha zile asilimia ambazo zinawekwa na zinatengwa kwamba, kwa kisheria asilimia 20 ndiyo inabaki asilimia 80 inakwenda Serikali Kuu.

Je, Serikali iko tayari kutengeneza mfumo ambao utafanya Halmashauri zinapokusanya fedha zile asilimia 20 zibaki moja kwa moja katika Halmashauri zake, badala ya kusubiri zirejeshwe kama ambavyo Serikali inakuwa hairejeshi wakati mwingine?

Swali langu la pili, kwa kuwa Halmashauri ndiyo watekelezaji wakuu wa sera na mipango ya Serikali Kuu kwa ngazi ya chini. Je, Serikali haioni umuhimu wa kurejesha vyanzo vyote vya mapato ambavyo vinakusanywa katika Halmashauri ili viweze kuwasaidia kuendesha Halmashauri hizo?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Tendega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza la Serikali kuwa tayari kutengeneza mfumo kwa ajili ya kubakiza asilimia hizi kulekule kwenye Halmashauri ni wazo zuri na tunalipokea, tutakaa na timu ya wataalam kuona wamefikia wapi kwa sababu tayari pia wao walikuwa wanalifanyia kazi kwa ajili ya kutengeneza mfumo huo. Tutakaa kuona wamefika wapi na wenzetu vilevile wa Hazina kuona wamefikia wapi kwa ajili ya kuweza kutengeneza mfumo huu lakini ni wazo zuri.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, tayari Serikali Kuu imeanza kuzirudishia Halmashuri vyanzo vile ambavyo wanakusanya. Mfano, katika mwaka wa fedha huu tunaoenda kuuanza wa 2023/2024 vyanzo vya makusanyo vile vya mabango ya matangazo vimerudishwa kule kwenye Halmashauri zenyewe ili ziweze kukusanya na tunaendelea kuangalia kama Serikali kwa ujumla wake ni vyanzo vipi viweze kuendelea kurudishwa kwenye Halmashauri zile ili kuziongezea uwezo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali kuu imekuwa ikipeleka fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri hizi hata zile ambazo hazina uwezo kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kuwasaidia katika ujenzi wa madarasa, katika ujenzi wa zahanati, katika ujenzi wa vituo vya afya na kadhalika ili kuwapunguzia mzigo Halmashauri hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, badala ya kuingia Wizara ya Fedha na Mipango tutalitazama kwanza swali la Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro Mbunge wa Ngara.

Na. 745

**Ujenzi wa Soko la Mnada wa Ng'ombe – Murusagamba**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa soko la mnada wa ng'ombe wa Murusagamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifungo na Uvuvi, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Jimbo la Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya mnada wa mpakani wa Murusagamba umekamilika na ulihusisha ujenzi wa uzio, mazizi na ukarabati wa ofisi. Baada ya ujenzi kukamilika Wizara inaandaa utaratibu wa kuanza kuhamasisha wafanyabiashara na wafugaji kuanza kutumia mnada huo ili kufanikisha mauzo ya mifugo nje ya nchi na kuongeza maduhuli kwa Serikali Kuu na Halmashauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru Serikali, majibu ni mazuri sana. Sasa swali la kwanza, kwa kuwa ujenzi umefanyika kwa muda mrefu na sasa kuna *cracks* nyingi zimetokea pale. Je, Wizara iko tayari kwenda kufanya ukarabati eneo lile ili uzinduzi utakapofanyika eneo lile liwe linafaa kwa ajili ya mnada, swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba kukuuliza Mheshimiwa Waziri uko tayari kuambatana na mimi baada ya Bunge hili twende pale Ngara, Murusagamba tukazindue huo mnada? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; cha kwanza nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na kwamba mnada umekamilika na hayo mapungufu machache ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha tutayarekebisha kabla ya kuzindua na mimi niko tayari kwenda mara baada ya Bunge lako tukufu kuahirishwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 737

**Kubadilisha mfumo wa uandaaji mpango wa bajeti**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha Mfumo wa Uandaaji Mpango wa Bajeti ili uwe wa zaidi ya miaka mitano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali unaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambapo katika kutekeleza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Serikali iliandaa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa miaka 15 kuanzia 2011/2012 hadi 2025/2026 uliogawanywa katika vipindi vitatu vya muda wa kati wa miaka mitano ya utekelezaji (Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa 2011/2012 hadi 2015/2016, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017 hadi 2020/2021 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 2021/2022 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mfumo wa uuandaji wa mpango na bajeti wenye kutoa mwelekeo wa zaidi ya miaka mitano ambapo mpango na bajeti unaoandaliwa kila mwaka ni

sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari sasa Serikali imeshazindua Tume ya Mipango ya Taifa, je, Serikali haioni ni wakati sahihi sasa kuwa na mipango ya miaka 100 na kuendelea ya Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, je, Serikali haioni ni wakati sahihi sasa kuanza kuwa na mpango wa maendeleo wa miaka 100 na kuanza kuitekeleza kwa kipindi cha miaka mitano mitano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba nijibu kwa pamoja. Ni jambo zuri kuwa na mpango wa muda mrefu sana wa hiyo miaka 100 au zaidi ya hapo lakini kwa kuwa Tume ya Mipango imeshaanzishwa au inaendelea kuanzishwa kwa sasa, huko siku za mbeleni tutaangalia suala hilo. Serikali imechukua shauri hilo na litafanyiwa kazi kadiri uwezekano utakapopatikana ikionekana kama iko tija. Kwa kuwa tayari sasa hivi tupo tunaandaa Dira ya Taifa 2050 itakayoanzwa kutekelezwa mwaka 2026 mara tu Dira ya 2025 itakapohitimishwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake.

Na. 738

**Mradi wa Maji Tarafa ya Suba – Rorya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji wa Tarafa ya Suba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Suba ina vijiji 17 ambapo kati yake vijiji 16 vinapata huduma ya maji kupitia Vyanzo vya Ziwa Victoria, visima virefu na visima vifupi. Hata hivyo, kulingana na jiografia sio vitongoji vyote kwenye vijiji hivyo vinafikiwa na huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wa vijiji hivyo 16 wanapata huduma ya maji salama na ya kutosheleza ikiwemo Wananchi wa Kijiji cha Kibui ambacho wananchi wake hawana maji, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 itafanya usanifu wa mradi wa kutoa maji kwenye bomba kuu litakalopeleka maji Miji ya Tarime na Rorya ili kupeleka maji Vijiji vya Tarafa ya Suba. Baada ya kujengwa kwa mradi huo wananchi wote katika Tarafa ya Suba watapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, pamoja na majibu mazuri na kazi nzuri

inayofanywa na Wizara hii kwa maana ya Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Suba yeye vijiji 20 na sio 17 vijiji vinne kwa maana ya Kijiji cha Ruhu, Muundwe, Kibuyu na Mkengwa ni vijiji ambavyo havina mradi wowote wa maji mpaka sasa. Ninataka nipate kauli ya Serikali juu ya vijiji ni lini sasa vitapata maji safi na salama?

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, pamoja na vijiji 16 kuwa na maji safi na salama lakini vitongoji katika vijiji hivi maji hayajatapakaa kwenye vitongoji. Nayo pia nilitaka nipate kauli ya Serikali, kwamba Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuhakikisha angalau vitongoji kwenye vijiji hivi 16 vinapata maji safi na salama kwa ajili ya huduma ya maji kwa wananchi hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niseme nimepokea marekebisho ya idadi ya vijiji vyake lakini vilevile katika maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge nipende kumuelekeza Meneja wa Wilaya aendelee kufanya jitihada za kuona anapata visima ili vijiji hivi vipate maji. Mheshimiwa Mbunge eneo lako ni moja ya maeneo yanayonufaika na mradi ya miji 28. Kwa hiyo, wakati miji 28 utekelezaji unaendelea na ni kwa sababu ni mradi wa muda mrefu, jitihada za miradi ya muda mfupi zitaendelea kufanyika na ushirikiano wako namna ambavyo umekuwa ukiufanya, tutahakikisha tunafanya yale tuliokubalina.

Mheshimiwa Spika, katika vijiji hivi 16, vitongoji ambavyo havina maji tutahakikisha tunasambaza maji, Meneja wa Wilaya tayari tumemuelekeza na ninamsisitiza ili ahakikishe maeneo yote yanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Mpango wa kutekeleza mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kata za Magata, Muleba, Buleza, Chikuku na Kagoma utaanza lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Kagera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge Oliver, kwanza tulishakaana naye ofisini na tulishamwelekeza. Mheshimiwa Mbunge nakupongeza kwa ufuatiliaji, hizi kata ulizozitaja kama tulivyokubaliana ni lazima mwaka ujao wa fedha tuhakikishe na zenyewe zinakwenda kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 739

**Ukarabati wa miundombinu ya maji - Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa miundombinu ya maji iliyochakaa na kusababisha upungufu wa maji – Chemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya maji katika Wilaya ya Chemba na imeanza kuchukuwa hatua kwa Vijiji vya Humekwa na Mlongia ambapo manunuzi ya vifaa kwa ajili ya ukarabati yanaendelea. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itafanya usanifu na kufanya ukarabati wa miradi ya maji kwa Vijiji vya Njoeni Muone, Mtakuja, Bugenika, Msera, Mengu, Pangalua, Wahilo, Wisuzaje, Msaada na Mwailanje. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, mwaka 2018, Serikali ilichimba kisima kwenye Kijiji cha Mayi lakini mpaka leo hakijaweka miundombinu na hivyo hakitumiki, nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mwaka wa 2021/2022 Serikali ilitangaza kandarasi ya visima 13, mpaka leo imechimba vitatu tu na hivyo tunawadanganya wananchi. Naomba kujua Waziri anasema nini juu ya visima hivyo ambavyo havijachimbwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Monni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kisima kilichochimbwa mwaka 2018, Mheshimiwa Mbunge tutakisimamia kuhakikisha tunaleta usambazaji kwa wanufaika wote kwenye kile kisima. Kwa visima hivi ambavyo tulivipitisha mwaka wa fedha 2022, Mheshimiwa Mbunge Serikali haiwezi kudanganya kwa sababu suala letu sisi ni kuhakikisha tunapeleka huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, vile

visima vilivyobaki lazima tuvifanyie kazi tutakuja kuvichimba kadiri tunavyopata fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini visima vilivyochimbwa katika majimbo ya Ndanda, Nanyumbu na Tandahimba wananchi wake wataanza kuyatumia maji hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hokororo naye pia ameshafika ofisini na tumeweza kujadiliana masuala ya visima vyote vilivyochimbwa kwenye haya majimbo aliyoyataja. Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuonane ili tuweze kupanga mkakati baada ya Bunge hili twende kule *site* tutaangalia namna gani ya kuona tunatekeleza kwa pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sengerema kuna mitambo imewekwa kwa ajili ya kuchimba visima na visima vilivyochimbwa ni vitano kati ya visima 38. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na mitambo hiyo kukaa leo mwezi wa pili iko Sengerema na visima havichimbwi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tabasam, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mitambo hii tumeisambaza mikoa yote na Mkoa wa Mwanza ni mnufaika kwa mitambo ambayo iko Sengerema ilikuwa na michakato inafanyika ili kuona tunaendelea kutenda kazi na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili kazi zitaendelea na mitambo ile itamaliza visima 38 na kuhamia wilaya nyingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 740

**Eneo mbadala wa Vijiji vya Kata ya Nyantwari – Bunda**

**MHE. AGNES M. MARWA** aliuliza:-

Je, Serikali imewatafutia eneo mbadala wananchi wa Vijiji vya Kata ya Nyantwari – Bunda wanaofanyiwa uthamini kupitia uhifadhi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kutwaa eneo la ghuba ya Speke lenye ukubwa wa ekari 14,250 kwa manufaa ya umma ili kuimarisha uhifadhi endelevu wa mfumo ikolojia wa Hifadhi ya Taifa Serengeti na usalama wa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, zoezi la uthamini lipo katika hatua za mwisho na baada ya hapo wananchi watalipwa fidia kwa mujibu

wa sheria. Fidia itakayolipwa kwa wananachi husika, itahusisha gharama za thamani ya ardhi, mazao, majengo, posho ya kujikimu, usafiri na posho ya usumbufu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Mji wa Bunda imetenga na kupima viwanja 350 katika Eneo la Virian, Kata ya Stoo ambapo wananchi watakaohama kutoka Kata ya Nyantwari watapewa kipaumbele wakati wa uuzaji wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Halmashauri ya Mji wa Bunda imeandaa mpango wa kutwaa na kulipa fidia maeneo mbadala ya makazi yenye ukubwa wa ekari 1,625 katika maeneo ya Manyamanyama, Bitaraguru, Butakale na Guta. Maeneo yote hayo yatapimwa na kupewa kipaumbele kwa wananchi wanaotoka Kata ya Nyantwari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa wananchi waliambiwa kwamba watalipwa kwa ekari moja shilingi milioni mbili, kutokana na uhalisia wa maisha, maisha yamepanda juu sana, wananchi waliomba waongezewe kutoka milioni mbili kulipwa shilingi milioni sita. Je, nini tamko la Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, kwa kuwa Kata ile ya Nywatwari kuna wavuvi na wafugaji, je, wafugaji wamekwisha tafutiwa maeneo kwa ajili ya mifugo yao na wavuvi wataangaliwa vipi kwa ajili ya maeneo rafiki ya kuendeleza uvuvi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Agnes na kumpongeza kwa namna ambavyo anaendelea kutetea Wananchi wa Mkoa wa Mara akiwa kama Mbunge wa Mkoa wa Mara. Hili suala la stahili ya hawa wanaopaswa kuhama

linafanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ambapo Wizara ya Ardhi wamekuwa wakifanya uthamini na miongozo yote wanaitumia ili kuhakikisha kwamba suala hili linaendana sambamba na sheria na taratibu na kanuni zilizopo. Endapo kutakuwa na uhitaji wa kuangalia uthamani au namna ya kuongezewa basi tutakaa na Wizara ya Ardhi ili tuweze kujadili kama kuna uwezekano huo.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili la pili la wafugaji na wavuvi, kwenye upande wa kuwahamisha tayari uthamini umefanyika ikiwemo mifugo yao, ardhi yao waliyokuwa wanaitumia. Kwa hiyo, watakapokuwa wameenda kwenye makazi mapya yatazingatiwa hayo ikiwemo kutengewa maeneo ya mifugo lakini kwenye suala hili la uvuvi sheria za uhifadhi zitaongozwa kwa sababu maeneo ambayo tunaenda kuyatwaa mengi tutakuwa tunayahifadhi. Kwa hiyo tutaangalia utaratibu unasemaje ili tuweze kukaa pamoja na wavuvi waweze kuangaliwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha VIijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 741

**Migogoro kati ya *TFS* na wafanyabiashara wa mazao ya misitu**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya wafanyabiashara wa mazao ya misitu wanaozuiwa kufanya biashara na *TFS*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Misitu Sura ya 323 na Kanuni zake za mwaka 2004 zimeelekeza utaratibu unaopaswa kufuatwa ili kuvuna, kusafirisha na kuuza mazao ya misitu kwa kuzingatia umiliki wa misitu au miti ambao ni ya watu binafsi, Serikali za vijiji, Serikali za mitaa au Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TFS* haizuii kufanya biashara ya mazao ya misitu isipokuwa inasimamia sheria na kanuni ambazo zinahakikisha kunakuwa na usawa katika biashara hiyo pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu nchini. Natoa rai kwa wadau au wafanyabiashara wote wenye nia njema ya kuvuna au kufanya biashara ya mazao ya misitu wafuate sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili kulinda misitu yetu ambayo ni muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa majibu yao. Nitakuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majibu yameonesha kanuni zipo na wananchi wanafahamu lakini kule bado kuna changamoto kwenye Jimbo la Kibaha Vijijini, je, Waziri atakuwa yuko tayari baada ya Bunge hili twende tukasaidiane kuwaelekeza kanuni na taratibu za uvunaji wa mazao hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa wazo hili tunatamani sana tuendelee kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kufahamu umuhimu wa uhifadhi lakini kuwepo na uvunaji endelevu wa mazao wa misitu. Kwa hiyo natoa ukubali na utayari wa Wizara, tuko tayari kukutana na Wananchi wa Kibaha na maeneo mengine ili kutoa elimu na kuzungumza nao kwa ajili ya kutoa miongozo sahihi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Suma Ikyenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 742

**Ujenzi kwa kiwango cha lami mchepuo wa barabara ya *Pipeline***

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami kilometa 2.8 za barabara ambazo ni mchepuko kwenye barabara ya *Pipeline*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa 2.8 za barabara za mchepuo eneo la Inyala. Kazi za ujenzi zilikamilika tarehe 24 Juni, 2023, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha ambazo zilikwenda kukamilisha ujenzi ule na usimamizi wa *Engineer* Masige pamoja na Mkuu wa Mkoa barabara ile hatimaye ikakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ni lini itaanza ujenzi wa barabara kutoka Katumba – Kapugi - Ushirika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kutoka Kiwira – Isangati kutokea Mbalizi ambao huo ni mpango ulio kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na barabara ya kwanza bahati nzuri hizi barabara zote nazifahamu mimi binafsi, lakini Barabara ya kwanza ya Katumba – Kapugi hadi Ushirika hii barabara bado ilikuwa haijafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na Meneja wa Mkoa hii ni pamoja na Kiwira na Isangati ameshaanza kuzitembelea hizo barabara ili aweze kubaini gharama za kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara yote ya Katumba – Kapugi - Ushirika lakini pia Ushirika – Isangati - Mbalizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa ndiyo Serikali itaanza kufikiria kuijenga kwa kiwango cha lami baada ya kukamilisha usanifu wa kina, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi; je, ni lini barabara ya kutoka Kimo – Iponjola – Ikuti – Ibungu mpaka Kafwafwa itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hiyo ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Mbeya kwa maana ya Wilaya ya Rungwe na Wilaya ya Ileje na katika mwaka huu wa fedha tunaouendea imetengewa Bajeti kwa ajili ya kuanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kutoka Ibungu – Katengele – Kafwafwa hadi Kimo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mji wa Njombe kwa sababu ya wingi wa malori unahitaji kuwa na *bypass.* Je, ni lini Serikali itaanza kufanya *bypass* kutoka Kibena kwenda mpaka Yakobi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulishatoa maelezo hapa kwamba tuna mambo mawili tutafanya. Moja, kuanzia hapo Kibena tunategemea kujenga barabara za njia nne kwa ajili ya kupunguza msongamano, lakini pia sasa hivi Meneja wa Mkoa kulingana na ukuaji wa Mji wa Njombe wameanza kufanya *study* ya kuona wapi barabara ya *bypass* itapita na hasa tukizingatia kwamba Mji wa Njombe umekua, kwa hiyo wanaangalia maeneo ambayo hawataingia gharama kubwa ya kutoa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa hivi wako wanatembea, baada ya hapo sasa wataweka hiyo ramani kwenye maandishi kwa ajili ya kuiombea fedha kuanza hiyo kazi ya kutengeneza hiyo *bypass*, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutoka Iyombwe – Kisanga – Malolo mpaka Kilolo ni barabara ambayo inahudumiwa na *TAZAMA* lakini ni barabara muhimu sana ya kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Iringa.

Je, Serikali ina kauli gani kutumia barabara hii kama mbadala wa barabara kuu ya kutoka Mikumi kwenda Mbeya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyotaja ni kweli ni muhimu na kwa sasa Serikali inachofanya ni kuhakikisha kwamba inakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia usanifu ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY. A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mwaka 2018 Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga Barabara ya kutoka Mbambo – Ntaba – Ipinda; je, Serikali imefikia wapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mlaghila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema kwamba Kiongozi wa Taifa alishaahidi, atakubaliana nami kwamba barabara hii tayari

imeshafanyiwa usanifu wa kina na sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 743

**Ujenzi wa barabara ya Lupingu hadi Kyela**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Lupingu hadi Kyela inayopita kandokando mwa Ziwa Nyasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Lupingu hadi Matema yenye urefu wa kilometa 126 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Mbeya na inapita sehemu zenye mvua nyingi, milima na miteremko mikali. Kwa upande wa Mkoa wa Njombe barabara hii inafunguliwa kwa awamu ambapo jumla ya kilometa 3.6 zimefunguliwa na kwa upande wa Mkoa wa Mbeya jumla ya kilometa 4.0 zimefunguliwa ikiwa ni pamoja na kufanya ujenzi wa daraja moja *(box culvert)* na *drift* moja. Serikali kupitia *TANROADS* itaendelea kuifungua barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ningependa kuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kutambua umuhimu wa ulinzi na usalama wa mpaka ule wa Ziwa Nyasa na vivutio vya utalii, nini mkakati wa Serikali kuongeza fedha ili kasi ya ufunguaji wa barabara hii iongozeke?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nini mpango wa Serikali kuongeza fedha kwenye barabara inayoanzia Mlangali – Lupila – Makete ili vikwazo vya eneo la Lusala na Ng'elamo viweze kuondolewa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba umuhimu wa barabara hii ukiachilia mbali kwamba ni barabara ya ulinzi, lakini pia wananchi wanaoishi kando kando ya ziwa hawana namna nyingine ya kuwasiliana panapokuwa kuna changamoto ya usafiri wa majini, ndiyo maana Serikali imeanza kwa awamu. Hata hivyo, mpango wa Serikali ni kutafuta fedha ambayo itaifungua hii barabara yote ambayo nimeielezea kwamba ni barabara ambayo inapita kwenye milima na mabonde makubwa sana. Kwa hiyo mpango huo upo ndiyo maana tumeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hii Barabara ya Mlangali kwenda Ikonda najua ni muhimu sana kuunganisha Ludewa na Makete na hasa Hospitali ya Ikonda. Serikali imetenga fedha mwaka huu kuhakikisha kwamba maeneo yote yale korofi inakarabatiwa ili iweze kupitika kwa kipindi chote, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 744

**Ujenzi wa barabara ya Handeni – Kibirashi – Kondoa hadi Singida**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Handeni – Kibirashi - Kondoa hadi Singida kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kibaya – Chemba – Kwa Mtoro hadi Singida yenye urefu wa kilometa 424.24 kwa awamu. Ujenzi wa sehemu ya Handeni – Mafuleta kilometa 20 umefikia 11.61% na sehemu ya Mafuleta – Kileguru kilometa 30 mkataba umepelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mapitio *(vetting)*.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu iliyobaki…

*(Hapa king'ora cha kuashiria hali ya hatari kililia ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge nadhani hiyo inaashiria tutoke humu ndani kwa haraka kila mtu atafute mlango ulio karibu naye atoke. Sote twende ile sehemu ya kukusanyikia watu kule.

Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka jambo hili litakaporekebishwa.

*(Saa 4.01 Asubuhi Bunge liliahirishwa kwa muda ili kupisha wataalam kufanya ukaguzi)*

*(Saa 4.25 Asubuhi Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ulikuwa umeshasoma alikuwa ameshauliza ya nyongeza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, bado.

**SPIKA:** Haya sasa tusaidie lijibiwe upya hili swali. Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini.

Na. 744

**Ujenzi wa barabara ya Handeni – Kibirashi – Kondoa hadi Singida**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Handeni – Kibirashi - Kondoa hadi Singida kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya Handeni – Kibirashi – Kibaya – Chemba – Kwa Mtoro hadi Singida yenye urefu wa kilometa 424.24 kwa awamu. Ujenzi wa sehemu ya Handeni – Mafuleta kilometa 20 umefikia 11.61% na sehemu ya Mafuleta – Kileguru kilometa 30 mkataba umepelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mapitio *(vetting)*.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu iliyobaki ya Kibirashi – Kwa Mtoro – Singida yenye urefu wa kilometa 384.33 utekelezaji wake upo kwenye miradi itakayojengwa kwa utaratibu wa *EPC+F*. Hadi sasa mkandarasi wa kujenga barabara hii amepatikana na mkataba wa kuanza ujenzi umesainiwa tarehe 16 Juni, 2023, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Kampuni hii ya *Henan Highway Engineering Group* iliyopewa kipande cha Handeni – Mafuleta kilometa 20, umepita mwaka mzima sasa tangu kampuni hii ipewe kandarasi hiyo, lakini ujenzi unasuasua. Kwa nini ujenzi huu unasuasua na unaenda kwa kuchelewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza; ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Turiani – Mziha – Handeni kilometa 104 kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mkandarasi hajaenda kwa *speed* ama kwa kasi ambayo tulikuwa tunaitegemea na hii ni kutokana na sababu kadhaa. Moja ya sababu wakati amekabidhiwa barabara hii kulikuwa na changamoto kubwa sana ya mahali pa kutolea *materials* ambayo ilichukua muda mrefu sana mpaka ku-*acquire* hilo eneo kwa sababu lilikuwa na mgogoro. Kwa sasa suala hilo limeshakamilishwa na sasa anaendelea kupata yale *material* ambayo alikuwa anahitaji kutoka kwenye hiyo sehemu ya kutolea *materials.*

Mheshimiwa Spika, suala lingine kulikuwa na changamoto kwenye *management* ya kwake, lakini hilo suala pia limeshakamilishwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama alivyomsikia Waziri wa Fedha madai yale ya wakandarasi akiwepo huyu mkandarasi wa barabara hii ya Handeni – Mafuleta malipo yao yatatolewa ili waweze kuendelea, lakini pia wanapokuwa wanapewa kazi hawa wakandarasi moja ya sifa ni uwezo wao kifedha na hatutegemei akiwa 11% aweze kusimama, anatakiwa aendelee lakini pia vifaa ikiwa ni pamoja na *management* yake kwa kweli ndiyo maana wanafanyiwa *due diligence. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti hii ambayo tunaendelea nayo tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza ama kuendelea na ujenzi pale tulipoishia ya Turiani – Mziha hadi Handeni kwa mwaka ujao wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 746

**Utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, lini mkataba na mwekezaji utakamilika ili Mradi wa Liganga na Mchuchuma uweze kufanya kazi na kuchangia pato la Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuona mradi unganishi wa Liganga na Mchuchuma unatekelezwa, kwa kuzingatia dhamira hiyo, hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ili kuanza utekelezaji wa mradi huo muhimu. Hatua hizo ni pamoja na kulipa fidia ya kiasi cha shilingi za Kitanzania 15,424,364,900 kwa wananchi 1,142 na kuanza upya majadiliano na mwekezaji wa mradi ili kuhakikisha kuwa mradi unatekelezwa pasipo kuleta hasara kwa Taifa, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali la kwanza; lini Serikali italipa fidia ya Mradi wa Makaa ya Magangamatitu na Katewaka, Wilaya ya Ludewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana ya kupitia upya Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma, amekwenda mpaka China sambamba na kulipa fidia. Sisi tunataka kujua, majadiliano na mwekezaji yamefikia hatua gani, lakini tunataka kujua vile vile mkataba utasainiwa lini ili mradi huu uanze kufanya kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kuhusu suala la fidia kwa Mradi wa Magangamatitu na Katewaka kwa sababu tumeshaanza kulipa fidia kwenye mradi mkubwa, tukikamilisha zoezi hili maana yake zoezi litakalofuata ni kuangalia tena miradi hii ya

Magangamatitu na Katewaka ili kuona nako fidia zinalipwa kwa wananchi wanaopisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Serikali inatambua umuhimu wa Mradi huu mkubwa wa Liganga na Mchuchuma ambao kwa kweli utakuwa na manufaa makubwa kwa Taifa letu. Kama alivyosema Mbunge, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anafanya kazi kubwa sana, Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia Diplomasia ya Kiuchumi tumeweza kufikia hatua nzuri sana kuweza kukamilisha majadiliano na hawa wawekezaji ambao mwanzoni walikuwa hawaji kwenye majadiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie kwamba juhudi zinazochukuliwa na Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuhakikisha mradi huu unaanza mapema ziko kwenye hatua nzuri na tunaamini majadiliano haya sasa yatakamilika mapema kwa sababu nao wameanza kuonesha nia ya kutekeleza mradi bila kuleta vikwazo au vivutio vile ambavyo walikuwa wanadai mwanzo ambavyo vina hasara kwa Taifa letu, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba Abbas swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ikiwa haya ndiyo majibu ya Serikali.

Je, Serikali iko tayari sasa kutengeneza kitu kinachoitwa *Program and Plan of Action* kikionesha tarehe na miezi na mwaka kuelekea kuanzishwa kwa mradi huu badala ya kusema tu majadiliano yanaendelea? Watupe *commitment* ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kama nilivyosema ni kweli tumekuwa na majadiliano ya muda mrefu na sababu kubwa

ilikuwa ni upande wa pili kwa maana ya huyu mwekezaji ambaye kidogo alikuwa haji kwenye majadiliano kwenye vikao. Sasa kama nilivyosema, Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaweka mahusiano mazuri na nje wanakotoka wenzetu wawekezaji hawa. Kwa hiyo tunaamini sasa kwa sababu wameshaanza kuja maana yake tutafikia muafaka karibuni, halafu tutatoa hiyo programu kwamba *schedule* ya utekelezaji wa mradi huu itakuwaje, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Naomba tu nimuulize Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma awali ulikuwa unaipa Serikali ya Tanzania 20% na 80% ilikuwa inakwenda kwa mwekezaji wakati uwekezaji wake ulikuwa ni dola milioni 600 tu kati ya dola bilioni tatu zilizokuwa zinahitajika. Je, Serikali imeweka mkakati gani wa dhati wa kuhakikisha kwamba sisi tunanufaika zaidi ukizingatia kwamba chuma cha Liganga ni jiwe ambalo liko juu wala huchimbi unafanya kukata tu kama keki ya harusi? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli mradi huu gharama yake jumla kwa tathmini za wakati ule ilikuwa ni bilioni tatu, mwekezaji huyu katika mkataba ule wa awali alikuwa awekeze kwa maana ya fedha kianzo dola milioni 600.

Mheshimiwa Spika, tunaamini katika majadiliano ambayo tunaendelea nayo sasa tutaona namna gani sasa kuhakikisha mwekezaji huyu anaweka fedha au mtaji wa kutosha ili sisi kama nchi tuweze kunufaika, zaidi katika mkataba huu hatuweki fedha yoyote lakini zaidi kupitia sheria zetu tutakuwa wanufaika wakubwa kwa sababu zile asilimia 20 ni *interest* ambayo sisi kama nchi hatuwekezi fedha bali kutokana na utekelezaji wa mradi huu

sisi hizo ni asilimia ambazo tayari Serikali tunapata bila kuingiza mtaji wowote katika mradi huu.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mwita Biniphace Getere swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Waziri yananipa wasiwasi, kwa sababu mimi nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na inavyosemekana kwamba huyo mwekezaji wa kwanza ana matatizo na Serikali, inaonekana kwamba uwezo wake haupo. Sasa majibu ambayo anatupa Waziri ni ya Mkandarasi mwekezaji mpya au mwekezaji wa kwanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli Mkandarasi huyu baada ya kutokutekeleza mradi huu kwa wakati kulingana na mkataba ule wa awali, Serikali tuliweza kufanya ufuatiliaji wa uwezo wa mkandarasi huyu. Kweli katika moja ya vitu ambavyo vilionekana ni kwamba alikuwa na uwezo mdogo, lakini baada ya majadiliano ya hivi karibuni amesema anaweza kufanya lakini bado tunaendelea kuona kama kuna mwekezaji mwingine ambaye anaweza kuwekeza baada ya kumalizana na huyu aliyeko mwanzo kama atashindwa.

Mheshimiwa Spika, katika majadiliano haya mojawapo ni kuona na kutathmini uwezo wa mwekezaji huyu wa mwanzo Sichuan Hongda na tukiona kwamba hana uwezo kulingana na taarifa ambazo tumezipata na vyanzo vya kutoka nchini kwake *then* tunaweza kutafuta sasa mwekezaji mwingine kulingana na utaratibu wa mkataba wa awali ambao lazima tuuvunje au tutafute namna nyingine ili kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa manufaa ya nchi. Kwa hiyo, haya yote katika majadiliano haya ya sasa hivi yanazingatiwa. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani hoja ya msingi mjipe muda, majadiliano na huyu aliyepo yanaisha lini ili haya

mkishaona kwamba ameshindikana tafuteni mwingine siyo lazima mkae naye miaka na miaka. Kama alishindwa kuonesha uwezo huko nyuma sasa hizi mnaona huenda anao basi malizaneni naye, jipeni muda kwa maana ya kwamba ili Bunge lipate picha kwamba Serikali inayo nia ya kuwekeza kwenye hili eneo, kwa sababu pungufu ya hapo hili jambo litakuwa linarudi, linarudi, linarudi na mkiendelea kumshikilia huyo huyo tunakuwa hatuelewi kidogo. Kwa nini mnang'ang'ania mtu ambaye mmejadiliana naye weee, na imeshindikana mpaka leo?

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo Mheshimiwa Neema Mgaya hili swali lake nadhani utembee nalo Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana, haya maswali yote ya nyongeza yaliyoulizwa muyazingatie kwenye hayo majadiliano. Wabunge wanataka majibu ya kuanza kwa mradi huu. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 747

**Kukamilisha usambazaji wa umeme wa REA – Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme wa *REA* katika Kata na Vijiji 23 vya Jimbo la Mbulu Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa II ambapo vijiji vyote visivyokuwa na umeme vitafikiwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unahudumia vijiji 45 vilivyopo katika Jimbo la Mbulu Vijijini, ambapo kati ya hivyo, vjijiji 15 vimekwishawashiwa umeme na vijiji 30 kazi mbalimbali zinaendelea. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2023. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Gregory Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata za Eshkesh, Yaeda Chini na wakati unajibu swali mwaka jana ulisema mwezi wa saba ndiyo watapata umeme lakini sasa umepeleka mwezi wa 12. Je, huoni kwamba utakuwa unatucheleweshea kupata umeme katika Kata hizi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Waziri ametupa vijiji kadhaa ambavyo vitapa umeme kama *underline*. Kwa sisi wa vijijini, vijiji vyetu lazima umeme upelekwe ndio uweze kupatikana umeme na kama utapeleka umeme katika maeneo ya *underline* peke yake ni kwamba sisi wa vijijini hatutapata umeme.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari sasa kubadilisha kauli hii na mpango huu ili kuhakikisha sisi wa vijijini tupate umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikuwa tunatarajia kumaliza mradi wa *REA III Round II* kwa awamu tofauti tofauti katika maeneo mbalimbali na sasa kwa walio wengi imekwenda mpaka Desemba mwaka huu na sababu kubwa ni mbili ambazo nyingine tulishazieleza huko nyuma za UVIKO na kuongezeka kwa bei za vifaa. Sababu nyingine iliongeza mwezi wa kumi wa mbili kuwa ndio *deadline* sasa ni kuongezeka kwa zile kilometa mbili ambapo Wakandarasi takribani wote 31 tayari wameshasaini ile mikataba ya kuongeza hilo loti kilometa mbili ili tuweze kuwa sasa kuwa na kilometa tatu za kupeleka umeme. Yote hiyo inatakiwa ikamilike kufikia mwezi Desemba.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Flatei pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wote tusaidiane katika hili tumalize kazi hii ya upelekaji wa umeme katika vijiji vyote ifikapo Desemba mwaka huu ikiwa na *extention* ya hizo kilometa mbili.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili naamini alikuwa anazungumzia vitongozi japokuwa ametaja vijiji ambavyo viko *underline,* kwa sababu vijiji vyote vitakamilika Desenba mwaka huu. Tunafahamu kwamba tuna vitongoji 15 ambavyo tutapeleka kwa kila Jimbo. Kumekuwa kuna *concern* za Waheshimiwa Wabunge kwamba wapo ambao hawana vitongoji ambavyo viko chini ya *line* ambazo ni *existing* kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali sikivu ya Daktari Samia Suluhu Hassan tumerudi tena mezani kutizama namna ambavyo tunaweza tukapanua wigo wa mradi na tunatafuta aidha tupate pesa ya nyongeza au tubadilishe *procurement process* ili tuweze kupata vifaa na kuwapa Wakandarasi kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote.

Mheshimiwa Spika, hili tunalifanyia kazi na ninaamini litakuja na majibu mazuri katika muda mfupi ujao.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa mliosimama mko wengi ukipewa nafasi nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika Mji wa Kasulu lipo tatizo la umeme kukatikakatika wakati wa mchana na kurudishwa usiku. Je, ni lini tatizo hilo litakwisha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mafupi kama maswali yanavyokuja.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, katika maeneo yote ambayo kuna tatizo la kukatikakatika kwa umeme tunafatilia sababu huenda ni kuongezeka kwa mzigo au ni kutotosha kwa umeme tutafuatilia na hapo ili tatizo hilo tulimalize lakini tunaamini tukifikisha gridi kubwa Mkoa wa Kigoma tatizo hilo litakwisha kwa upana wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Massare swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi vitongoji ambavyo viko *underline* havidi vitano.

Je, Serikali iko tayari sasa kutoa jibu la uhakika kwamba vitongoji katika Jimbo langu navyo vitapatiwa umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swali la msingi tunatafuta mbinu mbadala ambayo itatuwezesha kupata mradi utakaofikia vitongoji 15 vilivyo *underline* na visivyo *underline* kwenye Majimbo yote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daud Protas swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante katika vijiji vipya ambavyo mnapeleka umeme, kumekuwa na tatizo la Mkandarasi kufunga vifaa vilivyoko chini ya viwango na kusababisha umeme kukatikakatika na kukosa umeme zaidi ya siku 40.

Je, nini usimamizi wa Serikali kusababisha hili tatizo kutokuwepo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, vifaa ambavyo tunavifunga kule tunavihakiki kabla ya kuvilipa, inawezekana labda ni matumizi vimefika muda wake lakini nimwombe Mheshimiwa Mbunge tutashirikiana kuhakikisha kwamba tunahakiki tatizo hasa ni nini kama ni vifaa mbavyo havikidhi basi tuviondoe na mkandarasi arekebishe tatizo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mkandarasi anayeitwa Giza anasuasua sana miradi yake katika Jimbo la Kiteto. Je, ni lini miradi ya umeme ya vijiji vya Kiteto itakamilika?

**SPIKA:** Anaitwa Giza

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, Giza.

**SPIKA:** Ni Mkandarasi wa umeme halafu anaitwa Giza

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, yes! na miradi yake inasuasua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, mkandarasi *Giza Cables* ni mkandarasia anayetoka Misri na Misri kuna Mji ambao unaitwa Giza na ndio jina lake linapotokea na alikuwa anafanya kazi Manyara na Mara. Ameshakamilisha loti yake ya Manyara na kwa Manyara tunaendelea kumsimamia ili akamilishe kazi yake kabla ya Desemba atakuwa amekamilisha kazi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma Kata ya Chiwezi bado haijafikiwa na umeme. Serikali mna mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wa Chiwezi wanapata huduma ya umeme? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Chiwezi watapata umeme kabla ya mwezi Desemba mwaka 2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinga swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, Serikali imefikia hatua gani kutafuta mkandarasi kwa ajili ya Visiwa vya Kilwa Kisiwani pamoja na Songo Mnara kupeleka umeme wa *REA*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, wenzetu wa *REA* wanakamilisha mradi wa kupeleka umeme katika visiwa ambao unajitegema tofauti na wa *REA* kwa sababu *REA* inaunganisha kwenye gridi, lakini maeneo ya visiwani bado hatujaweza kufikisha gridi lakini tunakamilisha kwenye visiwa takribani kama 358 vya kupelekea umeme. Mradi huo utakapokamilika Mheshimiwa Kassinge ataona tukiutekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushurukuru sana. Katikakatika ya umeme Jimbo la Kibiti, Rufiji, Mkuranga imekuwa ni donda sugu. Nini mkakati wa Serikali kukomesha tatizo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani ni Mkoa wenye viwanda vingi sana na unao-*consume* umeme mwingi zaidi, lakini tunahakikisha kwamba katika mradi

wetu wa Gridi Imara tunautizama kwa karibu ili kuhakikisha wanapata umeme wa kutosha na wa uhakika na katika eneo lake la Kibiti tatizo hilo litakwisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Kabla sijaleta tangazo la wageni kwenu nielezee jambo ambalo lilitufanya tuahirishe Bunge kwa muda.

Waheshimiwa Wabunge, huu Ukumbi wetu wa Bunge pia majengo yote kwa maana ya Jengo la Utawala, Jengo la *Utawala Annex* na hili la Bunge yote yamewekewa vifaa ambavyo vinaweza kutambua uwepo wa moshi ama kama siyo moshi basi jambo lingine ambalo linaweza kuleta athari kwenye haya majengo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa siku ya leo jengo letu hili la Bunge kwa sababu ukiacha hapa tunapokaa Waheshimiwa Wabunge, kuna sehemu ya chini ya ukumbi huu. Sasa ile sehemu ya chini pia huwa ina matumizi mbalimbali, na kuna watu ambao huwa wanatumia huko chini. Sasa kule chini kuna chumba kimojawapo ambacho kilikuwa na hitilafu, hiyo hitilafu imetokana na kwamba walikuwa wanafanya marekebisho kwa hiyo, inabidi watindue eneo. Sasa katika kule kutindua vumbi ikatoka, kwa sababu vile vinavyonasa hitilafu, vikanasa ile vumbi kama moshi kwa hiyo ndiyo maana ikapiga kelele kuashiria kuna shida kwenye jengo hili.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuwatoa hofu kwamba hilo jambo limeshadhibitiwa kwa hiyo marekebisho yanaendelea lakini kwa utaratibu mzuri. Sasa katika kueleza hivyo niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge kila mtu ametoka kwa usalama hatujapewa taarifa ya mtu yeyote aliyeumia. Kwa hiyo,

Wabunge wote baada ya kulipokea lile tangazo kila Mbunge ameelekea mlango ambao upo upande wake. Tuna milango ya kutokea Nane na nimeona kila Wabunge walikuwa wanaelekea kwenye mlango ulio karibu na yeye ili watu wasisongamane. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa hilo.

Waheshimiwa Wabunge, pia nitoe sasa ufafanuzi kwamba Mbunge siku zote lazima ufahamu mlango ulio karibu na wewe ni upi, usiende kuutafuta ulio mbali. Pia ukishatoka kwenye huo mlango usibaki hapo ulipotoka kwa sababu tunayo maeneo ambayo inabidi uende hapo ndiyo pako salama zaidi pia ndiyo matangazo yanaweza yakatoka hapo. Kwamba, hitilafu hii itatuchukua muda gani kurekebisha au ni hitilafu ambayo itatuchukua muda mrefu kwa hiyo watu tuendelee na shughuli zingine mpaka tutakapopata matangazo tena.

Waheshimiwa Wabunge, sasa maeneo yetu ambayo ni salama ikishatokea changamoto kama hii kwa hapa Bungeni yako matatu. Kwa humu ndani yaani wageni pamoja na Wabunge tunaokuwa tumetokea kwenye hili jengo la Vikao vya Bunge, tukitoka milango yote Nane unaruhusiwa kutoka na ndivyo inavyotakiwa. Ukishatoka huko nje wote tunaelekea kwenye Lango C ndiyo eneo la kukusanyika wote tukitoka humu ndani. Lango C kwa wale ambao hawalifahamu ni lile lango ambalo huwa wanapita wageni ndiyo eneo ambalo inabidi wote tukakusanyike hapo ili tujue nini kilichotokea na mambo kama hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale wanaokuwa upande wa Utawala sehemu ya kukusanyika ni ile sehemu ya wazi upande wa nyuma ya jengo. Kwa hiyo, Mbunge ukijikuta uko kwenye Kamati na Kamati yako inafanyakazi pengine kwenye jengo la Utawala ukasikia kelele kama ile tuliyoisikia humu ndani, unaelekea ile sehemu ya nyuma ya lile jengo ambalo ni katikati ya eneo lile la Habari, lile Jengo la Habari na Jengo la Utawala. Kama hupafahamu ni vizuri ukapafahamu, kwa sababu ukishatoka humu ndani tunashukuru kulikuwa hakuna giza ama moshi, maana wakati mwingine unaweza ukatoka ukawa huelewi uelekee wapi, sasa ni viziuri kufahamu wapi wenzako

wameelekea na maana yake kama kuna haja ya uokozi wa kutokea hapa, uokozi utakuwa kwenye hayo maeneo matatu, ukiwa sehemu nyingine itabidi tuanze kukutafuta. Nadhani nimeeleweka Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wa Jengo la *Utawala Annex* vivyo hivyo upande wake wa nyuma kuna sehemu ya wazi na imeandikwa kwamba hapo ndiyo sehemu ya kukusanyika kukiwa na jambo la dharura. Kwa hiyo, hicho ndicho kilichotokea nimeona nitoe huo ufafanuzi pia wananchi ili wafahamu kwamba hatujapata madhara ya mtu yeyote. Baada ya kutoa hayo maelezo ya jumla nilete tangazo la wageni tulionao Bungeni siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Wageni wageni waliopo Jukwaa la Spika.

Ninao wageni ambao ni walimu kutoka Shule ya Msingi Lyoto ya Jijini Mbeya na hawa ni Ndugu Emmanuel Ndunguru, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Seth Masisi, karibu sana; yupo Ndugu Imelda Nkeka, karibu sana; yupo Ndugu Nikusubila Kornel, karibu sana; yupo Ndugu Catherine Mwasubila, karibu sana; yupo Ndugu Niwako Amosi, karibu sana; yupo Ndugu Glory Mushi; yupo pia Ndugu Anna Chiwinga, karibuni sana, hawa ni walimu kutoka Shule ya Msingi Lyoto, Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao pia wageni watano kutoka nchini Marekani na hawa ni Ndugu Tausi Likokola, karibu sana. *(Makofi)*

Huyu mnaweza kuwa mnamfahamu ni mwanamitindo ambaye anafanya kazi huko lakini Mtanzania, karibu sana. Ameongozana na Ndugu Neema Newton, karibu sana, yuko pia na Ndugu Musa Denes, karibu sana; yuko pia Ndugu Mosses Londo, karibu sana; sijui kama ni Ndugu yake Mheshimiwa Dennis Londo lakini huyu ni Mosses Londo. Haya yupi pia Ndugu Jacqueline Jones, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Ummy Nderiananga ambaye ni Naibu wa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na hawa ni viongozi wa Taasisi ya *CBM International* inayoshughulika na masuala ya watu wenye ulemavu kutoka Ujerumani. *(Makofi)*

Hapa yupo pia Ndugu Nesia Mahenge ambaye ni *Country Director CBM International - Tanzania Office,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Dominique Schulkopthen ambaye ni *Director Of Disability Inclusion from CBM International, Germany Office,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Albert Kombo ambaye *Regional Director for East Africa and Southern Africa* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Richard Dallu ambaye ni *Programme Manager,* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yuko mgeni wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ambaye ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na huyu ni Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita ambaye ni Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Mheshimiwa Angelina Mabula ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na huyu ni Ndugu Qayllah Bilal, huyu ni Mjumbe wa Kamati ya Uendeshaji ya Chipukizi CCM binti mwenye miaka 11, karibu sana ambaye ameambatana na baba yake mzazi ambaye ni mwanamuziki wa kizazi kipya wa bongo wa fleva Ndugu Nurdin Bilal, maarufu kama Shetta, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wetu sisi sote; tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Angeline Mabula (Mb), tena ambao ni Machinga kutoka Jijini Mwanza, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora hawa ni walimu wakuu kutoka Jimbo la Kibakwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 40 wa Mheshimiwa George Simbachawene ambao hawa ni wanafunzi na walimu 40 wa Shule ya Msingi Idunda, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 54 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria nao ni wanafunzi 47 na walimu saba kutoka Shule ya Msingi *St. Joseph* kutoka Jijini Dar es salaam, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tano wa Mheshimiwa Omari Juma Kipanga ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoka Mafia, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Lushoto na Mjumbe wa Baraza la Usalama Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Simon Songe kutoka Busega Mkoa wa Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Yustina Rahhi ambaye ni Mtoto wake kutoka Jijini Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo kutoka Mbagala Jijini Dar es Salaam, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Hassan Mtenga ambao ni watoto wake kutoka Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Edward Olelekaita ambao ni Wakuu wa Shule Wilaya ya Kiteto, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni watoto wake kutoka Kishapu Mkoa wa Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 13 wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Kishapu Mkoa wa Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Regina Qwaray kutoka Babati, Mkoa wa Manyara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mufindi Mkoa wa Iringa, karibuni san. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Dorothy Kilave ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Amina Daud Hassan ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Almas Maige kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Said Issa ambaye ni mtoto wake kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani (Mb), kutoka Singida Kaskazini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Nkoma kutoka Meatu Mkoa wa Simiyu, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tano wa Mheshimiwa Joseph Kamonga kutoka Ludewa Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambao ni watangazaji wa *Rubondo FM* kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Husna Sekiboko ambao ni familia yake kutoka Lushoto Mkoa wa Tanga, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Almas Maige nadhani hawa wameshatangazwa.

Tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Abbas Tarimba ambao ni Viongozi wa Jumuiya ya Vijana kutoka Kinondoni Jijini Dar es salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 31 wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni Timu ya *Mailisita FC* ambao ni Washindi wa Ligi ya *Saashisha Cup* wameambana na Mwenyeviti wa CCM Kata zote Jimbo la Hai na Viongozi wa Chama cha Mpira kutoka Wilaya ya Hai, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 54 wa Mheshimiwa Samweli Hhayuma ambao ni Chama cha Walimu Wilaya ya Hanang, viongozi na watumishi wa CWT Wilaya, walimu waliofanya vizuri katika masomo yao kwenye Matokeo ya Mitihani ya Kitaifa 2022 na Kamati ya Utendaji ya Wilaya, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao Bungeni asubuhi hii.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Haya kuna Mheshimiwa Condester Sichalwe, halafu Mheshimiwa Hussein Amar.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Nimesimama kwa Kanuni ya 76 niombe mwongozo wako na maelekezo yako.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Juni, niliuliza swali la nyongeza hapa Bungeni, kuhusiana na changamoto ambayo tumeipata kwenye Jimbo la Momba kuhusiana na maji. Wanafunzi wa katika shule mbili tofauti wamepoteza maisha. Shule ya Sekondari Momba pamoja na Shule ya Sekondari Kamsamba kwa kutumbukia mtoni kwa ajili ya kwenda kutafuta maji kwa mwendo mrefu.

Mheshimiwa Spika, nikauliza swali la nyongeza hapa na Wizara ya Maji wakanijibu kwamba wangeweza kufanyia jambo hili maana yake niliomba kisima cha dharula ili kuweza kunusuru maisha ya wanafunzi hawa. Wakasema kwamba wangeweza kutuchimbia kisima au kama kuna kisima cha jirani kuongeza *extension* ili maji yaweze kwenda kwenye shule hizo.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha tarehe 23 Juni, Ijumaa iliyopita niliwasiliana na Meneja wa Mkoa wa *RUWASA* pamoja na Meneja wa Wilaya hawana taarifa zozote za dharula za kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Sisi watu wa Momba tumejisikia unyonge sana na kuona kwamba Wizara ya Maji walituhadaa baada ya kusema jambo hili wangelichukua kwa dharula. Je, sisi wananchi wa Jimbo la Momba pamoja na watoto kwenye hizo Sekondari tutaendelea kufa kwa ajili ya kwenda kufuata maji mtoni? Hata pale tulipo omba tupate visima vya dharula ili kwa ajili ya kuwasaidia watoto hawa?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa Kanuni hiyo hiyo ya 76 kutokana na tukio ambalo limetokea asubuhi hii ya leo nimeona kidogo kama vile kuna tofauti.

Mheshimiwa Spika, nataka nipate mwongozo inapotokea hatari kama hii na *alarm* kulia inatuhitaji tuondoke mara moja lakini kwa tukio la leo *alarm* hiyo imelia Kiti kikachukua kama dakika mbili kutoa maelekezo kwamba tutoke haraka kwenda nje. Je, tuwe tunasubiri mpaka Kiti kinatoa taarifa ama *alarm* ikilia tutoke mara moja nje?

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huo utakuwa mwongozo wa mwisho. Mheshimiwa Justin Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 54 ambayo inaweza kuliomba Bunge kusitisha Shughuli kwa muda kwa ajili ya kujadili jambo maalum.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Iringa, kumejitokeza jambo ambalo limeleta taharuki kubwa na hakuna utulivu. Kuna simba ambao hawajulikani idadi yao, ambao wametoroka katika Mbuga ya Ruaha mwanzoni walikuwa kwenye Jimbo la Kalenga na kwa kuwa ni wa Kilolo nilitulia tu nikajua wataishia hapo. Lakini baadaye kufikia jana nikasikia wameingia Kilolo kama hiyo haitoshi nimesikia asubuhi wapo Iringa Mjini tena maeneo ya Gangilonga ambako ni maeneo mashuhuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichosema tu ni tahadhari kwamba tusitoke nje na kutembea hovyo hovyo na sisi wakulima hata chakula cha kutosha tu nyumbani huwa hatuweki unaenda unavuna, unakoboa mahindi unapika unakula ugali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naliomba Bunge lako. Kwa sababu hii ni taharuki na watu wa Dar es salaam wasifikiri wako salama kama mimi nilivyofikiri niko Kilolo niko salama. Hawa simba

hatujui watafika wapi? ningeomba kutoa hoja kwamba Bunge lisitishwe shughuli kwa muda liweze kujadili jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Hoja haijaungwa mkono hata hivyo. *(Kicheko/ Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Amesimama Mheshimiwa Condester Sichalwe kwa kutumia Kanuni ya 76 akieleza jambo ambalo lilitokea yeye kwa maelezo yake amesema tarehe 12 Juni, 2023; kwamba aliuliza swali hapa linalohusu Wizara ya Maji na akaeleza udharula, kwanza hilo jambo haliwezi kuombewa Mwongozo leo. Lakini katika maelezo yake ameeleza kuhusu vifo vya watoto wa shuleni kwa kukosa maji.

Sasa nilikuwa najaribu kutazama hapa namuona Waziri wa Nchi ndiyo yupo simuoni Waziri wa Maji wala Naibu Waziri siwaoni wote wawili. Sasa Waziri wa Nchi upo na Mheshimiwa Mbunge anasema aliuliza swali. Mheshimiwa swali lako lilikuwa la nyongeza ama swali la msingi?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa lilikuwa swali la nyongeza? Lakini hata hivyo Mheshimiwa Waziri wa Nchi naomba ulichukue hili kwa sababu linahusisha vifo vya wanafunzi kwa maelezo aliyoyatoa yeye. Sasa kwamba wanafunzi walikufa kweli ama hawakufa mimi nawewe hatuwezi kujua anajua Mbunge mwenye Jimbo. Maadam jambo hilo limehusisha vifo vya wanafunzi ni Wizara ya Maji ichukue hatua ili hawa wanafunzi tuwaepushe na hayo madhira ambayo upo uwezokano wakayapata hata hawa ambao wapo, kama hiyo kadhia itaendelea na hili. Kwa sababu Serikali tayari imefanya hatua kubwa sana kwenye hili eneo la maji ile mitambo ilionunuliwa ya kuchimba maji imepelekwa kila mkoa.

Kwa hiyo, kama uwezokano upo basi hilo eneo lipelekewe hiyo mitambo ikachimbe maji kama yapo na kama hayapo basi hatua mbalimbali Serikali ichukue kuzinusuru hizi shule mbili watoto waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mwongozo mwingine uliyoombwa na Mheshimiwa Hussein Amar akieleza kuhusu hili jambo la dharula lilitokea hapa ndani na swali lake anataka kujua kama inabidi tusubirie baada ya kusikia lile jambo tusubiri maelekezo ama vipi? Kasema dakika mbili, hazikuwa dakika mbili Mheshimiwa ni sekunde kama thelathini hivi. Kwa hiyo, dakika hazikufika wala hata moja haikufika.

Hoja ya msingi ambayo imekufanya usimame nadhani ile kwamba maamuzi ya haraka tunaposikia jambo kama hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa asimame hapa mbele akizungumza, kwa hivyo ikabidi nimsimamishe ili nijue huo ni mlio wa simu au ni mlio wa kuhashiria kwamba kuna jambo la dharula. Kwa hiyo, mtagungua nilimwambia Mheshimiwa Naibu Waziri aache kujibu hili niweze kusikia maana wakati mwingine mnaziacha simu zenu hapa na simu zina milio ya kila aina.

Kwa hiyo, nilipojiridhisha kwamba ni mlio unaohashiria kwamba kuna jambo la hatari ama jambo la dharula, ndiyo nikasema Waheshimiwa Mbunge mlio huo mnaousikia unaashiria kwamba tunatakiwa tutoke humu ndani. Sasa Wabunge mkaanza kusimama na kwenda na mimi nikasema sasa nahairisha shughuli za Bunge mpaka tutakapo taarifiana.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani katika mazingira haya ni ngumu sana Mbunge kuanza kunyanyuka na kukimbia kwakusikia tu maana inaweza kuwa ni simu. Kwa hiyo, ikiwa tuko katika mazingira kama haya pengine ni vizuri kusikilizana na ndiyo maana huwa tunasisitiza Wabunge tuongee kwa sauti ya chini ili itusaidie kusikia na haya mengine. Kwa hiyo niwashukuru kama nilivyo washukuru mwanzo kwamba mmetoka kwa utaratibu wa kutumia milango yote iliyoko hapa Bungeni na hatujapata madhara.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Amar yeyote kwa kweli anaekuwa amesikia na ana uhakika ni mlio huo wala hakuna shida anapaswa yeye kutoka. Lakini inabidi uwasaidie na wenzako ili wajue uwe ujasikia peke yako, Kwa hivyo unaweza ukakimbia Kiti kama chenyewe hakijasikia ili kitoe hiyo taarifa lakini kimsingi ukishasikia hautakiwi kusubiria maelekezo kama umejiridhisha kwamba ni hali ya hatari.

Kwa hiyo, kwa mwongozo ukishajua ni jambo la hatari wewe shika njia siyo lazima mimi niseme kwanza. Lakini kwa mazingira ya leo ilikuwa lazima tu, kwa sababu kulikuwa na mtu anazungumza hapa ikawa kidogo ngumu kujua kama ni mlio wa simu ama wa vifaa vyetu tulivyoviweka.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama pia Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga akieleza kuhusu jambo la dharula na akitaka tutumie Kanuni ya 54 kujadili simba ambao kwa maelezo yake anasema wako huko kwenye mitaa ya Iringa na sasa wameishafika Mjini kabisa wakitembea huko, kwanza jambo lenyewe ni kweli ni jambo la hatari. Kwa sababu watu wanaweza kupata madhara, kwa hiyo, ni jambo kweli la dharula kumuona simba mjini akitembea ni jambo la dharula.

Kwa maana ya Wabunge kujadili nafikili Mheshimiwa Mbunge alikusudia kwamba Bunge pengine tuweze kujadili kwa maana ya kuiambia Serikali nini cha kufanya? Lakini sasa simba kwa sababu siyo kitu cha kawaida simba kutembea mjini hata sisi Wabunge hakuna ushauri ambao tunaweza kuwa nao wa kuipa Serikali. Sasa isipokuwa ni Serikali kuchukua hii taarifa kwamba simba inawezekana ni mmoja ama wawili lakini simba yeyote hata akiwa mmoja tu anaweza kuleta madhara.

Kwa hiyo, ni upande wa Waziri hapa pamoja na kwamba hoja inayokuja mbele ni ya kwako. Lakini fanya namna ufanye mawasiliano na vituo vyako vilivyoko Ruaha, vilivyoko huko Iringa ili waweze kushirikiana na polisi kuweza kudhibiti hawa simba hawa simba kabla hawajaleta madhara. Ikiwezekana siyo hoja tu ya kuua simba lakini pengine kuwalaza ili wawabebe wakawarudishe huko wanakopaswa kuwa. Kwa sababu tukisema

pia wauwawe popote watakapokutwa na sisi tunataka simba waendelee kuwepo ila wakae maeneo yao.

Kwa hiyo, ninyi fanyeni mawasiliano ili jambo hili lisije likawafikia watu watu wa Dar es salaam kama alivyosema Mbunge wa Kilolo, kwamba wa Dar es salaam wasijione wako salama sana maana na wenyewe wana simba kule wako karibu nao na wengine wanatoka kwako Rufiji.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri alishaweka hoja zake mbili hapa. Sasa kwa utaratibu wetu tutamwita atawasilisha hoja ya kwanza, baadaye atakuja Mwenyekiti wa Kamati, baadaye atakuja tena Waziri halafu tutamwita Mwenyekiti halafu tutaendelea na utaratibu uliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Katibu naona umenigeukia nilikuwa sijakuita bado kabla ya hiyo miongozo? ahaa haya

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi
### na
### Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa karibu uwasilishe hoja yako.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 924 la mwaka 2019 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 7460. Lengo la kuanzishwa kwa Hifadhi hii lilikuwa ni kuimarisha uhifadhi na hivyo kukuza utalii, uchumi kuwezesha kufanyika kwa tafiti na kutoa elimu kwa vitendo kwa wananchi watakao tembelea hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi kwa Pori la Akiba Kigosi na baadaye Hifadhi ya Taifa Kigosi sehemu ya Hifadhi hii ilikuwa ni Hifadhi ya Msitu Mto Nikonga na Usungwa ambapo wananchi wenyeji kutoka Wilaya za Bukombe, Mbogwe, Kahama na Ushetu walikuwa wakitumia maeneo hayo kwa ajili ya ufugaji nyuki na uvuvi wa samaki kwa lengo wa kujipatia kipato na kuinua uchumi, kufanya shughuli za kimila na hivyo kujenga mahusiano mema katika shughuli za uhifadhi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa Kigosi, eneo hilo linasimamiwa na Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282, ambayo pamoja na masuala mengine inazuia kufanyika kwa shughuli za kibinadamu ikiwemo ufugaji nyuki, uvuvi wa samaki na shughuli za kimila. Hivyo, wananchi kutoka maeneo jirani waliokuwa wanafanya shughuli endelevu za kiuchumi ndani ya hifadhi wanakosa fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa fursa hizo kwa wananchi, Serikali imeona ni vyema kufuta Hifadhi ya Taifa Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu Kigosi ambao utasimamiwa na Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania *(TFS)* kwa Sheria ya Misitu, Sura namba 323 inaruhusu kufanyika kwa shughuli za kiuchumi ndani ya Hifadhi za Misitu kwa kuzingatia matakwa ya uhifadhi na utaratibu maalum.

Mheshimiwa Spika, kukubalika kwa hoja hii kutatoa fursa na manufaa ya kimazingira, kijamii na kiuchumi kama ifuatavyo:-

(i) Kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu Kigosi yenye ukubwa wa kilometa za mraba 7,460 itakayosimamiwa na Sheria ya Misitu, Sura ya 323. Hifadhi hiyo ya Msitu itakuwa na manufaa ya

kiuchumi kwa wananchi wa Mikoa mitano (Geita, Kagera, Kigoma, Shinyanga na Tabora). Wilaya sita za Bukombe, Mbongwe, Biharamulo, Kakonko, Kahama na Kaliua; na Kata 25. Aidha, vijiji 126 na kaya 113,547 vitanufaika na uamuzi huu. Wananchi wataruhusiwa kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi ndani ya Hifadhi hiyo ikiwemo ufugaji nyuki na uvuvi wa samaki kwa mujibu wa sheria.

(ii) Kuchochea kwa shughuli za ufugaji nyuki kibiashara ambapo takriban wafugaji 1,764 wenye mizinga zaidi ya 521,406 waliokuwepo awali kwenye maeneo hayo wataongezeka maradufu. Hatua hiyo itachangia ongezeko la uzalishaji wa asali nchini kutoka wastani wa tani 32,691 hadi 138,000 kwa mwaka na kuongeza mazao ya nyuki nje ya nchi. Kwa sasa nchi yetu inauza nje takriban tani 1,700 zenye thamani ya Dola za Marekani 14,000,000 ambayo ni sawa 5% ya kiasi chote kinachouzwa kwa sasa.

(iii) Kupata uhakika wa malighafi kwa viwanda sita vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki ambavyo ujenzi wake umewezeshwa na Serikali kwa zaidi ya Shilingi bilioni 2.5 kwenye Wilaya za Mlele, Kibondo, Bukombe, Nzega, Sikonge na Wilaya ya Manyoni;

(iv) Kufanyika kwa shughuli za kimila na hivyo kujenga mahusiano mema kati ya wananchi na wahifadhi kupitia Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998; na

(v) Kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Misitu na Nyuki katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282, Rais amepewa mamlaka ya kurekebisha mipaka ya eneo lolote lililotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa, baada ya kupata idhini ya Bunge na kwa Tamko litakalochapishwa na Gazeti la Serikali. Aidha, Mheshimiwa Rais ameridhia kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa

Kigosi na kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu Kigosi kutokana na manufaa niliyoyaeleza hapo awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu ya Kigosi kama ifuatavyo: -

Kwa kuwa Sera ya Misitu inalenga kuimarisha mchango wa Sekta ya Misitu kwa kuleta maendeleo endelevu ya nchi na kuhifadhi na kusimamia maliasili kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;

Na kwa kuwa Sera hiyo inahamasisha wananchi wanaopakana na hifadhi ya misitu kushiriki kwenye uhifadhi na kufanya shughuli rafiki kwa mazingira, ikiwemo ufugaji nyuki. Inatambua ufugaji nyuki kama shughuli muhimu katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na inaelekeza kwamba mpango wa usimamizi wa misitu ujumuishe shughuli za ufugaji nyuki;

Na kwa kuwa kanda za ufugaji nyuki na kwa kuwa Sheria ya Misitu, Sura ya 323 inatambua na kuruhusu kufanyika kwa shughuli nyingine za kiuchumi tofauti na uhifadhi wa misitu, ikiwemo ufugaji nyuki pamoja na uvuvi wa samaki ndani ya hifadhi ya msitu kwa kibali maalum;

Na Kwa Kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali namba 924 la mwaka 2019 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 7,460 kwa mujibu wa jira nukta zilizoambatanishwa kwenye tangazo hilo;

Na kwa kuwa kabla ya kuanzishwa kwake sehemu ya Hifadhi hiyo ilikuwa ni Hifadhi ya Msitu ya Mto Mkonga na Usumbwa ambapo wenyeji wa Wilaya ya Bukombe, Mbogwe, Kahama, Halmashauri ya Ushetu na Kaliua walitumia maeneo hayo ya misitu kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kimila na shauri nyinginezo za kiuchumi zikiwemo ufugaji wa nyuki na uvuvi wa samaki kwa lengo la kujipatia kipato na kuinua hali zao za uchumi ambapo pia viwanda vitano vya kuchakata na kufungasha

mazao ya nyuki vilijengwa kwa wilaya ya jirani za hifadhi hiyo na jumla ya wafugaji 1,764 wenye mizinga 521,406 walitundika mizinga ya nyuki ndani ya hifadhi hiyo;

Na kwa kuwa baada ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi wananchi wa maeneo ya jirani na wanaopakana na Hifadhi ya Taifa walipoteza fursa ya kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii ndani ya hifadhi hiyo kwa kuwa Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura 282 pamoja na mambo mengine inazuia kufanyika kwa shughuli za ufugaji nyuki, uvuvi na shughuli za kimila kwenye maeneo ya Hifadhi ya Taifa;

Na kwa kuwa kutokana na uwepo wa shughuli hizo za kijamii, kiuchumi hata kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi na kwa kuzingatia idadi kubwa ya wafugaji nyuki na mizinga iliyotundikwa, Serikali imejiridhisha kwamba hakuna eneo mbadala litakalofaa kuwapeleka wananchi hao kwa ajili ya kuendeleza shughuli hizo na kwamba njia pekee ni kuleta suluhisho la kudumu kwa changamoto zinazowakabili wananchi wa maeneo hayo ni kuifuta Hifadhi ya Taifa ya Kigosi na kuanzishwa kwa Taifa ya Msitu wa Kigosi;

Na kwa kuwa kufutwa kwa hifadhi ya Taifa ya Kigosi kutawezesha kupatikana eneo la hekta 746,000, sawa na kilomita za mraba 7,460 ambazo zilitumika kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa Kigosi kwa kuzingatia kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Misitu, Sura 323 shughuli za kiuchumi zikiwemo ufugaji nyuki na uvuvi wa samaki pamoja na shughuli nyinginezo za kijamii zikiwemo shughuli za kimila zinaruhusiwa kufanyika kwenye maeneo hayo;

Na kwa kuwa masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282 inatoa mamlaka kwa Mheshimiwa Rais kurekebisha mipaka ya hifadhi ya Taifa baada ya kupata ridhaa ya Bunge;

Na kwa kuwa kwa kuzingatia manufaa yanayopatikana kutokana na kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa Kigosi ikiwemo kuendeleza shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanywa na wananchi wa maeneo husika na kujenga na kudumisha

mahusiano mema baina ya wananchi na Serikali yatakayoimarisha uhifadhi na maliasili kwenye maeneo husika;

Hivyo basi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Masharti ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282 linaazimia kuridhia kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi yenye ukubwa wa kilomita za mraba 7,460 kama ilivyoainishwa kwenye kiambatanisho cha azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimwite sasa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, aje awasilishe Maoni ya Kamati.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(3) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(8)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la azimio hili ni Sheria ya Misitu, Sura ya 323 kutambua na kuruhusu kufanyika shughuli nyingine za kiuchumi tofauti na uhifadhi misitu ndani ya hifadhi ya msitu kwa kibali maalum. Sheria hiyo inaruhusu shughuli nyingine za kiuchumi kama ufugaji nyuki na uvuvi wa samaki ndani ya hifadhi ya msitu kwa kibali maalum. Hivyo kuanzishwa kwa hifadhi

ya msitu kutawezesha wananchi wa Wilaya za Bukombe, Mbogwe, Kahama, Ushetu na Kaliua kuendesha shughuli za kiuchumi kama vile ufugaji nyuki na uvuvi wa samaki, pamoja na shughuli za kimila.

Mheshimiwa Spika, aidha, sheria inatilia mkazo malengo ya Sera ya Misitu ambayo ni kuimarisha mchango wa Sekta ya Misitu kwenye maendeleo endelevu, kuhifadhi na kusimamia maliasili kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo kwa kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye uhifadhi na kufanya shughuli rafiki kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, uliamua kulileta azimio hili kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili iweze kulifanyia kazi. Aidha, kutokana na masharti ya Kanuni ya 60(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana kuanzia tarehe 29 Mei hadi 26 Juni, 2023 kwa lengo la kuchambua hoja hii muhimu na kuitolea maoni.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati kwa kuanza na manufaa ya azimio hili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati manufaa yatakayotokana na azimio hili ni pamoja na wananchi kupata maeneo kwa ajili ya ufugaji nyuki kama shughuli muhimu katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na uvuvi wa samaki kwa lengo la kujipatia kipato na kuimarisha uchumi. Aidha, wananchi wataruhusiwa pia kufanya shughuli za kimila, jambo ambalo litasaidia kuimarisha mahusiano mema baina yao na mamlaka za uhifadhi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, kabla ya kuanzishwa kwa Pori la Akiba Kigosi na baadaye kupandishwa hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi na hivyo kuwa chini ya usimamizi wa Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282, maeneo hayo yalitumiwa na wananchi katika shughuli za kijamii pamoja na kiuchumi kama vile ufugaji nyuki ambao ulichochea kuanzishwa

kwa viwanda vya kuchakata mazao ya asali katika maeneo ya jirani na hivyo kutoa ajira na kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, hatua ya kuianzisha Hifadhi ya Taifa ya Kigosi iliwakatili wananchi kwani walilazimika kusitisha shughuli zao katika maeneo hayo, kwa sababu Sheria ya Hifadhi za Taifa, hairuhusu shughuli yoyote ya kijamii ndani ya hifadhi. Aidha, viwanda vya kuchakata mazao ya asali vilivyoanzishwa maeneo yanayozunguka hifadhi, viliathirika kwa kukosa malighafi na hivyo kusababisha hasara kwa wamiliki na kuathiri kipato cha wananchi na wafanyakazi kupoteza ajira.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kufuta Hifadhi ya Taifa ya Kigosi utawezesha kuanzisha hifadhi ya Msitu ya Kigosi yenye ukubwa wa kilometa za mraba 9,861 ambayo itasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu chini ya Sheria ya Misitu, Sura 323. Hatua hiyo mbali na shughuli za uhifadhi wa misitu, itawezesha wananchi kuruhusiwa kwa kibali maalum kuendeleza au kutekeleza shughuli za kijamii na kiuchumi, hii ikiwa ni pamoja na kurejea shughuli walizokuwa wakizitekeleza katika maeneo hayo kabla ya kuwa hifadhi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kufuta Hifadhi ya Taifa ya Kigosi utatoa unafuu wa kiuendeshaji kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa *(TANAPA)* kwani itasimamia hifadhi 21 badala ya hifadhi 22 sambamba na kuzingatia kwamba Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ilikuwa haizalishi mapato ya kutosha. Aidha, uamuzi huu utachangia ongezeko la uzalishaji wa asali kutoka tani 38,000 hadi tani 148,000 na hivyo kuongeza mapato ya fedha za kigeni kutoka Dola za Marekani 15,000,000 hadi dola 58,000,000.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo sasa ni maoni na ushauri wa Kamati. Uamuzi wa kufuta Hifadhi Taifa ya Kigosi na kuanzisha Hifadhi ya Msitu wa Kigosi utaimarisha shughuli za kiuchumi na kukuza pato la wananchi wa ukanda huo na Taifa kwa ujumla. Hivyo Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Wananchi na wawakilishi wao waelimishwe na kushirikishwa kikamilifu katika michakato ya kubadili mipaka au

matumizi ya maeneo ili wawe na uelewa wa pamoja kuhusu dhamira ya Serikali na mantiki ya michakato hiyo. Hii inatokana na Kamati kubaini kwamba, wananchi na wawakilishi wao hawakushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa kufuta Hifadhi ya Kigosi na kuanzisha hifadhi ya Msitu wa Kigosi;

(ii) Wananchi waelimishwe kuhusu dhana nzima ya uchumi shirikishi ili waweze kutumia kikamilifu fursa ya kutekeleza shughuli za kiuchumi na kijamii katika eneo la hifadhi ya msitu utakaoanzishwa. Hatua hiyo itawawezesha wananchi kushiriki katika uhifadhi endelevu wa misitu na kunufaika na fursa zinazopatikana katika hifadhi hiyo ya msitu;

(iii) Serikali iandae mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo ya hifadhi inayokusudia kubadili mipaka au matumizi yake au kuyaweka bayana kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo ili kuepusha uvamizi na migogoro pale wananchi wanapotakiwa kuhama ndani ya muda ili kupisha maeneo hayo;

(iv) Serikali ihakikishe inaimarisha mipaka ya Hifadhi ya Msitu wa Kigosi itakayoanzishwa kwa kuwekwa alama (vigingi) ambavyo vinaonekana na kulima barabara kuzunguka eneo hilo ili kuepusha uvamizi kutoka kwa wananchi waishio jirani, jambo linaloweza kuibua migogoro baina ya wananchi na hifadhi hiyo;

(v) Kwa kuwa eneo la hifadhi ya msitu inayokusudiwa kuanzishwa lina uoto wa misitu inayochukua zaidi ya 60% ya eneo hilo; na kwa kuwa eneo hilo ni chanzo cha mikondo ya maji inayoungana na kutiririka kwenda Bonde la Malagarasi, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaimarisha ulinzi na uhifadhi wa vyanzo hivyo vya maji ili kutoathiri ustawi wa uhifadhi wa maeneo hayo na upatikanaji wa maji kwa jamii zinazozunguka eneo hilo;

(vi) Kwa kuwa hifadhi inayokusudiwa kuanzishwa itakuwa na wanyama wakali na waharibifu kama vile simba, chui na viboko na kwa kuwa wananchi wataruhusiwa kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii hifadhini, Kamati inashauri Wakala wa Misitu *(TFS)* ihakikishe inaimarisha ulinzi ili wanyama hao wasisababishe madhara kwa wananchi na mali zao; na

(vii) Kwa kuwa miongoni mwa sababu za kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ilikuwa ni kuimarisha ulinzi hasa kutokana na eneo hilo kukabiliwa na vitendo vya kijangili na kugeuka maficho ya wahalifu, Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba, kufutwa kwa hifadhi ya Kigosi hakuathiri mikakati ya kiulinzi na kiusalama katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nihitimishe kwa kuomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyotimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa kwa hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha kushughulikia azimio hili. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati natumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary Masanja na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbasi kwa ushirikiano wao ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika utaratibu wa usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono azimio na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**27 JUNI, 2023**

**MAONI YA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA KUFUTWA KWA HIFADHI YA TAIFA YA KIGOSI ILI KURUHUSU KUANZISHWA KWA HIFADHI YA MSITU WA KIGOSI - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 60 (3) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(8) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili Kuruhusu Kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi.

## 2.0 CHIMBUKO LA AZIMIO

**Mheshimiwa Spika,** chimbuko la azimio hili ni Sheria ya Misitu, Sura ya 323 kutambua na kuruhusu kufanyika shughuli nyingine za kiuchumi tofauti na uhifadhi misitu ndani ya hifadhi ya msitu kwa kibali maalum. Sheria hiyo inaruhusu shughuli nyingine za kiuchumi kama ufugaji nyuki na uvuvi wa samaki ndani ya hifadhi ya msitu kwa kibali maalumu. Hivyo kuanzishwa kwa hifadhi ya msitu kutawezesha wananchi wa Wilaya za Bukombe, Mbogwe, Kahama, Ushetu na Kaliua kuendesha shughuli za kiuchumi kama vile ufugaji nyuki na uvuvi wa samaki, pamoja na shughuli za kimila.

Aidha, sheria inatilia mkazo malengo ya sera ya misitu ambayo ni kuimarisha mchango wa sekta ya misitu kwenye maendeleo endelevu, kuhifadhi na kusimamia maliasili kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo kwa kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye uhifadhi na kufanya shughuli rafiki kwa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uliamua kulileta azimio hili kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili iweze kulifanyia kazi.

Aidha, kutokana na masharti ya Kanuni ya 60 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana kuanzia tarehe 29 Mei hadi 26 Juni, 2023 kwa lengo la kuchambua hoja hii muhimu na kuitolea maoni. Naomba niwasilishe mbele ya Bunge lako tukufu maoni na ushauri wa Kamati kwa kuanza na manufaa ya azimio hili.

## 3.0 MANUFAA

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati manufaa yatakayotokana na azimio hili ni pamoja na wananchi kupata maeneo kwa ajili ya ufugaji nyuki kama shughuli muhimu katika uhifadhi wa raslimali za misitu na uvuvi wa samaki kwa lengo la kujipatia kipato na kuimarisha uchumi. Aidha wananchi wataruhusiwa kufanya shughuli za kimila, jambo ambalo litasaidia kuimarisha mahusiano mema baina yao na mamlaka za uhifadhi katika maeneo hayo.

Itakumbukwa kwamba, kabla ya kuanzishwa kwa Pori la Akiba Kigosi na baadaye kupandishwa hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi na hivyo kuwa chini ya usimamizi wa Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282, maeneo hayo yalitumiwa na wananchi katika shughuli za kijamii pamoja na kiuchumi kama vile ufugaji nyuki ambao ulichochea kuanzishwa kwa viwanda vya kuchakata mazao ya asali katika maeneo ya jirani na hivyo kutoa ajira na kipato kwa wananchi.

Ni wazi kwamba, hatua ya kuianzisha hifadhi ya taifa ya Kigosi iliwakatili wananchi kwani walilazimika kusitisha shughuli zao katika maeneo hayo kwa sababu sheria ya hifadhi za Taifa, hairuhusu shughuli yoyote ya kijamii ndani ya hifadhi. Aidha, viwanda vya kuchakata mazao ya asali vilivyoanzishwa maeneo yanayozunguka hifadhi, viliathirika kwa kukosa malighafi na hivyo kusababisha hasara kwa wamiliki, kuathiri kipato cha wananchi na wafanyakazi kupoteza ajira.

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa Serikali kufuta hifadhi ya Taifa ya Kigosi utawezesha kuanzishwa hifadhi ya Msitu ya Kigosi yenye ukubwa wa kilometa za mraba 9,861 ambayo itasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu chini ya Sheria ya Misitu, Sura 323.

Hatua hiyo mbali na shughuli za uhifadhi wa misitu, itawezesha wananchi kuruhusiwa kwa kibali maalumu kutekeleza shughuli za kijamii na kiuchumi, hii ikiwa ni pamoja na kurejea katika shughuli walizokuwa wakizitekeleza katika maeneo hayo kabla ya kuwa hifadhi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa kufuta Hifadhi ya Taifa ya Kigosi utatoa unafuu wa kiuendeshaji kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA) kwani itasimamia hifadhi 21 badala ya hifadhi 22 sambamba na kuzingatia ukweli kwamba Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ilikuwa haizalishi mapato ya kutosha. Aidha uamuzi huu utachangia ongezeko la uzalishaji wa asali kutoka tani 38,000 hadi tani 148,000 na hivyo kuongeza mapato ya fedha za kigeni kutoka Dola za Marekani miliioni 15 hadi 58.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** uamuzi wa kufuta hifadhi Taifa ya Kigosi na kuanzisha Hifadhi ya Msitu wa Kigosi kutaimarisha shughuli za kiuchumi na kukuza pato la wananchi wa ukanda huo na taifa kwa ujumla. Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

i) Wananchi na wawakilishi wao waelimishwe na kushirikishwa kikamilifu katika michakato ya kubadili mipaka au matumizi ya maeneo ili wawe na uelewa wa pamoja kuhusu dhamira ya Serikali na mantiki ya michakato hiyo. Hii inatokana na Kamati kubaini kwamba, wananchi na wawakilishi wao hawakushirikishwa kikamlifu katika mchakato wa kufuta hifadhi ya Kigosi na kuanzisha hifadhi ya Msitu wa Kigosi.

ii) Wananchi waelimishwe kuhusu dhana nzima ya uchumi shirikishi ili waweze kutumia kikamilifu fursa ya kutekeleza shughuli za kiuchumi na kijamii katika eneo la hifadhi ya msitu utakaoanzishwa. Hatua hiyo itawawezesha wananchi kushiriki katika uhifadhi endelevu wa misitu na kunufaika na fursa zinazopatikana katika hifadhi hiyo ya msitu.

iii) Serikali iandae mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo ya hifadhi inayokusudia kubadili mipaka au matumizi

yake na kuyaweka bayana kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo ili kuepusha uvamizi, na migogoro pale wananchi wanapotakiwa kuhama ndani ya muda mfupi ili kupisha maeneo hayo.

iv) Serikali ihakikishe inaimarisha mipaka ya hifadhi ya Msitu wa Kigosi itakayoanzishwa kwa kuwekwa alama (vigingi) zinazoonekana na kulima barabara (mkuza) kuzunguka eneo hilo ili kuepusha uvamizi kutoka kwa wananchi waishio jirani, jambo linaloweza kuibua migogoro baina ya wananchi na hifadhi hiyo.

v) Kwa kuwa eneo la hifadhi ya msitu inayokusudiwa kuanzishwa lina uoto wa misitu inayochukua zaidi ya asilimia 60 ya eneo hilo, na kwa kuwa eneo hilo ni chanzo cha mikondo ya maji inayoungana na kutiririka kwenda Bonde la Malagarasi, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaimarisha ulinzi na uhifadhi wa vyanzo hivyo vya maji ili kutoathiri ustawi wa uhifadhi wa maeneo hayo, na upatikanaji wa maji kwa jamii zinazozunguka eneo hilo

vi) Kwa kuwa hifadhi inayokusudiwa kuanzishwa itakuwa na wanyama wakali na waharibifu kama vile Simba, Chui na Viboko na kwa kuwa wananchi wataruhusiwa kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii hifadhini, Kamati inashauri Wakala wa Misitu (TFS) ihakikishe inaimarisha ulinzi ili wanyama hao wasisababishe madhara kwa wananchi na mali zao

vii) Kwa kuwa miongoni mwa sababu za kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ilikuwa ni kuimarisha ulinzi hasa kutokana na eneo hilo kukabiliwa na vitendo vya kijangili na kugeuka maficho ya wahalifu, Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba, kufutwa kwa hifadhi ya Kigosi hakuathiri mikakati ya kiulinzi na kiusalama katika eneo hilo.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyotimiza majukumu yenu kwa weledi na

umakini mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha kushughulikia azimio hili.

Kwa umuhimu wake, natamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Muntazar Giga, Mb – M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Shaabani Omar Shekilindi, Mb
4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb
5. Mhe. Innocent Seba Bilakwate, M
6. Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
9. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb
10. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
11. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb
12. Mhe.Nancy Hassan Nyarusi, Mb
13. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb
14. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
15. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
16. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
17. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
18. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
19. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb
20. Mhe. Munira Mustafa Khatib, Mb
21. Mhe. Dkt. Florence G. Samizi,Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati natumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Mary Masanja (Mb) na

Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbasi kwa ushirikiano wao kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi (*ndc*) kwa kuongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** ninaunga mkono azimio, naomba kuwasilisha.

Timotheo Paul Mnzava, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**
27 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Waziri kuja kuleta azimio lingine linalohusu kubadili mipaka kwa hifadhi ya Ruaha, wapo wageni ambao nimejulishwa kwamba wako humu ndani na hawajatangazwa.

Wako wageni 10 wa Mheshimiwa Olelekaita ambao ni Chama cha Wakulima wa Alizeti, Engusero *AMCOS* kutoka Kiteto, karibuni sana. Hawa wanaongozwa na Diwani wa Kata ya Kaloleni. Sijui Diwani ndio yupi? Mheshimiwa Diwani karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa ujumbe na Mheshimiwa Balozi Mulamula kwamba wapo wajukuu zake humu Bungeni, sijui wako upande gani? Haya karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Angeline Mabula anao wageni wake wengine ambao hawakutangazwa. Yupo Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Ndugu Emmanuel Ngaga Golani. Yupo pia Naima Malaika Mvaru, karibu sana huyo sijaambiwa ni nani, lakini

nimeambiwa yule ambaye ni Kiongozi wa Chipukizi kwamba kaja na mdogo wake anaitwa Kamla. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii aje awasilishe azimio lake lingine. Mheshimiwa Mohammed Omar Mchengerwa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa Ruaha ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 464 la Mwaka 1964, likiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 10,300 na baadaye kufanyiwa marekerebisho kupitia Tangazo la Serikali Namba 28 la Mwaka 2008 kwa kuongeza eneo la Bonde la Usangu na kufikia ukubwa wa kilomita za mraba 20,300. Lengo la kuanzishwa kwa hifadhi hii lilikuwa ni kuhifadhi na kulinda bioanuai hususan wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki na mtiririko wa maji kwenye Mto Ruaha Mkuu ambao ni chanzo kikuu cha maji kwenye mabwawa ya kufua umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uhifadhi wa wanyamapori, Hifadhi hii ni muhimu kiuchumi kwa Taifa kwa sababu inahifadhi chanzo cha maji ya Mto Ruaha Mkuu na inahifadhi wanyama adimu ambao hawapatikani maeneo mengine nchini mfano, choroa na tandala mkubwa. Aidha, hifadhi hii inahifadhi ardhi oevu kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya wakulima, wafugaji na wavuvi wengi zaidi katika bonde la Rufiji *(downstream users)*.

Mheshimiwa Spika, hifadhi hii ilipoanzishwa Mwaka 1964 haikujumuisha eneo la Bonde la Usangu. Bonde la Usangu lilikuwa Pori Tengefu Utengule lililoanzishwa mwaka 1953 likiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 500 kwa lengo la kuhifadhi bionuai katika ardhioevu ya Ihefu. Kutokana na uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji uliofanyika miaka ya 1990, Serikali iliamua kulipandisha hadhi eneo la Utengule na kuwa Pori la Akiba la Usangu kwa Tangazo la Serikali namba 436A la tarehe 24 Julai, 1998. Hata hivyo, kasi ya uharibifu wa mazingira iliendelea kwa kasi na kulazimu Serikali kulipandisha hadhi eneo hilo kwa kulijumuisha katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kupitia Tangazo la Serikali namba 28 la Mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutangazwa marekebisho ya mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha mwaka 2008, Serikali ilianza zoezi la uwekaji vigingi vya mpaka hatua ambayo ililalamikiwa na wanavijiji kuwa maeneo yao yametwaliwa bila kushirikishwa. Hivyo kuzua migogoro wa mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uwepo wa migogoro mbalimbali ya matumizi ya ardhi nchini ambayo inawahusisha ama wananchi wenyewe au Serikali katika maeneo mbalimbali nchini, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, tarehe 15 Januari, 2019 aliwaelekeza Waheshimiwa Mawaziri Nane wa Wizara za Kisekta ambao Wizara zao wanazoziongoza zinaathiriwa kwa namna moja ama nyingine na uwepo wa migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi husika, kuandaa mapendekezo ya ufumbuzi wa kudumu wa migogoro hiyo. Kamati hiyo ilifanya kazi yake ya kutoa mapendekezo ambayo yaliridhiwa na Mheshimiwa Rais kuwa, maeneo yote ya hifadhi ambayo yameshakaliwa na wananchi na kupoteza hadhi ya uhifadhi yaondolewe kwenye hifadhi na kurudishwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hifadhi ya Taifa ya Ruaha Serikali, kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika mkutano wake wa hadhara na wananchi uliofanyika tarehe 18 Januari, 2023 eneo la Kapunga, Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya, alitoa maelekezoo ya kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kuzingatia mapendekezo yaliyowasilishwa na kamati ya Mawaziri Nane wa kisekta. Kukubalika kwa hoja hii kutatoa fursa za manufaa ya kimazingira, kijamii na kiuchumi kama ifuatavyo:-

i. Kupatikana kwa eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 478 ambalo litamegwa kutoka kuwa sehemu ya hifadhi kwenda kwa wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi, kama vile kilimo na ufugaji katika vijiji 29;

ii. Kuhifadhi vyanzo vya maji vilivyopo katika Bonde la Usangu na kuimarisha mtiririko wa maji kwenye Mlima wa

Kipengele na Uporoto kuelekea Lindi Maji na Ihefu ambao ni chanzo cha Mto Ruaha Mkuu unaotegemewa katika kuzalisha umeme wa maji katika Bwawa la Mtera, Kidatu na Bwawa la Mwl. Julius Nyerere, ili kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini;

iii. Kuboresha mifumo ya ikolojia ya Bonde la Usangu ili kurejesha wanyamapori na uoto wa asili kwenye Hifadhi ya Taifa ya ruaha;

iv. Kuimarisha uhifadhi wa maliasili, hususan wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki na viumbemaji wengine;

v. Kuondoa mgogoro wa mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na vijiji husika;

vi. Kuongeza mchango wa pato la Taifa kupitia utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha;

vii. Kuwezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya shughuli nyingine za kiuchumi ikiwemo kilimo, ufugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika usimamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kufanya yafuatayo:-

i. Kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha pamoja na matumizi ya maji;

ii. Kuweka miundombinu inayofaa yenye viwango vinavyokubalika ndani na nje ya hifadhi kwa ajili ya kuendeleza utalii;

iii. Kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi kwa vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Masharti ya Nyongeza ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282, Mheshimiwa Rais amepewa mamlaka ya kurekebisha mipaka ya eneo lolote linalotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa baada ya

kupata idhini ya Bunge na kwa tamko litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Kufanyika kwa Marekebisho ya Mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali, Namba 464 la mwaka 1964, baadae kufanyiwa marekebisho kupitia Tangazo la Serikali, Namba 28 la mwaka 2008 kwa kuongeza eneo la Bonde la Usangu;

Na kwa kuwa marekebisho hayo yalifanyika kwa kuzingatia Sera ya wanyamapori inayohimiza kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda bayoanuai katika mtandao wa Hifadhi ya Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu;

Na kwa kuwa tangu kuongezwa kwa Eneo la Bonde la Usangu kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kumekuwepo na migogoro ya muda mrefu baina ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na vijiji vilivyopo kwenye Bonde la Usangu vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha;

Na kwa kuwa katika kuhakikisha kuwa migogoro ya mipaka kati ya maeneo yha ardhi ya vijiji na maeneo yaliyohifadhiwa inapatiwa ufumbuzi wa kudumu, Serikali imekuwa ikichukua juhudi za dhati na za maksudi kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro hiyo;

Na kwa kuwa baada ya mashauriano ya muda mrefu baina ya Serikali na pande zinazohusika na mgogoro huo, uchambuzi wa kina wa mgogoro husika, Serikali imeridhia kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kumega eneo lenye ukubwa wa kilometa za mrada 478 kwenda kwa wananchi;

Na kwa kuwa Serikali inaamini kwamba, urekebishwaji wa mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha utapunguza migogoro ya mipaka baina ya hifadhi na vijiji vilivyopo kwenye eneo la Bonde la Usangu pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kutaimarisha mahusiano baina ya Serikali na wananchi, uhifadhi wa bayoanuai, hususan Wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki na mtiririko wa maji kwenye Mto Ruaha Mkuu, ambao ni chanzo kikuu cha mabwawa ya kufua umeme;

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282, Mheshimiwa Rais amepewa mamlaka ya kutangaza eneo lolote la ardhi kuwa Hifadhi ya Taifa baada ya kupata idhini ya Bunge na kwa tamko litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali;

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282, sheria imeweka katazo la kubadili, kurekebisha au kufuta Hifadhi ya Taifa isipokuwa kwa Masharti ya Sheria ya Bunge;

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Masharti ya Nyongeza ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282, Mheshimiwa Rais amepewa mamlaka ya kurekebisha mipaka ya eneo lolote lililotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa baada ya kupata idhini ya Bunge na kwa tamko litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali;

Na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anakusudia kutumia mamlaka hayo ya kisheria, ili kurekebisha eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha;

Na kwa kuwa uidhinishwaji wa pendekezo la marekebisho ya mipaka ya eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kutaleta manufaa yafuatayo kwa Taifa letu:-_

i. Kusaidia kulinda mfumo wa ikolojia katika Bonde la Usangu ili kurejesha uoto wa asili kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika Mto Ruaha Mkuu, unaotegemewa kuzalisha umeme wa maji katika

Mabwawa ya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere ili kuimarisha upatikanaji wa umeme, kuimarisha uhifadhi wa maliasili, hususan wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji,

ii. Kuondoa mgogoro wa mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na vijiji vilivyopo kwenye Bonde la Usangu vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuongeza Pato la Taifa kutokana na hifadhi hiyo kuendelea kuwa kivutio cha watalii,

Hivyo basi, kwa kuzingatia manufaa ambayo Serikali, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wananchi wa maeneo husika watayapata, kutokana na marekebisho yanayopendekezwa. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 11 na kwa mujibu wa Masharti ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura 282, linaazimia kuridhia marekebisho ya mipaka ya eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kumega kilometa za mraba 478 kutoka kwenye hifadhi hiyo na baadae kufanya marekebisho hayo ili yaweze kufanyika. Hifadhi ya Taifa ya Ruaha itakuwa na ukubwa wa kilometa za mraba 19,822 kama ilivyoainishwa kwenye kiambatanisho cha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, aje awasilishe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa

Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(3), ikisomwa pamoja na kifungu cha 6 (8)(b) ya Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha Mipaka kwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Azimio; tarehe 18 Januari, 2023 Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akihutubia wananchi kwenye mkutano wa hadhara eneo la Kapunga, Wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya, alitoa maamuzi ya Serikali ya kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kuzingatia mapendekezo yaliyowasilishwa na Kamati ya Mawaziri Nane wa Kisekta. Sehemu ya mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri Nane ambayo yaliridhiwa na Mheshimiwa Rais ni kwamba, maeneo ya hifadhi ambayo tayari yanakaliwa na wananchi na yamepoteza sifa ya uhifadhi yaondolewe kwenye hifadhi na kurudishwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja mapendekezo hayo timu za wataalamu zilipokwenda uwandani kwa lengo la kujiridhisha zimebaini na kupendekeza kwamba, baadhi ya maeneo ambayo yanapendekezwa kupewa hawa wananchi ni ya muhimu sana kwa mustakabali mzima wa uhifadhi, hivyo wananchi wanapaswa kuondolewa kwa mustakabali wa uhifadhi endelevu wa Taifa na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Aidha, yapo maeneo ambayo yaliingizwa hifadhini, lakini hakuna athari iwapo yataondolewa hifadhini ili wapewe wananchi kwa ajili ya shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha yatafanyika kwa kumega eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 478 kutoka hifadhini na kuwapatia wananchi ili kupunguza migogoro ya mipaka baina ya hifadhi na vijiji vilivyopo katika Bonde la Usangu, pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Hatua hiyo, itapunguza eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kutoka kilometa za mraba 20,300 hadi kilometa za mraba 19,822.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, ulileta hoja hiyo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili iweze kufanyiwa kazi. Aidha, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 60(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Kamati ilikutana kuanzia tarehe 29 Mei, 2023 hadi tarehe 9 Juni, 2023 na kuifanyia kazi hoja hiyo muhimu. Vilevile tarehe 22 Juni, 2023 Kamati ilitembelea Wilaya ya Mbarali, Mkoani Mbeya ili kujionea eneo linalolalamikiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi ni kwamba, zoezi la kuwaondoa katika eneo hilo halikuwa la haki kwani limemuacha Mwekezaji wa Shamba la Kapunga kuendelea na shughuli za kilimo. Vilevile ziara hiyo ilikuwa na tija kwani imesaidia kuondoa mtanziko uliojitokeza baina ya Kamati na Wizara ya Maliasili na Utalii wakati wa kulifanyia kazi azimio hilo. Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati, nikianza na manufaa ya uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya uamuzi. Ili kuweka uhifadhi wenye tija kwenye hifadhi zetu ni lazima Serikali ihakikishe migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya ardhi ya vijiji na maeneo yaliyohifadhiwa inapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Aidha, ni muhimu kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na wananchi, ikiwa ni pamoja na wawakilishi wao ili kuwafanya wananchi wajione ni sehemu ya uhifadhi, hivyo wana wajibu wa kutunza na kulinda maeneo ya hifadhi nchini.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, kukubaliwa kwa hoja hii iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kutachangia kupatikana kwa manufaa mbalimbali ya kimazingira na kijamii na kiuchumi. Manuafaa hayo ni kama yalivyooneshwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha sio tu utapunguza au kuondoa migogoro ambayo imedumu kwa muda mrefu baina ya wananchi wa vijiji vinavyopakana na hifadhi, bali pia utaimarisha

jitihada za Serikali za kulinda maliasili zetu, kuboresha mahusiano baina ya Serikali na wananchi, wananchi na wawekezaji na wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kunusuru Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, hasa kwa kuzingatia kwamba, ni muhimu kwa ajili ya mtiririko endelevu wa maji ambao unategemewa kwenye uzalishaji wa nishati ya umeme wa maji katika vituo vya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati. Kwa kuzingatia kwamba, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ilianzishwa kwa maksudi ya kuhifadhi na kulinda bayoanuai, hususan wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki na mtiririko wa maji kwenye Mto Ruaha Mkuu ambao ni chanzo kikuu cha maji kwenye mabwawa ya kufua umeme. Kamati inaunga mkono juhudi za Serikali za kulinda hifadhi hii kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha una dhamira njema kwani eneo linalopunguzwa linarudi kwa wananchi na hivyo, kuwawezesha kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii, ili kukuza Pato la Taifa na wananchi kwa ujumla. Aidha, uamuzi huo utasaidia kuimarisha ulinzi na kujenga mazingira bora ya kuendeleza utalii katika hifadhi hii, kuboresha mahusiano baina ya wadau wa uhifadhi na baina ya wananchi na wawekezaji wanaopakana na maeneo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu kupitisha hoja hii, lakini kwa kuikumbusha Serikali kuhakikisha inatekeleza yafuatayo:-

1) Ili kuepusha uwezekano wa mpaka mpya wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kukabiliwa na mgogoro dhidi ya vijiji vinavyopakana na hifadgi hiyo, Serikali ihakikishe zoezi la kuhakiki na kuweka alama za mipaka linawashirikisha wananchi na wawakilishi wao.

2) Kwa kuwa, wananchi wa maeneo ya vijiji hivi na vitongoji vilivyoingizwa hifadhini wameridhia kuachia maeneo hayo kwa sharti kwamba, ni kulinda ikolojia na si vinginevyo, wanaomba mwekezaji aliyeko eneo la jirani naye aondolewe, ili kutenda haki kwa pande zote. Kamati inashauri wananchi waelimishwe sababu za eneo la mwekezaji kuachwa nje ya hifadhi, ili kuondoa dhana kwamba hawakutendewa haki katika zoezi la kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza, ili kulinda hifadhi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo kusiwe na jambo lolote litakalozuwia Serikali kuchukua hatua stahiki kwa manufaa ya Taifa hata kama kufanya hivyo kutakuwa na gharama kubwa.

3) Kwa kuwa, wananchi waliokuwa wanalima katika eneo la Mpunga Mmoja lililoko jirani na mwekezaji wa Kapunga wanaondolewa kwa mdai kwamba, eneo hilo linaathiri mtiririko wa maji kwenda hifadhini kwa sababu, halina miundombinu ya umwagiliaji ingawa eneo hilo lina sifa sawa na eneo la mwekezaji, Kamati inashauri Serikali imege sehemu ya eneo hilo na kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji na baadae kuwakabidhi wananchi ili waweze kuliendesha kwa mfumo wa ushirika. Hatua hiyo itasaidia wananchi kuendelea na shughuli za kilimo sambamba na kudhibiti watu wenye pesa ambao hupora maeneo kutoka kwa wananchi kwa gharama ndogo na kuyakodisha kwa gharama kubwa. Aidha, Serikali ihakikishe inatekeleza ushauri huu na kuleta marekebisho hayo kwenye Mkutano wa Bunge unaofuata kama ambavyo Serikali imekubaliana na Kamati.

4) Kwa kuwa, zoezi la kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha limegusa vijiji 34 ambavyo kati ya hivyo, vijiji vitano vimeondolewa kabisa hifadhini, vitongoji 14 vimetolewa nje ya hifadhi na vitongoji 25 vimemegwa na sehemu kuingizwa hifadhini na vitongoji 11 vimeingia vizima ndani ya hifadhi. Serikali ihakikishe wananchi walioathirika wanafanyiwa uthamini na kupewa fidia stahiki haraka iwezekanavyo ili wasiathirike. Jambo linaloweza kuibua chuki au malalamiko dhidi ya Serikali.

5) Wananchi na wawakilishi wao wamedai kutoshirikishwa kabisa au kushirikishwa kwa kiwangi kidogo katika mchakato wa kubadili mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha uliotokana na *GN* 28 ya mwaka 2008. Hali hiyo imecchangia kukuza migogoro na kuibua hisia kwamba, Serikali inawabagua wananchi na kupendelea wawekezaji waliopo kwenye maeneo ya jirani na hifadhi hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha na kuwashirikisha kikamilifu wananchi na wawakilishi wao katika mchakato wa kurekebisha mpaka wa hifadhi ya Taifa ya Ruaha, ili kuondoa hisia potofu kwamba, wananchi wanaonewa na wawekezaji wanapendelewa.

Aidha, Serikali itumie taratibu stahiki na zenye staha wakati wa kuwaondoa wananchi waliovamia maeneo ya hifadhi, ili kuepusha uhasama baina ya wananchi na Serikali na wananchi na mamlaka za uhifadhi. Vilevile mbali na kuweka vigingi kuwa alama za mpaka ni vyema Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa barabara kuzunguka maeneo ya uhifadhi nchini, hasa yenye migogoro ili zitumike kama alama za mipaka.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha kushughulikia Azimio hili. Kwa umuhimu wake natamani niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja majina yao, hata hivyo kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao ninaomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati natumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Mary Masanja, watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbas kwa ushirikiano wao kwa Kamati

ambao umechangia kuwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika kuratibu usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono Azimio na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MAPENDEKEZO YA KUREKEBISHA MPAKA WA HIFADHI YA TAIFA YA RUAHA – KAMA LILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(3) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(8)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunce, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako TUkUfU, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kUhUSU Azimio la Bunge laKuridhia Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

**2.0 CHIMBUKO LA AZIMIO**

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Januari, 2023 Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuwa akihutubia wananchi kwenye mkutano wa hadhara eneo la Kapunga, Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya, alitoa maamuzi ya Serikali ya kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa Ruaha kwa kuzingatia mapendekezo yaliyowasilishwa na Kamati ya Mawaziri Nane (8) wa kisekta. Kamati ya Mawaziri 8 wa Wizara za kisekta zinazoathiriwa na uwepo wa migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi, iliundwa tarehe 15 Januari, 2019 na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt John Pombe Joseph Magufuli, ili kuandaa mapendekezo ya ufumbuzi wa kudumu wa migogoro hiyo.

Mapendekezo ya Kamati hiyo mbali na mambo mengine yanalenga kuhakikisha kuna uzingatiaji wa Sera ya Wanyamapori ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo yaliyohifadhiwa na kulinda bioanuai katika mtandao wa Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu.

Sehemu ya mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri 8 ambayo yaliridhiwa na Mheshimiwa Rais ni kwamba, maeneo ya hifadhi ambayo tayari yanakaliwa na wananchi na yamepofeza sifa ya uhifadhi yaondolewe kwenye hifadhi na kurudishwa kwa wananchi. Hata hivyo, pamoja na mapendekezo hayo, timu za wataalamu zilipokwenda uwandani "site" kwa lengo la kujiridhisha zilibaini na kupendekeza kwamba, baadhi ya maeneo ambayo yamependekezwa wapewe wananchi ni ya muhimu sana kwa mustakabali mzima wa uhifadhi, hivyo wananchi wanapaswa kuondolewa kwa mustakabali wa uhifadhi endelevu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Aidha, yapo maeneo ambayo yaliingizwa hifadhini, lakini hakuna athari iwapo yataondolewa hifadhini ili wapewe wananchi kwa ajili ya shughuli za kijamii. Marekebisho ya mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha yatafanyika kwa kumega eneo lenye UkUbwa wa kilomita za mraba 478 kutoka hifadhini na kuwapatia wananchi ili kupunguza migogoro ya mipaka baina ya hifadhi na vijiji vilivyopo katika bonde la Usangu pembezoni mwa hifadhi ya taifa ya Ruaha. Hatua hiyo itapunguza eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kutoka kilomita za mraba 20,300 hadi kilomifa za mraba 19,822.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako TUkUfU kwamba ulileta hoja hiyo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 60(3) ya Kanuni za Bunge ili iweze kulifanyia kazi. Aidha, ili kuzingafia masharti ya Kanuni ya 60(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilikutana kuanzia tarehe 29 Mei, 2023 hadi tarehe 09 Juni, 2023 na kuifanyia kazi hoja hii muhimu. Vilevile, tarehe 22 Juni, 2023 Kamati ilitembelea Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya ili kujionea eneo linalolalamikiwa na wananchi. Malalamiko ya Wananchi ni kwamba, zoezi la kuwaondoa katika eneo hilo halikuwa la haki kwani limemwacha mwekezaji wa shamba la

Kapunga kuendelea na shughuli za kilimo. Vilevile, ziara hiyo ilikuwa na tija kwani imesaidia kuondoa mtanziko uliojitokeza baina ya Kamati na Wizara ya Maliasili na Utalii wakati wa kulifanyia kazi azimio hili.

Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako TUkUfU maoni na ushauri wa Kamafi nikianza na manufaa ya uamuzi.

**3.0 MANUFAA**

Mheshimiwa Spika, ili kuwe na uhifadhi wenye tija kwa hifadhi zetu, ni lazima Serikali ihakikishe migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya ardhi za vijiji na maeneo yaliyohifadhiwa inapatiwa UfumbUZi wa kUdumu. Aidha, ni muhimu kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na wananchi, ikiwa ni pamoja na wawakilishi wao ili kuwafanya wananchi wajione ni sehemu ya uhifadhi hivyo wana wajibu wa kutunza na kulinda maeneo ya hifadhi nchini. Ni wazi kwamba, kukubaliwa kwa hoja hii iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako TUkUfU kutachangia kupatikana kwa manufaa mbalimbali ya kimazingira, kijamii na kiuchumi kama ifuatavyo:-

i. Kuhifadhi vyanzo vya maji vya Kaskazini Magharibi mwa Bonde la Usangu, ambavyo vinaanzia kwenye gema la milima ya Chunya/Mbeya. Vyanzo hivyo ni muhimu sana kwani vinaboresha mitiririko ya maji kutoka milima ya Kipengere na Uporoto na hivyo kuhakikisha maji ya kutosha yanafika kwenye maeneo oevu ya Bonde la Usangu;

ii. Kusaidia kulinda mifumo ya ikolojia katika Bonde la Usangu ili kurejesha uofo wa asili kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika Mfo Ruaha Mkuu ambao unategemewa katika uzalishaji wa Umeme wa Maji katika vituo vya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere;

iii. Kusaidia kuimarisha uhifadhi wa maliasili, hususani wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji;

iv. Kusaidia kupunguza au kuondoa migogoro ya mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa Ruaha na vijiji vilivyopo kwenye Bonde la Usangu ambavyo vinapakana na Hifadhi ya Taifa Ruaha;

v. Kuongeza pato la Taifa kwa msingi kwamba kurekebishwa kwa mpaka wa Hifadhi ya Taifa Ruaha kutaendeleza hifadhi hiyo kuwa Kivutio cha Utalii; na

vi. Kuwezesha upatikanaji wa maeneo pamoja na maji ya uhakika kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na UVUVi kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Rucha siyo tu utapunguza au kuondoa migogoro ambayo imedumu kwa muda mrefu baina ya Wanachi wa vijiji vinavyopakana na Hifadhi, bali pia utaimarisha jitihada za Serikali za kulinda Maliasili zetu, kuboresha mahusiano baina ya Serikali na wananchi, wananchi na wawekezaji, na wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa. Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kunusuru Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, hasa kwa kuzingatia kwamba, ni muhimu kwa ajili ya mtiririko endelevu wa maji ambao unategemewa kwenye uzalishaji wa nishati ya umeme wa maji katika vituo vya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere.

**4.0 MAONI YA KAMATI**

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ilianzishwa kwa makusudi ya kuhifadhi na kulinda bioanuai hususan wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki na mtiririko wa maji kwenye mto Rucha MkUU ambao ni chanzo kikuu cha maji kwenye mabwawa ya kufua umeme, Kamati inaunga mkono juhudi za Serikali za kulinda hifadhi hii kwa maslahi mapana ya taifa. Uamuzi wa Serikali kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa Ruaha una dhamira njema kwani eneo linalopunguzwa linarudi kwa wananchi, na hivyo kuwawezesha kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii ili kukuza pato lao na taifa kwa ujumla. Aidha, uamuzi huo ufasaidia kuimarisha ulinzi na kujenga mazingira bora ya kuendeleza utalii katika hifadhii hii, kuboresha mahusiano baina ya wadau wa uhifadhi na baina ya wananchi na wawekezaji wanaopakana na maeneo ya uhifadhi.

Kamati inalishawishi Bunge lako tUkUfU kupitisha hoja hii, lakini kwa kuikumbusha Serikali kuhakikisha inatekeleza yafuafayo:-

(i) Kuepusha uwezekano wa mpaka mpya wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kukabiliwa na migogoro dhidi ya Vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo, Serikali ihakikishe zoezi la kuhakiki na kuweka alama (vigingi) za mpakalinawashirikisha wananchi na wawakilishi wao;

(ii) Kwa kuwa Wananchi wa maeneo ya vijiji na vitongoji yaliyoingizwa hifadhini wameridhia kuachia maeneo hayo kwa sharti kwamba ni kulinda ekolojia na si vinginevyo, wanaomba muwekezaji aliyeko eneo la jirani naye aondolewe ili kutenda haki kwa pande zote. Kamati inashauri wananchi waelimishwe sababu za eneo la muwekezaji kuachwa nje ya hifadhi, ili kuondoa dhana kwamba hawakufendewa haki katika zoezi la kurekebisha mpaka wa hifadhi ya Taifa ya Rucha. Aidha, Kamati inaendelea kusisifiza ili kulinda hifadhi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo, kusiwe na jambo lolote litakalozuia Serikali kuchukua hatua stahiki kwa manufaa ya taifa, hata kama kufanya hivyo kutakuwa na gharama kubwa.

(iii) Kwa kuwa, wananchi waliokuwa wanalima katika eneo la Mpunga Mmoja lililoko jirani na mwekezaji wa Kapunga, waliondolewa kwa madai kwamba eneo hilo linaathiri mtiririko wa maji kwenda hifadhini kwa sababu halina miundombinu ya umwagiliaji, ingawa eneo hilo lina sifa sawa na eneo la muwekezaji, Kamati inashauri Serikali imege sehemu ya eneo hilo na kutengenezea miundombinu ya umwagiliaji na baadaye kuwakabidhi wananchi ili waweze kuliendesha kwa mfumo wa ushirika. Hatua hiyo itasaidia wananchi kuendelea na shughuli za kilimo, sambamba na kudhibiti wału wenye pesa ambao hupora maeneo kutoka kwa wananchi kwa gharama ndogo, na kuyakodisha kwa gharama kubwa. Aidha, Serikali ihakikishe inaŕekeleza ushauri huu na kuleta marekebisho hayo kwenye mkutano wa Bunge unaofuata.

(iv) Kwa kuwa zoezi la kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha limegusa vijiji 34 ambapo kati ya hivyo vijiji vitano (5)

vimeondolewa kabisa hifadhini, vitongoji 1 4 vimetolewa nje ya hifadhi, vitongoji 25 vimemegwa na sehemu kuingizwa hifadhini na vitongoji 11 vimeingia vizima ndani ya hifadhi. Serikali ihakikishe wananchi walioathirika wanafanyiwa uthamini na kupewa fidia stahiki haraka iwezekanavyo ili wasiathirike, jambo linaloweza kuibua chuki au malałamiko dhidi ya Serikali.

(v) Wananchi na wawakilishi wao wamedai kutoshirikishwa kabisa au kushirikishwa kwa kiwango kidogo katika mchakato wa kubadili mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha uliotokana na GN. 28 ya mwaka 2008. Hali hiyo, imechangia kukuza migogoro na kuibua hisia kwamba, Serikali inawabagua wananchi na kupendelea wawekezaji waliopo maeneo ya jirani na hifadhi. Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha na kuwashirikisha kikamilifu wananchi na wawakilishi wao katika mchakato wa kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, ili kuondoa hisia potofu kwamba wananchi wanaonewa na wawekezaji wanapendelewa.

Aidha, Serikali itumie taratibu stahiki na zenye staha wakati wa kuwaondoa wananchi waliovamia maeneo ya hifadhi ili kuepusha uhasama baina ya wananchi na Serikali, na wananchi na mamlaka za uhifadhi. Vilevile, mbali na kuweka vigingi kuwa alama za mipaka, ni vyema Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa barabara (maza) kuzunguka maeneo ya uhifadhi nchini hasa yenye migogoro ili zitumike kama mipaka.

## 5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunce, kwa namna mnavyotimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha kushughulikia azimio hili. Kwa umuhimu wake, natamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii

yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mwenyekiti
Mhe. Najma Muntazar Giga, Mb - M/Mwenyekiti
Mhe. Shaabani Omar Shekilindi, Mb
Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb
Mhe. Innocent Seba Bilakwate, Mb
Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb
Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb
Mhe. Neema William Mgaya, Mb
Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb
Mhe. Nancy Hassan Nyarusi, Mb
Mhe. Festo Richard Sanga, Mb
Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb
Mhe. Munira Mustafa Khatib, Mb
Mhe. Dkt. Florence G. Samizi, Mb

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati natumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Mary Masanja (Mb) naWatendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbasi kwa ushirikiano wao kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi (ndc) kwa kuongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono azimio, naomba kuwasilisha.

**Timotheo Paul Mnzava, Mb**
MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII
27 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ameshawasilisha maazimio yote mawili, lakini pia Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii wameshatoa Maoni ya Kamati juu ya Maazimio yote haya mawili. Sasa kwa utaratibu wetu tutaanza na uchangiaji, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia, halafu baadae tutahitimisha na maamuzi ambayo tutakuwa tumeyafanya kupitia Maazimio.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Neema William Mgaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuunga mkono mapendekezo ya maazimio haya yote mawili, Azimio la kwanza la Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Ruaha na Azimio la Kushusha Hadhi Hifadhi ya Kigosi kwenda kuwa Hifadhi ya Misitu ya Kigosi.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nia njema na ya dhati ya kutaka kutatua migogoro mbalimbali kati ya hifadhi na wananchi. Tukianza na mgogoro wa Mbarali, mgogoro wa Mbarali ni mgogoro mrefu wa tangu mwaka 2008 ilipowekwa *GN* ya 28.

Mheshimiwa Spika, tukianza na mgogoro wa Mbarali, mgogoro wa Mbarali ni mgogoro mrefu wa tangu mwaka 2008 ilipowekwa *GN* ya 28. Mheshimiwa Rais alituma Mawaziri nane kwenda kutatua mgogoro huu, vilevile viongozi wakubwa wa Serikali, akiwemo Waziri Mkuu, walikwenda pia Mbarali katika kutatua tatizo hili la mgogoro wa Mbarali. vilevile Mheshimiwa Rais

hajaishia hapo, aliamua kutoa hekta 74,432.12 na kuwapa wananchi ili waweze kuendelea na shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mama yetu ana nia njema, ana nia ya dhati, tumuunge mkono. Ametoa pesa nyingi, vigingi vimewekwa, mipaka imewekwa ili kuzuia uvamizi na kuweza kudhibiti migogoro isiweze kuendelea tena.

Mheshimiwa Spika, kwa nia hii njema, ya dhati, ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameionesha, naiomba Serikali sasa tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza haya yafuatayo; ombi la kwanza, Serikali itayarishe mipango na utaratibu wa uwekezaji ambao unaonesha tarehe na lini zoezi litakwenda kuisha sambamba na kukamilisha zoezi hili la wakati.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la pili kwa Serikali; tathmini ifanyike haraka, walipwe fidia wale wote ambao wamekutwa kwenye mpaka huo wa Hifadhi ya Ruaha ili kuweza kupisha na waweze kuondoka. Fidia zao zilipwe kwa wakati. maana yake matatizo huwa yanakuja kuanza hapa kwenye kuchelewesha fidia, mmalize ili mambo yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuridhia kushusha hadhi Hifadhi ya Kigosi na kuweza kuruhusu Hifadhi hii ya Kigosi kuwa Hifadhi ya Misitu ya Kigosi. Kwenye Kamati mara nyingi tumekuwa tukilalamika kwamba *TANAPA* ina mzigo mkubwa wa kuendesha hifadhi hizi.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* ina takribani hifadhi 22. Tangu ilivyokuwa na hifadhi 16, bado *TANAPA* walikuwa na bajeti ya bilioni 104, hifadhi zikaongezeka kuwa 22, *TANAPA* wakawa wanapewa bilioni 111. Hitaji halisi la pesa ili *TANAPA* waweze kuendesha hifadhi hizi ni takribani bilioni 222.

Mheshimiwa Spika, kwa uhaba wa pesa ambazo wanapewa *TANAPA* kuendesha hifadhi hizi, naona suala hili ni muhimu, linaendelea kushusha gharama za uendeshaji wa hifadhi za *TANAPA*. Ukizingatia kwamba Hifadhi hii ya Kigosi mwaka huu

wamekwenda watalii 10 tu, kwa hiyo, mapato ni madogo na uendeshaji *TANAPA* inalemewa mzigo.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze Rais kwa kuona umuhimu wa kushusha Hifadhi hii ya Kigosi kwa sababu hifadhi hii inakwenda kuwa Hifadhi ya Misitu ya Kigosi, itaruhusu wananchi kuweza kufanya shughuli za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kurina asali, uvuvi na kufanya shughuli zao za matambiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuruhusu uzalishaji wa asali kuendelea itatusaidia vile viwanda vyetu tulivyovianzisha vya asali kupata malighafi ya asali kwa wingi. Kwa hiyo, malighafi hii itakwenda kulisha viwanda vyetu vya asali na yale mazao ya asali tutaweza kuyauza nje ya nchi na Serikali itapata pesa za kigeni, na inasemekana kwamba tutakwenda kupata takribani dola milioni 50 kwa kuruhusu shughuli hizi za uzalishaji wa asali ndani ya Hifadhi hiyo ya Misitu ya Kigosi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, nimpongeze Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kutatua migogoro, sambamba na kuona matumizi sahihi ya Hifadhi hii ya Misitu ya Kigosi ambayo itakwenda kuleta manufaa zaidi kuliko ikiendelea kuwa hifadhi, tunapata watalii wachache, na pesa tunapata kidogo na *TANAPA* inapata mzigo mkubwa wa kuhudumia hifadhi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea haya machache, naunga mkono hoja ya mapendekezo haya yote mawili. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Niendelee kukushukuru sana wewe kwa kazi nzuri ambazo unatuongoza. Leo ni takribani miezi minne ukiendelea kuongoza mhimili huu mkubwa, kazi inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya, namna anavyoshughulikia migogoro ya hifadhi zetu. Kashughulikia mgogoro wa Ngorongoro, wananchi wamesafirishwa kwa uhakika kabisa na sasa hivi wanafurahia maisha mapya bila kelele yoyote, na Mheshimiwa Rais anashughulikia migogoro ya nchi kwa uhakika kabisa. Tuendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli unastahili maua yako, pamoja na Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wizara yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Makamishna wa Uhifadhi wa *TANAPA* na *TFS;* kazi nzuri wanaendelea kufanya. Wanatambua nafasi ya kazi ambayo mmewapa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hili suala wananchi walikuwa wamelisubiri kwa kasi kubwa sana, na hatimaye limeweza kufika. Nikupongeze Mheshimiwa Mary Masanja, ulifika kwa wananchi wa Ushetu, uliongea nao, uliwasikiliza na uliwaahidi. Na leo wanaona matunda mazuri ya Mheshimiwa Rais; ni kazi nzuri ambayo imefanyika.

Mheshimiwa Spika, niendelee kukuomba tu Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wetu, kwa sababu sasa tunakwenda kulirudisha pori hili kwenye uhifadhi wa wananchi wetu, kutoka Hifadhi ya Taifa ya Kigosi sasa inakwenda kuwa Hifadhi ya Kigosi; nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, tuna wananchi wetu wafugaji, wanaorina asali, wavuvi pamoja na wachimbaji, sasa wanakwenda kufaidika na rasilimali hizi.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo moja naomba tulifanyie kazi; tuwasajili wafugaji na warina asali, tuweze kuwatambua; wachimbaji wadogo tuweze kuwatambua. Lakini pia na wenzetu ambao wanaingia pale kuvua samaki na wenyewe waweze kutambulika ili tujue kazi hii sasa wanapoingia kwenye kurina asali tuweze kujua, ili tunapojua sasa kwamba idadi yao ni wangapi, inatusaidia sana namna ya usimamizi mzuri kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kafanya kazi kubwa sana. Ukiangalia leo katika Jimbo la Ushetu peke yake, Kata zinazokwenda kufaidika na eneo hili, kuna Kata kubwa sana ya Ulowa, inakwenda kufaidika; Kata za Ubagwe, Ulewe, Idahina, Nyankende na Bulungwa. Wote hawa wanazungukwa na pori hili ambalo sasa wanakwenda kufaidika wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna Wilaya zetu za Bukombe, Kaliua, Mbogwe kwa ndugu yangu, Waziri, Mheshimiwa Doto Biteko. Wananchi hawa wote wanazunguka pori hili. Ni kazi nzuri, kubwa sana Mheshimiwa Rais ameifanya. Mheshimiwa Rais ni msikivu, pamoja na kwamba ametuma Mawaziri wote wamezunguka maeneo haya, lakini anaporudishiwa ripoti anaifanyia kazi hapohapo na kutoa matokeo. Sasa haya ni matokeo ya Mheshimiwa Rais jinsi anavyosimamia rasilimali za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kukupongeza sana wewe, lakini niipongeze sana Serikali, niwapongeze sana Kamati, Kamati imefanya kazi kubwa sana; hongereni sana Kamati. Kazi iliyofanyika ni kubwa, imeishauri Serikali kwa uhakika bila upendeleo, na leo wananchi wetu migogoro inakwenda kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kuiomba Wizara, endeleeni pia kushughulikia na migogoro ya maeneo mengine, endeleeni pia kushughulikia na mipaka ya maeneo mengine. Ili Mheshimiwa Rais anapoelekea 2025 tuendelee kumpa maua yake, aendelee kubeba kura zake, tuendelee kumtendea haki. Kazi anayoifanya leo Mheshimiwa Rais ni matokeo atakuja kuyapata maua yake 2025, ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo niendelee kupongeza kazi nzuri imefanyika, wananchi wa Ushetu sasa wanakwenda kufurahi, kufaidika. Kama Mbunge naahidi kuongeza nguvu kuhakikisha tunaendelea kuwapa elimu ili waendelee kui-*support* Serikali katika tukio hili.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze tena; naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo amejionesha kwa vitendo kwamba anapenda amani kwa sababu anakwenda kutatua migogoro. Na naunga mkono maazimio yote mawili kwa sababu yana faida kubwa na tija kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote yenye migogoro haitawaliki, kwa hiyo Mheshimiwa Rais anataka kuondoa migogoro. Nitaanza na mgogoro wa Mbarali; mgogoro huu umekuwepo tangu 2008 pale ilipowekwa *GN* 28. Baada ya *GN* 28 kuwekwa wananchi hawakuridhika kwa sababu kuna maeneo ya uzalishaji ambayo yalikwenda kwao.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya au nzuri kuna eneo la mwekezaji ambalo lenyewe lilibaki, eneo la Kapunga. Kwa hiyo, hili eneo lilisababisha wananchi waone kama wao hawakutendewa haki. Kiukweli eneo hili lilibaki kwa sababu lina miundombinu mazuri ya maji, kwa hiyo, maji hayapotei.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati tumekwenda pale tumejionea na tumeridhika na yale maamuzi. Lakini ili kuondoa mgogoro wa Mbarali, Kamati tunashauri lile eneo ambalo liko sambamba na mwekezaji ambalo ni Mpunga Mmoja ambapo maeneo yote haya mawili awali yalikuwa ya wananchi, wananchi waliyatoa yale maeneo bure kwa ajili ya mwekezaji, basi nalo liwekewe miundombinu ambayo itasababisha maji yasipotee, na eneo hili wananchi walitumie kwa kilimo. Hili likifanyika wananchi wa Mbarali wameelewa kabisa na wanaunga mkono jitihada za

Mheshimiwa Rais kwa sababu wanaona kabisa uharibifu unaotokea.

Mheshimiwa Spika, tumejionea jinsi gani uharibifu unatokea katika hili Bonde la Ihefu. Hili beseni ambalo tunasema ni la maji, maji hakuna, yamekauka, maji yapo kidogo sana. Kwa hiyo, hii inakwenda kuathiri uzalishaji wa umeme Kidatu na Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatua hizi ambazo Serikali imechukua ni mahususi, tunaunga mkono asilimia 100 kwa sababu miradi hii imetumia pesa nyingi, Rais Dkt. Samia ameweka pesa nyingi kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bila kufanya hivi basi bwawa hili halitazalisha.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mbarali wanatambua kwamba wanahitaji umeme. Tunachotakiwa kufanya tusimamie yale tuliyoyaamua sasa. Tunayasimamia vipi, basi hivi vigingi viwekwe mahali pote ili mipaka iimarishwe. Kwa sababu bila mipaka kuimarishwa siku ya siku wananchi watarudi.

Mheshimiwa Spika, tumeona mpaka ng'ombe wameanza kwenda kule. Kwa hiyo, hii mipaka isipoimarishwa uharibifu utaendelea kufanyika katika Bonde hili la Ihefu. Kwa hiyo, miradi yetu ya umeme itaharibika. Tutaharibu mazingira yote, maji hayatapatikana ambayo yanatiririka kwa ajili ya kwenda kwenye Mto Ruaha.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali pia iweke mkuza kuzunguka yale maeneo muhimu, na siyo huko tu, nchi nzima, ili haya maeneo yetu tuweze kuyadhibiti kwa sababu tunavyokuwa tumelegalega ndiyo wananchi wanaingia, kuwatoa tunawatoa kwa gharama kubwa sana. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba tumejikinga kabla ya hatari ili wananchi wasiweze kuingia.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji ni kitu ambacho wananchi wametuambia, wanaomba kushirikishwa. Washirikishwe kuanzia awali, waelimishwe ili wasione kama Serikali inawaonea, ili wasione kama Serikali inapendelea wawekezaji, ili wasione

kwamba Serikali inawanyanyasa; waelimishwe na wapate elimu ya kutosha wao na wawakilishi wao.

Mheshimiwa Spika, sisi tulipata bahati ya kukutana na Madiwani na hili waliliongelea, kwamba sisi ni Madiwani, tukielewa tutawafahamisha wananchi wetu. Kwa hiyo, wawakilishi na wananchi wafahamishwe ili wananchi wetu waweze kuelewa.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumesikia, kuna vijiji vitano vitaondoka kabisa. Hawa watu wapewe fidia kwa wakati kwa sababu sasa baada ya kuambiwa kwamba wao wanaingia kwenye hifadhi hawawezi kuendelea kufanya chochote, hawawezi kuendelea kulima wala kuendeleza maisha yao. Kwa hiyo, watakuwa wamesimama, kama ikichukua muda mrefu basi wananchi hawa wataingia hasira na Serikali na kusababisha migogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa juhudi hizi alizozifanya Mheshimiwa Rais, na hayo niliyoyasema yakizingatiwa, basi tuna uhakika kwamba bonde letu litaendelea kuwa salama, umeme utapatikana na migogoro itaisha.

Mheshimiwa Spika, niongelee Kigosi, Kigosi pia tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anajali wananchi wake. Haya matatizo ya wafugaji nyuki kukosa mahali pa kuweka mizinga yapo katika mapori mengi, ikiwemo Kigosi, hata Moyowosi kule ambako ni hifadhi ya wanyamapori, hii shida ipo.

Mheshimiwa Spika, ikishakuwa hifadhi, wananchi wetu ambao walikuwa wanafuga nyuki hapo awali kwenye hiyo misitu wanakosa pa kuweka mizinga. Kwa hiyo, kwa hatua hii ya Mheshimiwa Rais kuruhusu kwamba hii ishushwe hadhi ina maana wananchi wanaruhusiwa kufanya shughuli zao. Watafanya shughuli hizo za ufugaji nyuki, watafanya shughuli za uvuvi na za matambiko.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa Serikali kufanya uratibu mzuri kwa sababu bado ni hifadhi ya misitu, bado tunahitaji

kulinda misitu yetu, haimaanishi misitu ikatwe sasa, hapana, ametoka *TAWA* lakini sasa *TFS* anachukua *charge*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Serikali iweke uratibu mzuri na hasa wa zile tozo. Tozo zieleweke; anayekwenda na baiskeli anakwendaje, na pikipiki anakwendaje, kwa sababu hizi tozo pia ni moja ya sehemu ambazo zinapigiwa kelele.

Mheshimiwa Spika, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais, anawajali wananchi wake ndiyo maana anaachia maeneo, maeneo yote anayoachia anasema wapelekewe wananchi kwa sababu anataka waweze kuendelea na uzalishaji. Amerudisha maeneo hifadhi hii iwe na misitu ili viwanda viweze kufanya kazi ili sasa wananchi waweze kuweka mizinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema sisi sasa hivi ondoa shoka uweke mzinga. Kwa hiyo tunaamini miti yetu sasa badala ya kukatwa, mtu hawezi kukata kwa sababu yeye mwenyewe anataka kuweka mzinga, kwa hiyo, kwa kuwashirikisha wananchi wao wenyewe watakuwa ni wahifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa haya machache, naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa ushirikiano mkubwa aliotupa; Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima. Wao ndio wamesababisha tuweze kuratibu jambo hili na tuweze kufika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika maazimio haya mawili, Azimio la Kigosi pamoja na lile la Ruaha.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kumpongeza kwa moyo wa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hakika sisi Wanakamati tunaona sasa namna gani sekta ya maliasili na utalii inakwenda kuwa na tija katika Taifa letu, na hasa kwa kuendelea kutatua migogoro ambayo imekuwa ikiikabili sekta yetu ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuchangia kwa eneo la Ruaha kwa maana ya kule Mbarali. Niendelee kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa ekari zaidi ya 74,000 na kuweza kuwagawia wananchi. Mheshimiwa Rais ana nia njema na Watanzania na ndiyo maana ameweza kutoa sehemu hii ya eneo hili ili wananchi hawa waweze kwenda kujiendeleza kimapato kwa maana ya kuyatumia sasa maeneo haya kwa uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutumie nafasi hii kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuungana na Kamati na kwenda Mbarali na kuona tatizo na changamoto ambayo imeweza kuwakuta wananchi, kero ambayo ilikuwa Kapunga I kupitia Kapunga II ambayo amepewa mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuipongeza Serikali kwa kuwa sikivu kwa kuona sasa ni busara kutoa baadhi ya maeneo na kuikabidhi Serikali ili wananchi waweze kupatiwa na kuendelea kutatua mgogoro kati yao na zile hisia walizokuwa nazo kuhusu kupendelewa kwa mwekezaji. Kwa hiyo, niipongeze Serikali kwa kuitoa hiyo sintofahamu kwa wananchi kuhusu kupendelewa kwa mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa tuiombe Serikali, wananchi wanakuwa na mgogoro na mwekezaji kwa sababu eneo lake lina manufaa, lina miundombinu ya kutosha ambayo inaweza kumzalishia na kumpatia kipato. Tuombe sasa na upande huu wa wananchi ambapo ni eneo la Kapunga I liweze kuwekewa miundombinu, na hii Wizara ya Kilimo pia ishirikishwe ili wananchi

wale lile eneo ambalo wamepatiwa liweze kuwa na tija ya uzalishaji na kuondoa migogoro ambayo imeweza kuonekana kati yao na mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, eneo lile likiwekewa miundombinu litaendelea kuwapunguzia wananchi gharama kwa sababu hata kwa sasa kule kwa mwekezaji wanakodisha lakini wanakodisha kwa gharama kubwa sana. Wakipewa eneo lao hili wataweza kupata ghrama nafuu na kuweza kunufaika nalo.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kutoa rai kwa timu ya Mawaziri nane. Tumeona mfano leo Azimio hili limeweza kuingia huku Bungeni na linakwenda kupita kwa sababu ni azimio ambalo lina tija kwa Watanzania. Ile timu ya Mawaziri nane ina kazi sasa ya kuleta kile ambacho wamekwenda kukifanya kwa sababu ni maeneo makubwa na mengi wameweza kwenda kuyafanyia kazi, Serikali imegharamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa waje watuambie ni maeneo yapi ambayo tayari migogoro imekwisha ili wananchi kuendelea kuondoa sintofahamu na wabaki wakiendelea kuifurahia Serikali yao kama ambavyo wanaifurahia sasa huko Mbarali pamoja na Kigosi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, niende sasa kwenye eneo lingine la Kigosi. Tunaipongeza sana Serikali na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa zaidi ya shilingi bilioni 2.5 kuwekeza miundombinu ya kisasa kwa ajili ya viwanda vya kuchakata asali.

Mheshimiwa Spika, hii italeta tija sana kwa wananchi na hasa wananchi wa maeneo ya Mlele, Kibondo, Nzega, Sikonge, Bukombe. Nitoe rai kwa wananchi hao, Mheshimiwa Rais ana nia njema, eneo hili limeenda kutolewa kwa wananchi, basi tuombe Serikali kupitia *TFS* ambayo ndio inaenda kuwa msimamizi kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapewa nafasi ya kuingia na wasipewe vikwazo, tusianze habari ya vibali vingi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wafuate utaratibu na Wizara watumie nafasi hii sasa kutoa elimu kwa wananchi, nini ambacho wanatakiwa kufuata na taratibu zipi za Kiserikali zinatakiwa kufutwa ili wananchi hawa sasa waende kunufaika kama ambavyo walikuwa wakinufaika mwanzo kwa kufanya matambiko, lakini pia kuweka mizinga yao. Pia bila kusahau wahakikishe kwamba wanaenda kuhakikisha vijana wanakwenda kupewa elimu ili na wao, hili eneo ambalo limetolewa na Mheshimiwa Rais liweze kuwa na tija ya kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza Wizara kwa kuendelea kutafuta masoko China pamoja na Marekani. Bado malighafi, nyingi zitahitajika hapa kwa hiyo ni jukumu la Wizara sasa kwenda kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili maeneo haya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa yaweze kwenda kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza sana Wizara kwa kuendelea kutatua changamoto na huu ni mfano mzuri, sisi kama Kamati tutaendelea kuwaunga mkono katika kuhakikisha kwamba tunalinda rasilimali zetu, tunazitunza, tunazihifadhi lakini pia tunatoa fursa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja kwa maazimio yote mawili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia Maazimio mawili yaliyoletwa hapa na Kamati yangu. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai mpaka sasa tumekaa hapa miezi mitatu tupo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia suala la Azimio la Bunge la kuridhia kufutwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi na kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi. Napenda

nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa na Naibu wake, Mheshimiwa Masanja lakini na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya mpaka tumefikia leo hapa tupo kwenye majadiliano ya Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kufutwa Hifadhi ya Kigosi na kuanzisha Hifadhi ya Msitu wa Kigosi. Ninazo sababu za kumpongeza, kwa sababu inapokuwa hifadhi wananchi hawaruhusiwi kuingia ndani ya hifadhi, lakini inapokuwa hifadhi ya misitu wananchi wa eneo hilo wataweza kupata fursa za kuingia kwenye hifadhi na wataweza kwenda kufanya shughuli zao za kijamii kama kutundika mizinga, kuvua samaki lakini pia na kufanya mambo yao ya asili kama matambiko.

Mheshimiwa Spika, eneo hili ni kubwa ni kilometa za mraba takribani elfu saba mia nne na kitu. Ni eneo kubwa ambalo wananchi wanaozunguka maeneo hayo watafaidika nalo. Pia eneo hili linakwenda kuifungua nchi kiuchumi kwa sababu tunaweza kupata wawekezaji wakawekeza hata kwenye mambo ya hewa ya ukaa. Mbali na hapo kutakuwa na viwanda, viko kule viwanda vitano ambavyo vinachakata mazao ya asali kama nta, lakini asali pia inapouzwa nje ya nchi inaleta pesa za kigeni na wananchi wanapata manufaa kutokana na mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita na nalipongeza azimio hili na naunga mkono kuwepo kwa azimio hili na naomba Wabunge wenzangu waliunge mkono kwa faida ya wananchi na faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kupongeza Azimio la Ruaha kwa sababu linakwenda kutatua matatizo yaliyopo pale Ruaha, lakini pia ni faida kwa wananchi kwa sababu maji yanayotokana hapo yanakwenda kujaza Ziwa la Kidatu na pia yanakwenda mpaka Ziwa la Mwalimu Nyerere ambako Serikali imewekeza mradi mkubwa kwa ajili ya kufua umeme.

Mheshimiwa Spika, eneo hili ni eneo ambalo maji yanayokwenda kwenye Ziwa la Mwalimu Nyerere yanatokea sehemu hiyo. Hivyo basi, kupitishwa kwa azimio hilo kutasababisha yale maji yaweze kuwepo kwa wingi na kwenda kwenye Ziwa hili ambalo litatengeneza umeme mwingi ambao tutaweza pia kuuza hata kwenye nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, kwenye Azimio hili la Ruaha, niombe sana wale watendaji ambao watakuwa wanakwenda kutekeleza ile mipaka wawe marafiki na wananchi wa maeneo hayo. Vilevile niombe Wizara ya Maliasili na utalii, sisi kama Kamati tulikuwa tumeomba sehemu ya eneo ambalo liko karibu na yule mwekezaji mkubwa Kapinga *One,* wananchi wapewe hilo eneo ili na wao waweze kuendeleza shughuli zao za kilimo kwa sababu hili eneo limeleta mgogoro maana yake wapo wananchi wanaolalamika kwamba kwa nini yule mwekezaji ameachwa pale. Tuliomba na yeye eneo lake la juu, tulikubaliana kwamba waweze kwenda kupima lile eneo la Kapinga *one* wananchi waweze kugawiwa ili nao waweze kufanya shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Spika, viko vitongoji ambavyo vimechukuliwa vitakuwa ndani ya hifadhi kwa maana kwamba vile vijiji vitano vinaenda kufa kama vijiji. Ombi langu kwa Wizara ni hili, wale wananchi walioko kwenye hivyo vijiji na vitongoji vinavyoenda kufa, wafanyiwe uthamini wa mali zao waweze kulipwa haraka iwezekanavyo. Pia kama Serikali itaona jicho la huruma, iweze kuwaonesha sehemu nyingine ili wananchi hawa waweze kwenda kujenga nyumba zao kwa sababu vile vijiji na vitongoji vinakufa. Viko vijiji vitano vinaenda kufa kabisa kwa sababu vitakuwa ndani ya hifadhi, lakini pia vipo vitongoji vingine ambavyo vinaenda kufa.

Mheshimiwa Spika, tuombe malipo yao yaharakishwe na sio Sheria ipite hapa Bungeni halafu inapofika wakati wa malipo ije iwe shida. Jambo hili litaleta mgogoro kwa wananchi kwa sababu kama umechukua eneo, basi ni wajibu wa Serikali kufanya uharaka wa kulipa hayo maeneo ambayo watakuwa wameyachukua, lakini kuwaangalia wananchi kwa jicho la huruma waweze kuwasaidia kupata maeneo mengine ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni suala la vibali. Niombe sana hawa Idara ya Misitu ambao wanakwenda kuangalia hii Hifadhi ya Misitu ya Kigosi waangalie jinsi ya kutoa vibali. Vibali visigeuke kuwa manyanyaso kwa wananchi, wanapokwenda kuomba vibali kwenda kutundika mizinga au wanapokwenda kuomba vibali vya kwenda kuvua samaki, basi wale wafanyakazi wawe rafiki kwa wananchi ili kutoa migogoro ambayo inaweza kutokea kati ya wale wahifadhi wanaolinda hiyo misitu, watu wa *TFS* pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Spika, hapa Azimio linaweza likapita kwamba ni azimio rafiki ambalo Mheshimiwa Rais amelileta linalokwenda kuwafaidisha wananchi, lakini pia linaweza likageuka likawa kitega uchumi kwa yule Mhifadhi ambaye atakuwa analinda ule msitu. Kwa hiyo ombi langu ni kwamba, wale wahifadhi ambao watakuwa wamepewa jukumu la kutoa hivyo vibali wawe rafiki kwa wananchi ili hivyo vibali visije vikageuka tena vikawa ni kitega uchumi cha Mhifadhi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la mwisho kabisa ambalo nataka kulizungumza hapo, niombe wale wataalam wetu wanapokwenda kwenye maeneo haya yote ya Hifadhi ya Kigosi lakini pamoja na kule Ruaha wakawe marafiki na wananchi, waitishe mikutano, sio mwananchi anaamka asubuhi anakuta mpaka umewekwa, ni bora mikutano wakashirikisha Wenyeviti wa Vijiji pamoja na wananchi kwa kuitisha mikutano ya hadhara na wananchi waone ile mipaka inavyowekwa.

Mheshimiwa Spika, naona umewasha taa, naomba kuunga mkono hoja suala la Azimio la Hifadhi ya Kigosi pamoja na Azimio la Ruaha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwanza naomba kusema naunga mkono

hoja zote mbili; hoja ya kuibadilisha Kigosi kuwa Hifadhi ya Misitu na hoja ya Kurekebisha Mipaka ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, nimepata bahati ya kufika Kigosi na ukubwa wake wa hizo takribani *square kilometer* 8,000 lakini nimepata bahati pia ya kufika Ruaha. Nafahamu mateso waliyokuwa wanayapata wananchi wa vijiji vinavyozunguka Ruaha hasa inapotokea mgongano wa kifikra kati ya Wahifadhi na wananchi na lengo ni jema.

Mheshimiwa Spika, kazi tuliyowapa wahifadhi ni kuhakikisha kwamba maeneo tuliyowapa yanalindwa, lakini pia lazima tukubali kwamba kutokana na nchi yetu kuendelea kuongezeka kwa watu imekuwepo haja ya watu kwenda kwenye maeneo yaliyohifadhiwa ambako kweli ndio maeneo yenye rutuba na maeneo yenye uzalishaji wenye uhakika kwenda kutafuta maeneo ya kilimo.  Kwa hiyo kuridhia kurekebisha mipaka ni kuepuka kesi zisizo za lazima, lakini pia kuridhia kurejesha Pori la Kigosi kwa *TFS* ni kuruhusu shughuli zingine za kiuchumi ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa maeneo ambayo Kigosi ilikuwa inazunguka wanarudishiwa maeneo yao kwa sababu historia inaonesha mwaka 1983, Serikali ndio ilibadilisha kuwa *Game Reserve* na baadae imekuja tukabadilisha ikawa *National Park* na Sheria zetu zilivyo hazitambui sana kwamba wananchi wa asili ya maeneo haya walikuwa wanafanya kazi gani.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa asili ya maeneo yale ambao kwa asili, maeneo yale ninayoyazungumzia yana watu wa Makabila ya Wasumbwa, Wasukuma, Waha, Wanyamwezi na Wasubi. Hawa ni wafugaji wa nyuki na walinaji wa asali. Kwa hiyo tulipobadilisha sheria tukaweka kizuizi na hii ilikuwa ni kazi kubwa ya kiuchumi na ukiangalia ndio maeneo ambapo Wizara pia ilipeleka Viwanda vingi vya asali kwa ajili ya ku-*capture* soko la China.  Kwa hiyo tulikuwa tumezuia kazi za kiuchumi lakini tulikuwa tumetengeneza mradi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa haiwezekani kabisa watu wakaacha kwenda, walikuwa wanaingia na wakiingia wanakamatwa, kwa hiyo tukajikuta tumegeuza makosa kuwa chanzo cha mapato na kwa sababu watu hawawezi kuacha ndio kazi ya uchumi walikuwa wanaingia. Kwa hiyo maamuzi haya ni maamuzi sahihi, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na Kamati kwa kuridhia jambo hili liweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, tunapobadilisha kuwa msitu, hatumaanishi kwamba tunakwenda kuua uhifadhi, bado *TFS* wana wajibu wa kuendeleza ikolojia ya eneo lile kwa sababu hata *TFS* wana utalii unaitwa *eco-tourism* ambao unahusisha utalii wa ikolojia na katika maeneo yote yaliyohifadhiwa wanyama wamo. Kwa hiyo bado *TFS* wanaweza kulilinda eneo hilo likaendelea kuwa na wanyama na likaendelea kufanya utalii, lakini likaendelea kuruhusu wananchi kufanya kazi ambazo hazina athari kubwa kwenye misitu.

Mheshimiwa Spika, wito wangu hapa ni kwamba utaratibu huu uangaliwe pia na maeneo mengine. Nataka kutoa mfano, niliwahi kutembelea Ugala nikakuta kuna mto pale ambao ni mto unao-*feed* Ziwa Tanganyika. Wakati wa kiangazi ule mto unakauka unaacha mabwawa, yale mabwawa yanakuwa na samaki wengi sana, kwa hiyo wananchi wanavizia kwenda kuvua kwa kuiba, lakini wale samaki wasipovuliwa wanakufa kwa sababu maji yanakauka na wanakufa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa unaona sheria inazuia watu wasiende kuvua samaki, kiangazi kikiwa kikali samaki wanakufa wenyewe, kwa hiyo tuangalie utaratibu ambapo hata ndani ya *National Park* kama kinachoenda kufanyika hakina madhara kama ni uvuvi wa samaki watu wakavue samaki. Kwa sababu kwa *nature* ilivyo hata usipowavua wewe watakufa, kwa hiyo jambo hili litufundishe.

Mheshimiwa Spika, la pili, mchango mkubwa wa wananchi kwa maeneo husika. Tunatarajia kwamba baada ya kuwa

limerudishwa *TFS* wananchi wa maeneo yale kwa sababu ni misitu mikubwa watafaidika pia kwenye mazao mengine ya misitu.

Mheshimiwa Spika, nitoe angalizo kidogo, Kigosi ni *catchment area* kubwa ya Malagarasi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu hicho kisemeo chako ukishika na mkono wa kulia kinazuiwa, kwa hiyo sauti haitoki vizuri. Ukishika na mkono wa kushoto unatusaidia tunakusikia vizuri zaidi.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nilikuwa nasema kwamba pamoja na kuunga mkono nataka kuishauri Serikali mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Kigosi ni *catchment area* ya Malagarasi ambayo Malagarasi ndio inayotengeneza maji yanayokwenda mpaka Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, tunapoirudisha *TFS* jukumu la kuendelea kulinda ikolojia ile na uasili wake, lifanyike kama ambavyo lilikuwa linafanyika lilipokuwa chini ya *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, la pili, Kigosi ni makazi ya wanyamapori na hawa wanyamapori hawatajua kwamba tumebadili Sheria tumewatoa *TANAPA*, watabaki kwenye misitu na wataendelea kuingia kwa wananchi. Tuliwahi kuishauri Serikali kwamba *TFS* lazima wajiandae kuthibiti wanyamapori walio kwenye misitu yao. Kuna tembo wa kutosha, kuna simba wa kutosha ambao wakiondoka *TANAPA*, wakaondoka wale watu wa *Game Reserve* wakabaki *TFS* lazima wajiandae kisaikolojia kwamba hawa simba waliokuwa wanazungumzwa hapa wataingia kwenye hizo wilaya zingine. Kwa hiyo lazima jambo hili lifanyiwe uwekezaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, la tatu, kuna misitu minene ambayo ndio chanzo cha mvua cha Mikoa ya Kigoma, Geita, Kagera na Tabora. Kwa hiyo aina yoyote ya matumizi lazima iwe rafiki kulinda ikolojia hii kwa sababu tunapofurahia mvua lazima tujue mvua inatoka kwenye misitu.

Mheshimiwa Spika, la nne, niipongeze kwa kweli Wizara, eneo lile tuna hifadhi nyingine nyingi. Tunazo Hifadhi Burigi Chato, Rubondo, Ugala, kuna *Game Reserve* ya Moyowosi, sasa ni muda wa kuwekeza kwa nguvu kubwa Ugala kwenye *National Park* ili watalii waweze Kwenda. Nasema hivi kwa sababu hatuwezi kujisifia kwamba kuna watalii kumi tu walienda, hapana, lazima tujue kwa nini watalii hawaendi. Kama watalii wanasafiri kwenda kuangalia magofu Vietnam na wapi, tuwalete Ugala ili waweze kufaidika na ikolojia iliyopo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hajaanza kuchangia Mheshimiwa Ramadhan Sima, wako wageni walioingia hapa Bungeni baada ya matangazo ya wageni yaliyopita.

Tunao wageni 42 wa Mheshimiwa Justine Nyamoga ambao ni Wanakwaya wa KKKT Usharika wa Nyamhanga Jimbo la Kusini Magharibi Dayosisi ya Iringa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 96 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi wa Jiji la Dodoma, wanafunzi wa Chuo cha Mipango na Walimu wa *Sunday School* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Maimuna Pathan ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 96 wa Chuo Kikuu Cha Kilimo Sokoine, *SUA* Mkoa wa Morogoro, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi na Walimu wa *St. Francis De Sales Mission School* kutoka Mkoa wa Tabora, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, ninachukua fursa hii kukushukuru lakini na mimi pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhati kabisa ya kutuletea Maazimio haya mawili muhimu sana. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Kaka yangu Mohamed Mchengerwa, kwa jambo hili muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kueleza kuwa mwaka 2018/2019 nilibahatika kuwa katika timu ya awali ya Mawaziri Nane ambao tulipewa jukumu la kwenda kuangalia migogoro ya vijiji 925. Maeneo yote haya mimi nilipata fursa ya kuyatembelea.

Mheshimiwa Spika, katika migogoro yote ambayo inafahamika, jambo kubwa linaloonekana ni kwamba, wahifadhi wanasimamia Sheria lakini pia wananchi ambao tunasema wanavamia, wanalazimika kuvamia kwa sababu hayo ni mahitaji yao ya msingi kulingana na mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema nini? Maazimio haya mawili kuja, nadhani ni mpango mzuri ambao hata mimi sikuutarajia katika kipindi kile na hata kipindi hiki ambacho tunaendelea, kwamba sasa hivi tunapoamua kwa mfano, tumeeleza Azimio la kurekebisha mipaka pale Mbarari kwenye Ruaha Mkuu, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana faida ya kurekebisha mipaka. vilevile, siyo kurekebisha tu, wameamua kugawa eneo kilometa za mraba 478, hili ni jambo kubwa sana na Mheshimiwa Waziri ninakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya msingi hapa nyepesi sana ambayo ni mahusiano katika ya wananchi wa Mbalali na Wahifadhi. Sasa, kugawa tu maeneo inaweza isitoshe, kinachoweza kutusaidia sisi kama Serikali lakini sisi kama

wananchi, tukae pamoja tukubaliane na tuwe na mahusiano mazuri kati ya wahifadhi na sisi ambao tunahitaji kutumia maeneo yale. Tofauti na hapo maana yake tutakuwa hatujatatua tatizo la Msingi.

Mheshimiwa Spika, tunajua hapa kuwa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere tunategemea maji kutoka katika Ruaha Mkuu, pia imetajwa Kidatu na maeneo mengine kote, watakaolinda maeneo haya ni wananchi na siyo wahifadhi peke yake, lakini kama wao ndiyo wanalinda maeneo haya, tunatarajia kuona Serikali inawaunganisha wananchi na wahifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Hifadhi ya Taifa ya Kigosi, historia imeelezwa vizuri, kwamba awali lilikuwa pori, ikawa hifadhi ya misitu na baadaye ikawa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi. Kwa nini? Ndilo eneo ambalo limehifadhiwa vizuri. Sasa umefika wakati ambao ndiyo mimi naipongeza Serikali imekuja na njia nzuri ya kuhakikisha kwamba wananchi watakuwa na sehemu ya kutumia lakini pia Serikali itakuza uchumi kupitia hifadhi hii ya Kigosi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili na maeneo mengine ni muhimu sana. Tunazo hifadhi nyingi na sisi kule Mugori pia tunahitaji eneo hili liweze kuhifadhiwa lisibaki kuwa ni hifadhi ya misitu lakini pia liende kuwa Hifadhi ya Taifa na hata baadae kurudi kuwa hifadhi ya misitu ni jambo jema kwa sababu ya matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano; hata kule Kagera Nkanda nilishawahi kufika. Ule msitu wa Kagera Nkanda ule msitu ni mkubwa sana. unaweza kuutazama ukaona kwamba msitu umehifadhiwa, lakini kule katikati tayari kuna kilimo, ufugaji na vinginevyo kiasi kwamba kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira. Sasa, maeneo kama haya Serikali inapokuja na mpango kama huu ni vizuri ikaangalia maeneo yote ambayo yana changamoto ili tuweze kushirikishana kwa pamoja, wananchi wapate sehemu ya kuweza kufuga, kulima kwenye hifadhi hiyo hiyo lakini pia na hifadhi iweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, ninataka kushauri nini hapa? jambo la kwanza ni elimu. Tunatunga Sheria lakini pamoja na kutunga sheria wananchi wanahitaji waeleimishwe namna ya kuhifadhi mazingira, namna ya kushiriki katika hifadhi zetu hizi kwenye kilimo na shughuli nyingine. Usipotoa elimu kama Serikali utakuwa haujatatua tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni hifadhi ya mazingira na hifadhi ya maji. Maeneo haya yote yamehifadhiwa vizuri sana na ni vyanzo vya maji lakini mazingira yake ni mazuri sana. Sasa, tunaporuhusu shughuli za kibinadamu maana yake tumeruhusu shuguli za kuuchumi ambazo zinaweza kuleta athari nyingine kama sisi hatujchukua hatu za kuwaelimisha watu wetu kwamba, athari hii ikitokea maana yake turekebishe isitokee tena athari nyingine, turudi hapa tuone kuwa tulichokiamua hakiko sawa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la msingi sana na niiombe Serikali kabla haijaamua kuanza kufanya iende ikatoe elimu na ijue hapa tunahitaji kuhifadhi mazingira na hapa tunahitaji kuhifadhi maeneo ya maji ili wananchi wetu waweze kujua jukumu lao kubwa na maisha yao yanategemea hizi hifadhi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa nishauri ni matumizi bora ya ardhi. Kamati imeseama vizuri na niwapongeze kwa kazi nzuri. Matumizi bora ya ardhi ni eneo muhimu sana ambalo wenzetu wa Wizara ya Ardhi nao wanapaswa kushirikishwa ili waende kutoa elimu ya matumizi bora ya ardhi. Hatuwezi kufika na kusema tu eneo hili litakuwa ni eneo la kichumi, eneo hili litakuwa ni eneo la hifadhi lakini matumizi yake tunatumiaje?

Mheshimiwa Spika, wenzetu ambao tumewapa hii sheria waweze kuismamia nao washiriki kwa ajili ya kutoa elimu ya matumizi bora ya ardhi badala ya kuachia tu jambo hili likaenda kiholela na baadaye kurudi kuanza kutatua mgogoro wa ardhi, hii inaweza kutuletea changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia hata katika hiyo mipaka tunapoamaua kwenda kuweka alama *(beacons)* wananchi

wawepo, tusizungumze tu kwamba tumetenga eneo la kilometa za mraba 478 lakini tunapokwenda kule wenzetu wakaamua kusogeza kwa sababu wananchi hawapo hii itatuletea changamoto. Wananchi wawe sehemu ya kuweka mipaka ambayo na wao wataiheshimu ili kesho tukirudi sisi tusiwe sehemu ya hiyo migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikushukuru sana na niendelee kukupongeza, miezi minne siyo jambo dogo, sisi tumekaa hapa tumekupa ushirikiano na kwa kweli tukutakie kila la heri kwenye safari yako hiyo ya kidunia. Wewe ndiyo utakuwa *icon* ya Tanzania. *Icon* hii tunaitarajia na wewe kufikisha ujumbe, hata wenzetu wa maliasili na wengine tunataka tuone wanakuunga mkono kwa sababu uwepo wako kule Serengeti itajulikana, kila kitu kitajulikana na Tanzania itajulikana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu akubariki sana na ninaunga mkono Azimio hili, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Christopher Ole-sendeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi ya kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa zawadi ya siku ya leo. Pia, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa jinsi ambavyo unaliongoza Bunge letu Tukufu. Siku zote nimekuwa shahidi na Watanzania wamekuwa mashahidi juu ya uwezo wako na umakini wako katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. Siku zote ukikaa hapo linapokuja jambo gumu, taaluma yako, uzoefu wako na umakini wako linakuwa ni jawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana tu peke yake umeendelea kuonesha hivyo tulipokuwa tunapitisha Muswada wa *Finance Bill*. Katika Kifungu kile ulilazimika kuwaimamisha baadhi ya Wabunge waliokuwa kwenye Kamati ile kulikuwa na jambo dogo lakini kulikuwa na athari kubwa, lakini wewe mwenyewe uliliona kwa

jicho lako na ukatufanya wote tulione. Nakupongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika watu wa Mbeya wanaendelea kuona na kwa kweli ninahakika kelele zile hazitamnyima Tembo kunywa maji na mambo yatakaa vizuri tu, nichukue nafasi hii sasa kurudi kwenye hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Spika, ni kweli usiofichika kwamba hatua ya leo ya kuleta pendekezo na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *Comrade* Mohamed Mchengerwa na Wasaidizi wake wote, baada ya maamuzi ya Mheshimiwa Rais, kwanza, nichukue nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uamuzi huu wa busara. Mimi nitamke bayana kwamba maazimio yote mawili ninayaunga mkono kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kulinda, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za nchi ni jukumu la kila raia kwa mujibu wa Katiba, lakini suala la kumaliza migogoro kati ya Hifadhi za Taifa, maeneo yaliyohifadhiwa au maeneo yanayopzunguka hifadhi zetu za Taifa kwa kweli Wizara yako inayo dhamana hiyo na nafasi kubwa ya kusaidia katika kumaliza migogoro hiyo. Leo umeonesha kwa vitendo kwamba yale uliyosema wakati wa ziara zako ulipokuwa unatembelea Hifadhi za Taifa kwamba utahakikisha kero hizi zinashughulikiwa, leo umeshughulikia mpaka umeweza kumpelekea Mheshimiwa Rais na kwa mamlaka aliyonayo Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa sheria ameridhia kupunguzwa kwa hifadhi hizi mbili na moja kubadilishwa matumizi kutoka Hifadhi ya Taifa Kwenda *TFS,* hatua hii ni ya kimapinduzi na hatua hii ni faraja sana kwa wapiga kura wetu na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, nichukue nafasi hii sasa kumpongeza mwenye mamlaka mwenyewe aliyeridhia hifadhi hizi mbili, moja iweze kumegwa na nyingine iweze kubadilishwa kutoka katika hadhi ya Hifadhi za Taifa na kwenda kuwa chini ya *TFS* naye si mwingine ni Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninampongeza sana jinsi alivyowajali wapiga kura wake na Watanzania na ni jambo lake la kawaida, mimi nataka niseme

wazi kwamba *GN* Na. 28 ya mwaka 2008, Kamati imethibitisha na wewe mwenyewe umethibitsha kwamba kwa kweli ushirikishwaji haukutosha, ndiyo maana wananchi walikuwa wanalalamika sana katika maeneo hayo ambayo *GN Na*. 28 iliweza kuondoa baadhi ya maeneo ya wakulima, wafugaji na kuyaingiza maeneo hayo katika Hifadhi ya Taifa bila ushirikishwaji wa kutosha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu tu kwamba sasa mmefanya maamuzi ya hekima, maamuzi haya yamefanyika baada ya ziara yako Mheshimiwa Waziri lakini pia baada ya ziara ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Ninataka nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati, kukupongeza wewe na msaidizi wako Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mtendaji Mkuu wa *TANAPA* na Mtendaji Mkuu wa *TFS*.

Mheshimiwa Spika, niseme bayana kwamba, kama tukifanya hivi katika maeneo mengine kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi wetu katika kuinua na kushughulikia masuala yao ya kiuchumi tutakuwa tunafanya maamuzi ya kushughulikia ustawi wa watu wetu. Ni dhahiri basi kwamba haya yaliyofanyika Ruaha, yaliyofanyika Kigosi yakiendelea pia kufanyika Kanda ya Kaskazini mwa nchi yetu itasaidia sana kupunguza migogoro iliyoko huko.

Mheshimiwa Spika, nieleze bayana kwamba Mheshimiwa Waziri nina imani nae kubwa sana, ninaimani kwa sababu anatoa muda wa kusikiliza Wabunge, na mimi amenisikiliza katika suala la migogoro tuliyonayo katika eneo lile, ninaamini busara uliyoitumia baada ya kwenda kule Ruaha, ninakuomba na nikualike rasmi uje Kanda ya Kaskazini kwa maana ya Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Arusha, ndipo mtakapoweza kujua kwamba changamoto kubwa waliyonayo wafugaji katika Wilaya za wafugaji na hata migogoro ambayo inatokana na mchakato unaoendelea wa timu inayofanya tathmini ya maeneo yenye rasilimali za wanyamapori katika mapori ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, hali hii imeleta taharuki kubwa sana kwa sababu tumetoa kama wafugaji maeneo ya hifadhi mnazozijua, haibishaniwi kwamba tumetoa mchango mkubwa Serengeti,

Tarangire, Lake Manyara, Ngorongoro na tumetoa mchango mkubwa Mkungunero lakini bado mpaka leo katika ardhi ambayo iko kwenye nyanda kame, ardhi ambayo haitoshelezi malisho ya mifugo iliyoko leo, bado kuna mawazo na watu wanaopita katika kuangalia maeneo ambayo tumeyatenga kwa ajili ya malisho ya mifugo, ambapo tunapotenga maeneo ya mifugo ndiyo hayo hayo ambayo wanyama wetu ambao ni rasilimali za nchi wanapopata malisho kwa muda kabla hawajarudi katika Hifadhi za Taifa, mapori tengefu na mapori ya akiba.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza sasa zoezi linaloendelea ambalo linajumuisha Wizara kadhaa linachukua sura sasa ya kutaka kuanzisha hifadhi nyingine katika eneo la Olokisale *Game Controlled Area*, eneo lote la Simanjiro *Game Controlled Area,* eneo lote la *Southern Ruvu Masai Game-Controlled Area*, eneo la *Lake* Natron *Game Controlled Area,* eneo la *Longido Game Controlled Area.*

Mheshimiwa Spika, nikueleze athari inayojitokeza ni hii, ni dhahiri kwamba maeneo niliyoyataja yanaifanya Simanjiro kwa ujumla kuwa ni eneo ambalo awali kulingana na Sheria ya *Fauna Conservation ordnance* ya Mwaka 1951 ilikuwa ni Wilaya nzima za Masai zilikuwa chini ya *game-controlled area.* Sasa kama maeneo yale tumeshayatoa kwenye hifadhi hizo na tumebaki na maeneo madogo ya malisho ambayo hayatutoshelezi leo, Mheshimiwa Waziri, nachukua nafasi hii kukualika naomba uje tutembee na wewe kijiji kwa kijiji, eneo kwa eneo ujue umaskini ulioingia huko umasaini katika Wilaya za wafugaji hao kutokana na maeneo kutowatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Kanda yetu ya Kaskazini mwa Wilaya ya Simanjiro na Ukanda wa Mashariki, mvua iliyopita mwaka huu haijanesha katika ukanda huo, maana yake mifugo yote ya Simanjiro iko katika Kata mbili za Loiborsiret na zingine zimevuka mpaka kuingia Kata ya Makame na Ndedo katika Wilaya Kiteto.

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea leo ni kutaka tena kuchukua maeneo yale na kuyageuza kuwa Hifadhi au *Game*

*reserve* au *Game Controlled Area*. Ninataka niiombe Serikali yangu sikivu ya CCM kwamba jambo hili naomba mliache. Liacheni maana maamuzi yenu haya ya juu yasiyo shirikishi, yana athari kubwa katika ngazi za msingi, ngazi zetu za Majimbo, Kata, Vijiji na Mitaa. Tunaomba sana tushirikishane.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji unaotakiwa kwa mujibu wa sheria, kushirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ardhi za vijiji ni mikutano mikuu ya vijiji, Halmashauri za Vijiji na Halmashauri za Wilaya ziweze kutoa maoni yao juu ya namna bora ya kutoka pale. Ninaimani sana na Mheshimiwa Mchengerwa, ninaomba ufike uione hali halisi, usiletewe na wataalam usije ukauziwa mbuzi kwenye gunia.

Mheshimiwa Spika, juzi liliendelea zoezi moja lililokuwa Kimotoro Kata ya Kimotoro katika Wilaya ya Simanjiro na kijiji kilichopo Wilaya ya Kiteto katika eneo linalopakana na Mkungunero *Game Reserve,* kinachoshangaza Mawaziri Nane wakiongozwa na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, walifika katika maeneo hayo na kueleza maeneo ambayo Serikali imeridhia kuyarudisha kwa wananchi. Kilichokuja kutekelezwa katika uhalisia wake siyo kile ambacho kilitangazwa na Mheshimiwa Lukuvi.

Mheshimiwa Spika, kinachoogopesha kuliko yote kwa sababu mpaka wa Simanjiro na Kondoa ndiyo mpaka wa Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Dodoma, kilichokuja kujitokeza katika tafsiri iliyokuwa inafanywa pale, kimsingi hata mtu aliyeishia darasa la saba anajua kabisa kwamba kilichofanyika hapa siyo sahihi, ninaomba Waziri mkae na Makongoro Nyerere awasaidie. Makongoro Nyerere alikuwa sahihi katika suala la mpaka wa Dodoma na Manyara kwa maana ya mpaka wa Wilaya ya Kondoa na mpaka wa Wilaya ya Simanjiro.

Mheshimiwa Spika, ile *GN* iko bayana hauhitaji kwenda kwenye darasa kubwa sana ili kujua, unaambiwa tu wazi kwamba, unatoka katika Mlima uliotajwa kwenye *GN* hiyo ya kuanzisha Wilaya ya Masai ambayo ndiyo *GN* ya kuanzisha Wilaya ya Kondoa, inaweka bayana kabisa na ninaomba ninukuu na

ninatangaza tu *point* moja ambayo ndiyo inaleta mgogoro na ndiyo *GN* ilipo, inasema wazi kwamba, *"… South - South East to a point four Miles, West South West of* Mikuyuni Mikunga …."

Mheshimiwa Spika, Mikuyuni Mikunga ndiyo *beacon* tunayogombania na wenzetu ambayo inahamisha leo nusu ya Kitongoji cha Kijiji cha Kimotoro kwenda Wilaya ya Kondoa. Badala ya kwenda hiyo Magharibi *mile* Nne ambayo Mlima uko hapa nilipo, kisima kipo hapo alipokaa Waziri wa Nchi, unatarajia *Four Miles West South West* ya alipokaa Mheshimiwa Jafo ndiyo inafanya kuwa kile kisima kinachotamkwa. *West south west Four miles,* kama hapo ulipo maana yake unakwenda kulia lakini wao wanakwenda kule alikokaa Mheshimiwa Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Spika, sasa unajiuliza hapa nilipo ndiyo mlima ulipo unaambiwa nenda *west south west four miles* kutoka kwenye kisima hicho ambako ndiko aliko Mheshimiwa Jafo, badala ya kunyooka kwenda kutafuta *point* upande wa Magharibi, unakwenda kutafuta *point* upande wa Mashariki na kuweka jiwe, kwa maana hiyo, unahamisha mpaka wa Mkoa badala ya kwenda magharibi ambayo inaingia *TANAPA* ndani ya eneo la Tarangire unalazimisha kwenda mashariki ambapo unaathiri Kijiji kizima cha Kimotoro kuihamishia Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, sasa *GN* hii ni yam waka 1961 *GN* Na. 65…

**SPIKA:** Mheshimiwa dakika moja malizia mchango wako muda umekwisha.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba tu uniongeze dakika moja ikikupendeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa ndiyo hiyo niliyokuongeza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru Mkuu.

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni nini? Kiacheni kitongoji cha Arkasupai kilichopo pale Kimotoro katika Wilaya ya Simanjiro kwa sababu *GN* yenyewe inawataka wabaki pale. Ninaomba Mawaziri mje wenyewe mshuhudie tafsiri potofu iliyotolewa hapo. Hatuna taabu hata ikitamkwa kwamba mpaka ndiyo huu lakini Rais anahitaji eneo hili kwa ajili ya hifadhi. Sisi ni wahifadhi lakini zaidi Mheshimiwa Waziri nikualike tuangalie njia za mapito ya wanyama uone jinsi sisi tulivyo wahifadhi wazuri. Angalia eneo la Natron linaathiri mno Longido, angalia lile eneo lingine la *GN* zile *GSA* za Simanjiro tusaidie ili tutoke pale.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nikiwa ninaimani kabisa kwamba Mheshimiwa Mchengerwa atatupatia muda wake wa ziada basi ninaomba niunge mkono hoja katika mapendekezo haya yote mawili na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutubeba katika barabara yetu kubwa ya kihistoria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na muda wetu kama utasalia Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Mimi nianze kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake mzuri na kwa maono yake makubwa aliyonayo kwa Watanzania hasa kwa kuendelea kufungua fursa kwa Watanzania kujiajiri kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze na Waziri wa maliasili na utalii pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo na kwa kweli kwa kuweza kutafsiri maono na mapenzi makubwa ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Watanzania. Sasa tunaona kwamba sasa baada ya Mama kuleta unafuu kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji hapa nchini sasa leo ameangazia eneo la wafuga nyuki na eneo hilo sasa naona linachagizwa na Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu

Waziri wake kwa kweli mnastahili maua yenu, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia kwenye mchango wangu nikupongeze wewe Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Tulia kwa uongozi wako mzuri. Ni vizuri tusiwe tunasemea pembeni, tukupongeze hapa usikie na hata Wananchi wa Mbeya wasikie kwamba Wabunge tunakukubali na Watanzania wanakukubali na wewe unastahili maua yako, hongera sana kwa kazi nzuri, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme ninaunga mkono hoja mazimio yote mawili azimio la kurekebisha mipaka ya Ruaha, vilevile azimio la kushusha Kigosi kutoka kwenye Hifadhi ya Taifa kwenda kwenye Mamlaka ya Hifadhi za Misitu Tanzania *(TFS)*.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba maamuzi haya na maazimio yote haya mawili yanakwenda kuleta unafuu mkubwa sana kwa Watanzania. Mathalani kule Ruaha migogoro ilikuwa ni mingi sana Watanzania tulikuwa tunashuhudia watu wanagombania mipaka sasa azimio hili la kwenda kurekebisha hiyo mipaka huu ndio mwarobaini wa kwenda kupeleka suluhisho la kudumu kwa wananchi wale waweze kufurahia kuishi ndani ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, nikija upande wa Kigosi niseme tu kwamba Mataifa ya Kongo, Rwanda na Burundi kwa sehemu kubwa yamekuwa yaki-*import* asali inayotoka kwenye Hifadhi ya Kigosi. Sisi wananchi wa Ngara ni watumiaji wazuri sana wa asali. Asali yote tunayoitumia Ngara tumekuwa tukinunua asali inayozalishwa pale Kigosi.

Mheshimiwa Spika, mathalani na wananchi wote wa Kanda ya Ziwa na wale wa Mkoa wa Kagera wote tumekuwa tukitegemea asali ambayo imekuwa ikilinywa pale kwenye Hifadhi ya Kigosi. Sasa kitendo cha kuondoa hifadhi hii kutoka kuwa Hifadhi ya Taifa na kwenda kuwa hifadhi ya misitu kinakwenda kufungua ajira kwa Watanzania zaidi ya 5000 ambao

hawa wanakwenda kujiajiri moja kwa moja kwenye shughuli mbalimbali ikiwemo ufugaji wa nyuki kwenye eneo lile la msitu.

Mheshimiwa Spia, kuna Watanzania zaidi ya 10,000 ambao wanakwenda kupata ajira *indirectly* kutokana na uwekezaji wa Watanzania ambao wanakwenda kuwekeza pale kufuga nyuki.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na nia nzuri kabisa kupitia *TFS* ambapo viwanda vitano vimejengwa kwa ajili ya kuchakata asali mbichi na kwa siku moja viwanda hivi vilikuwa vinachakata zaidi ya tani nne ya asali ambayo inazalishwa na hawa wananchi waliojiajiri eneo lile. Kwa mwaka mmoja viwanda hivi vilikuwa vinauwezo wa kuchakata tani za asali 1460.

Mheshimiwa Spika, tani moja ya asali inauzwa shilingi 4,000,000, sasa ukizidisha kwa mwaka mmoja ni takribani eneo hili lilikuwa linazalisha shilingi 5,800,000,000 kutokana na uwekezaji ambao wananchi wanaofugia asali mle wameufanya. Lakini eneo hili mara tu baada ya kuchukuliwa na *TANAPA* likawa chini ya Hifadhi ya Taifa shughuli zote hizi zilisitishwa.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi hebu fikiri kwa mwaka huu pekee watalii waliokwenda Kigosi ni watalii kumi, *imagine* nchi yetu inawekeza pale tumewalipa watu mishahara watu wanaweka mafuta kwenye magari wanafanya kampeni *promotion* mwaka mzima wanapatikana watalii kumi huku tumezuia Watanzania kutengeneza shilingi 5,800,000,000 kwa mwaka. Kwa kweli yalikuwa ni maamuzi ambayo yanaturudisha nyuma bdala ya kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi ambacho eneo hili limekaa chini ya *TANAPA* tumepoteza shilingi bilioni 30, ukifanya mahesabu zaidi ya bilioni 30 zimepotea. Sasa kwa kweli dhamira nzuri ya Serikali inaonekana pale ambapo Serikali inafanya *cost benefit analysis* inaonyesha kwamba tukiendelea hivi hasara yake ni kubwa lakini tukifanya hivi tunaenda kupata faida tunaenda kutengeneza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maamuzi mazuri aliyoyafanya tunakwenda sasa kuwasaidia Watanzania waweze kujiajiri kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe na watu wa *TANAPA* hili liwe funzo kwao yako maeneo mengine ndani ya nchi hii kwa mfano Hifadhi ile ya Manyara eneo lile la Mayoka. Eneo lile lina *vein* zina madini ya vito, yale Madini ya Vito uchimbaji wake hauhitaji matumizi ya kemikali ni kuruhusu mtu anakwenda na greda anachimbua analeta kadude kamoja kadogo kanauzwa mpaka Dola laki moja. Nchi yetu tuko katika wakati ambapo tunahitaji fedha lakini yaani *TANAPA* wakisikia mtu yoyote anazingumzia hilo eneo wanatamani kukukamata hata kabla hujafika huko. Kitendo tu cha kuzungumza kwamba eneo fulani ni *potential* kwa nchi hii linaweza likatumika kusaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kazi nzuri uliyoifanya huko Ruaha na huko Kigosi inaonekana na inaenda kuleta matunda makubwa kwa Watanzania. Katika eneo hilohilo Mheshimiwa Waziri endelea basi ruhusu hata Taasisi za Serikali ziende zifanye utafiti tujue tuna-*reserve* kiasi gani tujue kama Taifa madeni tunayodaiwa nje ya nchi tunaweza tukawekeza kidogo eneo lile tukapata fedha nyingi tukaingizia Serikali fedha na tukaenda kutatua matatizo ya Watanzania. Kaeneo kenyewe kako mwishoni mwa Hifadhi ya Manyara hekta zenyewe hata 2000 hazifiki hata ukikata hekta 200, 300 Watanzania wataweza kuwekeza pale na tutapata fedha. Maamuzi yaliyofanyika Ruaha na Kigosi ikawe fundisho watu wa *TANAPA* fungueni moyo wenu muone kwamba haya mambo yanawezekana na hii iwe ni mwanzo wa kuangalia maeneo mengine *potential* kwa ajili ya Taifa letu ili yaweze kuachiliwa ili uwekezaji ufanyike na nchi yetu iweze kupata faida kutokana na rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu alitujalia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ninakushukuru sana kwa fursa hii niseme tu ninaunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, niongeze mchango kwenye hoja zilizoko mbele yetu leo. Kwa pekee kabisa niungane na wenzangu kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya ya kujali Maisha ya wananchi wa nchi hii. mazimio haya ni Ushahidi wa moja kwa moja wa Mheshimiwa Rais namna anavyowajali na kuwapenda na kuwasikiliza Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwenye kuchakata na kuandaa mazimio haya ambapo kufikia hatua hii kuja kujadiliwa ndani ya Bunge lako. Mwisho kwenye pongezi nikupongeze wewe mwenyewe na nikushukuru kwa namna ulivyotoa uongozi mzuri uongozi imara kwenye jambo hili mpaka tumefika hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama niongeze mchango kidogo na nianze kwa kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu Kamati yako ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi Maliasili na Utalii inayofanya kazi kwa niaba ya Bunge lako kulisimamia na kuishauri Serikali kwa upande wa Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwenye jambo hili imefanya kazi hii kwa umakini mkubwa sana. Imefanya kazi hii kwa kuangalia na ku-*balance* maslahi makubwa ya Taifa na kuangalia Maisha ya wananchi wa nchi ya Tanzania. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono mazimio haya na kuwasaidia watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nitoe mchango kwenye maeneo hayo mawili. Eneo la kwanza kwenye eneo hili la Ruaha kama tulivyosema tunaipongeza Serikali kwa kazi hii nzuri lakini kwenye mchakato wa jambo la Ruaha nimejifunza mambo makubwa mawili ambayo naomba Serikali niishauri. Moja, nimejifunza kwamba Elimu kwa watu wetu juu ya tunayoyafanya kwa ajili ya Maisha yetu lakini kwa ajili ya nchi yetu ni jambo muhiu

sana. Niiombe sana Serikali si kwenye jambo hili, siyo kwa mamlaka ya maliasili peke yake lakini Elimu kwa wananchi wetu ni jambo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nimejifunza, Serikali inafanya kazi kubwa inafanya kazi nzuri. Niwaombe Serikali iendelee kukubali kuwa na moyo huu mzuri wa kutafakari na kufikiria Maisha ya watu wetu wanaotoka kwenye jambo hili la Ruaha. Kwenye kazi iliyofanywa na Timu ya Mawaziri Nane mapendekezo yaliyotolewa kwenye kushughulikia jambo la Ruaha moja ya jambo nililojifunza yako baadhi ya maeneo machache ambayo taarifa zilizotumika kufikia maamuzi yale hazikuwa zimekaa sahihi kule uwandani kule chini kwenye ardhi. Naishukuru Serikali kwa busara yake baada ya kuona kuna haja ya kuongeza vitu vya ziada Serikali imefanya hivyo na leo tumefika hapa kuja kwenye haya maazimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Serikali nitoe mfano tu wa kule Tanga kwenye eneo la Kaka yangu Mkinga, kwa Mheshimiwa kaka yangu Kitandula, Wilaya ya Korogwe kuna eneo kule kwenye Mto Umba, eneo la Bonde la Umba kuna eneo kwenye Kata ya Mwakijembe, kuna eneo kwenye Kata ya Kalawani kwenye Wilaya ya Korogwe taarifa zilizotumika tunaamini wataalam wakienda uwandani watakuja na picha kamili ya kusaidia kutatua mgogoro huu na kuwanufaisha wananchi kama vile wananchi wa Ruaha wanakwenda kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyohivyo na kwenye Kata ya Magambo kwa Lukonge kwenye Jimbo la Korogwe Vijijini kwenye Kijiji kile cha Magamba kwa Lukonge eneo la Chang'andi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili tutume tena timu yale maeneo ambayo bado wataalam wetu hawajarudi kwa mara ya pili, wakafanye uhakiki wa hali iliyopo kule chini pia tujitahidi kuongeza kasi ili maeneo yale yote ambayo yalipitiwa na Timu ya Mawaziri nane kazi ambayo mmewaachia wakuu wa mikoa ifanyike ikamilike ili tufunge mambo haya mogogoro hii iwe imekwisha na itakuwa ni utatuzi wa kudumu kwa migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili eneo la Hifadhi ya Kigosi, nirudishe tu historia kidogo kwa Neema ya Mungu nilipata nafasi ya kuwa sehemu ya Bunge la 11 mwaka 2019 nikiwa Mjumbe wa Kamati, ndiye niliweka mezani Taarifa ya Kamati kuhusu maoni kuhusu kupandisha hadhi eneo la Hifadhi ya Ugalla na Hifadhi ya Kigosi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kama kuna kazi ngumu tuliwahi kufanya kwenye Bunge hili ilikuwa ni kazi ya kupandisha Kigosi na kupandisha Ugalla. Wabunge wa maeneo haya walikuja wakilia walikuja wakilalamika wanaomba maeneo haya yasipandishwe hadhi ili wananchi wao wapate maeneo ya kufanya shughuli zao kwa sababu ya mazingira na sababu mbalimbali jambo hili halikuwezejana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hiki kilichokuwa kinafanyika sasa. Kimekuwa ni kilio cha muda mrefu sana cha watu hawa kimekuwa ni kilio kikubwa cha Wabunge na wananchi wa maeneo haya. Ninaamini jambo hili linalokwenda kufanyika linakwenda kuwafanya wananchi wa maeneo yanayokaribiana na eneo la Kigosi yanayonufaika na eneo la Kigosi kurudisha moyo wa kuendelea kuipenda na kuithamini Serikali. Ninaomba jambo hili likasimamiwe vizuri lifanyike vizuri ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaushauri kwenye maeneo madogo matatu; moja tuna hifadhi nyingi sana za Taifa lakini hifadhi zetu nyingi hazifanyi vizuri na kwenye uhifadhi, Hifadhi ya Taifa ndiyo hatua ya juu kabisa ya uhifadhi ambayo kwenye hatua hiyo shughuli za kibinadamu haziruhusiwi kabisa. Ni wakati sasa kama nchi tufanye tathmini sahihi kuhusu hifadhi zetu za Taifa zipi zinafanya vizuri, zipi ambazo tunaweza tukazibadilisha baadaye kupata mapori ya akiba ili mambo yaweze kwenda vizuri. Lakini kama yako maeneo ya kupandisha na kwenyewe pia yaendelee kupandishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kama nilivyosema tuongeze kasi kwenye kukamilisha utatuzi wa migogoro yale maeneo ambayo Kamati ya Mawaziri nane imefika.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne niishauri Wizara, mambo yanayokwenda kufanyika na mazimio haya yanatusaidia kupunguza migogoro kati ya wananchi na hifadhi wananchi na Serikali. Lakini hii peke yake haitoshi Mheshimiwa Waziri ni wakati sasa na Mheshimiwa Rais alishasema na ametoa maelekezo kalitafakarini upya namna ya kuliboresha na kuliimarisha Jeshi Usu ili kulipa elimu zaidi kulipa weledi zaidi na kulifanya liwe rafiki na wananchi tupunguze migogoro kwenye haya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ni wakati wa kwenda kuliunganisha Jeshi hili, leo tunakwenda kuirudisha Kigosi ambayo ni kubwa sana, moja ya sababu tutaipandisha wakati huo na mambo ya kiusalama pia yalikuwepo. Tutampa *TFS* kufanya kazi lakini tusipoliimarisha jeshi hili tunahitaji utunzaji na uangalizi zaidi wa weledi na taaluma wanaopewa watu wa misitu ili mambo yaweze kwenda vizuri. Tukaliimarishe Jeshi Usu ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nishauri, narudia tena kwa mara nyingine na nitaendelea kurudia hili. Kama nchi tukajidhatiti kwenye eneo la mipango ya matumizi bora ya ardhi. Siyo kweli kwamba tuna uhaba mkubwa kiasi hicho wa maeneo ya kufanya shughuli maeneo ya kulima, maeneo ya kuchunga na maeneo mengine. Moja ya changamoto tuliyonayo hatujatengeneza mipango vizuri ya matumizi ya maeneo yetu. Kuna *ranch* nyingi lakini ng'ombe wanaletwa maeneo ya kwenda kufuata malisho lakini *ranch* tunazo nyingi. Niombe sana Serikali jambo hili tukalipe uzito kwa wakati tuliokuwa nao ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hojanakubaliana na mazimio yote mawili nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge naona dakika zimetuishia nilikusudua Mheshimiwa Waziri wa Ardhi angetoa mchango wake sasa lakini muda wetu umekwisha kwa hivyo atachangia jioni na yeye.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kikao chetu hiki cha leo. Hoja hizi zote mbili zitahitimishwa baadae na tutaendelea na ratiba kama inavyoonyesha kwenye orodha ya ratiba yetu ya leo.

Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ataanza nasi mchana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii atafuatia, mtoa hoja atahitimisha hoja yake.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge tujitahidi sote kurejea kwa wakati kwa sababu muda huo tutafanya maamuzi kwa ajili ya hoja hizi mbili.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo

*(Saa 7.00 Mchana, Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

**Azimio la Bunge la Kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi**
**na**
**Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa Ruaha**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Masanja, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na Mtoa Hoja ajiandae.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia katika Azimio hili hasa la Kurekebisha Mpaka katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye baada ya kuingia tu madarakani jambo la kwanza lilikuwa ni kupitia ile migogoro 975, mmojawapo ukiwa ni huu wa Hifadhi ya Ruaha na alielekeza Kamati ya Mawaziri Nane kutumia busara na hekima katika utatuzi wa migogoro hiyo. Pia akatuasa tusilete taharuki katika suala nzima hili. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, niwashukuru Wabunge ambao walianza kwa kuleta hoja hizi ambazo zilikwenda kuzaa hiyo Kamati ya Mawaziri Nane. Vilevile niishukuru Kamati, kwanza kwa kuunga mkono Azimio la Serikali lililoletwa hapa kwa sababu Kamati pia imeunga mkono na wachangiaji wengi walikuwa wanaunga mkono. Kwa hiyo, nawashukuru pia kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Spika, katika hoja za Kamati ambazo zimeletwa pamoja na wajumbe waliochangia nitajikita katika

chache ambazo nataka kuzitolea ufafanuzi ambazo wameulizia. Jambo la kwanza ni suala la fidia ambayo wamelizungumzia. Nataka tu niseme ya kwamba kazi ya fidia mpaka sasa hivi imeshafikia karibu asilimia 80, watu wameshafikiwa kwa ajili ya kuweza kutathminiwa maeneo yao watakaokwenda kulipwa.

Mheshimiwa Spika, malipo watakayokwenda kulipwa ni pamoja na posho ya makazi ambayo watapewa posho ya pango la nyumba kwa miezi 36, kwa maana ya kufika kipindi kile atakachokuwa anaandaa makazi mengine aweze kupata pesa za kupanga, lakini atalipwa posho ya usumbufu, atalipwa posho ya usafiri atalipwa thamani ya ardhi yake pamoja na thamani ya nyumba. Haya yote yanafanyiwa tathmini na tayari asilimia zaidi ya 80 wameshafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwatoe hofu tu Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesema kazi hii ikamilike haraka, nadhani tunaenda nayo vizuri. Vile vile, jambo lingine ni suala zima la ule mpaka, baada sasa ya kubadilisha mipaka ya *GN* 28, zoezi la kuweka zile *beacon* katika mpaka limekamilika. *Beacon* zaidi 671 zimewekwa katika mpaka wa urefu wa kilometa 344, lakini na mkuza pia ambao wamesema uwekwe, mpaka sasa umewekwa kwa kilometa 177. Haujakamilika wote kwa sababu tu ya hali halisi ya hewa, kulikuwa eneo lingine lina maji hawawezi kuweka mpaka ule, kwa hiyo sasa hivi kwa sababu pameanza kukauka baadhi ya maeneo basi watamalizia. Kwa hiyo, mkuza nao umebaki asilimia kidogo kuweza kumalizia. Kwa hiyo, haya yote yanafanyika kwa sababu ni masuala ambayo ni maelekezo pia ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa, lakini wakaomba pia na ile suala zima la kutenganisha maeneo hayo ili yasilete mtafaruku mwingie.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi hili zima hasa katika kuweka mpaka, wananchi kule wameshirikishwa sana kwa maana ya kwamba Uongozi wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa Ndugu Homela alikuwa pale kwa muda wote katika suala zima hilo lakini uongozi wa wilaya pia wameshirikishwa. Kwa hiyo, mpaka huu mpya uliowekwa umeshirikisha hawa wengine. Kwa yale ambayo sasa hivi pengine Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaona labda

hayajakaa sawa sana, kama Serikali nadhani bado tunao muda wa kuweza kutafakari vizuri kuyafanyia kazi. Kwa sababu kazi hii tumeifanya kwa muda mrefu, mpaka kufikia hapa kazi imefanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, rai yangu ambayo naitoa tu na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba, kazi tuliyotoa ile ya hekta zaidi ya 74,000 kwa wananchi tukienda kuifanyia mpango wa matumizi bora ya ardhi tutaweza kubaini nani anapata heka ngapi na nani atapata za kilimo na kwa maana ya wafugaji. Kwa hiyo zile hekta mpaka sasa hivi bado hazijagawiwa katika yale maeneo, kwa sababu ukikamilisha hili moja basi na mpango wa matumizi ya ardhi unaanza. Tusingeweza kufanya mpango wa matumizi ya ardhi kama hata azimio lenyewe halijapita na hatuweza kujua mipaka imefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe rai tu kwamba, tupitishe azimio hili ii twende kule tuwapange wananchi vizuri, wale wafugaji ambao wameachiwa eneo la Ruaha kule waweze kupangwa vizuri, lakini na wananchi hawa ambao wanatakiwa pia kupangwa katika yale maeneo yaliyoachiwa, kwa sababu katika kuondoka ni jumla ya vijiji vitano ambavyo vinatakiwa kuondoka katika yale maeneo lakini kuna vitongoji kama kumi na kitu ambavyo navyo vinatakiwa kuondoka. Sasa wale wote tunawapangia mahali pa Kwenda.

Mheshimiwa Spika, katika hili pia tayari tumeshabainisha vijiji kumi na mbili ambako watakwenda kule lakini pamoja na hayo watapewa ile gharama ya usafiri kwa kule wanapokwenda kwa mujibu wa kisheria. Kwa hiyo, tunasema hakuna mwananchi ambaye hatatendewa haki katika hili, kwa sababu tunajua walikuwa kwenye vijiji ambavyo vinatambulika kisheria, Serikali ilikuwa imevisajili. Kwa hiyo kuwaondoa kwao pale sio kwamba ni wavamizi kwa maana ya uvamizi, lakini vilitambuliwa vijiji, kwa hiyo mipaka ndio ilikuwa inaleta taharuki kutokana na ule uhifadhi. Pia, kwa sababu wote tunaona kwamba uhifadhi ni muhimu iendelee kuwepo, basi nadhani wote tutakuwa na

dhamira njema ya kuweza kupitisha azimio hili ili kazi iweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niwaombe Waheshimiwa Wabunge walipitishe azimio hili wote, kwa ujumla wao kwa sababu linakwenda kuondoa changamoto kubwa ambayo imekuwepo, lakini linakwenda kuwapa nguvu za uchumi wale wananchi ambao wataondoka. Kwa sababu maeneo watakayopangiwa yatapimwa na kila mmoja atamilikishwa kwa hati yake katika lile eneo ambalo atakuwa amepangiwa. Kwa hiyo, hapo tayari kiuchumi tutakuwa tumeshawaongezea nguvu. Kwa hiyo niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ina dhamira njema na ndio maana tunaongeza kasi ya kukamilisha michakato ya maeneo yenye migogoro ili watu waweze kuishi kwa amani, watu waondokane na kukimbiakimbia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme tu azimio hili limekuja kwa wakati muafaka, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge waikubali. Dhamira njema ya Serikali ni kuhakikisha tunalinda hifadhi zetu, lakini vile vile hatuleti changamoto kwa wananchi kwa sababu wao ni sehemu ya ulinzi wa zile hifadhi, wakipata maeneo wakakaa vizuri maana yake pia watakuwa ni sehemu ya uhifadhi na hapatakuwa na changamoto zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono azimio. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Masanja, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Waziri ujiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nisiwe mchoyo wa fadhila, nianze kwa kumpongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo amesimamia mazoezi haya ya migogoro, hatimaye leo tumeanza sasa harakati za kuleta maazimio ili turekebishe baadhi ya maeneo. Nampongeza kwa moyo wa dhati kwa sababu hata Wabunge wenyewe wamekiri leo

kwamba safari ilikuwa ni ndefu, lakini hatimaye tunaanza kuiona nuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe umekuwa ukitusimamia vizuri sana, miongozo ni mingi sana iliyokuwa inatoka humu Bungeni ikihusiana na maeneo haya yenye migogoro, lakini umetusimamia vizuri sana. Tunakupongeza na tunakuahidi kwamba tutaendelea kushirikiana na Wabunge na wewe binafsi ili kuhakikisha kwamba tunaitendea haki Serikali lakini pia tunawatendea haki Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameendelea kutusimamia kutuongoza pale ambapo tunakwama ametuonyesha njia. Tuendelee kumshukuru na awe na moyo huo huo pale ambapo tunamhitaji hasa kwenye harakati hizi za kutatua migogoro. Pia, niendelee kumshukuru sana bosi wangu Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kwa namna ambavyo tunaendelea vizuri kuyaangalia haya maeneo, lakini pia kwa hatima ya zoezi hili la kupitisha haya Maazimio mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikumbuke tu na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati yetu, Makamu Mwenyekiti lakini na Waheshimiwa Wajumbe. Hawa wamekuwa nguzo, wametupa maelekezo mahususi, wametusimamia na hatimaye leo tumeingia Bungeni tukiwa kifua mbele tukitetea Maazimio hayo mawili. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na tunakiri kwamba tutaendelea kushirikiana nao na yale maelekezo yote ambayo wametupa kwenye Kamati na hata yaliyotoka kwenye ripoti yao hapa tumeyapokea na tutaendelea kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamechangia, tunawashukuru sana kwa michango yao mizuri na tunaendelea kuwaomba waendelee kutuelekeza ili tuendele kufanya kazi nzuri ili Watanzania wapate haki yao, lakini pia Serikali iendelee kuhifadhi na kulinda rasilimali za Taifa kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ningependa nitoe mchango wangu katika maeneo mawili, eneo la kwanza linahusiana na Azimio la Kushusha Hadhi Pori la Hifadhi ya Taifa Kigosi kuwa *Forest Reserve*. Kwenye Sekta yetu hii ya Maliasili na Utalii tumekuwa na mchakato mzima wa uanzishwaji wa viwanda vya uchakataji wa mazao ya misitu hususan mazao yanayotokana na nyuki. Tuna viwanda 97 nchini, lakini tuna viwanda sita katika Wilaya ya Mlele, Kibondo, Bukombe, Nzega, Sikonge na Manyoni. Hivi viwanda vipo kwa ajili ya kuchakata asali na viwanda hivi vipo kwa ajili ya kutegemea rasilimali inayotokana na mazao yanayotokana na nyuki.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kutembelea Wilaya ya Bukombe, wazalishaji wakubwa wa zao la asali na ni moja ya wilaya hizi nilizozitaja. Changamoto tuliyoikuta pale ni kwamba tulikuwa tunawaondoa wale wananchi waliomo ndani ya hifadhi, kwa sababu hifadhi hii imepanda hadhi kuwa *National Park*. Nakumbbuka nilifanya ziara na tukaomba pamoja na kuwa *nature* ya *reserve* ile imeshazuia shughuli za kibinadamu lakini uzalishaji wa mazao ya nyuki ulikuwa ni wa hali ya juu. Kwa bahati nzuri kabisa Serikali imepeleka kiwanda pale na kiwanda kinazalisha vizuri na wananchi uchumi wao umeimarika, Watanzania wanapata ajira kutokana na mazao hayo. Kwa hiyo tuliweza kuwaruhusu hawa wananchi waendelee kurina asali na kufuga nyuki, lengo lake ni kuwafanya waendelee kuzalisha mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa hadhi ya mapori haya, kutasaidia sana wananchi kuimarika kiuchumi, kimapato, lakini pia tunaamini ajira za Watanzania zitaendelea kuongezeka. Eneo hili linazungukwa na mikoa minne, Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Geita, Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Shinyanga. Kwa hiyo kushuka kwa hadhi kwa pori hili kutasaidia mikoa minne iende kufaidika na mazao ya uchakataji wa asali lakini yanayotokana pia na nyuki.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili lingine la Azimio la Ruaha pia niendelee kukushukuru, niwashakuru Wabunge kwa namna ambavyo wamelipokea vizuri. Kama ambavyo nimesema

mwanzo, eneo hili limekuwa na mgogoro wa muda wa siku nyingi, lakini niwapongeze sana Kamati ya Mawaziri nane. Tumeenda mara kadhaa kule lakini hatimaye leo tumeleta azimio Bungeni. Kuna mawazo mbalimbali yametolewa na Waheshimiwa Wabunge ikiwemo kuendelea kuwashirikisha wananchi, lakini pia wametuomba sana mipaka iweze kuonekana kwa uwazi zaidi na iwe shirikishi kwa wananchi. Tunaahidi kwamba tutaendelea kuwashirikisha wananchi, lakini pia mipaka tutaweza kuiweka kwa ufasaha kabisa ili kila mtu aone na eneo hili liweze kuhifadhiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amekubali kupunguza eneo hili kuwaachia wananchi hususan wakulima na tunaendelea kuwaomba wananchi kwamba kila ambacho kinaombwa Mheshimiwa Rais anawasikiliza na anatekeleza. Kwa hiyo tuendelee kushirikiana pamoja na Serikali tuendelee kushirikiana pamoja na Mheshimiwa Rais na tuendelee kumuunga mkono ili migogoro hii ifikie hatma na hatimaye tuweze kuendeleza rasilimali hizi tulizoachiwa na waasisi wetu kwa maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mtoa Hoja uje uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya na uzima na kutuwezesha kukutana mbele ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ridhaa yake yeye mwenyewe kuona umuhimu wa utekelezaji wa maazimio yote haya mawili na haya ndio maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio yanatoa muelekeo wa Serikali na kututaka sisi kama Serikali kuangalia maslahi ya Watanzania, hasa

Watanzania wa kawaida kabisa. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe tu kwamba michakato hii hasa ya maazimio haya haikuanza chini ya utawala au uongozi wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, yalianza na viongozi waliomtangulia na sasa ni takribani zaidi ya miaka saba, tumehangaika tumekwenda na kurudi. Sisi kama Serikali tumejitahidi katika nyakati zote kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hizi hasa za wananchi wetu hawa wa kawaida, kuwapatia maeneo ambayo watakwenda kuyatumia kwa maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, tatu, nikushukuru sana wewe na Kiti chako kwa kuendelea kutupatia miongozo mbalimbali, lazima nikiri mafanikio na leo sisi kama Serikali kuwepo hapa ni kwa sababu ya miongozo yako, jitihada zako, kuhakikisha kwamba unasimama vyema kusimamia yale yaliyoelekezwa katika Ibara ya 63 na Ibara ya 64 na mengine katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakupongeza sana kwa sababu kuna wakati kulikuwa kuna giza kidogo lakini ukasema unataka kuona mwanga. Hayo yote uliyoyafanya kwa sababu ulizingatia maslahi ya wananchi ambao wao ndio wametuweka hapa Bungeni, tunakupongeza na tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba dhamira ya Serikali yoyote, Serikali yoyote halali, dhamira ya Serikali yoyote iliyo madarakani, Serikali yoyote makini, ni ustawi wa wananchi wake, ndio dhamira ya Serikali yoyote. Serikali imepewa mamlaka yake na wananchi kwa misingi ya Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali imepewa mamlaka na wananchi kwa sababu nchi hii ni ya wananchi na wananchi wameelekezwa moja kwa moja kwa misingi ya Katiba kushiriki katika maamuzi yanayofanywa na Serikali na wananchi wanashiriki katika maamuzi ya Serikali kwa misingi iliyoainishwa katika Ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania wanashiriki kwenye maamuzi ya moja kwa moja yanayoamuliwa na Serikali. Ibara ya 21 imetoa mwongozo wa namna gani wananchi watashiriki kwenye maamuzi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaipongeza Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi, kwa sababu viongozi wa Mataifa mengine wangeweza kuamua wao wenyewe kama viongozi. Mheshimiwa Rais angeweza kuamua yeye mwenyewe, lakini akaona kwamba, Serikali ya Chama hiki ikaona kwamba ni muhimu wananchi wakashirikishwa moja kwa moja na ndio msingi ulioainishwa katika Ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanashiriki kwenye maamuzi katika mikataba, katika majadiliano, katika mambo kama haya ya kupandisha hadhi hifadhi na kuzishusha hadhi hifadhi. Ibara ya 21 imetoa maelekezo ni namna gani wananchi watashiriki kwenye maamuzi ya Serikali na namna ambavyo wananchi wanakwenda kushiriki kwenye maamuzi ya Serikali ni kupitia wawakilishi wa wananchi waliochaguliwa na wananchi wao na hao wawakilishi ndio hao tunaowazungumzia, Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wametoa maoni mengi sana katika maeneo yote haya mawili, eneo la Kigosi lakini pia eneo la Ruaha, nasi kama Serikali tumesikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Kwanza tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, katika maoni ya Waheshimiwa Wabunge, Wabunge takribani 10 wote wameunga mkono Maazimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia taarifa ya Kamati imeunga mkono Maazimio lakini nikushukuru pale ambapo ulipoagiza Kamati hasa kwenye hoja moja ya eneo la Ruaha, ukatutaka tuende tukajiridhishe, tunakushukuru sana sana kwa sababu haukutoa mwongozo tu kwa Kamati lakini ulitoa mwongozo kwa sababu unalinda maslahi ya wananchi na hiki ndicho kilichotuleta hapa Bungeni, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi na Kamati tulipata fursa ya kwenda kujionea kule Ruaha na yale ambayo hoja za Kamati kuhusu ni kwa nini Mwekezaji ameachwa na wananchi wameondolewa. Mimi nilipata fursa ya kujionea hali hii na Wajumbe wa Kamati,

tulifanya vikao kadhaa na baadae tukaenda *site* kujionea hali halisi, niliporejea niliwaambia wenzangu kwamba sisi ni wawakilishi wa wananchi lakini pia kilichofanyika pamoja na jitihada kubwa na kazi nzuri ambayo imefanywa na Waheshimiwa Mawaziri Nane waliozunguka kuhakikisha kwamba wameyaangalia maeneo yale ambayo hayana hadhi wakapendekeza yaondolewe, ni lazima tuwapongeze kwa kazi kubwa na kazi nzuri sana ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakatoa takribani hekta 74,000 kwa wananchi kule eneo la Ruaha lakini baada ya kwenda kujionea eneo lile, mimi nilishawishika pia na niliporejea nikawaambia wenzangu hapa ni lazima tufanye jambo ili kulinda maslahi ya wananchi, kwa sababu hiki ndicho ambacho wananchi wametuweka hapa kwa sababu ya kulinda maslahi yao na kama ambavyo nimesema dhamira yetu sisi Serikali ni kulinda na kuendeleza ustawi wa wananchi wetu, kwa hiyo isingelikuwa na maana yoyote ya safari yetu kule Mbarali kama tusingeliweza kuliona hili na tukaona kwamba hili changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliporejea tulifanya kikao na nimshukuru Mwenyekiti wetu nae aliridhia kwa sababu mchakato huu unapita taratibu za kisheria, taratibu za kitathmini. Sisi kama Serikali baada ya kuwa tumefanya mapitio kwa viongozi wetu tukaona kwamba ipo haja ya kuwafikiria hawa wananchi katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa michakato hii ni michakato ya kisheria, kwa kuwa michakato hii ina taratibu zake za kufanya tathmini ili tuweze kujiridhisha ni eneo gani ambalo wananchi wataweza kulitumia kwa sababu kama mwekezaji amebakizwa kwenye eneo hilo hilo ambalo tunasema ni ardhi oevu wananchi walipoondolewa, basi ili kutenda haki, mwekezaji naye alipaswa kuondoka kwenye eneo lile, lakini kama Serikali tumeridhia tunasema kwamba mwekezaji ana miundombinu ya maji kwenye eneo hili, sisi kama Serikali ni lazima tujitathmini kwamba hapa kama tumemuacha mwekezaji, ni muhimu tukalinda maslahi ya wananchi pia katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili tuliliangalia na tukasema kwamba ipo haja ya kulifanyia tathmini hili na tunafanya *commitment* mbele ya Bunge lako Tukufu kwa sababu Kamati imetuagiza na inapoagiza Kamati maana yake imeagiza Bunge kwa misingi ya Kanuni. Sisi tunaliomba Bunge lako liridhie kupitisha Azimio hili lakini tunaomba tuliahidi Bunge kwamba tutarejea hapa mwezi Septemba ili kufanya marekebisho tuwaangalie wananchi wa eneo lile la Mbarali ambao wameondolewa, katika maono ambayo mimi nimejiridhisha kabisa kwamba kulikuwepo na haja ya kufanya tathmini ya kina ni kwa nini wananchi wameondolewa kwenye eneo lile. Kwa hiyo, tunaomba tuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutarejea mwezi Septemba na kwa kuwa tumekwishampa taarifa Mheshimiwa Waziri Mkuu haja ya kufanya tathmini kuwaangalia wananchi katika eneo lile ambalo tutaleta mapendekezo iwapo Bunge litaridhia, basi eneo lile hatutalirejesha kwa wananchi kwa sababu tunajua tukilirejesha kwa wananchi watu wachache watanufaika na eneo hili. Kwa hiyo, tutalirejesha kwa Serikali pengine kupitia Mkoa au TAMISEMI au kupitia Wizara ya Kilimo ili liweke utaratibu wa kuandaa miundombinu ya maji na wananchi waweze kunufaika katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ina migogoro jumla karibu 836, na kama uliusikiliza maoni mengi ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi, wapo wengi wamekuwa na imani na mimi. Mimi ni mtu wa *field,* naomba niwathibitishie katika kipimo ambacho nitaomba Wabunge wanipime ni kwenda kumaliza migogoro hii 836. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Ndugu yangu Ole-Sendeka alikwenda nje kidogo ya hoja kuzungumza kule Jimboni kwake lakini nimpe taarifa kwamba nitafika huko Jimboni kwako. Mara nyingi huwa sipendi kuletewa taarifa mezani, ninapenda nifike kule *field* nijionee mimi mwenyewe ili pale tunapopeleka maoni au ushauri kwa Mheshimiwa Rais uwe ni ushauri ambao unakwenda kulinda maslahi ya wananchi hasa wanyonge kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo pamoja na migogoro hii 836 lakini tumeongezewa mgogoro mwingine jumla migogoro 837 wa kule Iringa kwa sababu ya simba ambao wameingia kwenye maeneo yetu tayari tumekwishapeleka *helicopter,* tumepeleka askari wetu zaidi ya 21 wapo kule wanaendelea kuwasaka wale simba, lakini migogoro hii mingine ninaomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge nitafika kila kona kuhakikisha kwamba tumetatua migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipopewa nafasi hizi tuliaminiwa na Mheshimiwa Rais lakini ukweli ni kwamba wapo Watanzania wana uwezo mkubwa huko nje pengine wangepewa nafasi hizi wangefanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, tuna jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba tunalinda na kutetea maslahi ya wananchi na hapa ndipo tunakiri kabisa kwamba kazi aliyofanya Rais wetu kurejesha maeneo haya kwa wananchi ni lazima tumpongeze na tumshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walijaribu wengi lakini Rais Dkt. Samia ameweza kurejesha maeneo haya kwa wananchi. Tulisimama hapa katika hotuba ya bajeti yetu tukaeleza Mheshimiwa Rais aliendeleza yale ambayo yalianzishwa na Rasi wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ya kwenda kufanya mapitio kwenye maeneo ya migogoro na wakati nahitimisha hotuba yangu ya bajeti tulisema, kufikia Tarehe 28 mwezi wa Sita, wale waliokasimiwa mamlaka ya kuhakikisha kwamba wanatatua migogoro kwenye maeneo yao wafanye hivyo, lakini pamoja na hilo tunatambua yako maeneo mengine bado kuna vuguvugu la migogoro. Nitafika huko ili nitakapokuja kwa wenzangu tutawashauri namna bora ya kwenda kumaliza migogoro tuliyonayo kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msingi wa hoja zetu zote mbili nimeona hapa kumekuwepo kidogo na hofu ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kukabidhi eneo la Kigosi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Misitu chini ya *TFS* chini ya Sheria Namba 323. Wahifadhi wetu tulipowapa nafasi katika maeneo yao tuliwakabidhi majukumu katika misingi ya sheria ambayo nimeitaja hapa.

Mheshimiwa Spika, *TFS* itakwenda kuandaa mpango wa usimamizi wa misitu hasa Msitu wetu huu wa Kigosi ambao tumeuzungumza. Mpango huu utaandaliwa katika kutimiza matakwa ya Sheria ya Hifadhi ya Misitu sura Namba 323. Kwa hiyo, ninaomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, *TFS* hawa ni wahifadhi lakini hawa wote ni Askari Jeshi. Kwa hiyo, jukumu lao kubwa ni kulinda hifadhi ya misitu lakini pia ikumbukwe kwamba maeneo mengi yenye vyanzo vya maji wanaolinda ni hawa wahifadhi - *TFS*. Kwa hiyo, naomba niwatoe hofu wale wote ambao walikuwa na hofu. Hili ni Jeshi kamili, wamepata mafunzo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika eneo ambalo hatutakuwa na msamaha ni wale wahifadhi ambao tumewakabidhi mamlaka ya kwenda kufanya kazi na kusimamia kwenye maeneo yao na wao wakaenda kutuangusha kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tutatoa kipindi cha maangalizo ili tumpime kila mmoja uwezo wake, kwa namna ambavyo anakwenda kutekeleza maelekezo ambayo ninyi Bunge mtatushauri katika Kikao hiki. Kwa hiyo, naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba *TFS* ni Jeshi kama lilivyo Jeshi la *TAWA*, *TFS* ni Jeshi kama lilivyo Jeshi la *TANAPA*, wanapata mafunzo sehemu moja kwa hiyo hawa ni wanajeshi na kwa marekebisho ya sheria na kimuundo ambao tumekuwa tukiendelea kuyafanya tumeendelea kuwapandisha hadhi kuwa ni Jeshi USU. Kwa hiyo niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ushirikishwaji wa wananchi tumelipokea hili, na sisi tunakiri kabisa moja ya changamoto kubwa ambayo tumeikuta kwenye Wizara hii, maamuzi mengi yalikuwa yakifanyika bila kuwashirikisha wananchi. Hili tunalikubali kabisa, nilikwishatoa maelekezo kwa Wakuu wa Hifadhi katika maeneo yote kuhakikisha kwamba wanashuka kuzungumza na wananchi na kazi hii tumekwishaianza kwa *TANAPA, TAWA* na *TFS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunapozungumza wanapita na kuzunguka katika kila Mkoa na wanavyopita katika kila Mkoa, wanakwenda kuzungumza na Viongozi wa Serikali katika kila Mkoa, Viongozi wa Chama Tawala katika kila Mkoa ili waweze kubeba maono ya wananchi kwenye maeneo yao. Tunaamini kabisa ushirikishwaji wa wananchi utatusaidia sisi kama Wizara kwenda kutatua migogoro hii ambayo nimeitaja zaidi ya 800 inayotukabili leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa hapa ni kuhusu uwekaji wa alama za mipaka. Kama ambavyo nimesema na kama ambavyo tayari tumekwisha waagiza wataalam wetu wahakikishe kwamba uwekaji wa alama za mipaka unakuwa shirikishi. Nimesema hapo awali, migogoro mingi imetengenezwa kwa sababu wananchi wengi wamekuwa hawashirikishwi kwenye maamuzi. Kwa hiyo, kwa kuwa tayari tumekwishatoa maelekezo na kwa kuwa tayari wataalam wetu wanaendelea kuhakikisha kwamba wanakwenda kuwashirikisha wananchi katika utatuzi wa migogoro kwenye maeneo mbalimbali, uwekaji wa alama za mipaka ni lazima wawashirikishe wananchi na haya tayari tumekwisha waagiza wataalam wetu, katika maeneo mengi tayari hili linaendelea kutekelezwa na niseme tu kwamba nimepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge wale ambao walikuwa na hofu na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitahakikisha katika maeneo ambapo tunaendelea kufanya tathmini ya ardhi, katika maeneo ambapo tunaendelea kufanya tathmini ya hifadhi zetu tutaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wameshirikishwa moja kwa moja. Tunapozungumza kuhusu wananchi siyo tu viongozi wawakilishi, Wabunge na Madiwani, lakini pia mpaka chini kwenye vitongoji, kwenye vijiji na wananchi wenyewe washirikishwe kwenye vikao mbalimbali ili tunapofanya maamuzi yawe ni maamuzi ambayo hayataleta hitilafu na kuturejesha hapa katika mijadala ambayo tungeliweza kuitatua mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utolewaji wa elimu. Tutaendelea kutoa elimu hasa katika maeneo ambayo tumeyarejesha kwa wananchi na kama ambavyo mwenzangu amezungumza

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri Nane amekwishalisema hilo kwamba tutaendelea kutoa elimu ili yale maeneo ambayo yamerejeshwa kwa wananchi yaweze kutumika katika minajili iliyokusudiwa na Serikali. Kwa hiyo, hili tutaendelea nalo na nikuthibitishie tu kwamba mimi na taasisi zangu zote tunaendelea kutoa elimu na kupitia *TAWA, TANAPA, TFS* tunaendelea kutoa elimu, hivi sasa wanaendelea kuzunguka kama ambavyo nimesema awali na tutaendelea kutoa mafunzo kwa askari wa vijiji ili kuendelea kuhakikisha kwamba wanatatua baadhi ya changamoto za wanyama wakali kwenye baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili kwa kuwa Bunge hili tayari limekwishatupitishia bajeti, tutakwenda kuanza kulitekeleza baada ya kuahirishwa kwa Bunge letu hili Tukufu, lakini nikuthibitishie tu kwamba yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wametuletea hapa tutakwenda kuyafanyia kazi. Naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba maeneo mengi ambayo wameshauri, pamoja na kwamba wameunga mkono kwa asilimia 100 hoja zote zilizotolewa yale mengine machache ambayo tunaamini kabisa tuna haja ya kwenda kuyafanyia kazi ili kulinda maslahi ya wananchi wetu tutakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kimsingi hoja ambazo zimekwishazungumzwa tayari nimekwishazitolea ufafanuzi wa kina kabisa ili tuweze kuhakikisha kwamba Azimio hili linakuwa na msingi lakini Maazimio haya yanakuwa ni ya kulinda maslahi ya wananchi wetu tunaowawakilisha kwenye maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya mwisho ambayo imezungumzwa hapa ni kuhusu mazoezi haya ambayo tumeyafanya hasa kwenye Hifadhi yetu ya Kigosi lakini Hifadhi yetu ya Ruaha yaweze kupita kwenye maeneo mengine. Zoezi hili halitaishia katika maeneo haya ya Ruaha na Kigosi, tutaendelea nayo. Hakuna sifa yoyote ya kuendelea kupata hasara kwenye maeneo wakati tunaweza kufanya jambo ambalo likasaidia Taifa letu. Kwa hiyo, tutaendelea kuyapitia kwenye baadhi ya maeneo kuhakikisha kwamba maeneo yetu yote yanakuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ambayo yameshauriwa na Waheshimiwa Wabunge yamekuwa na tija na sisi tunasema tu kwamba kama Serikali tutakwenda kuyafanyia kazi. Nikiri tu kwamba kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumza kuhusu eneo letu lile la Kigosi hasa kuhusu eneo la uzalishaji wa asali, nikuthibitishie kwamba sisi tumejipanga vyema kuhakikisha kwamba eneo hili tunaliandaa kwa ajili ya wafugaji wa asali na shughuli nyingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe tu kwamba leo hii Serikali inaingiza karibu takribani dola milioni 14 peke yake katika sekta hii na hicho ni kiwango cha asilimia tano tu cha asali ambayo inauzwa nje ya nchi, lakini kwa zoezi hili ambalo tumelifanya hapa hasa la eneo la Kigosi itatusaidia kama Serikali kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji wa asali kutoka tani 38,000 mpaka tani 132,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki kitaisaidia Serikali kukusanya zaidi ya dola milioni 50. Kiwango hiki kitasaidia Serikali kukusanya takribani dola milioni 50 kwa asali ambayo itauzwa nje ya nchi. Nilitaarifu tu Bunge lako Tukufu kwa eneo ambalo tutalirejesha ukanda huu ndiyo ukanda ambao kwa Afrika unaongoza kuwa na asali nzuri. Tuseme kwa Afrika ni namba mbili, ukanda huu ambao tunarejesha eneo la Kigosi, kwa hiyo, tutaongeza jitihada.

Mheshimiwa Spika, na hivi karibuni tutazindua mpango tunaouita, "Ondoa shoka kamata mzinga." Mpango huu utakwenda kuzihusisha Wilaya zote, mpango huu utakwenda kuhusisha Mikoa yote inayoguswa na Azimio hili hasa Azimio la Kigosi ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanashiriki moja kwa moja kwenye shughuli hii ili tuweze kuongeza mapato. Hatuna sababu hata kidogo ya kuwaambia Watanzania ni kwa nini leo hii mchango wetu kwenye Sekta ya Wizara ya Utalii ni asilimia 25 hasa kwenye fedha za kigeni, hatuna sababu ya kushindwa. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuongeza jitihada na mpango wa Ondoa shoka kamata mzinga utakwenda kuongeza fedha za Serikali, fedha za kigeni lakini pia utatoa mchango

kwenye Pato la Taifa ili tuweze kutoka kwenye asilimia 22 na sisi dhamira yetu tutoke asilimia 22 tuende mpaka asilimia 30 kama mchango kwenye Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, licha ya uamuzi wa Serikali wa kumega eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 478 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwenda kwa wananchi, Serikali itaendelea kufanyiakazi ushauri uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii wa kufanya tathmini ya eneo lingine linalopakana na Shamba la Kapunga kwa upande wa Kusini Mashariki ili kujiridhisha kama eneo hilo bado lina hadhi.

Mheshimiwa Spika, nami nimesema inawezekana kwamba ni vema tukaangalia maslahi ya wananchi katika eneo hili, na nilithibitishie tu Bunge lako Tukufu kwamba tayari wataalam wamekwishaanza, wako uwandani na tayari wamekwishaanza kufanya tathmini ya kiwango gani tutarejesha kwa wananchi na baada ya hapo tutarejea kwa wenzetu chini ya Mwenyekiti wetu ili kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu na kushauri mamlaka waridhie kiwango ambacho tutaona kwamba ni muhimu kukitoa kwa ajili ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ninaomba sasa kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ngoja, ili tuongozane vizuri umehitimisha hoja zote mbili kwa wakati mmoja. Sasa ili Bunge liweze kufanya maamuzi kwa maana ya wewe kutoa hoja, toa hoja moja moja. Kuhitimisha umehitimisha pamoja nilikuacha tu uendelee ili umalize hoja zako zote. Toa hoja moja moja unatoa moja unaenda zako kukaa Bunge linaulizwa lifanye maamuzi halafu utaleta hoja nyingine. Kwa hiyo, unaweza kuanza na mojawapo kati ya hizi mbili, yoyote tu ambayo iko karibu hapo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja ili Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liridhie katika Mkutano huu wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha Nne cha Sheria ya Hifadhi ya

Taifa, Sura ya 282 inayoazimia kuridhia kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi yenye ukubwa wa kilometa za mraba 4,760 kama ilivyoainishwa kwenye kiambatanisho ili iwe Hifadhi ya Misitu ya Kigosi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Sasa nitawahoji, waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana Azimio hili limepita nitayazungumzia yote mawili kwa pamoja baadaye kidogo. Nimkaribishe tena Mheshimiwa Waziri aweze kutoa hoja ya hili Azimio lingine kuhusu Ruaha.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia manufaa ambayo Serikali imekwishazungumza kuhusu Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wananchi wa maeneo husika watayapata kutokana na marekebisho yaliyopendekezwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa Sura 282, inaazimia kuridhia marekebisho ya mipaka ya eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kumega kilomita za mraba 478 kutoka kwenye hifadhi hiyo na baadaye marekebisho hayo kufanyika. Hifadhi ya Taifa ya Ruaha itakuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 19,822 kama ilivyoainishwa kwenye kiambatanisho.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha waseme ndio, wasioafiki weseme sio.

Waheshimiwa Wabunge, ambaye hajaafiki ni mmoja kwa hiyo wengine wote wameafiki nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hivi punde limehojiwa na limefanya maamuzi kuhusu kuridhia kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi. Kwa hiyo, nitangaze rasmi kwamba Bunge limepitisha Azimio la Kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi na sasa kupitia Azimio hili imeanzishwa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia muda Serikali mrefu uliopita Bunge limepitisha Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kadiri ya ramani ambayo Serikali imeileta na muktadha huo maazimio haya mawili yamepita. Kwa upande wa Ruaha mipaka itarekebishwa kwa kadiri ya hiyo ramani iliyoridhiwa na Bunge kupitia azimio hili. Pia kwa upande wa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi sasa itakuwa ni Hifadhi ya Msitu ya Kigosi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kupitisha maazimio haya kwa upande wa Kigosi Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo marefu na hayakuwa na jambo ambalo linahitaji kufanyiwa kazi. Kwa kuitazama Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii na ushauri waliokuwa wameutoa na maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyasema hapa. Ni dhahiri kwamba azimio

hili ambalo Bunge limepitisha ni kwamba Serikali inaenda kuanza kufanyia kazi sasa ile mipaka ambayo tumeiweka. Lakini sehemu ya hiyo mipaka ambayo wanaenda kuweka ni kwamba, wao ndani ya Serikali wataendelea kujipanga vizuri ili ile sehemu iliyokuwa inaleta changamoto ambayo ndio ilifanya kamati iende mpaka kule waweze kuifanyia kazi kusiwe na malalamiko kutoka kwa wananchi.

Sababu kamati imeeleza katika ukurasa wa sita na wa saba sina haja ya kurejea kwa sababu Mwenyekiti alipata nafasi ya kusoma hapa. Pia Mheshimiwa Waziri ametoa ufafanuzi mzuri sana kwamba sababu pekee ambayo ililifanya lile eneo mpaka uliguse ni kwa sababu halina miundombinu mizuri ya kilimo kwa maana ya umwagiliaji, kwa hivyo maji yanapotea na yakipotea yanaharibu sasa ile ekolojia nzima.

Sasa kwa sababu mwekezaji ambaye yuko eneo hilo hilo ameachwa kwa sababu miundombinu ni mizuri na maji yanaweza yakatumika na bado yakaenda kutengeneza ikolojia vizuri. Basi kwa maneno aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri hapa pamoja na kupitisha azimio hili Taarifa hii ya Kamati kwenye hiyo sehemu ambayo wametoa maelezo kuhusu yale malalamiko ya wananchi kuhusu mwekezaji kuachwa na wao kuambiwa kwamba wanaondoka. Kwa Azimio hili tumeazimia kwamba ile mipaka wananchi waendelee kuwa na utulivu Serikali itaweka ile mipaka lakini itatengeneza utaratibu mzuri ili eneo liwekewe miundombinu ya kilimo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa Serikali itaweka utaratibu mzuri nani aweze kulima pale na sisi wananchi wote tuweze kufaidika. Kwa hiyo, nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri na sisi kwa upande wa Bunge tumepokea shukrani zako kwa huo uongozi lakini nitumie fursa hii pamoja na kukupongeza wewe nianze safari hii tofauti kabisa na utaratibu ulivyo.

Niipongeze sana Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kuendelea kushauri Serikali, kwa kuendelea kutoa ushirikiano mzuri, lakini mmetoa uongozi mzuri mpaka

tumefika sehemu hii bila malalamiko, bila kuvutana kwa sababu na ninyi mmekuwa mkisikilizana na Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nihamie upande wa Serikali nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote kwa kusikiliza mawazo ya kamati baada ya kamati kuwasilikiliza wadau na kuonesha kwamba kuna haja ya kwenda huko na ninyi mkaona uko umuhimu huo. Maana tungeweza kubishana hapa hapa halafu mambo bado yakawa yanaenda kwa kuvutana hivi lakini mmefanya jambo zuri sana kuisikiliza kamati, kusikiliza mawazo yao ambayo yametokana na wadau na ninyi mmechukua hatua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri tunakutakia kila la heri katika kufanya marekebisho hayo ili eneo lile la Ruaha liwe na utulivu na kwa ahadi ulitoa tunaamini kwamba hakutakuwa na utulivu Ruaha pekee kutakuwa na utulivu maeneo mengine yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye eneo la Kigosi kulikuwa na michango hapa ambayo ilitolewa hasa kuhusu namna ambavyo Wabunge ambao wanatoka maeneo hayo walichangia kwa nguvu sana kuashiria kwamba eneo hili halikuwa na sifa la kupandishwa kuwa hadhi ya Hifadhi ya Taifa.

Sasa maamuzi huwa yanatokea kwa sababu mbalimbali. Pengine wakati huo sababu zilikuwepo sasa hazipo ama wakati huo pia sababu hazikuwepo na hatukuchukua hatua ambazo tumezichukua sasa. Kwa maana ya kwamba Kamati ya Bunge ilipaswa iende baada ya kuwasikia Wabunge wa maeneo hayo tusingefika pengine hatua hii ambayo imetufanya tupoteze hizo bilioni 30 katika kipindi hiki.

Waheshimiwa Wabunge, maana yake ni nini? Ushirikiano ambao Serikali sasa inautoa pale kamati inapotoa maoni yao ni wa muhimu sana kwa sababu wanapowasikiliza wadau Serikali mkienda huko mkijiridhisha basi tunaweza kufuka mahali ambapo tumefika siku ya leo.

Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwasikiliza Wabunge hasa wanaotoka hayo maeneo na kwa sababu upo uwezekano sisi Wabunge pia ni wanasiasa ukawa unataka kulifanya jambo fulani kisiasa pia kwa sababu na sisi ni wanasiasa. Serikali inao viongozi ngazi zote inao uwezo wa kupata taarifa mahususi kuhusu hayo maeneo lakini kwa lile ulilosema Mheshimiwa Waziri tunakutakia kila la heri katika kuhakikisha migogoro yote inakwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa mambo machache kwa sababu eneo hili litaendelea kufanyiwa kazi. Mheshimiwa Naibu Waziri jana utakumbuka na Waziri uko hapa na wewe jana ulikuwepo. Wabunge wengi walisimama kuhusu hoja ya Tembo na leo hapa nimeletewa ujumbe mwingine tena kwamba inaonekana bado kuna maeneo Tembo wanaendelea kwenda kwenye maeneo ya wananchi. Kwa hiyo nafikiri muongeze nguvu, muongeze kasi kwenye hayo maeneo ambayo Wabunge wameshaonesha kuna shida tusije tukapata taarifa hapa kuna mtu ameuawa kwenye hayo maeneo mtusaidie kwenye hilo eneo.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ulipewa nafasi hapa katika na wewe kuchangia na nikushukuru sana kwa mchango mzuri ulioutoa. Ila nafikiri twende mbali zaidi kama Mheshimiwa Waziri alivyopendekeza hapa kwamba ninyi nyote mshirikiane. Tunahitaji hifadhi ziwepo wakati huo huo tunahitaji ustawi wa wananchi lakini sasa wananchi tunaongezeka maeneo ya hifadhi hayaongezeki. Ni muhimu sana matumizi bora ya ardhi yakapewa kipaumbele ili wananchi wajue ni wapi pa kulima, wapi pa kufuga, wapi pa kujenga, wapi ardhi ni Serikali imeweka benki ya ardhi kwa ajili ya wawekezaji.

Waheshimiwa Wabunge, tusipofanya hivyo haya maeneo sijui kama tutamega tutamega tutamega mpaka wapi, lazima tufike mahali nchi yetu iwe imepangwa kwa namna ambayo kwa kweli hili la kupanga liko chini yako Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na TAMISEMI, kwa kushirikiana na Waziri wa Maliasili. *(Makofi)*

Hata michango wanayotoa Wabunge sio kwamba Wabunge wanataka kila eneo wapewe wananchi hapana lakini kwa kuwa maeneo yetu mengi hayajapimwa wananchi wakishaingia hapo amekaa miaka kumi mpaka kumi na tano kuja kumwondoa ni ngumu lakini ukipima mapema Serikali ifanye ulinzi wa maeneo haya yaliyopimwa halafu vijiji vifanye ulinzi wa maeneo yake katika mazingira hayo tutakuwa tumeondokana na hii changamoto ambayo inatupata sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri utakumbuka ndio maana kuna hoja kutoka kwenye kamati hii hii kwamba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tungependa kuona unaipa hii sehemu ile Tume yako Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, pesa nyingi za kutosha ili kuondokana na hii migogoro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeona niseme hayo na nashukuru Mheshimiwa Waziri yuko tayari kabisa kwa hiyo, naamini kamati yetu itafanya usimamizi mzuri sana wa haya maeneo mawili; Matumizi Bora ya Ardhi pia Serikali itafanya kwa sehemu yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Uchambuzi wa Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa iliyopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG)* kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Uchambuzi wa Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa iliyopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

## Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uchambuzi wa Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa iliyopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa hizi za kamati zinaletwa kwetu siku ya leo ni utaratibu mpya kidogo hatujazoea ni utaratibu mpya na ni utaratibu ambao tunataka kuona mzunguko wa ile taarifa inaishia wapi. nitazungumza zaidi baadaye lakini kwa sasa tuzisikilize kamati zetu zinasema nini kuhusu maazimio ya Bunge ambayo tuliyatoa mwaka 2022 Novemba, wakati tukijadili Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali. Sasa kamati zetu ziko tayari kwa ajili ya kutueleza Serikali imeshayafanyia kazi maazimio mangapi, mangapi bado sababu ni zipi tutazisikiliza kamati zetu.

Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *PAC* Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka. *(Makofi)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, yatokanayo na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi wa Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PIC)* Kuhusu Utekelezaji wa Mazimio ya Bunge, yatokanayo na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi wa Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujalia zawadi ya

uhai hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa leo hii. Aidha, ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika, kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uongozi wako mahiri, leo hii Bunge letu Tukufu kwa namna ya pekee limepata fursa adhimu ya kupokea Taarifa ya Kamati yenye maoni kuhusu hali halisi ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni muhimu na litaimarisha misingi ya uwajibikaji wa Serikali kwa Bunge na hivyo kuongeza usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Mnyororo wa uwajibikaji *(Proper accountability chain)* katika matumizi ya fedha za umma utaimarishwa kwa Bunge kuwa na utaratibu kama huu wa kufuatilia utekelezaji wa Maazimio yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katika mkutano wa Tisa wa Bunge uliofanyika kati ya tarehe 01 hadi tarehe 11 Novemba, 2022, Bunge lilipokea na kujadili Taarifa ya Kamati ya *PAC* iliyotokana na Kaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa hiyo mnamo tarehe 05 Novemba 2022, Bunge lilipitisha Maazimio mahsusi 14 na Azimio moja la ujumla. Maazimio mahsusi 14 yalihusu hoja za utekelezaji wa Taasisi mbalimbali za Serikali wakati Azimio moja la ujumla lilitaka Serikali kutekeleza mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowekwa mezani mwezi Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji. Bunge lilitoa maazimio 15 kwa Serikali kwa ajili ya utekelezaji katika maeneo yafuatayo:-

(i) Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kiasi cha shilingi trilioni 2.81;

(ii) Dosari Katika Usimamizi wa Mikataba na Athari zake katika Matumizi ya Fedha za Umma;

(iii) Hali ya Ukwasi Katika Baadhi ya Taasisi za Kimkakati za Serikali *(TPDC, TANESCO na STAMICO);*

(iv) Kaguzi Maalum za *REA*, Uhamiaji na Hombolo;

(v) Kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Sura namba 348;

(vi) Umiliki na Uendeshaji wa Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO);

(vii) Utendaji wa Kifedha wa Benki za Serikali *(TCB na TIB);*

(viii) Ubadhirifu Katika Upanuzi wa Bandari ya Tanga;

(ix) Kuharibika kwa Dawa na Kutokuwepo kwa Dawa Katika Baadhi ya Maeneo ya Kutoa Huduma za Afya;

(x) Mapitio na Tathmini ya Hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

(xi) Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake;

(xii) Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani;

(xiii) Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi;

(xiv) Usimamizi Usioridhisha wa Taarifa na Huduma Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF);* na

(xv) Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 12 Aprili, 2023 Serikali iliwasilisha kwa Katibu wa Bunge Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokanayo na Taarifa ya Kamati ya *PAC* iliyojadiliwa hapa Bungeni mwezi Novemba, 2022. Taarifa hiyo ilitoa ufafanuzi wa kina wa hali halisi ya utekelezaji wa kila Azimio la Bunge kama lilivyokuwa limepitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kufuatia hatua hiyo, Kamati ilikutana kati ya tarehe 1 Juni, 2023 hadi tarehe 05 Juni, 2023 ili kupitia na kujadili taarifa hiyo. Aidha, katika kipindi hicho Kamati ilipata fursa ya kupitia na kujadili Taarifa ya *CAG* inayohusu uhakiki wa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla utekelezaji wa maazimio ya Bunge ulikuwa umefanyika kwa hatua mbalimbali. Kwa mujibu wa Taarifa ya *CAG* ilibainika kwamba kati ya maazimio yaliyotolewa Novemba 2022 ni maazimio matatu sawa na asilimia 20 yalikuwa yametekelezwa kikamilifu, narudia ni maazimio matatu tu sawa na asilimia 20 yalikuwa yametekelezwa kikamilifu. Aidha, maazimio tisa sawa na asilimia 60 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na maazimio matatu sawa na asilimia 20 hayajatekelezwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa mapendekezo ya *CAG* kwa miaka iliyopita, taarifa ya *CAG* imebainisha kuwa kwa upande wa Serikali Kuu, kati ya mapendekezo 6,947 ya miaka iliyopita ni mapendekezo 2,380 tu (84%) yametekelezwa; mapendekezo 2,506 (36%) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo 1,104 (16%) hazikutekelezwa kabisa; mapendekezo 637 (9%) yamejirudia; na mapendekezo 320 (5%) yamepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mashirika ya Umma, kati ya mapendekezo 126 ya ripoti yake ya miaka iliyopita, mapendekezo 53 (44%) yametekelezwa; mapendekezo 63 (50%) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo tisa (7%) hayakutekelezwa kabisa; na pendekezo moja (1%) limepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla; kwa ujumla Kamati ina maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

(a) Hali ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokanayo na Taarifa za *CAG* kwa ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 bado ina changamoto za kiutekelezaji. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane maana yanawahusu sana. Mathalani, hadi uhakiki wa *CAG* unakamilika mwezi Juni, 2023, kwa Maazimio ya Bunge ya mwezi Novemba, 2022, ni asilimia 20 tu ya Maazimio ya Bunge yalikuwa yametekelezwa kikamilifu, asilimia 60 yalikuwa katika hatua za utekelezaji na asilimia 20 hayakuwa yametekelezwa kabisa. Kwa msingi huo, kunatakiwa jitihada zaidi katika kutekeleza Maazimio ya Bunge kwa upande wa Serikali.

(b) Kamati ina maoni kuwa utekelezaji wa mapendekezo ya *CAG* kwa miaka iliyopita bado haujafanyiwa kazi ipasavyo. Maoni haya yanadhihirishwa na uwepo wa mapendekezo 1,104 ambayo hayajatekelezwa kabisa katika Serikali Kuu na mapendekezo tisa ambayo hayajatekelezwa kabisa katika Mashirika ya Umma. Hivyo jitihada za makusudi lazima zichukuliwe kuongeza uwajibikaji kwa mapendekezo ya *CAG*.

(c) Aidha, Kamati ina maoni kuwa kumekuwepo na mapungufu katika mfumo uliopo ndani ya Taasisi za Serikali zinazohusika na utaratibu mzima wa uratibu, ukusanyaji na utekelezaji wa Hoja na maazimio ya Bunge. Mapungufu haya yanaathiri utekelezaji wa Hoja na Maazimio ya Bunge kwa hali ya juu sana;

(d) Aidha, Kamati ina maoni kuwa baadhi ya Maafisa Masuuli hawawajibiki ipasavyo katika kutekeleza Masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, kwa mfano Dhahiri, ikiwa ni kuchelewa kuwasilisha nyaraka na vielelezo mbalimbali kwa *CAG* ili vifanyiwe uhakiki. Kwa mfano, kwa uhakiki wa *CAG* uliofanyika katika Taarifa hii, nyaraka ziliwasilishwa kwa *CAG*

tarehe 25 Mei, 2023, lakini vielelezo vyake vikawasilishwa tarehe 29 Mei, 2023. Hivyo *CAG* hakupata muda wa kutosha kuhakiki nyaraka na vielelezo, hivyo kuathiri kazi ya kupitia nyaraka hizo;

(e) Kamati ina maoni kwamba ni muda muafaka kwa Bunge hili nasisitiza, Kamati ina maoni kwamba ni muda muafaka kwa Bunge kuangalia uwezekano wa kuboresha sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia Maafisa Masuuli kujibu na kutekeleza hoja za *CAG* na Maazimio ya Bunge. Jambo hili lifanyike kwa kuweka muda mahsusi *(Time frame),* ambao utatakiwa kuzingatiwa na kila Afisa Masuuli katika kujibu hoja za *CAG* na Maazimio ya Bunge; na

(f) Kamati ina maoni kwamba ni muda muafaka kuboresha sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma hasa katika eneo la adhabu *(sanctions)*. Ni jambo la muhimu kuweka adhabu mahsusi kwa Maafisa Masuuli wanaoshindwa kutekeleza Maazimio ya Bunge kwa wakati na wale wanaoshindwa kutekeleza mapendekezo ya *CAG* bila ya kuwa na sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, maoni mahsusi. Baada ya kutoa maoni hayo ya ujumla, naomba kuwasilisha maoni mahsusi ya Kamati kwa kuzingatia hali halisi ya utekelezaji wa kila Maazimio ya Bunge ya Mwezi Novemba, 2022 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa baadhi ya Maazimio ya Bunge yametekelezwa kikamilifu mathalani Kamati imeridhishwa hali halisi ya utekelezaji uliofanywa na Serikali katika maazimio yafuatayo:-

(a) Kuongeza mtaji kwa Mashirika ya Kimkakati ya Serikali ya *TPDC* na *TANESCO;*

(b) Kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu kwa Watumishi wa Chuo cha Hombolo waliobainika kujihusisha na ubadhirifu wa fedha za umma;

(c) Kuifungia Kampuni ya Amandi *Holding Limited* kutokujihusisha na shughuli zozote hapa nchini baada ya kubainika kushindwa kusimika mifumo ya TEHAMA katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* wakati ikiwa amelipwa fedha nyingi za umma; na *(Makofi)*

(d) Kukamilisha ukaguzi maalum wa Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ina maoni kuwa baadhi ya Maazimio ya Bunge yapo katika hatua za utekelezaji. Hivyo jitihada zifanyike ili kukamilisha utekelezaji wake, maazimio hayo ambayo yapo katika hatua za utekelezaji kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

(a) Kukamilisha mapitio ya mfumo mzima wa kodi hapa nchini ili kuondoa changamoto zilizopo; *(Makofi)*

(b) Kuongeza mtaji wa Benki za Serikali *(TIB* na *TCB)* ili zikidhi masharti ya Benki Kuu;

(c) Kuanza ukaguzi maalum wa *DART* na Shirika la Masoko Kariakoo;

(d) Kuanza mchakato wa Utungaji wa Sheria ya Viwanja vya Ndege ili kurejesha shughuli za uendeshaji wa *KADCO* chini ya *TAA;*

(e) Kuweka mikakati ya kudhibiti uharibifu wa dawa katika *MSD;*

(g) Kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani katika *NHIF* ili kuepuka ubadhirifu na udanganyifu;

(h) Kulipa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inayoidai Serikali;

(i) Kukamilika kwa Kaguzi za Kiuchunguzi zilizofanywa na *PPRA* kwa Mashirika ya *TANESCO* na *TPA;* na

(j) Kuendelea kutekeleza mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Tume ya Madini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati ina maoni kuwa baadhi ya Maazimio ya Bunge hayajatekelezwa kabisa hivyo ni muhimu Serikali ikayatekeleza kama Bunge lilivyoagiza ili kuimarisha hali ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Haiwezekani mhimili kama huu wa Bunge unatoa maagizo au maazimio halafu watendaji wanayapuuzia, hii inashusha hadhi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo inatakiwa kwamba watendaji wa Serikali na Mashirika ya Umma hakika wanatakiwa wajiongeze. Maazimio hayo ambayo yalitekelezwa kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:-

(a) Kufanya uchunguzi ili kubaini uhalali wa riba zinazotokana na kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi wa miradi ya ujenzi wa Barabara;

(b) Kufanya uchunguzi wa baadhi ya Watumishi wa *TRA* kuhusiana na makadirio yasiyokuwa sahihi ya kodi; na *(Makofi)*

(c) Kuchukua hatua za kisheria kwa Watumishi wa *TPA* na Kampuni ya China *Harbor Engineering Company Limited* iliyohusika na ubadhirifu katika zabuni ya upanuzi wa Bandari ya Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, shukrani; napenda kutumia fursa hii tena kwa mara nyingine kukushukuru wewe binafsi pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wako makini na thabiti ambao unaliwezesha Bunge letu Tukufu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ambapo kwa muda wote umekuwa ukitupa ushirikiano na miongozo thabiti kila inapohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nikushukuru na kukupongeza kwa mara nyingine kwa kuliwezesha Bunge

kufuatilia utekelezaji wa maazimio yanayokuwa yamepitishwa hapa Bungeni. Bunge lako litakuwa limeshuhudia jinsi ambavyo ni maazimio machache sana asilimia 20 tu ambayo yamefanyiwa kazi. Kwa hiyo najua utatoa mwongozo kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali na kipekee namshukuru Makamu wangu Mwenyekiti Mheshimiwa Japhet Hasunga kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya Kamati ili kwa ufanisi wa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba majina yote ya Waheshimiwa Wajumbe wa *PAC* yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Sekretarieti ya Bunge chini ya Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa ushauri na uongozi wake kwa Kamati, Sekretarieti ya Bunge imefanikisha shughuli za uratibu, ushauri wa kitaalam na masuala ya kiutawala kwa shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa uliopata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(NAOT)* kwa kuwasilisha Taarifa za Ukaguzi wa Mafungu mbalimbali kwa wakati. Aidha, naishukuru Wizara ya Fedha na Mipango na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho japo siyo kwa umuhimu, natoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge kwa kuratibu mchakato mzima wa kukusanya majibu ya utekelezaji ya maazimio ya Bunge kutoka katika Wizara, Idara, Wakala, Taasisi mbalimbali na Mashirika ya Umma. Zoezi hilo la uratibu pamoja na kuwa na changamoto kadhaa limeiwezesha Kamati yangu kukamilisha uundaji na uwasilishaji wa taarifa hii ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, wasilisho; nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, naomba kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali, kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa iliyopita ya CAG kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YATOKANAYO NA TAARIFA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA UKAGUZI WA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujalia zawadi ya uhai hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa leo hii. Aidha, ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa mafanikio makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uongozi wako mahiri, leo hii Bunge letu Tukufu kwa namna ya pekee limepata fursa hii adhimu ya kupokea na kujadili Taarifa ya Kamati yenye maoni kuhusu hali halisi ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Jambo hili ni muhimu na litaimarisha misingi ya uwajibikaji wa Serikali kwa Bunge na hivyo kuongeza kasi ya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.Mnyororo bora wa uwajibikaji (Proper accountability chain) katika matumizi ya fedha za umma

utaimarishwa kwa Bunge kuwa na utaratibu kama huu wa kufuatilia utekelezaji wa Maazimio yake.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mkutano wa tisa (9) wa Bunge uliofanyika kati ya tarehe 01 hadi tarehe 11 Novemba,2022, Bunge lilipokea na kujadili Taarifa za Kamati tatu (3) za Bunge zilizotokana na Kaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 na Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu Uwekezaji wa Umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati hizo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC).

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya tarehe 02 – 05 Novemba, 2022, Bunge lilijadili Hoja za Kamati hizo tatu (3) za Kudumu za Bunge zilizowasilisha Taarifa zake hapa Bungeni.Kufuatia hatua hiyo,mnamo tarehe 05 Novemba, 2022, Bunge lilipitisha Maazimio yaliyotokana na Taarifa za Kamati hizo kwa kuzingatia mjadala na hoja mahsusi za kila Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Kamati ya PAC, Bunge lilipitisha jumla ya Maazimio mahsusi 14 na Azimio 1 la ujumla.Maazimio mahsusi 14 yalihusu hoja za utekelezaji kwa Taasisi mbalimbali za Serikali wakati Azimio 1 la ujumla lilitaka Serikali kutekeleza mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowekwa mezani mwezi Aprili, 2022.

**1.2 Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Majukumu hayo ni:-

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na mashirika ya umma

yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa wizara za Serikali na mashirika ya umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyofafanuliwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**1.3 Miongozo Iliyotumika na Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu yake**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya rejea ya kina katika nyaraka zifuatazo:-

a) Taarifa ya Kamati ya PAC iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Novemba, 2022;

b) Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2020/21);

c) Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio Bunge yaliyotolewa Mwezi Novemba,2022;

d) Taarifa ya CAG kuhusu Uhakiki wa Majibu ya Serikali kwa Taarifa ya PAC iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Novemba, 2022;

e) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia mbinu zifuatazo:-

a) Kupokea, kuchambua na kujadili maelezo mafupi "briefs" ya Sekretarieti kuhusu Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Novemba,2022;

b) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Maazimio husika ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Mwezi Novemba,2022;

c) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya CAG kuhusu utekelezaji wa Maazimio husika ya Bunge; na

d) Kuandaa taarifa ya Kamati yenye Maoni kuhusu hali halisi ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**1.4 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi tunachokitolea taarifa, shughuli ya msingi ya Kamati ilikusudia kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokanayo na Taarifa za Mdhbiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa hapa Bungeni mwezi Novemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji wa utekelezaji uliofanywa na Kamati umehusisha jumla ya Maazimio mahsusi 14 na Azimio 1 la ujumla . Maazimio 14 ambayo yamefanyiwa tathmini na ufuatiliaji yamegawanyika katika vipengele kadhaa. Kwa lengo la kuweka bayana hali halisi ya utekelezaji wa Maazimio husika, kila Azimio katika kila kipengele limefanyiwa tathmini yake pekee.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya kina ya uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge imechambuliwa katika sehemu ya 2 ya taarifa hii na maoni ya Kamati kwa Maazimio ambayo utekelezaji wake haujakamilika yamefafanuliwa katika sehemu ya 3 ya taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### 2.1 Maelezo ya Jumla Kuhusu Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuweka msingi madhubuti wa uchambuzi na mjadala wa hoja ya Kamati, napenda kulikumbusha na kulipitisha Bunge lako Tukufu katika chimbuko la hoja hii, kwa kufanya uchambuzi wa kina wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,ambazo ndio zilikuwa msingi wa kufikiwa kwa Maazimio ya Bunge mapema Mwezi Novemba, 2022. Baada ya uchambuzi wa kina wa kila Azimio na msingi wake, Kamati imepitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kama ilivyowasilishwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya mapitio na uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji ya Serikali, Kamati pia ilipata fursa ya kupokea na kujadili maoni ya CAG kuhusu utekelezaji wa kila Azimio la Bunge. Hivyo basi, maoni ya Kamati yaliyochambuliwa kwa kina katika sehemu ya tatu ya taarifa hii yamefikiwa baada ya mapitio na uchambuzi kama ulivyofafanuliwa hapo awali.

### 2.2 MAAZIMIO YA BUNGE YATOKANAYO NA TAARIFA ZA CAG KWA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** Ili kulipa Bunge lako Tukufu mwendelezo wa ufuatiliaji wa Maazimio ya Bunge yaliyofikiwa Mwezi Novemba, 2022 napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu Maazimio hayo. Sambamba na hilo, Taarifa hii inatanabaisha kwa Bunge lako Tukufu hoja za msingi zilizopelekea kufikiwa kwa Maazimio husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia mjadala wa taarifa ya Kamati kukamilika na baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhitimisha Hoja yake, Bunge lilipitisha Maazimio yafuatayo: -

### 2.2.1 Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kiasi cha Sh. Trilioni 2.81

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilibainisha nakisi ya kiasi cha **Sh. Trilioni 2.81** cha mapato ambayo hayakukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na mapungufu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na dosari hiyo ambayo ilisababisha TRA kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato, Bunge liliazimia kwamba:-

a) Serikali ifanye mapitio ya kina ya mfumo mzima wa ukusanyaji kodi (Comprehensive tax regime review) ili kuhakikisha kodi zote zinakusanywa kama ambavyo Bunge linakuwa limeidhinisha hapa Bungeni; na

b) Serikali ifanye uchunguzi na kuchukua hatua stahiki kwa Watumishi wote wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) waliohusika kwa kukadiria kodi chini ya kiwango, kutoshughulikia madeni ya kodi kwa wakati, kuchelewa kusajili mapingamizi ya kodi kwa wakati, kutosimamia ushuru wa forodha kwenye bidhaa za mafuta na magari pamoja na usimamizi usioridhisha wa matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD) hali iliyosababisha ongezeko la madeni ya kodi kwa zaidi ya 95% ndani ya mwaka 1 wa fedha hivyo kuikosesha Serikali mapato ya kuhudumia wananchi.

### 2.2.2 Dosari Katika Usimamizi wa Mikataba na Athari Zake katika Matumizi ya Fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kupitia taarifa za ukaguzi wa hesabu wa mafungu mbalimbali, ilibainisha mapungufu katika uingiaji na usimamizi wa mikataba kwa baadhi ya taasisi za Serikali hali inayosabisha hasara kwa Serikali ikiwamo **Sh. Bilioni 68.7** kwa TANROADS, TANESCO **Dola za Marekani Milioni 153.43** na NFRA Dola za **Marekani Milioni 33.4** na TPA **Bilioni 137.38**.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mapungufu hayo, Bunge liliazimia kwamba:-

a) Serikali ifanye uchunguzi ili kubaini iwapo riba zilizotokana na mikataba ya ujenzi wa barabara katika TANROADS zilikuwa na uhalali na ulazima wa kuwepo. Hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi huo;

b) Serikali ichukue hatua stahiki kwa Watumishi wa Wizara ya Nishati, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango na TANESCO walioshiriki katika mchakato mzima wa uingiaji, usimamizi, utekelezaji na uvunjaji wa mkataba kati ya TANESCO na Symbion; na

c) Serikali ichukue hatua stahiki za kisheria kwa mkandarasi aliyechelewesha kukamilika ujenzi wa gati la kuegeshea meli katika bandari ya Mtwara.

**2.2.3 Hali ya Ukwasi Katika Baadhi ya Taasisi za Kimkakati za Serikali (TPDC, TANESCO na STAMICO)**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG ilibainisha changamoto za mtaji katika mashirika ya umma ya kimkakati kama Shirika la Taifa la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Taifa la Madini (STAMICO).

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hoja tajwa hapo juu, Bunge liliazimia kwamba, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, iongeze mtaji katika mashirika ya mkakati ya Serikali kwa kufanya marekebisho ya msingi katika madeni ya Taasisi hizo ili kuyageuza kuwa mtaji (Equity). Pamoja na hatua hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ahakikishe matumizi ya fedha na mikataba inayoingiwa na TANESCO, TPDC na STAMICO inakuwa na maslahi makubwa kwa Taifa.

**2.2.4 Kaguzi Maalumu za REA, Uhamiaji na Hombolo**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 zilibainisha

mambo muhimu katika kaguzi maalumu 4 zilizopitiwa na kuchambuliwa na Kamati ambazo zilibainisha mapungufu katika usimamizi wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia matokeo ya Kaguzi hizo za ufanisi, Bunge liliazimia kwamba:-

a) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa mkandarasi kampuni ya DERM Electrics (T) Limited kwa udanganyifu na ubadhirifu, pamoja na hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wa REA na TANESCO waliohusika kusimamia mradi wa REA awamu ya Pili Mkoa wa Mara kwa kutotimiza majukumu yao ipasavyo;

b) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi 32 wa Idara ya Uhamiaji waliotajwa kuhusika katika mauzo ya stika viza bandia katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA) kwa kuzingatia uhusika wa kila 1 na matokeo ya ukaguzi maalumu; na

c) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi 2 waliobainika kujihusisha na ubadhirifu wa fedha za ada za wanafunzi katika chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo.

**2.2.5 Kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Sura, 348.**

**Mheshimiwa Spika**, Kupitia Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ilibaini ukiukwaji wa Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 hivyo kuchangia upotevu wa fedha za Serikali katika baadhi ya taasisi za umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na dosari hizo, Bunge liliazimia hoja mahsusi kama ifuatavyo:-

**a) Shirika la Masoko Kariakoo**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, afanye ukaguzi wa kiuchunguzi (Forensic audit) wa Shirika la Masoko Kariakoo ili kubaini iwapo kuna ubadhirifu wa fedha za umma uliofanyika na kufichwa baada ya soko hilo kuungua moto. Aidha, vyombo vya

Dola vianze uchunguzi wa uliokuwa uongozi wa Soko la Kariakoo kubaini iwapo walihusika na jinai katika kuficha nyaraka za fedha kwa wakaguzi.

**b) Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aombwe kufanya ukaguzi maalumu (Special audit) wa malipo ya fidia kiasi cha **Sh. Bilioni 1.0** na malipo ya fedha za usumbufu kiasi cha **Sh. Milioni 434** yaliyofanyika DART ili kubaini iwapo yalifanyika kwa mujibu wa Sheria.

**c) Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi – Fungu 28**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye ukaguzi maalumu (Special audit) wa matumizi yote ya mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi tangu ulipoanzishwa na kisha kutoa taarifa yake kwa Bunge mapema iwezekanavyo. Aidha, Mlipaji Mkuu wa Serikali aandae Kanuni za kusimamia uendeshaji wa mfuko huo na malipo yote kutoka kwenye mfuko yafanyike kwa kuzingatia kanuni zilizoandaliwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

**2.2.6 Umiliki na Uendeshaji wa Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO).**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi ya CAG kuhusu KADCO ilibainisha kuwa, Mkataba wa uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro kati ya Serikali na Kampuni ya KADCO (Concession agreement) unakosa misingi ya kisheria ya kuendelea kuwepo kwake tangu mwaka 2010 wakati ambapo Serikali ilinunua hisa 100% za KADCO baada ya malipo ya fedha za umma **Dola za Marekani Milioni 5.3**.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuweka uwajibikaji wa rasilimali za umma katika KADCO, Bunge liliazimia kwamba, Serikali irejeshe shughuli zote za uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kama ambavyo inafanyika kwa viwanja vingine vya ndege hapa nchini, kwa kuzingatia majukumu ya kisheria ya TAA na uamuzi

wa Serikali uliokuwa umetolewa hapo awali. Aidha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina (Comprehensive audit) wa mapato na matumizi ya KADCO kuanzia mwaka 2010 baada ya kuanza kumilikiwa kwa 100% na Serikali hadi sasa na Bunge lijulishwe ipasavyo.

**2.2.7 Utendaji wa Kifedha wa Benki za Serikali (TCB na TIB).**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG ilibainisha kutokuwepo kwa mtaji wa kutosha kwa benki za Serikali za TIB na TCB hivyo kukwamisha shughuli za Benki husika na kuhatarisha fedha za umma zilizowekezwa katika Benki hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia kwamba, TCB na TIB zikusanye mikopo yote ambayo haijakusanywa kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na kutaifisha mali za dhamana zilizowekwa na wakopaji husika kwa mujibu wa Sheria ili kurejesha mtaji wa benki kama inavyotakiwa kisheria. Aidha, vyombo vya dola vifanye uchunguzi wa mikopo yote chechefu iliyotolewa katika TCB na TIB ili kubaini iwapo ilitolewa kwa kuzingatia taratibu za kibenki na kuchukua hatua dhidi ya watu wote waliohusika kupata mikopo kinyume cha sheria.

**2.2.8 Ubadhirifu Katika Upanuzi wa Bandari ya Tanga.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) 14 Juni 2021 aliomba kufanyika ukaguzi wa kiuchunguzi na kuainisha tuhuma za ubadhirifu wa fedha na matumizi mabaya ya madaraka uliofanywa na watumishi wa TPA katika utoaji wa tuzo ya zabuni za uboreshaji wa Bandari ya Tanga kwa Kampuni ya China Harbour Engineering Company (CHEC) Ltd, na kwamba ukaguzi huo ulikamilika na kubaini ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma takribani **Sh. Bilioni 64.30** ambayo ni hasara kwa Serikali. Na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 81 (a) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU alipewa matokeo ya ukaguzi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hoja hiyo, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ichukue hatua za kisheria kwa makampuni na watumishi wote wa TPA waliotajwa katika taarifa ya ukaguzi maalumu kwa kuhusika kwao katika ubadhirifu wa fedha za umma wakati wa utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa bandari ya Tanga.

**2.2.9 Kuharibika kwa Dawa na Kutokuwepo kwa Dawa Katika Baadhi ya Maeneo ya Kutoa Huduma za Afya.**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Bohari ya Dawa (MSD) ilibainisha uwepo wa dawa zenye thamani ya **Sh. Bilioni 23.04** zilizokwisha muda wake zinazotakiwa kuharibiwa. Pamoja na hilo ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa dawa kwa baadhi ya maeneo ya kutolea huduma za afya wakati ambapo kuna dawa zilizomaliza muda wake wa matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuondokana na dosari hiyo, Bunge liliazimia kwamba, Bohari ya Dawa wasitoe dawa, vitendanishi au chanjo ambazo muda wake wa matumizi upo chini ya miezi 6 ya kutumika (Shelf life). Aidha, Serikali isipokee dawa, vitendanishi au chanjo za msaada ambazo pia muda wake wa matumizi upo chini ya miezi 6. Na MSD ipeleke dawa kwa wateja ndani ya siku 30 baada ya kupokea malipo ya wateja bila kuchelewa. Na iwapo MSD haina dawa hizo, wazifahamishe taasisi husika ndani ya muda wa saa 24.

**2.2.10 Mapitio na Tathmini ya Hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa ya CAG ulibainisha kupungua uwezo wa mfuko wa PSSSF kulipa mafao yake pamoja uwepo wa deni ambalo mifuko ya PSSSF na NSSF inadai kwa Serikali takribani **Sh. Trilioni 1.5**.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutatua changamoto hiyo, Bunge liliazimia kwamba, Serikali iwasilishe Bungeni mpango wa malipo ya mikopo ya mifuko ya hifadhi ya jamii (Loan repayment schedule) kwa madeni yote ambayo mifuko inadai Serikalini.

Mpango huo wa malipo uwasilishwe Bungeni kabla ya kukamilika mwaka wa fedha 2022/2023.

**2.2.11 Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake.**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG ilibainisha kuwa baadhi ya taasisi za umma zimekiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ifanye ukaguzi wa kiuchunguzi katika ununuzi wenye dosari uliofafanuliwa na Kamati katika Taasisi za TANESCO na Fungu – 57 Wizara ya Ulinzi na kisha kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi. Aidha TAKUKURU ianzishe uchunguzi kwa wahusika waliofanya manunuzi bila ya kuzingatia sheria katika taasisi hizo na kuchukua hatua stahiki.

**2.2.12 Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani.**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za CAG katika mafungu mbalimbali zilibainisha mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani hivyo kupelekea upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuimarisha udhibiti wa fedha za umma, Bunge liliazimia kwamba:-

a) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa Watendaji na kampuni zilizohusika na ununuzi na usimikaji wa mifumo ambayo imeshindwa kufanya kazi kwa ufanisi katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Aidha, Kampuni hizo zifungiwe na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi Serikalini (PPRA) kujihusisha na shughuli za usimikaji mifumo hapa nchini; na

b) Bodi ya SUMA – JKT ichukue hatua za kinidhamu na kisheria kwa Watendaji waliokuwa wakisimamia mradi wa mauzo ya matrekta kwa kuruhusu uuzaji wa matrekta bila mikataba ya mauzo.

### 2.2.13 Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa 4 za ukaguzi wa ufanisi zilibainisha masuala kadhaa katika taasisi za Serikali yanayohusu dosari katika usimamizi wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuondoa matumizi mabaya ya fedha za umma katika taasisi husika, Bunge liliazimia kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina (Comprehensive Audit) katika mchakato mzima wa ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB). Aidha, Katika kipindi cha kila miezi 3 Serikali ihakikishe inawasilisha Bungeni taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi yaliyotolewa na CAG kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Tume ya Madini, TANROADS na BRELA.

### 2.2.14 Usimamizi Usioridhisha wa Taarifa na Huduma Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG ilibainisha dosari katika usimamizi na udhibiti wa taarifa muhimu za wanufaika wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na gharama za matibabu ambapo pamoja na mambo mengine ilibainika utolewaji wa huduma za uzazi kwa upasuaji kwa wanaume 731. Aidha, ukaguzi ulibaini NHIF kukataa kulipa malipo ya **Sh. Bilioni 3.18** kwa hospitali za Serikali zilizotoa huduma kutokana na kuwa na mfumo wenye mapungufu wa utambuzi na usimamizi wa taarifa.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuondoa matumizi mabaya ya fedha za umma katika mfuko wa NHIF, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ifanye uchunguzi wa Idara ya usimamizi na udhibiti wa huduma katika NHIF ili kubaini iwapo inatekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, uchunguzi ufanyike kubaini watoa huduma ambao wamekuwa wakiihujumu NHIF kwa kuongeza gharama za matibabu kwa njia za udanganyifu na kisha kuchukua hatua stahiki.

**2.2.15 Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Mashirika ya Umma.**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia kwamba Mapendekezo yote yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kujumuishwa kwenye Taarifa zake zilizowekwa mezani mapema mwezi Aprili,2022 yatekelezwe ikiwa ni sehemu ya Maazimio haya ya Bunge.

**2.3 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA SERIKALI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YATOKANAYO NA TAARIFA ZA CAG KWA UKAGUZI WA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 12 Aprili, 2023, Serikali iliwasilisha kwa Katibu wa Bunge Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokanayo na Taarifa ya Kamati ya PAC iliyojadiliwa hapa Bungeni mwezi Novemba, 2022. Taarifa hiyo ilitoa ufafanuzi wa kina wa hali halisi ya utekelezaji wa kila Azimio la Bunge kama lilivyokuwa limepitishwa na Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia hatua hiyo, Kamati ilikutana kati ya tarehe 01 Juni, 2023 na tarehe 05 Juni, 2023 ili kupitia na kujadili taarifa hiyo. Aidha, katika kipindi hicho Kamati ilipata fursa ya kupitia na kujadili Taarifa ya CAG kuhusu uhakiki wa majibu ya Serikali. Hivyo napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokanayo na Taarifa ya PAC iliyowasilishwa Bungeni mwezi Novemba, 2022 ni kama ifuatavyo: -

***2.3.1 Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kiasi cha Sh. Trilioni 2.81***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Azimio la Bunge linalohusu nakisi ya makusanyo ya **Sh. Trilioni 2.81** katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imebainisha hatua kadhaa za utekelezaji kama ifuatavyo:-

a) Kwanza, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliunda Tume ya kutathmini na kutoa mapendekezo ya kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali ambapo baadhi ya mapendekezo yameanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/23. Aidha, Serikali inaendelea kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Tume hiyo ikiwemo yale ya muda wa kati na mrefu; na

b) Pili, Serikali inaendelea kufanya uchunguzi ili kujiridhisha na taarifa ya CAG kuhusiana na kiasi cha fedha ambacho hakijakusanywa na TRA ili hatimaye iweze kuchukua hatua stahiki kwa watumishi waliohusika kwa mujibu wa Sheria.

***2.3.2 Dosari Katika Usimamizi wa Mikataba na Athari zake katika Matumizi ya Fedha za Umma***

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji ya Serikali, katika Azimio hili ufafanuzi uliotolewa kuhusiana na dosari katika usimamizi wa mikataba ni kama ifuatavyo:-

a) Riba zinazolipwa katika miradi ya maendeleo zinatokana na kuchelewa kufanyika malipo baada ya Hati za Malipo kuidhinishwa na wasimamizi wa miradi. Hii inatokana na uchelewaji unatokana na kusubiri mgao wa fedha kutoka Serikali Kuu na mchakato unaohitajika ili kukamilisha taratibu za taasisi inayotekeleza mradi na Wizara mama na baadaye Wizara ya Fedha na Mipango na sababu nyingine ni taratibu za kuhuisha mikataba kuchukua muda mrefu.

b) Aidha, Taarifa imeendelea kubainisha kwamba, Serikali inaendelea kufuatilia utekelezaji wa usimamizi wa miradi ya maendeleo ili kubaini na kujiridhisha na thamani ya fedha kwa kila mradi unaotekelezwa. Mikataba ya ujenzi inabainisha muda ambao madai ya Wakandarasi na Washauri Elekezi yanapaswa kulipwa, na vipengele vya mikataba vinaelekeza riba inayopaswa kulipwa endapo malipo yanachelewa kufanyika;

c) Serikali itafanya uchunguzi ili kubaini endapo katika mikataba tajwa mbali na sababu zilizotajwa hapo juu, kuna

ucheleweshaji wa makusudi wa kufanya malipo na hatua stahiki zitachukuliwa kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi huo utakaojumuisha ucheleweshaji wa ujenzi wa gati la kuegeshea meli katika Bandari ya Mtwara. Kwa upande wa Mkataba kati ya Symbion na TANESCO, uhakiki umebaini kwamba hakuna Sheria au taratibu zilizokiukwa wakati wa uingiaji, usimamizi na uvunjaji wa mkataba huo; na

d) Mradi wa kuongeza gati moja lenye urefu wa mita 300 katika Bandari ya Mtwara, ulitekelezwa kupitia Mkandarasi M/S JV of China Railway Construction Engineering Group (CRCEG) and China Railway Major Bridge Engineering Group Co. Ltd (CRMBEG). Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 4 Machi, 2017 na ulikamilika tarehe 31 Desemba, 2020 baada ya kuwa umeongezewa muda wa miezi 17 kutokana na changamoto za udongo hafifu na UVIKO-19 vilivyoathiri kazi za ujenzi kuendelea na hivyo kulazimika kuongeza muda wa kukamilisha kazi za ujenzi wake.

Vilevile Taarifa ya Serikali imebainisha kuwa, Gati hilo kwa sasa lipo kwenye muda wa matazamio ya kiufundi (Defect Liabilibity Period) tangu tarehe 31 Desemba 2020 hadi tarehe 31 Desemba, 2023. Kutokana na ucheleweshaji wa ukamilishaji wa kazi zilizokubalika kimkataba, TPA ilichukua hatua ya kuzuia **Shilingi 6,390,964,743.70** (Kati ya jumla ya **Shilingi 15,780,159,851.99** kilichosababishwa na ucheleweshaji wa Mkandarasi) kutoka kwenye malipo ya mwisho ya Mkandarasi kama "Delay Damages".

Hata hivyo, baada ya kukatwa gharama hizo, Mkandarasi hakuridhika na aliamua kuwasilisha mgogoro kwa ajili ya usuluhishi (Adjudication) kwenye Baraza la Ujenzi la Taifa (National Construction Council - NCC). Mgogoro huo, uliwasilishwa tarehe 20 Desemba, 2021 na TPA kuwasilisha majibu ya hoja za mgogoro huo tarehe 8 Februari, 2022 na usuluhishi unaendelea chini ya NCC. Hata hivyo, baada ya kuona kuwa suala hilo limechukua muda mrefu NCC, Wakili wa Serikali (Solicitor General) ameamua kuchukua suala hili kwa kushirikiana na TPA ili kufanya majadiliano (negotiations) na Mkandarasi nje

ya NCC kwa lengo la kufupisha muda wa usuluhishi na gharama kwa Serikali. Kwa sasa, gati hilo linatumika kwa shughuli za kuhudumia meli na shehena kama lilivyokusudiwa.

### *2.3.3 Hali ya Ukwasi Katika Baadhi ya Taasisi za Kimkakati za Serikali (TPDC, TANESCO na STAMICO)*

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha hali ya kifedha ya mashirika ya TANESCO na TPDC, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kubadili madeni ya TANESCO na ya TPDC kuwa mtaji wa Serikali katika mashirika hayo. Mathalan, Mwezi Septemba, 2022 Serikali iliridhia mapendekezo ya kubadili madeni yake kwa TANESCO yanayofikia kiasi cha **Shilingi trilioni 2.4** kuwa mtaji wa Shirika hilo na pia kubadili mkopo wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba na Mitambo ya Kuchakata Gesi Asilia kiasi cha **Dola za Marekani 1,193,611,687.49** kuwa mtaji wa Serikali kwa TPDC. Baada ya maamuzi hayo kutolewa, kwa sasa Serikali kupitia Hazina inaendelea na taratibu za ubadilishaji wa madeni hayo ili kuwa mitaji kwa Taasisi hizo mbili ambapo taratibu hizo zinatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali imeendelea kufafanua kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Nishati imejipanga kimkakati katika kuhakikisha kuwa mikataba yote inayoingiwa na Taasisi zilizopo chini ya Wizara zikiwemo TANESCO na TPDC inazingatia maslahi mapana ya nchi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa kunakuwepo na thamani ya fedha inayokusudiwa katika utekelezaji wa mikataba hiyo. Ili kuhakikisha kwamba suala hilo linatekelezwa, mikataba yote inayoingiwa na taasisi hizo ni lazima ipate maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

### *2.3.4 Kaguzi Maalumu za REA, Uhamiaji na Hombolo*

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Azimio la Bunge katika Kaguzi Maalumu zilizotajwa hapo juu umegawanyika katika sehemu tatu (3) mahsusi kama ifuatavyo:-

#### a) Ukaguzi Maalumu wa REA

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ukaguzi Maalumu wa REA, na kwa lengo la kuhakikisha kuwa hatua stahiki zinachukuliwa kwa

mkandarasi Kampuni ya DERM Electrics (T) Limited aliyekuwa anatekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili mkoani Mara, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) iliunda timu kwa ajili ya kufanya uhakiki wa vifaa na kujiridhisha na usahihi wa nyaraka zilizowasilishwa na mkandarasi huyo kwa ajili ya malipo.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali imefafanua kwamba, Timu hiyo ilibaini kuwa mkandarasi alirudisha vifaa kwa kazi ambazo hazikufanyika, ambavyo vilikabidhiwa kwa Meneja wa TANESCO Mkoa wa Mara. Aidha, uchunguzi uliofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mara ulibaini kuwa Kampuni ya Derm Electrics Limited ilirejesha vifaa ambavyo havikutumika ikiwa ni pamoja na Mita 4,168 za Njia Moja (Single Phase) na 545 za Njia Tatu (Three Phase). Hata hivyo, kwa kuwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilionesha kulikuwa na utata katika Hati za Kukabidhi Vifaa (Delivery Notes), Serikali kupitia REA imezuia malipo kwa Mkandarasi ya kiasi cha **Shilingi Milioni 106** zinazolingana na thamani ya vifaa vilivyokabidhiwa kwa Hati hizo hadi hapo tutakapojiridhisha na suala hili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa TANESCO, Katika kuhakikisha kuwa hatua stahiki zinachukuliwa kwa watumishi husika, TANESCO iliunda timu ya ufuatiliaji wa suala hilo ambapo baada ya uchunguzi wa kina ilionekana kuwa mtumishi huyo wa TANESCO alizingatia masharti ya kimkataba katika utekelezaji wa mradi huo ambayo yameelezwa katika Kifungu Na. 24 cha Masharti ya Jumla (General Conditions of the Contract – GCC).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa kazi ya usimikaji wa miundombinu ya mradi wa REA Awamu ya Pili mkoani Mara ilikuwa imekamilika tangu mwezi Desemba, 2016 na kwamba miundombinu hiyo ilikuwa inafanya kazi, Meneja wa Mradi alitakiwa awe ametoa Cheti cha Kukamilika Kazi, suala ambalo lilifanyika kwa mujibu wa Mkataba. Kwa muktadha huo, mamlaka ya nidhamu ya mtumishi huyo wa TANESCO ilijiridhisha kuwa alitekeleza majukumu yake kama ilivyopasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa watumishi wa REA, Timu iliyoundwa ilibaini kuwa aliyekuwa mtumishi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa nafasi ya Mkurugenzi Huduma za Ufundi alishauri mkandarasi (Kampuni ya DERM Electrics (T) Limited) kulipwa malipo husika kwa kuzingatia kuwa ankara zilizowasilishwa REA kutoka TANESCO kwa ajili ya malipo ziliambatishwa na Cheti cha Kupokelewa kwa Vifaa (Goods Acceptance Certificate) ambacho ndicho kinachothibitisha kuwa vifaa husika vimepokelewa. Hata hivyo, mtumishi huyo alistaafu kazi kwa mujibu wa Sheria mwezi Novemba, 2018 kabla taarifa ya uchunguzi kuhusu suala hilo haijakamilika. Hivyo, kutokana na kukoma kwa utumishi wa umma wa mtumishi huyo, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ambaye ndiye alikuwa mwajiri wake aliandika barua TAKUKURU yenye Kumb. Na. AG 124/143/01/145 ya tarehe 29 Desemba, 2022 ili suala hilo lishughulikiwe kisheria. Ufuatiliaji umeendelea kufanyika ambapo hadi tarehe 25 April 2023, TAKUKURU ilieleza kwamba inaendelea na uchunguzi wa suala hili.

**b) Ukaguzi Maalumu wa Idara ya Uhamiaji**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali imefafanua kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imechukua hatua zifuatazo kutokana na ukaguzi maalumu uliofanyika katika idara ya uhamiaji: -

i. Kuchukua hatua kwa mujibu wa Maelekezo na Maagizo ya Bunge kwa kuwachukulia hatua za Kisheria Watumishi 32, ambao baada ya uchambuzi walikuwa katika makundi ya Mamlaka ya Nidhamu yafuatayo: **Watumishi 20** waliopo chini ya Mamlaka ya Tume ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji; **Watumishi 03** waliopo chini ya Mamlaka ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na **Watumishi 09** waliopo chini ya Mamlaka ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji;

ii. Kwa kuwa hapo awali mwaka 2019, Watumishi hawa 32 walifunguliwa Shauri la Uhujumu Uchumi Na. 5/2019 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi mjini Moshi mkoani Kilimanjaro ambapo Shauri hilo liliondolewa Mahakamani tarehe 12 Julai, 2021 baada ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutokuwa na

nia ya kuendelea na Shauri hilo hivyo, Wizara iliwasiliana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa barua yenye Kumb. Na. CEA.309/384/02/53 ya tarehe 10 Novemba, 2022 ili kupata ushauri wa kisheria kuhusu namna Bora ya kushughulikia Agizo hili na hatimaye kuandaa taarifa ya utekelezaji. Mkurugenzi wa Mashtaka aliunda Kamati Maalum yenye Wajumbe Saba (07) kutoka Taasisi na Idara za Usalama ikiwemo Ofisi ya Rais – Usalama wa Taifa (01), Ofisi ya Mashtaka (01), Jeshi la Polisi (01), TAKUKURU (01) na Uhamiaji (03).

Kamati hiyo ilifanya mapitio kwa kufanya uchunguzi upya na hatimaye kubaini kwamba Shauri hili haliwezi kurudishwa tena mahamakani kutokana na kukosekana ushahidi wa kutosha kuweza kuthibitisha shauri hili mahakamani dhidi ya watuhumiwa na hatimaye kuwatia watuhumiwa hatiani, hivyo Kamati ilishauri kuwa; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ichukue hatua za kinidhamu dhidi ya wahusika kwa namna kila mmoja alivyoshiriki. Kwa muktadha huo, Wizara ilifungua Mashauri ya Kinidhamu dhidi ya wahusika kulingana na Mamlaka yao ya Nidhamu kama ilivyo fafanuliwa awali, na hatua za utekelezaji wa Mashauri ya Kinidhamu yapo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo;

- **Mamlaka ya Nidhamu kwa Ngazi ya Tume ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji, na Uhamiaji**

Tume imeshughulika na Maafisa wenye Ngazi ya Cheo kuanzia Mkaguzi Msaidizi hadi Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji ambao walikuwa **20**. Watuhumiwa walipatiwa **Notisi na Hati za Mashtaka. Kamati ya Uendeshaji wa Mashauri** hayo iliundwa na imeshafanya Kazi yake na Kuwasilisha Mapendekezo ambayo Kikao cha Tume kinatarajiwa kuketi ndani ya Mwezi Mei 2023 ili kupokea na kuchambua Taarifa ya Kamati zilizoendesha Mashauri hayo na hatimaye kutoa maamuzi dhidi ya watuhumiwa.Vivyo hivyo, kwa

- **Mamlaka ya Nidhamu ya Katibu Mkuu** na ile ya **Kamishna Jenerali wa Uhamiaji** zimekwishakamilisha kazi yake.Hivyo, Wizara inawasilisha Taarifa ya hatua ya Utekelezaji wa Mashauri haya kwa kutoa ahadi kwamba Maamuzi kuhusu Utekelezaji wa

Mashauri yote itatolewa pindi Kikao cha Tume kitakapohitimisha na kutoa Maamuzi ya Mwisho kuhusu mwenendo mzima na pengine adhabu zitakazoamuliwa.

**c) Ukaguzi Maalumu wa Chuo cha Hombolo**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali katika kutekeleza Azimio la Bunge linalohusu ukaguzi maalumu uliokuwa umefanyika katika chuo cha Hombolo imetoa maelezo kwamba, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kilianzisha mchakato wa mashauri ya kinidhamu dhidi ya wahusika wote waliotajwa katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum ya CAG ambao walihusika na upotevu wa mapato moja kwa moja walichukuliwa hatua ya kufukuzwa kazi. Wahusika hao ni wafuatao: -

i. Bw. Gidion Charles Mhagama (Afisa Hesabu Daraja la I) – kwa barua Kumb. Na. LGTI/MPF.33/33 ya tarehe 11/12/2020;

ii. Bw. Sailes Maine Marashi (Mhasibu Daraja la II) – kwa barua Kumb. Na. LGTI/MPF.156/16 ya tarehe 11/12/2020; na

iii. Bw. James William Kankila (Mhasibu Daraja la I) – kwa barua Kumb. Na. LGTI/MPF.166/63 ya tarehe 11/12/2020. Aidha watumishi hawa walifunguliwa jalada la polisi lenye Kumb. Na. DOM/RB/10409/2020 katika kituo cha Polisi Dodoma, bado Polisi inaendelea na utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, wahusika ambao hawakuhusika moja kwa moja na upotevu wa mapato ila walishindwa kusimamia ukusanyaji wa mapato kikamilifu walipewa adhabu ya kushushwa vyeo. Watumishi hao ni kama ifuatavyo: -

i. Bw. Ernest Tito Gele – Kutoka Msarifu (PGSS 14) kuwa Mhasibu Mkuu daraja la I (PGSS 12) barua yenye Kumb. Na. LGTI/MPF.220/38 ya tarehe 6/12/2021;

ii. Dkt. Joel Chongela – Kutoka Mhadhiri (PHTS 3.1) kuwa Mhadhiri Msaidizi (PHTS 2.1) kwa barua yenye Kumb. Na. LGTI/MPF.153/13 ya tarehe 6/12/2021; na

iii. Bw. Sylivester Shedrack Sanjah – Kutoka Mshauri wa Wanafunzi (PGSS 14) kuwa Mwangalizi wa Wanafunzi Mkuu Darala I (PGSS 11) kwa barua yenye Kumb. Na. LGTI/MPF.143/21 ya tarehe 6/12/2021.

***2.3.5 Kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Sura, 348***

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Azimio la Bunge linalohusu ukiukwaji wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 umegawanyika katika maeneo mahsusi. Maeneo hayo kwa mujibu wa Taarifa ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

**a) Shirika la Masoko Kariakoo**

OR-TAMISEMI imemuandikia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali barua yenye Kumb Na. CCB.86/167/01/61 ya terehe 21/12/2022 kumuomba afanye ukaguzi wa kiuchunguzi. Pia, OR-TAMISEMI imemwandikia barua yenye Kumb. Na. CCB.86/167/01/63 ya terehe 21/12/2022 Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Ikulu na barua yenye Kumb. Na. CCB.86/167/01/62 ya terehe 21/12/2022 kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuomba vyombo vya dola vifanye uchunguzi.

Suala hili kwa sasa linafanyiwa kazi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ambapo uchunguzi huo umeanza Machi, 2023 kwa viongozi wa uongozi waliopo sasa kufanyiwa mahojiano (Kaimu Meneja Mkuu; Kaimu Meneja wa Mipango na Biashara na Mkuu wa Kitengo cha Usalama). Aidha, TAKUKURU inaendelea na uchunguzi kwa Viongozi waliokuwepo mwanzo.

**b) Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)**

OR-TAMISEMI imeandika barua yenye Kumb. Na.CGB.7/402/01E/35 ya tarehe 28 Novemba 2022 kwenda kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kumuomba kufanya ukaguzi maalum kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) kama ilivyoazimiwa na Bunge.

### c) Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi – Fungu 28

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya Kanuni zitakazosaidia kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Tuzo na Tozo. Kwa sasa hatua inayofuata ni zoezi la kuwapitisha wadau muhimu kwenye Rasimu hiyo.

Vilevile, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amefanya ukaguzi maalumu (Special audit) wa matumizi ya mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi ambapo taarifa yake imewasilishwa Bungeni tarehe 06 Aprili, 2023 ambayo itafanyiwa kazi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, na Serikali itawasilisha majibu yake katika Mkutano wa 12 wa Bunge, Septemba 2023.

### *2.3.6 Umiliki na Uendeshaji wa Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO)*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali katika kutekeleza Azimio la Bunge kuhusu KADCO imebainisha kwamba, Serikali imeridhia kurejeshwa kwa shughuli za uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi) imeanza kutunga Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itakayowezesha TAA kusimamia viwanja vyote vya Ndege Tanzania Bara ikiwemo Kiwanja cha Kilimanjaro (KIA). Waraka wa Baraza la Mawaziri ulianza kujadiliwa tarehe 21 Desemba, 2022 katika ngazi ya Sekretariati ya Baraza la Mawaziri na unatarajiwa kujadiliwa wakati wowote katika kikao cha Makatibu Wakuu (IMTC) kabla ya kuwasilishwa kwenye ngazi ya Baraza la Mawaziri. Matarajio ni kuwa ridhaa ya Baraza la Mawaziri itapatikana kabla ya Julai 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Katika KADCO Bunge liliazimia pia kufanyika kwa ukaguzi wa kina (Comprehensive audit). Ukaguzi huo wa kina unaendelea.

*2.3.7 Utendaji wa Kifedha wa Benki za Serikali (TCB na TIB)*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali imefafanuwa kwamba, Benki ya Maendeleo TIB, katika kipindi cha 31 Machi 2022 hadi 31 Machi 2023 kimekusanya jumla ya **Shilingi billioni 1.5** kutoka katika kundi la mikopo chechefu. Kiwango cha mikopo chechefu kimefikia **Shilingi bilioni 77.95** Machi 2023 kutoka **Shilingi bilioni 357.90** kama ilivyokuwa kwa kipindi kilichoishia Machi 2022. Mbali ya makusanyo, benki imeondoa mikopo chechefu iliyokuwa kwenye vitabu vya benki katika kundi la hasara kwa zaidi ya robo nne(4) za mwaka kwa mujibu wa kanuni za Benki kuu ya Tanzania (The Banking and Financial Institutions (Management of Risk Assets) Regulations, 2014, Section 9 states that "A bank or financial institution shall, at every quarterly review, charge off all credit accommodations and other risk assets that have remained in the loss category for four consecutive quarters".)

Aidha, Taarifa ya Serikali imefafanua kwamba uwiano wa mikopo chechefu umepungua kutoka asilimia 55.11 kama ilivyokuwa hapo Machi 2022 kufikia asilimia 21.10 Machi 2023. Vilevile, makusanyo ya mikopo iliyokuwa imefutwa katika vitabu vya benki ni **Shilingi bilioni 1.30** katika kipiindi cha Machi 2022 hadi Machi 2023. Benki imeweka mikakati ya kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 57** kutoka kwenye mikopo iliyofutwa katika vitabu (carged off loans) kufikia Disemba 2023.Benki imekuwa ikichukua hatua kadhaa za ukusanyaji kutoka kundi la mikopo chechefu (NPLs) ndani ya mizania ya benki na mikopo iliyotolewa kwenye vitabu/mizania (Charges off loans) ili kupunguza gharama za tengo la mikopo chechefu na kuboresha ukwasi na hali ya mtaji wa benki. Hatua hizo ni pamoja na;

i. Kushirikisha wakusanyaji wa madeni (Debt collectors) ili kutaifisha mali za dhamana zilizowekwa na wakopaji husika kwa mujibu wa Sheria ili kurejesha mtaji wa benki;

ii. Ushiriki wa Timu ya Serikali ya Ukusanyaji wa Madeni ya Serikali iliyoundwa mahsusi kuisaidia TIB katika ufuatiliaji wa karibu, majadiliano, na makubaliano na wateja juu ya mipango ya ulipaji ili kuhakikisha urejeshaji wa madeni;

iii. Kushirikiana na Wakili Mkuu wa Serikali juu ya kufuatilia haraka kesi mahakamani ili kuhakikisha hukumu zinatoka kwa wakati na kuruhusu taratibu za ufilisi, pia kuruhusu majadiliano na makubaliano nje ya mahakama (Out of court setlements);

iv. Benki hiyo pia imewasilisha miradi ya uwekezaji katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ili kusaidia kutafuta wawekezaji wenye uwezo;

v. Kuimarisha urejeshaji kutoka kwa mikopo iliyotolewa kwenye vitabu vya benki. Benki inatarajia kukusanya **Shilingi bilioni 57** kutokana na mikopo iliyotolewa kwenye vitabu ambayo itaboresha mtaji wake wa msingi ifikapo mwishoni mwa mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) katika mwaka 2022 ilifanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 22.6** kutoka katika kundi la mikopo chechefu (NPL). Mikopo chechefu ilikuwa **Shilingi bilioni 72.3** hadi mwisho wa mwaka 2022 kutoka **Shilingi Bilioni 80.9** kama ilivyokuwa kwa kipindi kilichoishia Desemba 2021. Katika kipindi cha miezi minne ya mwaka 2023, Benki imekusanya **Shilingi bilioni 4.3** kutokana na mikopo chechefu ambayo ilikuwa hailipiki. Matarajio ni kukusanya zaidi ya **Shilingi bilioni 20** itakapofikia mwisho wa mwaka 2023.

Aidha, Taarifa ya Serikali imefafanua kwamba uwiano wa mikopo chechefu katika kipindi cha mwaka 2022 ilikuwa asilimia 8.43 ikilinganishwa na asilimia 10.94 katika kipindi cha Desemba 2021. Hadi kufikia Aprili 2023, baada ya Serikali kuipatia TCB kiasi cha **Shilingi bilioni 30** ili kusaidia katika kufuta mikopo chechefu, uwiano wa mikopo chechefu ukilinganisha na jumla ya mikopo yote umepungua kufikia **asilimia 5.89**. TCB ilikusanya mikopo iliyokuwa imefutwa (Charged off loans) ya jumla ya **Shilingi bilioni 5.4** kwa mwaka 2022 kutoka lengo la kukusanya shilingi bilioni 6. Ukusanyaji wa mikopo iliyofutwa (Charged off loans) umeendelea kuongezeka ambapo kwa kipindi cha miezi minne kuanzia Januari hadi Aprili 2023 kiasi cha fedha kilichokusanywa kutokana na mikopo iliyofutwa ilikuwa **Shilingi bilioni 4.2**. Lengo la kukusanya mikopo chechefu kwa mwaka 2023 ni **Shilingi bilioni 6**

kama ilivyokuwa kwa mwaka 2022. Uongozi wa Benki kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali unaendelea kutaifisha mali za dhamana zilizowekwa na wakopaji husika kwa mujibu wa Sheria, ingawa baadhi ya wadaiwa wameendelea kufungua mashauri mahakamani na kuweka zuio la kuuzwa mali zao walizoweka kama dhamana ya mikopo.

***2.3.8 Ubadhirifu wa Sh. Bilioni 64.30 Katika Upanuzi wa Bandari ya Tanga***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Serikali kuhusu Azimio la kuchukua hatua kwa ubadhirifu wa fedha za umma uliobainika katika upanuzi wa bandari ya Tanga umebainisha kwamba, Serikali imeliwasilisha suala hili Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa ajili ya hatua za Kisheria. Ili kujua hatua iliyofikiwa, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imefuatilia TAKUKURU na kuelezwa kuwa suala hili linaendelea kufanyiwa kazi na Ofisi hiyo.

***2.3.9 Kuharibika kwa Dawa na Kutokuwepo kwa Dawa Katika Baadhi ya Maeneo ya Kutoa Huduma za Afya***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali imebainisha kwamba, kwa kutambua kuwa dawa lazima zitaisha muda wake bila kutumika, kimewekwa kiwango cha ukomo vumilika wa dawa kuisha muda ambacho ni chini ya asilimia 5 ya thamani ya dawa zilizotumika kipindi husika kwa sababu mbalimbali ikiwemo:-

i. Kutokuwepo kwa mlipuko wa magonjwa kutokana na kuimarika kwa afua za kinga dhidi ya magonjwa kama vile kuimarika kwa usafi, matumizi ya sanitizer, kunawa mikono, kuvaa barakoa kuliliepusha Taifa na magonjwa kama Kipindupindu, magonjwa ya tumbo na magonjwa ya njia za hewa; hivyo dawa za magonjwa hayo nyingi hazikutumika;

ii. Uwepo wa mabadiliko ya Matibabu; ambapo kwa kipindi cha mwaka mwaka 2018 hadi 2021 kumetokea mabadiliko ya matumizi ya dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kutoka TLE kwenda TLD. Hivyo ujio wa dawa mpya za TLD kuliacha dawa

nyingi za TLE zenye thamani ya **TZS 16 Bilioni** ambazo hazikutumika hadi muda wake wa matumizi ulipoisha;

iii. Mabadiliko ya teknolojia ya upimaji wa magonjwa katika maabara huchangia kwa kiasi kikubwa baadhi ya vitendanishi kutotumika hadi muda wake wa matumizi kufikia ukomo. Mfano mabadiliko katika upimaji wa wingi wa kinga mwilini CD4 kutoka kutumia mashine za Facs Count na Facs Calibur Kwenda BD facs Presto na PIMA machine kuliacha vitendanishi vingi vyenye thamani ya TZS 6 Bilioni kuisha muda wake bila kutumika; na

iv. Mfumo wa maoteo unaotumika kukadiria mahitaji ya dawa una changamoto, hivyo huchangia kutokuwa na makadiro halisi ya dawa zinazohitajika na kusababisha dawa kutotumika hadi ku-expire; hasa kwa dawa za misaada kutoka kwa wadau.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali imeendelea kubainisha mikakati iliyopo kukabiliana na changamoto ya kuharibika kwa dawa ikiwa ni pamoja hii ifuatayo:-

i. Serikali imeanzisha utaratibu wa kupata maoteo ya bidhaa za afya kwa kushirikisha vituo tumizi ili kuongeza uwajibikaji kwa watumishi;

ii. Serikali kuongeza kasi ya kuteketeza dawa na bidhaa nyingine za Afya hasa katika mwaka wa fedha 2021/2022 na sasa 2022/2023. Kasi hii imetokana na ushawishi wa Serikali kwa wadau wanaotufadhili kuwataka watoe fedha za kuratibu uteketezaji wa bidhaa za afya zilizosalia au kuisha muda wake kufuatia mabadiliko ya matibabu na teknolojia nchini;

iii. Serikali imeandaa muongozo wa kuratibu mabadiliko ya matibabu au vitendanishi ili kuwezesha kupunguza masalia na gharama za uteketezaji;

iv. Serikali kuimarisha mawasiliano kati Bohari ya dawa na Vituo vya kutolea huduma za afya kabla ya kupokea na kuwapelekea dawa, vitendanishi na chanjo vyenye shelf-life isiyozidi miezi sita; na

v. Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha kupitia upya mongozo na utaratibu wa uteketezaji wa bidhaa za afya;

vi. Utaratibu wa kupata maoteo ya bidhaa za afya kwa kushirikisha vituo tumizi umeanza kutekelezwa mwaka 2021/2022 na umewezesha kupunguza kiwango cha dawa kuchina (expire) kutoka **Shilingi bilioni 34.5** (2020/2021) na sasa ni **Shilingi bilioni 13.9** (2021/2021);

vii. Juhudi za Serikali kuongeza kasi ya kuteketeza dawa na bidhaa nyingine za Afya zilizochina zimefanikiwa baada ya nchi kupewa **Dola za kimarekani 230,457.82** awamu ya kwanza mwaka 2020 na **Dola za kimarekani 236,918.09** zimeombwa kwa ajili ya awamu ya pili, hivyo kuiepusha nchi kuwa na bidhaa za afya zilizochina katika vituo vya kutolea huduma za afya;

viii. Serikali imeandaa muongozo wa kuratibu mabadiliko ya matibabu au vitendanishi ambao umeanza kutumika katika mabadiliko ya dawa za TB na kuiepusha nchi kuwa na dawa zilizo china, hasara ambayo ingeweza kufikia shingi bilioni nne (4);

ix. Serikali imeimarisha mawasiliano kati ya Bohari ya dawa na Vituo vya kutolea huduma za afya kabla ya kupokea na kuwapelekea dawa, vitendanishi na chanjo vyenye shelf-life isiyozidi miezi sita kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023 (Bottom-Up Quantification);

x. Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha zinaendelea kupitia upya mwongozo na utaratibu wa uteketezaji wa bidhaa za afya ili kuharakisha zoezi hilo la kuteketeza dawa na vifaa tiba kwa wakati.

### *2.3.10 Mapitio na Tathmini ya Hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali katika Azimio la Bunge linalohusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, imefafanuwa kwamba Serikali kupitia Mkaguzi wa Ndani Mkuu (IAG) ilifanya uhakiki wa

baadhi ya madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya jamii, kwa nyakati tofauti tofauti, kuanzia mwaka 2016 hadi 2021. Aidha, IAG kwa sasa amekamilisha uhakiki wa madeni ya fedha zilizotumika katika Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa uliogharamiwa na NHIF na Miradi ya Ujenzi wa Ukumbi wa Bunge na Ujenzi wa Chuo cha Nelson Mandela iliyogharamiwa na PSSSF (PPL).

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji imeendelea kubainisha kwamba, Serikali imeanza tena majadiliano mwezi Machi 2023 na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (NSSF, NHIF na PSSSF kuhusu mpango wa malipo wa madeni yaliyobaki. Aidha, deni lililohakikiwa na kukidhi vigezo kwa mifuko ya NSSF, NHIF, PSSSF na PPL lilikuwa **Shilingi bilioni 3,949.55**. kati ya kiasi hicho, Serikali imeshalipa **Shilingi bilioni 2,719.64** ikihusisha deni la pre-1999 la **Shilingi bilioni 2,170**.

### *2.3.11 Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Azimio hili la Bunge imebainisha kuwa, Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) iliunda timu za wakaguzi na kuanza ukaguzi tarehe 7 Desemba, 2022 ukihusisha kufanya vikao vya awali (Entry meetings) katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na TANESCO. Taarifa ya ukaguzi imekamilika na imewasilishwa kwa Mamlaka ikiwa imeainisha hatua stahiki za kuchukua.

### *2.3.12 Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani*

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Azimio la Bunge kuhusu mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani, taarifa ya Serikali imebainisha hatua zilizochukuliwa kama ifuatavyo:-

a) PPRA imekamilisha uchunguzi na kuchukua hatua ya kuifungia kampuni ya Amandi Holding Limited kushiriki kazi za ununuzi wa umma ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha miaka mitano (5). Kufuatia hatua hiyo. kampuni hiyo ilikata rufaa lakini Machi 31, 2023, PPRA ilipokea barua yenye

Kumb.Na.OSG/DSM/PPAA/FEB/2023/2/5 kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuhusu maamuzi yaliyofikiwa na Mahakama (PPAA) ya kampuni hiyo kuendelea na utekelezaji wa maamuzi ya PPRA; na

b) Serikali imechukua hatua za kinidhamu katika dosari zote zilizobainika katika mradi wa kusimamia uuzaji wa matrekta. Hatua hizo ni kusimamishwa kazi watendaji na wengine kuhamishwa vituo vya kazi na kuchukuliwa hatua za kinidhamu kulingana na taratibu za kijeshi. Aidha, SUMAJKT inaendelea na hatua za kuhakikisha fedha zote za Mradi wa Matrekta zinarejeshwa.

***2.3.13 Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Azimio la Bunge lililotaka taasisi mbalimbali za Serikali kutekeleza mapendekezo na ushauri uliotolewa na CAG katika taarifa za ukaguzi wa ufanisi imegawanyika katika maeneo kadhaa. Maeneo hayo ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

a) Katika Bodi ya Mikopo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameanza kufanya ukaguzi wa kina (Comprehensive audit) kuhusu utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu hapa nchini. Ukaguzi huu umeidhinishwa na CAG na Timu ya Ukaguzi inategemewa kuanza kazi tarehe 15 Mei, 2023.

Kuhusu suala la **Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,** Serikali kupitia Wizara ya Elimu imeunda Timu ya mapitio ya taratibu nzima za upangaji, utoaji na wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kazi hii kwa sasa inaendelea, ambapo Wizara imekwisha pokea taarifa ya awali na taarifa ya mwisho ya kazi hii inaatarajiwa kuwasilishwa Wizarani mwishoni mwa mwezi April 2023. Matokeo ya mapitio hayo yatawasilishwa katika mamlaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwa CAG kwa lengo la kupata maoni yenye lengo la kuboresha ufanisi wa huduma ya mikopo ya elimu ya juu kwa walengwa.

Vilevile, utekelezaji wa malekezo ya CAG utatolewa taarifa katika Bunge kwa kila robo mwaka kama ilivyopendekezwa na Kamati kwa kuzingatia matokeo na mapendekezo ya Timu iliyoundwa pamoja na Kaguzi nyingine zitakazoendelea kufanyika na CAG. Aidha, kwa upande wa ugharamiaji wa Elimu ya Juu, Serikali inaendelea na mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, ambapo eneo mojawapo la mapitio ni uhuishaji wa matamko ya ugharamiaji kwa lengo la kuruhu kuwa na vyanzo endelevu vya ugharamiaji wa elimu ikiwa ni pamoja na elimu ya juu. Pamoja na mapitio ya Sera, Serikali imeendelea kutafuta vyanzo vingine vya ugharamiaji wa elimu ikiwa ni pamoja na ushirikishaji wa wadau. Kwa mfano, kwa mwaka wa masomo 2023/24, Benki ya NMB imetenga **Shilingi Bilioni 200** kwa ajili ya mikopo ya Elimu ya Juu na wadau wengine wameonesha nia ya kuunga mkono jitihada hizo.

b) Kuhusu **BRELA**, CAG alitoa mapendekezo tisa (9). Kati ya hayo mapendekezo matatu (3) yamekwisha tekelezwa ikiwemo;-

i. Pendekezo la kuhakikisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja unakamilika na kusambazwa kwa wadau husika;

ii. Pendekezo la kuhakikisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathimini unakamilika;

iii. Pendekezo la kuwepo na Dawati la huduma kwa wateja lenye watumishi wenye ujuzi stahiki ili kuhakikisha changamoto zote zinazotumwa na wateja zinafanyiwa kazi kikamilifu na zinatolewa mrejesho;

iv. Pendekezo moja utekelezaji wake ni endelevu na linatekelezwa kwa kila robo ya mwaka; na

v. Kwa upande wa mapendekezo matano (5) yaliyobaki, mawili utekelezaji wake umepangwa kufanyika robo ya nne (4) ya mwaka wa fedha 2022/2023 na matatu utekelezaji wake unategemea kukamilika kwa mradi wa maboresho ya mfumo wa usajili kwa njia ya Mtandao (Online Registration

System – ORS) ambao unatarajiwa kuwa umekamilika kufikia tarehe 31 Disemba 2023.

c) Kuhusu **Tume ya Madini,** Serikali itaendelea kuwasilisha kwa CAG utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi yaliyotolewa na CAG kwa Tume ya Madini kila baada ya miezi mitatu (3).

***2.3.14 Usimamizi Usioridhisha wa Taarifa na Huduma Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)***

**Mheshimiwa Spika,** Katika Azimio hili la Bunge, taarifa ya utekelezaji ya Serikali imebainisha hatua ambazo Serikali imechukua kama ifuatavyo: -

i. Mashauri ya kinidhamu yamefunguliwa kwa watumishi 27 ambapo kati yao watumishi kumi na sita (16) walifukuzwa kazi, watano (5) walipewa onyo, wawili (2) walishushwa mshahara na mmoja (1) alishushwa cheo;

ii. Wanataaluma 111 wameripotiwa katika mabaraza yao ya taaluma kwa ajili ya hatua za kinidhamu kutokana na makosa mbalimbali;

iii. Mashtaka 5 yamefunguliwa kwa wanachama 67 waliobainika kufanya vitendo vya udanganyifu yamefunguliwa na Mfuko na yapo katika hatua mbalimbali kwa mujibu wa Sheria na taratibu za nchi;

iv. Serikali imesitisha mikataba ya vituo vya huduma 22 kutokana na vitendo vya udanganyifu;

v. Barua za Onyo 588 zimetolewa kwa vituo, wanachama na waajiri binafsi waliogundulika kufanya vitendo vya udanganyifu;

vi. Serikali imesitisha matumizi ya vitambulisho 347 vya wanufaika waliogundulika kufanya vitendo vya udanganyifu. Aidha, wanachama husika walitakiwa kurejesha gharama

zote zilizotokana na matumizi ya vitambulisho husika ambapo jumla ya **Shilingi 112,625,366.07** zimerejeshwa; na

vii. Kati ya **Shilingi 28,301,932,933.84** zilizobainika kuwa ni za udanganyifu, **Shilingi 22,501,188,116.73** tayari zimerejeshwa na kiasi kilichobaki kinaendelea kurejeshwa na vituo husika kupitia makato ya madai yao ya kila mwezi.

***2.3.15 Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Mashirika ya Umma***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji kuhusu azimio hili la jumla ambalo lilitaka mapendekezo yote ya CAG yafanyiwe kazi, imebainisha kuwa, Serikali imepokea ushauri wa Bunge na utaendelea kufanyiwa kazi.

**2.4 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA CAG KUTOKANA NA UHAKIKI WA MAJIBU YA SERIKALI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YATOKANAYO NA TAARIFA ZA CAG KWA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 05 Juni, 2023 , Kamati ilikutana na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Bungeni Dodoma. Lengo la Kikao hicho lilikuwa kupitia na kuchambua taarifa yake inayohusu uhakiki uliofanyika kwenye taarifa ya majibu ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla utekelezaji wa baadhi ya maazimio ya Bunge haukuwa umefanyika kikamilifu. Kwa mujibu wa Taarifa ya CAG, baada ya uhakiki wa majibu ya Serikali imebainisha kuwa, maazimio 3 sawa na asilimia 20 yalikuwa yametekelezwa kikamilifu na Serikali kwa kipindi cha miezi sita tangu kupewa maazimio hayo. Aidha, maazimio 9 sawa na asilimia 60 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mwisho, maazimio 3 sawa na asilimia 20 hayajatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge umefafanuliwa katika jedwali na 2.1 hapa chini:-

**Jedwali Na. 2.1: Hali halisi ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge**

| Maazimio ya Bunge | Na. | Asilimia |
|---|---|---|
| Yaliyotekelezwa kikamilifu | 3 | 20 |
| Yaliyotekelezwa kwa sehemu | 9 | 60 |
| Ambayo hayajatekelezwa | 3 | 20 |
| Jumla | 100 | 100 |

**Chanzo: Taarifa ya CAG Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, Juni 05, 2023 .**

**Mheshimiwa Spika,** Kama jedwali Na. 2.1 hapo juu linavyofafanuwa, hadi kufikia tarehe 05 Novemba, 2023 jumla ya maazimio 3 hayakuwa yametekelezwa kabisa. Aidha, maazimio 9 yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Naomba sasa kulipitisha Bunge lako Tukufu katika maazimio ambayo bado hayajatekelezwa na yale ambayo yapo katika hatua za utekelezaji. Maazimio hayo ni kama ifuatavyo:-

***2.4.1 Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kiasi cha Sh. Trilioni 2.81***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG imebainisha kuwa agizo hili lipo katika hatua ya utekelezaji. Uhakiki wa ukusanyaji wa mapato umefanyika na mambo yafuatayo yameboreshwa:- Mamlaka ya Mapato imeanzisha "Online VAT filing" kuanzia Machi, 2022 na maboresho mengine yamefanyika mwezi Februari 2023 na yanaendelea kufanyika, hii yaweza kupunguza mianya ya upotevu wa kodi ya Ongezeko la thamani.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uhakiki wake CAG alibaini kuwa, TRA iliandaa rasimu ya mpango wa mafunzo wa kuwajengea uwezo

wafanyakazi wake kwa mwaka wa fedha 2022/23. Kwa mwaka wa fedha 2021/22 Mamlaka iliweza kufanya kampeni 17 kwenye mikoa ya Rukwa, Ruvuma, Katavi, Mara,Manyara,Njombe, Shinyanga na Morogoro. Kamapeni hizo ziliweza kuwafikia walipa kodi 28,231.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya uhakiki ya CAG imebainisha kwamba, Kwa mwaka wa fedha 2020/21 makusanyo hayakufikiwa kama yalivyokadiriwa kutokana na mlipuko wa COVID 19, ingawaje mapato kwa mwaka 2021/22 yameongezeka ukilinganisha na mwaka uliopita. Uhakiki umebaini kuwa mapato yameongezeka kutoka **Sh. 16.62 trilioni** mwaka 2020/21 na kufikia **Sh. 21.3 trilioni** mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la 21%. Hata hivyo mapitio ya mfumo mzima wa ukusanyaji kodi hayajakamilika na uchunguzi kwa watumishi ambao walihusika katika ukadiriaji wa kodi wenye dosari pia haujakamilika.

***2.4.2 Dosari Katika Usimamizi wa Mikataba na Athari zake katika Matumizi ya Fedha za Umma***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya uhakiki ya CAG umebainisha kuwa agizo hili halijatekelezwa kwa upande wa TANROADS.Hadi sasa Bado Serikali haijafanya uchunguzi ili kubaini iwapo riba zilizotokana na mikataba ya ujenzi wa barabara katika TANROADS zilikuwa na uhalali na ulazima wa kuwepo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa TANESCO na Kampuni ya Symbion, azimio hili lipo katika hatua ya utekelezaji. Uhakiki wa CAG umebaini kwamba Serikali ilivunja mkataba huu ambapo ilipelekea kushtakiwa kwenye mahakama ya Kimataifa ya usuluhishi (ICC Arbitration) kwenye kesi namba Na.2261/70 na ICSID Arbitral No. ARB/19/17. Symbion ilishinda kesi hiyo ambapo Serikali iliamriwa kuilipa Kampuni ya Symbion ambapo Serikali na symbion walikubaliana kumaliza suala hilo nje ya mahakama. Hivyo, Serikali ililipa kampuni ya Symbion kiasi cha **USD 153.43 Milioni** kupitia Wizara ya Nishati.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu gati la kuegesha meli katika bandari ya Mtwara, uhakiki umebaini kuwa agizo hili limeanza kutekelezwa. Gati la Mtwara kwa sasa linatumika kama lilivyokusudiwa, na pia mazungumzo yanaendelea kati ya mkandarasi wa gati hilo na TPA na Wakili wa serikali ili kufikia muafaka wa malipo.

***2.4.3 Hali ya Ukwasi Katika Baadhi ya Taasisi za Kimkakati za Serikali (TPDC, TANESCO na STAMICO)***

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu TPDC, ukahiki umebaini kuwa agizo hili lipo katika hatua za utekelezaji. Mapitio ya CAG yalibaini kuwa Baraza la Mawaziri (BLM) kupitia kikao kilichofanyika tarehe 06 Septemba 2022 kiliridhia mapendekezo ya kubadili mkopo wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam pamoja na Mitambo ya Kuchakata Gesi Asilia iliyopo Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi) kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), wa kiasi cha **dola za marekani 1,193,611,687.49** kuwa mtaji wa Serikali kwa TPDC.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa madeni ya TANESCO, uhakiki umebaini kuwa azimio hili pia lipo katika hatua za utekelezaji. Kwenye mapitio ya CAG amethibitisha kuona barua kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina ikimpatia TANESCO kibali na kumjulisha kwamba suala hili la kubadilisha madeni ya **Shilingi 2,419,253,931,879** kuwa mtaji lilipitishwa na Baraza la Mawaziri kupitia kikao kilichofanyika tarehe 06 Seoptemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa STAMICO, taarifa ya uhakiki ya CAG imebainisha kuwa agizo hili halijatekelezwa. STAMICO haikuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa azimio linalohusu hali ya kifedha ya Shirika.

***2.4.4 Kaguzi Maalumu za REA, Uhamiaji na Hombolo***

**Mheshimiwa Spika,** Kwa maazimio yaliyohusu REA, uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya uhakiki ya CAG umebaini kuwa azimio lipo katika hatua za utekelezaji. Uhakiki umebaini kwamba, REA

imezuia malipo ya Mkandarasi ya **Sh.106 milioni** yanayohusu nyaraka zilizoghushiwa kwa mradi wa usambazaji umeme vijijini awamu ya tatu. Hata hivyo CAG hakupata uthibitisho wa kuzuiwa kwa malipo hayo. Vilevile kwa Mtumishi wa REA aliyetakiwa kuchukuliwa hatua, CAG alifahamishwa kuwa suala hilo lipo TAKUKURU.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa TANESCO ambapo watumishi kadhaa walitakiwa kuchukuliwa hatua kutokana uzembe wao katika mradi wa REA huko Mkoani Mara, CAG hakupata nyaraka zilizotumika kufikia hitimisho la kutochukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa TANESCO.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Idara ya Uhamiaji, uhakiki umebaini kuwa azimio hili lipo katika hatua za utekelezaji. Hatua za kinidhamu zimechukuliwa;ambapo watumishi 30 wamepewa barua ya onyo mnamo tarehe 24 Aprili 2023 na watumishi wawili wamepewa adhabu ya kutopandishwa cheo kwa muda wa miaka mitatu.

***2.4.5 Kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Sura, 348***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa taarifa ya uhakiki ya CAG kwa Shirika la Masoko Kariako umebaini kwamba, CAG amekamilisha mpango kazi kwa ajili ya Ukaguzi Maalumu wa Shirika la Masoko Kariakoo.Mpango kazi huu umepelekwa kwa Katibu Mkuu-TAMISEMI pamoja na hati ya madai mnamo tarehe 31.03.2023 kwa ajili ya uwezeshwaji wa timu ya ukaguzi ili ukaguzi huu uweze kufanyika. Hivyo azimio hili lipo katika hatua za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa DART, Taarifa ya uhakiki ya CAG imebainisha kuwa Ukaguzi Maalumu umeanza tarehe 15/05/2023 na unategemea kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Juni 2023. Hivyo azimio hili lipo katika hatua za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Fungu, 28 Jeshi la Polisi kuhusiana na Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi, Ukaguzi Maalumu ulikamilika. Kuhusiana na Mlipaji Mkuu wa Serikali kuandaa kanuni za kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Tozo na

Tuzo; Mchakato huo unaendelea na sasa hatua ya kupata maoni ya wadau imekamilika na rasimu ya kanuni imewasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa barua yenye Kumb. Na.CFB 9/337/01/24 ya tarehe 25 Mei 2023 kwa hatua zaidi ili iweze kuwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

### *2.4.6 Umiliki na Uendeshaji wa Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO)*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya uhakiki ya CAG imebainisha uwepo wa Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 2022/2023 kuhusu mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya mwaka 2023. Aidha, CAG anaendelea kufanya ukaguzi wa kina (Comprehensive audit) wa mapato na matumizi ya KADCO kuanzia mwaka 2010 hadi 2022. Ukaguzi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai 2023.

### *2.4.7 Utendaji wa Kifedha wa Benki za Serikali (TCB na TIB)*

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hoja iliyohusu Benki ya TCB, azimio hili la Bunge lipo katika hatua za utekelezaji. Taarifa ya uhakiki ya CAG kwa Kamati imebainisha kwamba, Taarifa za TCB zinazohusu mwaka wa fedha unaoishia 31 Desemba 2021 zilihakikiwa zikihusisha uwiano wa mikopo chechefu wa asilimia 10.94 ya mikopo yote kama ilivyo kwenye hesabu zilizosainiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa mwaka wa fedha unaoishia 31/12/2022 bado unaendelea, hivyo uhakiki zaidi utafanyika pindi hesabu zitakapohitimishwa. Aidha, CAG alihakiki na kuthibitisha kuwa Serikali imeipatia benki ya TCB kiasi cha **shilingi bilioni 30** kupitia“Exchequer EB/AG/159/22/2307” ya tarehe 22 Machi 2023 pamoja na TISS Advice kutoka kwa TR Kwenda TCB.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hoja iliyohusu Benki ya TIB, uhakiki wa CAG katika Taarifa ya Serikali pamoja na mambo mengine umebainisha kuwa azimio hili lipo katika utekelezaji. CAG amebainisha uwepo na ushiriki wa Timu ya Serikali ya Ukusanyaji wa Madeni ya Serikali iliyoundwa kuisaidia TIB ufuatiliaji,

majadiliano, makubaliano na wateja juu ya mipango ya ulipaji ili kuhakikisha urejeshaji wa madeni. Hadi kufikia tarehe 25 Mei 2023, benki ilikuwa imeingia makubaliano na wakusanya madeni 7 ambao wamekabidhiwa wateja 177 wenye mikopo ya jumla ya **shilingi bilioni 217.78** kwa ajili ya kukusanya na kuuza dhamana zao. Hadi tarahe 25 Mei 2023 madalali wameweza kukusanya kiasi cha **Shilingi milioni**
**85.84.**

**Mheshimiwa Spika,** CAG pia amehakiki na kuthibitisha kuwa, TIB imeanza kushirikiana na Wakili Mkuu wa Serikali juu ya kufuatilia haraka kesi mahakamani ili kuhakikisha hukumu zinatoka kwa wakati. CAG alithibitisha kuona orodha ya kesi 42 ambazo zipo kwenye hatua mbali mbali za kimahakama kuhusu malimbikizo ya mikopo ya TIB.

***2.4.8 Ubadhirifu Katika Upanuzi wa Bandari ya Tanga***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG kuhusu uhakiki wa azimio la Bunge katika eneo hili imebainisha kuwa, azimio hili lipo katika hatua za utekelezaji. Azimio hili linafanyiwa kazi na TAKUKURU hivyo, CAG ataendelea kufuatilia utekelezaji wake.

***2.4.9 Kuharibika kwa Dawa na Kutokuwepo kwa Dawa Katika Baadhi ya Maeneo ya Kutoa Huduma za Afya***

**Mheshimiwa Spika,** Mapitio ya Taarifa ya CAG kuhusu uhakiki wa utekelezaji wa azimio hili, umebaini kwamba azimio halijatekelezwa. Pamoja na Serikali kuanzisha mikakati ya kupunguza kuharibika kwa dawa na vifaa tiba, Serikali haijatoa majibu kuhusu azimio la Bunge kuitaka Bohari ya Dawa wasitoe au kupokea dawa, vitendanishi au chanjo ambazo muda wake wa matumizi upo chini ya miezi 6 ya kutumika (shelf life).

***2.4.10 Mapitio na Tathmini ya Hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii***

**Mheshimiwa Spika,** Uhakiki wa CAG katika azimio hili umebainisha kuwa azimio halijatekelezwa kikamilifu. Pamoja na

Serikali kuchukua hatua mbalimbali kuhusu madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii, bado haijaandaa mpango wa malipo ya mikopo ya mifuko ya hifadhi ya jamii (loan repayment schedule) kama Bunge lilivyoazimia.

### 2.4.11 Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake

**Mheshimiwa Spika,** Katika Azimio hili, Bunge liliitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kufanya uchunguzi wa ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi uliokuwa umefanywa katika Shirika la TANESCO na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya uhakiki ya CAG imethibitisha kufanyika kwa uchunguzi huo. Aidha, CAG ameifahamisha Kamati kuwa alipata mawasailiano kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwenda kwa mkurugenzi mtendaji TANESCO juu ya utekelezaji wa Azimio hili. Hata hivyo hatua zilizochukuliwa kwa wahusika hazijafafanuliwa.

### 2.4.12 Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

**Mheshimiwa Spika,** Uhakiki wa utekelezaji wa azimio hili umegawanyika katika sehemu mbili. Kwa upande wa TPA ilihusu kuifungia Kampuni ya "Amandi Holding Limited" inayofanya shughuli za kusimika mifumo kutofanya kazi hapa nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, Kampuni ya "Amandi Holding Limited" imechukuliwa hatua na kufungiwa kwa kipindi cha miaka (5) na shauri lao la kukata rufaa limekataliwa kama ilivyooneshwa katika barua yenye kumbukumbu na. OSG/DSM/PPAA/FEB/2023/2/5.

**Mheshimiwa Spika,** Upande wa pili wa azimio hili ilihusu kuchukua hatua kwa watendaji wa SUMA JKT waliohusika na kuuza matrekta bila mikataba. Azimio hili lipo katika hatua za utekelezaji. Taarifa ya CAG imefafanuwa kwamba, hatua zilizokwisha kuchukuliwa na Bodi ya SUMA JKT ni kiasi cha **Sh. 261,500,000** kimekusanywa kutoka kwenye deni la uuzaji la matrekta bila mikataba la **Sh. 981,400,000** Kiasi cha **Sh.**

**719,900,000** kimebaki bila kulipwa na mikataba mitatu ya mauzo ya matreketa imeandaliwa na kusainiwa. Hata hivyo CAG hakupata uthibitisho wa kimaandishi kuonesha hatua za kinidhamu kwa watendaji zilizo chukuliwa na Bodi ya SUMA JKT.

**2.4.13 Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa ukaguzi wa ufanisi katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Taarifa ya Uhakiki ya CAG imebainisha kuwa, utekelezaji wa ukaguzi wa HESLB ulianza rasmi tarehe 16 Mei 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni 2023. Aidha, Mapendekezo 8 kati ya 11 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.
Mapendekezo 3 hayajatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa BRELA hawakuwasilisha Taarifa ya utekelezaji kwa CAG hivyo utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa BRELA hayakufanyiwa uhakiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Tume ya Madini, Mapendekezo 7 kati ya 9 yapo katika hatua za awali za utekelezaji. Mapendekezo 2 hayajatekelezwa.Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa ni pamoja na kuweka mikakati ya ukaguzi wenye kulenga maeneo yenye viashiria -hatarishi ambavyo pia vitasaidia kubainisha maeneo yenye uwezekano mkubwa wa upotevu wa maduhuli; na kuanzisha utaratibu utakaohakikisha matumizi ya rasilimali watu waliopo kwenye Ofisi za Maafisa Madini Wakazi (RMOs) wanawezeshwa kufuatilia na kutathmini mapato ya mwaka yanayowasilishwa na makampuni ya madini.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya uhakiki ya CAG inatanabaisha kwamba,**Tume ya Madini** haijawasilisha taarifa mpya baada ya kikao cha PAC cha mwezi Oktoba 2022.

### 2.4.14 Usimamizi Usioridhisha wa Taarifa na Huduma Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG kuhusu utekelezaji wa azimio hili umebainisha pia kuwa azimio hili lipo katika hatua za utekelezaji. Mathalani, CAG hakupata uthibitisho wa hatua zilizochukuliwa kwa wanataaluma 111 walioripotiwa katika mabaraza stahiki kwa ukiukaji wa viapo vyao vya kazi. Aidha, hakuna uthibitisho wa kusitishwa kwa mikataba na vituo vya huduma vilivyobainika kufanya vitendo ya udanganyifu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika azimio hili CAG ameifahamisha Kamati kuwa hapakuwa na uthibitisho uliotolewa wa barua za onyo kwa vituo na waajiri binafsi waliogundulika kufanya vitendo vya udanganyifu. Vilevile hapakuwa na uthibitisho uliotolewa wa kusitishwa kwa vitambulisho 374 kufuatia udanganyifu.Mwisho, CAG hakupata uthibitisho wa kukusanywa kiasi cha **shilingi 22,501,188,116.73** kama ilivyowasilishwa na Serikali.

### 2.4.15 Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Uhakiki wa CAG katika utekelezaji wa azimio hili ulibaini kwamba, kwa upande wa Serikali Kuu, kati ya mapendekezo 6947 ya ripoti yake ya miaka iliyopita, mapendekezo 2380 (asilimia 34) yametekelezwa; mapendekezo 2506 (asilimia 36) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo 1104 (asilimia 16) hayakutekelezwa; mapendekezo 637 (asilimia 9) yamejirudia; na mapendekezo 320 (asilimia 5) yamepitwa na wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mashirika ya Umma, kati ya mapendekezo 126 ya ripoti yake ya miaka iliyopita, mapendekezo 53 (asilimia 42) yametekelezwa; mapendekezo 63 (asilimia 50) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo 9 (asilimia 7) hayakutekelezwa; na pendekezo 1 (asilimia 1) limepitwa na wakati.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YATOKANAYO NA TAARIFA ZA CAG KWA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA 2020/2021

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati yametokana na uchambuzi wa kina wa taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimo ya Bunge. Aidha, maoni ya Kamati yameboreshwa kwa kuzingatia uhakiki uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kila azimio kama taarifa ya Serikali ilivyobainisha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati ina maoni ya ujumla kama ifuatavyo:-

a) Hali ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokanayo na Taarifa za CAG kwa ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka 2020/2021 bado ina changamoto za kiutekelezaji. Mathalani, hadi uhakiki wa CAG unakamilika mwezi Juni, 2023, kwa Maazimio ya Bunge ya mwezi Novemba, 2022, ni asilimia 20 tu ya Maazimio ya Bunge yalikuwa yametekelezwa kikamilifu, asilimia 60 yalikuwa katika hatua za utekelezaji na asilimia 20 hayakuwa yametekelezwa. Kwa msingi huo, kunatakiwa jitihada zaidi katika kutekeleza Maazimio ya Bunge;

b) Vilevile, Kamati ina maoni kuwa utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa miaka iliyopita bado haujafanyika ipasavyo. Maoni haya yanadhihirishwa na uwepo wa mapendekezo 1104 ambayo hayajatekelezwa kabisa katika Serikali Kuu na mapendekezo 9 ambayo hayajatekelezwa katika Mashirika ya Umma. Hivyo jitihada za makusudi lazima zichukuliwe kuongeza uwajibikaji kwa mapendekezo ya CAG;

c) Kuna mapungufu katika mfumo uliopo ndani ya Taasisi za Serikali zinazohusika na mchakato mzima wa uratibu wa

ukusanyaji na utekelezaji wa Hoja na maazimio ya Bunge. Mapungufu hayo yanaathiri utekelezaji wa Hoja na Maazimio ya Bunge kwa wakati;

d) Baadhi ya Maafisa Masuuli hawawajibiki ipasavyo katika kutekeleza Masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura ya 348. Mfano Dhahiri ukiwa ni pamoja na kuchelewesha nyaraka na vielelezo mbalimbali kwa CAG ili vifanyiwe uhakiki. Kwa mfano, kwa uhakiki wa CAG uliofanyika katika Taarifa hii, nyaraka ziliwasilishwa kwa CAG tarehe 25 Mei, 2023 na vielelezo vikawasilishwa tarehe 29 Mei, 2023. Hivyo CAG hakupata muda wa kutosha kuhakiki nyaraka na vielelezo hivyo;

e) Kamati ina maoni kwamba, ni muda mwafaka wa Bunge kuangalia uwezekano wa kuboresha Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia Maafisa Masuuli kujibu na kutekeleza hoja za CAG na Maazimio ya Bunge. Jambo hili lifanyike kwa kuweka muda mahsusi (Time frame), ambao utatakiwa kuzingatiwa na kila Afisa Masuuli katika kujibu hoja za CAG na Maazimio ya Bunge; na

f) Kamati ina maoni kwamba, ni muda mwafaka wa kuboresha Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma hasa katika eneo la adhabu (Sanctions). Ni jambo la muhimu kuweka adhabu mahsusi kwa Maafisa Masuuli wanaoshindwa kutekeleza Maazimio ya Bunge kwa wakati na wale wanaoshindwa kutekeleza mapendekezo ya CAG bila ya kuwa na sababu za msingi.

### 3.2 Maoni Mahsusi

**Mheshimiwa Spika**, Maoni mahsusi ya Kamati kwa kuzingatia kila azimio ni kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kiasi cha Sh. Trilioni 2.81

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, azimio hili bado halijakamilika utekelezaji wake kwa kuwa mikakati iliyofanyika inajibu sehemu tu ya Azimio la Bunge Serikali inatakiwa kukamilisha mchakato wa mapitio ya mfumo mzima wa kodi kama Bunge lilivyoazimia ili kuhakikisha mapato stahiki ya Serikali yanakusanywa. Vilevile, Kamati ina maoni kuwa azimio la kufanya uchunguzi wa sababu za kushindwa kufikia malengo ya makusanyo ya kodi kwa mapungufu yanayohusu dosari za kimaadili na weledi kwa baadhi ya watumishi wa TRA halijafanyiwa kazi hadi sasa. Hali hii inakwaza dhima ya Bunge kuisimamia Serikali ipasavyo.

### 3.2.2 Dosari Katika Usimamizi wa Mikataba na Athari zake katika Matumizi ya Fedha za Umma

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo la riba zinazolipwa kwenye mikataba ya ujenzi kutokana na kuchelewa kwa malipo kwa wakandarasi na washauri wa miradi, Kamati ina maoni kwamba, azimio hili bado halijatekelezwa. Kwa kuzingatia uhalisia wa fedha zinazolipwa kama riba, kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa kufanyika uchunguzi wa kina katika eneo hili ili kuokoa fedha za umma ambazo zinaweza kutumika kwenye maeneo mengine yenye uhitaji na kuleta tija kwa Taifa.

### 3.2.3 Hali ya Ukwasi Katika Baadhi ya Taasisi za Kimkakati za Serikali (TPDC, TANESCO na STAMICO)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na imezingatia hatua za Serikali za kubadili madeni ya TPDC na TANESCO kuwa sehemu ya mitaji ya Mashirika hayo 2. Hata hivyo, Katika Shirika la STAMICO, Kamati haikuridhika na hatua ya STAMICO kutowasilisha kwa CAG utekelezaji wa Azimio la Bunge. Kamati ina maoni kuwa azimio hili kwa upande wa STAMICO bado halijatekelezwa kama Bunge lilivyokusudia.

### 3.2.4 Kaguzi Maalumu za REA, Uhamiaji na Hombolo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, TANESCO na REA hawajakamilisha utekelezaji wa Azimio la Bunge linalohusu uchukuaji wa hatua za kinidhamu kwa watumishi waliotajwa katika Taarifa ya CAG katika mapungufu ya utekelezaji wa mradi wa REA Mkoani Mara. Ni maoni ya Kamati kwamba, hatua za kiuwajibikaji kwa watumishi hao bado hazijakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Idara ya Uhamiaji Fungu 93, hatua kadhaa za kiuwajibikaji zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kushushwa vyeo kwa baadhi ya watumishi na kupewa barua za onyo. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa hatua zilizochukuliwa sio toshelevu. Hii ni kwa sababu, ukaguzi ulithibitisha kuwa watendaji husika walitenda makosa ya jinai ikiwa ni pamoja na kuingilia mfumo wa visa mtandao na kuiba fedha za umma takribani **Shilingi 2,427,255,600**.

### 3.2.5 Kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Sura, 348

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhika na utekelezaji wa Azimio la Bunge katika eneo hili. Ni Maoni ya Kamati kuwa Kaguzi Maalumu za DART na Shirika la Masoko Kariakoo zitakamilika kama zilivyopangwa. Kwa upande wa Ukaguzi wa Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi, Kamati imejipanga kupitia na kuchambua Taarifa ya Ukaguzi huo Maalumu Mwezi Agosti, 2023 na kisha kuwasilisha Taarifa yake hapa Bungeni.

### 3.2.6 Umiliki na Uendeshaji wa Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, Azimio hili la Bunge halijatekelezwa ipasavyo. Pamoja na uwepo wa Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri wa Kutunga Sheria ya Viwanja vya Ndege, bado Kamati ina maoni kuwa Serikali ingetekeleza Azimio la Bunge la kuirudisha KADCO chini ya TAA katika kipindi cha mpito. Maoni haya ya Kamati yanazingatia uchambuzi wa kina wa hoja za ukaguzi za KADCO hapo mwezi Novemba, 2022. Aidha, Kamati ina maoni kuwa ukaguzi wa kina wa Hesabu za

KADCO za mwaka 2010 hadi 2023 unaoendelea sasa ukamilike kama ilivyopangwa na Bunge lichukue hatua stahiki zaidi kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi huo.

### 3.2.7 Utendaji wa Kifedha wa Benki za Serikali (TCB na TIB)

**Mheshimiwa Spika,** Katika azimio linalohusu hali ya kifedha ya Benki za Serikali za TCB na TIB, Kamati imetambua jitihada za Serikali katika kutekeleza Maazimio ya Bunge. Aidha, Maoni ya Kamati kwa sasa ni kwamba, TCB na TIB ziendelee kudhibiti ongezeko la mikopo chechefu na kuzingatia kikamilifu Masharti ya Sheria ya Benki Kuu Kuhusu ukwasi wa Benki.

### 3.2.8 Ubadhirifu Katika Upanuzi wa Bandari ya Tanga

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa azimio hili halijatekelezwa kama Bunge lilivyoagiza. Ni muda mrefu umepita bila hatua za kisheria kuchukuliwa kwa suala la ubadhirifu katika zabuni ya upanuzi wa bandari ya Tanga. TAKUKURU wamepokea taarifa ya Ukaguzi Maalumu kwa takribani miezi 7 iliyopita hivyo walitakiwa kuchukua hatua stahiki kwa wahusika.

### 3.2.9 Kuharibika kwa Dawa na Kutokuwepo kwa Dawa Katika Baadhi ya Maeneo ya Kutoa Huduma za Afya

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili Kamati ina maoni kuwa, pamoja na Serikali kuanzisha mikakati ya kupunguza kuharibika kwa dawa na vifaa tiba, Serikali haijatoa majibu kuhusu Azimio la Bunge kuitaka Bohari ya Dawa wasitoe au kupokea dawa, vitendanishi au chanjo ambazo muda wake wa matumizi upo chini ya miezi 6 ya kutumika (Shelf life).

### 3.2.10 Mapitio na Tathmini ya Hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kulipa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama ilivyofafanuliwa hapo awali. Hata hivyo Kamati ina maoni kuwa ni muhimu Serikali ikatekeleza sehemu ya Azimio la Bunge ambalo

halijakamilika. Sehemu hiyo inahusu kuwasilisha hapa Bungeni Mpango na Ratiba ya Ulipaji wa Madeni hayo (Loans Repayment Schedule).

### 3.2.11 Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada ambazo PPRA imechukua kwa kufanya uchunguzi wa ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma katika Shirika la TANESCO na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, Serikali bado haijatoa Taarifa kwa CAG juu ya hatua ilizochukua kufuatia matokeo ya Kaguzi hizo 2. Ili kuweka misingi ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma, Kamati ina maoni kuwa, ni muhimu kwa Serikali kukamilisha hatua za kiuwajibikaji kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi pindi Ukaguzi Maalumu au uchunguzi unapokamilika.

### 3.2.12 Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa za kuifungia Kampuni ya Amandi Holding Limited kutofanya shughuli za kusimika mifumo ya TEHAMA hapa nchini. Pamoja na hilo, Kamati ina maoni kuwa hatua za ziada za kuwafikisha mahakamani watu wote waliohusika na ubadhirifu katika usimikaji wa mifumo katika TPA ziendelee kuchukuliwa.Aidha, kwa upande wa SUMA JKT, Kamati ina maoni kuwa Azimio la Bunge la kuwachukulia hatua watendaji waliohusika kuuza matrekta bila mikataba halijakamilika.

### 3.2.13 Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Tume ya Madini. Hata hivyo, kwa upande wa BRELA, Taasisi hiyo haikuwasilisha kwa CAG taarifa za utekelezaji wa Azimio la Bunge. Ni maoni ya Kamati kuwa Afisa Masuuli BRELA

hakuwajibika ipasavyo kujibu hoja za ukaguzi na Maazimio ya Bunge.

**3.2.14 Usimamizi Usioridhisha wa Taarifa na Huduma Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili, Kamati imepitia hatua kadhaa ambazo Serikali imechukua katika kuimarisha mifumo ya udhibiti kwenye Mfuko wa NHIF ili kuondoa changamoto za ubadhirifu. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa Azimio hili bado halijakamilika kutekelezwa ifapasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni haya ya Kamati yanatokana na hoja kuwa, CAG hakupata uthibitisho wa kuchukuliwa hatua kwa wanataaluma 111 walioripotiwa katika Mabaraza ya Kitaaluma kwa kukiuka viapo vyao vya kazi hivyo kuisababishia NHIF hasara.Aidha, hapakuwepo uthibitisho wa kusitishwa mikataba kwa vituo vilivyodanganya kutoa huduma. Vilevile CAG hakupata uthibitisho wa makusanyo ya **Sh. 22,501,188,116.73** katika mfuko wa NHIF kama ilivyowasilishwa katika taarifa ya Serikali.

**3.2.15 Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Mashirika ya Umma.**

**Mheshimiwa Spika,** Ni maoni ya Kamati kuwa bado kuna mrundikano mkubwa wa hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa na Serikali. Kamati ina maoni kuwa, Serikali iweke mfumo wa kupima utendaji wa Maafisa Masuuli kwa kuangalia vigezo mbalimbali ikiwemo namna wanavyoshughulikia na kujibu hoja za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni ya Kamati katika eneo hili yanathibitishwa na hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2020/2021. Mathalani kwa upande wa Serikali Kuu, kati ya mapendekezo 6947 ya miaka iliyopita, mapendekezo 2380 (asilimia 34) yametekelezwa; mapendekezo 2506 (asilimia 36) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo 1104 (asilimia 16) hayakutekelezwa;

mapendekezo 637 (asilimia 9) yamejirudia; na mapendekezo 320 (asilimia 5) yamepitwa na wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mashirika ya umma, kati ya mapendekezo 126 ya ripoti ya CAG ya miaka iliyopita, mapendekezo 53 (asilimia 42) yametekelezwa; mapendekezo 63 (asilimia 50) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo 9 (asilimia 7) hayakutekelezwa; na pendekezo 1 (asilimia 1) limepitwa na wakati.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO**

**4.1 Shukurani**

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii tena kwa mara nyingine kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini na thabiti ambao unaliwezesha Bunge letu tukufu kutekelezamajukumu yake kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ambapo kwa muda wote umekuwa ukitupatia ushirikiano na miongozo thabiti kila inapohitajika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee nikushukuru na kukupongeza kwa mara nyingine kwa kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa maazimio yanayokuwa yamefikiwa hapa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1) Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb – **Mwenyekiti**
2) Mhe. Japheti Ngailonga Hasunga, Mb – **M/ Mwenyekiti**

3) Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe, Mb
4) Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb
5) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
6) Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb
7) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
8) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
9) Mhe. Jackline Ngonyani Msongozi, Mb
10) Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
11) Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
12) Mhe. Bakar Hamad Bakar, Mb
13) Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
14) Mhe. Deus Clement Sangu, Mb
15) Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
16) Mhe. Janeth Maurice Massaburi, Mb
17) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
18) Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mb
19) Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb
20) Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb
21) Mhe. Condester Michael Sichalwe, Mb
22) Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa shukurani za pekee kwa Sekretarieti ya Bunge chini ya Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, ndc kwa ushauri na uongozi wake kwa Kamati. Sekretarieti ya Bunge imefanikisha shughuli za uratibu, ushauri wa kitaalamu na masuala ya kiutawala kwa shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kwa kuwasilisha taarifa za ukaguzi wa mafungu mbalimbali kwa wakati. Aidha naishukuru Wizara ya Fedha na Mipango na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho japo sio kwa umuhimu, natoa shukurani za dhati kwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge kwa kuratibu mchakato mzima wa kukusanya majibu ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutoka katika

Wizara, Idara, Wakala, Taasisi mbalimbali na Mashirika ya Umma. Zoezi hilo la uratibu limeiwezesha Kamati yangu kukamilisha uandaaji na uwasilishaji wa Taarifa hii ndani ya Bunge lako Tukufu.

**4.2 Kuwasilisha**

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa kuwasilisha.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)**
27 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKAlI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya *LAAC,* naomba kutoa taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 136(17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Naomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye *Hansard.* Taarifa ya Kamati yetu ina *page* zaidi ya 60, hii nayosoma ni *summary*. Kwa hiyo naomba na *summary* vilevile iingizwe kama isipojitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla. Awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kutujalia uzima hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa leo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa yenye Uchambuzi na Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu

za Serikali za Mitaa *(LAAC)*. Taarifa hii inatokana na Taarifa ya Hesabu pamoja na maoni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Ukaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji; baada ya kupokea Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa hiyo ili kubaini iwapo Serikali imetekeleza kikamilifu maazimio hayo. Uchambuzi huo umefafanuliwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla; baada ya *CAG* kupokea majibu ya Serikali na kuhakiki kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa na Serikali, Kamati imepata fursa ya kupitia na kufanya uchambuzi wa Taarifa ya *CAG* kuhusu utekelezaji wa maazimio hayo. Kwa kuzingatia uchambuzi wa taarifa hizo mbili zilizowasilishwa Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa hakuna Azimio hata moja lililotekelezwa kwa ukamilifu. Hali hii imetokana na uzembe wa makusudi uliofanywa na baadhi ya Maafisa Masuuli katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kudharau maazimio yaliyotolewa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika taarifa zote mbili umebaini kuwa, mengi yaliyoelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni ufafanuzi tu wa hoja ya namna ya kutekeleza maazimio hayo badala ya utekelezaji wenyewe. Vilevile kwa kiasi kikubwa, maelezo yaliyotolewa hayaendani na maazimio yaliyotolewa na Bunge. Mchanganuo wa utekelezaji wa Maazimio hayo kwa mujibu wa Taarifa iliyowasilishwa na *CAG* ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na.1 hapa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio la kwanza. Azimio hili lilikuwa na vipande au vipengele vinne. Mosi, Mfuko wa Mikopo wa Vikundi vya Akinamama, Vijana na Wenye Ulemavu

(a) Halmashauri 155 kushindwa kukusanya Shilingi Bilioni 47.01, azimio hili limetekelezwa kwa asilimia 34. *(Makofi)*

(b) Halmashauri 11 kushindwa kuhamisha Shilingi Bilioni 1.24 kutoka Akaunti ya Amana kwenda Akaunti ya Mifuko, haijatekelezwa. *(Makofi)*

(c) Halmashauri 17 zilitoa mikopo ya Shilingi Bilioni 3.26 kwa vikundi bila kuzingatia uwiano ulioanishwa, halijatekelezwa. *(Makofi)*

(d) Halmashauri 83 kutokuchangia jumla ya shilingi bilioni 6.68 kwenye Mfuko kutoka kwenye mapato yake ya ndani. Hili limetekelezwa kwa asilimia 36 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio la pili; Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Azimio hili lilikuwa na lina vipengele vitatu:-

(a) Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Matumizi ya Fedha zinazopitishwa na Bunge, halijatekelezwa. *(Makofi)*

(b) Kuweka angalau ukaribiano wa kiasi fulani cha ruzuku, halijatekelezwa. *(Makofi)*

(c) Kutorejesha HAZINA fedha zinazokuwa zimepelekwa katika Halmashauri, haijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio namba tatu; Uwekevu na Tija katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, halijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio namba nne; Manunuzi na Mikataba ya Upatikanaji wa Huduma na Bidhaa Mbalimbali, halijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio namba tano; Upatikanaji wa Stahili za Watumishi kwa mujibu wa Sheria, halijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio namba sita; Azimio hili lilikuwa lina vipengele viwili, azimio hili linahusu Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri:-

(a) Kuhakikisha kuwa Mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato *(TAUSI)* unaanza kutumika katika Halmashauri zote hili limetekelezwa kwa asilimia 92.

(b) Kuchukua hatua kali za kisheria kwa watendaji wote ambao wanakusanya mapato nje ya utaratibu na lenyewe halijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio namba saba; Matumizi Yasiyofaa ya Fedha katika Akaunti ya Amana, hili limetekelezwa kwa asilimia 41.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba nane; Upotevu wa Mapato katika Mifumo ya Kieletroniki ya Kukusanya Mapato, halijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio namba tisa; Hasara ya Kifedha Kutokana na Vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri, azimio hili lina vipengele vinne:-

(a) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, limetekelezwa kwa asilimia 33.

(b) Bohari ya Madawa, halijatekelezwa.

(c) Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini *(GPSA)* halijatekelezwa.

(d) Wakala wa Ufundi wa *TEMESA* Umeme, halijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 10. Kuhusu Uteketezaji wa Dawa za Binadamu katika Hospitali na Vituo vya Afya, tumeambiwa utekelezaji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 11 ni mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, halijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 12 ni mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa, hili kiujumla limetekelezwa kwa asilimia 42.

Mheshimiwa Spika, limebainika tatizo la CAG kutopewa baadhi ya nyaraka na vielelezo muhimu kwa ajili ya kufanya uhakiki pale anapohitaji kufanya hivyo. Kwa kufanya hivyo, kunakwamisha na kuchelewesha utekelezaji wa majukumu ya jicho la Bunge pamoja na jitihada za Bunge kuhakikisha matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha ya umma yanaondolewa na kunakuwa na ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni hayo ya jumla, Kamati ina maoni kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kwa kila Azimio lilitolewa na Bunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mikopo kwa vikundi vya akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Wakati wa uchambuzi wa hoja hii, Kamati ilishindwa kupata majina ya Wakurugenzi waliobainika kuisababishia hasara Serikali kwa kushindwa kwa uzembe kusimamia utoaji wa mikopo na hatua zilizochukuliwa dhidi yao. Aidha, uchambuzi wa Kamati katika Azimio hili umebaini kuwa, katika Halmashauri 155 ambazo zilishindwa kukusanya shilingi bilioni 47.01 zilizotolewa kwa vikundi mbalimbali ni Halmashauri 129 pekee zilizoweza kukusanya Shilingi Bilioni 16.17 ambayo ni sawa na asilimia 34 ya fedha zote zilizohojiwa na kiasi ambacho hakijakusanywa ni asilimia 66 ya fedha zote.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri 129 zilizokusanya fedha hizo, Halmashauri 31 zilitekeleza kikamilifu agizo la Bunge kwa kukusanya kiasi chote kilichohojiwa, Halmashauri 95

zilikusanya kiasi tu cha fedha kilichohojiwa na Wakurugenzi wa Halmashauri 29 waliamua kutotekeleza Agizo la Bunge kwa kutokusanya kiasi chochote cha fedha. Mchanganuo wa namna kila Halmashauri ilivyotekeleza agizo hili umefafanuliwa katika kiambatisho Namba 01 cha Taarifa hii ili kurahisisha hatua za kinidhamu dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini ukiukwaji wa Kanuni za uendeshaji wa Mfuko kwa Halmashauri 11 ambazo zilishindwa kuhamisha Shilingi Bilioni 1.24 kutoka akaunti ya Amana kwenda akaunti za mifuko ya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. Mpaka kuwasilishwa kwa Taarifa hii ya Kamati, hakuna majibu ya Serikali kuhusiana na azimio hili, hali inayotia mashaka kuhusu matumizi sahihi ya fedha hizo. Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuhamisha kiasi hicho cha fedha ni kiambatisho Namba 02 cha taarifa hii, kurahisisha uchukuaji wa hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya Halmashauri 17 zilizotoa mikopo ya shilingi bilioni 3.26 kwa vikundi bila ya kuzingatia uwiano, Serikali imeshindwa kutoa majibu kuhusu hoja hii na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ili kufahamu iwapo fedha hizo zimefikia walengwa ama kuna dalili yoyote ya ubadhirifu wa fedha za umma. Orodha ya Halmashauri zilizokiuka utaratibu huo ni kiambatisho Namba 03 cha taarifa hii, kuwasaidia kuchukua hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, nataka kunywa maji lakini kuna nzi ameingia, wanasema hizi ni *sunnah! (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, jumla ya Halmashauri 83 zilibainika kutochangia shilingi bilioni 6.68 kwenye mfuko kutoka kwenye mapato yake ya ndani, ambapo hadi Kamati ilipokutana na CAG kiasi kilichokuwa kimechangiwa ni shilingi bilioni 2.4 tu. Katika kiasi hicho kilichotolewa, Halmashauri 32 pekee ndizo zilizotekeleza kikamilifu agizo hilo kwa kuchangia kiasi chote cha fedha kilichohojiwa. Halmashauri 12 zilichangia sehemu ya kiasi cha fedha kilichohojiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imesikitishwa na utendaji wa Halmashauri 39 ambazo hazikuchangia kiasi chochote cha fedha kama ilivyoelekezwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, bado kuna kiasi cha shilingi bilioni 4.45 sawa na asilimia 64 ambacho hakijapelekwa katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutoka katika mapato ya ndani ya Halmashauri zilizotajwa katika Kiambatisho Na. 04 cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii ya mfuko wa mikopo kwa vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa ujumla wake kumekuwa na upotevu wa fedha za umma wa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 39.79 ambazo zingetumika katika uendeshaji wa mfuko huo. Vilevile, zimebainika Halmashauri zenye matatizo sugu ambapo matatizo yake yamekuwa yakijirudia katika hoja nyingi zilizoibuliwa na CAG. Baadhi ya Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Mji wa Geita, Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Halmashauri ya Jiji la Tanga, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Tumewatajia tena kuwarahisishia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa ruzuku ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika eneo hili, Azimio la Bunge lililenga kuhakikisha kunakuwa na uzingatiaji wa Kifungu cha 50 (a-c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 inazozitaka Taasisi za Serikali kutumia kiasi cha fedha ambacho hakizidi kile kilichoidhinishwa na Bunge katika bajeti yake. Hata hivyo, majibu ya Serikali hayajalenga kujibu azimio hili na kupeleka fedha pungufu au zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Azimio liliitaka Serikali kuhakikisha fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hazirejeshwi hazina ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha husika. Hata hivyo, rejea iliyofanywa na Serikali, ya Kanuni ya 21 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti haiondoi tatizo lililopo katika Halmashauri jambo ambalo ni kiashiria cha kudharau kwa maamuzi yaliyotolewa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, uwekevu na tija katika uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Wajibu ya Bunge ni kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinatumika katika kuleta maendeleo kwa wananchi. Hata hivyo, kumekuwa na utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo haina tija wala faida kwa wananchi wa maeneo husika. Hali hii inasababishwa na baadhi ya wataalam wa Halmashauri wasio na uwezo katika kuandaa miradi yenye kuzalisha mapato na kuwanufaisha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umebaini kutokutekelezwa kwa agizo hili kwa kuwa, taarifa ya Serikali haijaeleza mipango madhubuti ya kuondoa changamoto iliyoibuliwa katika Halmashauri zilizo nyingi nchini, badala yake imetoa taarifa ya Mwongozo ulioandaliwa Mwezi Julai, 2021 kabla ya kutolewa kwa maazimio haya ambao kimsingi haujaondoa tatizo ambalo Kamati ilibainisha katika taarifa yake ya Mwezi Novemba, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, manunuzi na mikataba ya upatikanaji wa huduma na bidhaa mbalimbali. Kumekuwa na ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Kanuni zake kwa baadhi ya Maafisa Masuuli katika Halmashauri mbalimbali nchini. Lengo la Azimio lilikuwa ni kuhakikisha Watendaji wote waliohusika na upotevu wa fedha za umma kulikosababishwa na kukiukwa kwa matakwa ya Sheria hiyo kuchukuliwa hatua stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imesikitishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali kwa kukiuka maazimio yaliyotolewa na Bunge kwa kuwaondoa katika nafasi zao Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi 23 waliobainika kuwa na utendaji usioridhisha na kusababisha hasara kwa kuwapangia majukumu mengine badala ya kuwawajibisha na kulipia hasara waliyoisababisha, kama ilivyoainishwa na Kanuni ya 53 ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298. Kwa kuwa kuwaondoa pekee ni kuzidi kuiongezea mzigo Serikali *(wage bill)* kwa kuwa watalipwa mishahara yao kama ambavyo walivyokuwa katika nafasi zao za awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hoja hiyo hiyo, Serikali imeeleza kuwabadilisha vituo vya kazi Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi 68 kinyume na Azimio la Bunge la kuwachukulia hatua kali za kisheria. Tafsiri ya haraka na maoni ya Kamati kuhusu hoja hii ni kuhamisha tatizo kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine, ikiwa ni pamoja na kuwaaminisha watumishi hao kuwa, hakuna hatua zozote za kisheria zitakazochukuliwa dhidi yao pindi watakapokiuka taratibu za kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa stahili za watumishi kwa mujibu wa

sheria. Hoja ya Kamati ilijikita katika watumishi 33,405 ambao wanadai malimbikizo ya muda mrefu ya mishahara yenye thamani ya shilingi bilioni 63.83 pamoja na madai mengine ya watumishi 71,670 yenye thamani ya shilingi bilioni 96.65. Hata hivyo, katika hali isiyo ya kawaida, Serikali imetoa maelezo ya kulipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi 66,233 kiasi cha shilingi bilioni 78.22, jibu ambalo ni tofauti na hoja iliyoibuliwa na Kamati. Aidha, *CAG* ambaye ndiye jicho la Bunge hajapelekewa vielelezo kuthibitisha kufanyika kwa malipo ya kiasi kilichotajwa katika taarifa ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali vilevile imeeleza kuwalipa watumishi wengine 64,531 kiasi cha shilingi bilioni 74.32 lakini hakuna vielelezo vilivyowasilishwa kwa *CAG* kuhusiana na malipo hayo. Vilevile, Serikali imeshindwa kuwasilisha kwa ajili ya uhakiki nyaraka zinazoonesha malipo ya shilingi bilioni 25.5 kwa watumishi na wazabuni. Kwa muktadha wa hoja iliyotolewa na Kamati, Azimio hili halijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri. Azimio la Bunge liliitaka Serikali kuhakikisha hadi kufikia mwezi Juni, 2023, Halmashauri zote 184 zianze kutumia mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato wa TAUSI. Hata hivyo, hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii ya Kamati, bado kuna Halmashauri 15 zilizopo katika Mikoa ya Kigoma na Singida ambazo hazijaanza kutumia mfumo huu. Jambo hili ni kinyume na maelekezo ya Bunge na linatoa viashiria vya upotevu wa mapato

yanayokusanywa katika Halmashauri hizo kwa kuwa mfumo wa awali wa ukusanyaji wa mapato ulishaonesha udhaifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Kamati haijajulishwa idadi ya Maafisa Masuuli ambao wamechukuliwa hatua kwa kukusanya mapato nje ya utaratibu wa kisheria na ambao hawapeleki fedha hizo benki. Kwa kuwa utaratibu huo ni kinyume na matakwa ya Kifungu cha 42 (2) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 ambacho kinaelekeza kuwa, stakabadhi zote zinazohusiana na Mamlaka ya Serikali ya Mitaa zitalipwa katika akaunti ya benki au akaunti iliyothibitishwa na Mamlaka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi yasiyofaa ya fedha katika akaunti ya Amana. Lengo la agizo hili lilikuwa ni kuhakikisha kunakuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha za Umma. Ripoti ya *CAG* ilibainisha matumizi mabaya ya shilingi bilioni 9.74 kutoka katika akaunti za Amana za Halmashauri 81. Hadi *CAG* anawasilisha taarifa yake ya uhakiki kwa Kamati, Halmashauri 19 zilizokuwa na hoja ya jumla ya shilingi bilioni 1.43 zimewasilisha vielelezo na kuhakikiwa na *CAG,* na jumla ya shilingi bilioni 2.57 zilizohojiwa kutoka Halmashauri 35 zimerejeshwa. Hata hivyo, bado kuna Wakurugenzi wa Halmashauri 27 ambao hawajarejesha fedha zilizochukuliwa kutoka katika akaunti ya Amana zenye jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 5.74 kinyume na maelekezo ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, upotevu wa mapato katika mifumo ya kielektroniki wa kukusanya mapato. Upotevu wa mapato unaotokana na matumizi yasiyo sahihi ya mifumo, umekuwa ni tatizo sugu linalosababishwa na kutokuwepo kwa uwajibikaji. Katika hoja hii, Kamati haijaridhishwa na taarifa iliyowasilishwa kwa kuwa, Serikali haijatoa maelezo yoyote juu ya namna kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kilichohojiwa kinaweza kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, uthibitisho wa vielelezo kuhusu ulazima wa kufanya marekebisho hayo kwenye mfumo kwa Halmashauri 17 kati ya 27 zilizohojiwa havijapatikana na havijawasilishwa kwa *CAG* kwa ajili ya uhakiki. Vilevile, Serikali

haijatoa orodha ya Wakurugenzi waliohusika na hasara hiyo kwa kufuta na kubadilisha miamala ya mapato iliyopo katika mfumo bila ya uthibitisho wowote.

Mheshimiwa Spika, hasara ya kifedha kutokana na vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri. Katika Azimio hili, Taasisi mbalimbali ambazo zinafanya kazi na Halmashauri zilihusika. Kwa upande wa Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF)* bado kuna kiasi cha shilingi bilioni 1.56 ambacho hakijalipwa kwa Halmashauri kutokana na huduma za tiba zilizotolewa kwa wanufaika wa Mfuko huo. Aidha, hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii, kiasi kilicholipwa kwa Halmashauri zinazodai ni shilingi milioni 788.97 ambacho ni sawa na asilimia 33 tu ya kiasi chote cha shilingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bohari ya Dawa *(MSD),* Azimio la Bunge lilikuwa ni kuitaka Serikali kupeleka dawa na vifaatiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.7. Hata hivyo, majibu yaliyotolewa na Serikali hayajalenga kabisa katika kujibu hoja ya msingi ya dawa na vifaatiba hivyo havijapelekwa katika Halmashauri husika na fedha husika hazijarejeshwa. Tatizo kama hilo liko vilevile kwenye *GPSA* na lipo vilevile kwenye *TEMESA*.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya jumla ya taarifa ya *CAG*. Mbali na Maazimio ya Bunge la Kumi na Mbili, Serikali ilielekezwa ikafanyie kazi Taarifa nzima ya *CAG*. Haya ndiyo matokeo: -

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto kubwa ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na *CAG* kwa Halmashauri mbalimbali nchini kwa kuwa, tangu Ripoti ya *CAG* iwasilishwe Bungeni mwezi Aprili, 2022, ni asilimia 42 pekee ya mapendelezo yote ya taarifa ile nzima ya *LAAC* ambayo yametekelezwa kikamilifu. Hali hii haitoi taswira nzuri kwa utekelezaji wa Halmashauri zetu kwa kuwa, kutotekelezwa kwa mapendekezo hayo kunaashiria kujirudia kwa matatizo yaliyobainishwa na *CAG* kila mwaka wa fedha pamoja na kutothamini kazi nzuri inayofanywa na Jicho la Bunge na Bunge lenyewe.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo, kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati. Vilevile, kwa namna ya kipeeke, tunapenda kukushukuru na kukupongeza kwa kuhakikisha jukumu la Bunge la kuisimamia Serikali linatekelezwa kikamilifu na kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Nichukue nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kukaa hapa, kuwashukuru kwa kura zenu mlizonipigia nikiwa sipo za kishindo, napenda vilevile kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*. Kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na Wasaidizi wake wote kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kusomwa kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho japo siyo kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG),* Ndugu Charles Kichere. Aidha, tunaishukuru Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Maafisa wao wote kwa ushirikiano wanaoutoa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na hizi changamoto kubwa sana tulizozielekeza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee Maoni ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Yatokanayo na Taarifa ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu Zilizokaguliwa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2021.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YALIYOTOKANA NA TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) KWA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa leo hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa yenye Uchambuzi na Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC). Taarifa hii inatokana na Taarifa ya Serikali pamoja na maoni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 05 Novemba, 2022, Bunge lako Tukufu lilipata fursa ya kupokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 na hatimaye kutoa maazimio.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha jukumu la Bunge la Kuishauri na Kuisimamia Serikali linafanyika kikamilifu, Kamati imepata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Maazimio yaliyotolewa na Bunge lako Tukufu ili kujiridhisha iwapo Serikali imetekeleza maazimio hayo kikamilifu.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, ili kurahisisha ufuatiliaji wa taarifa hii, sehemu kuu tatu zimebainishwa na sehemu ya nne inahusu hitimisho. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwa ni pamoja na utangulizi, muundo wa taarifa, majukumu ya Kamati na namna Kamati imefanya kazi. Lengo ni kubainisha mtazamo wa jumla wa taarifa kwa ajili ya kuwezesha ufuatiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya pili inabainisha rejea ya maazimio yaliyotolewa na Bunge pamoja na utekelezaji wa maazimio hayo kwa mujibu wa Taarifa ya Serikali pamoja na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika sehemu hii, Taarifa inafafanua maazimio ambayo yalitolewa na Bunge. Lengo la sehemu hii ni kubainisha hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza maazimio hayo. Sehemu hii inajenga msingi wa sehemu ya tatu inayohusu maoni ya Kamati.

### 1.3 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ulizingatia matakwa ya Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Majukumu hayo ni:-

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba, tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Umma linapungua.

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa kazi za Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa unatokana na Taarifa za hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 1.4 Njia zilizotumika katika utekelezaji wa kazi za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilitumia mbinu zifuatazo: -

a) Sekretarieti kuwapitisha Wajumbe katika maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge;

b) Sekretarieti kuwapitisha Wajumbe katika Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge;

c) Kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge; na

d) Kuandaa Taarifa ya Maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa hiyo ili kubaini iwapo Serikali imetekeleza kikamilifu maazimio hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 14(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri unaokuwa umetolewa na Kamati kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** jambo hili hufanyika kwa CAG kufanya uhakiki wa maoni na mapendekezo yanayokuwa yametolewa na Kamati kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika. Aidha, Halmashauri inapofika mbele ya Kamati, CAG huipitisha Kamati kwenye taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati kabla ya kuanza kupitia na kuchambua Taarifa ya Hesabu za Halmashauri hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia maelekezo uliyoyatoa ndani ya Bunge lako Tukufu siku ya tarehe 20 Aprili, 2023 na kuielekeza Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kupitia na kuchambua Taarifa iliyowasilishwa na Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kuwasilisha Taarifa ya Maoni ya Kamati ndani ya Bunge. Wakati wa utekelezaji wa jukumu hilo, mambo yaliyoangaliwa na kufanyiwa kazi na Kamati yamefafanuliwa katika sehemu hii ya pili ya Taarifa.

## 2.1 REJEA YA MAAZIMIO YA BUNGE YALIYOTOLEWA TAREHE 05 NOVEMBA, 2022

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kusimamia matumizi ya fedha za Umma inavyostahili, Kamati ilichambua Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2021 na kutoa jumla ya mapendekezo **Kumi na Mbili** (12) ambayo yalijadiliwa na hatimaye kuwa Maazimio ya Bunge kwenda Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, dhamira ya kuelezea maazimo hayo ni kulikumbusha Bunge lako kuhusu chimbuko la hoja zilizojadiliwa pamoja na maazimio yaliyotolewa na Bunge ili kuwaweka Wabunge katika nafasi ya kufuatilia mtiririko wa maoni ya Kamati. Aidha, maazimio yaliyotolewa ni kama ifuatavyo:-

### *2.1.1 Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya akina Mama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu*

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi uliofanywa na CAG ulionesha kasoro mbalimbali za uendeshaji wa mfuko huu ikiwemo Halmashauri 155

kushindwa kukusanya **Shilingi Bilioni 47.01** zilizotolewa kwa vikundi mbalimbali; Halmashauri 11 kushindwa kuhamisha **Shilingi Bilioni 1.24** kutoka Akaunti ya Amana kwenda Akaunti ya mifuko; Halmashauri 17 zilitoa mikopo ya **Shilingi Bilioni 3.26** kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu bila kuzingatia uwiano ulioainishwa; na Halmashauri 83 kutokuchangia jumla ya **Shilingi Bilioni 6.68** kwenye mfuko kutoka kwenye mapato yake ya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa ya CAG Bunge liliazimia kwamba, Mamlaka ya nidhamu ya Wakurugenzi ichukue hatua dhidi ya Wakurugenzi wote watakaobainika kushindwa kwa uzembe kusimamia kikamilifu utoaji na usimamizi wa mikopo hii kama inavyoelekezwa kwenye Kanuni ya 24 (2) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

***2.1.2 Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa Halmashauri 19 zilipokea ruzuku ya maendeleo zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa, Halmashauri 163 zilipokea ruzuku ya maendeleo pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa na Halmashauri 3 zilipokea kiasi halisi cha bajeti iliyoidhinishwa. Nia ya Serikali inaweza kuwa nzuri, lakini ni nje ya utaratibu ulioridhiwa na Bunge katika Sheria ya Matumizi ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hoja zilizoibuliwa, Bunge liliazimia Serikali ifanye yafuatayo:-

a) Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Matumizi zinazopitishwa na Bunge katika kila mwaka wa bajeti ili kuendelea kujijengea imani Bungeni na kwa wananchi;

b) Kuweka angalau ukaribiano wa kiasi fulani cha ruzuku endapo itabidi baadhi ya Halmashauri kuzidishiwa kuliko vile inavyotokea kwamba Halmashauri zingine hupewa kiasi kidogo mno wakati zingine hupewa zaidi ya 50%; na

c) Kutorejesha Hazina fedha zinazokuwa zimepelekwa katika Halmashauri kwa madai kuwa mwaka husika wa fedha umeisha ili kukamilisha miradi inayohusika.

### *2.1.3 Uwekevu na Tija katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibainisha dosari zinazohusu uwekezaji wa mitaji ya umma katika baadhi ya Halmashauri nchini. Dosari hizo ni pamoja na uwekezaji unaofanyika bila upembuzi yakinifu wala andiko la biashara, bali kwa kuiga uwekezaji unaofanyika katika Halmashauri nyingine. Dosari nyingine ni uwekezaji unaozingatia mikataba ya ujenzi yenye masharti yanayosababisha hasara katika Halmashauri zinazohusika. Hali hiyo inaathiri nia ya kuongeza mapato ya vyanzo vya ndani na kuwa na mtiririko madhubuti wa fedha ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya huduma bora.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa Halmashauri zote zinafanya uwekezaji unaozingatia fursa za uwekevu na tija katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri zao kuliko hali ilivyo sasa ambapo kila Halmashauri inataka soko na kituo cha mabasi tu. Aidha, Serikali iandae Mwongozo au Kanuni inayoelekeza namna bora ya uwekezaji kwa ngazi za Halmashauri kwa kuzingatia maandiko ya miradi yanayofuata taratibu zinazohusika na uwekezaji.

### 2.1.4 Manunuzi na Mikataba ya Upatikanaji wa Huduma na Bidhaa mbalimbali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini udhaifu katika ununuzi na upatikanaji wa huduma na bidhaa katika Halmashauri bila kufuata taratibu zinazohusika, hali inayoweka mwanya wa upotevu wa fedha za Umma. Kutokana na hoja hiyo, Bunge liliazimia kwamba, Serikali isimamie ipasavyo manunuzi yote ya Umma kwa kufuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa na kuridhiwa na Bunge. Aidha, Maafisa Masuuli wote watakaobainika kutosimamia ipasavyo agizo hili wachukuliwe hatua kali za kisheria kwa nia ya kukomesha ubadhirifu na kuliletea Taifa manufaa stahiki.

### 2.1.5 Upatikanaji wa Stahili za Watumishi kwa Mujibu wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG ulibaini malimbikizo ya muda mrefu ya mishahara yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 63.83** kwa watumishi 33,405 ambayo hayakulipwa. Vilevile kulikuwa na madai mengine ya watumishi 71,670 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 96.65** ambayo yalikuwa hayajalipwa yakiwa ni posho za likizo, gharama za uhamisho na posho nyingine. Kutokana na msingi wa hoja hiyo, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ishughulikie mara moja madai yote ya stahiki za Watumishi wa Halmashauri zilizopo kwa mujibu wa Sheria ambazo hazijatolewa na kuchukua hatua kali kwa waajiri wasiozingatia matakwa ya Sheria zinazohusika na stahili za watumishi.

### *2.1.6 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri*

**Mheshimiwa Spika**, ilibainika kwamba, Halmashauri zilizo nyingi zina udhaifu katika eneo la ukusanyaji wa mapato ya ndani kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uvujaji wa mapato kwenye mifumo ya kielektroniki, rushwa na kutosimamia ipasavyo Sheria, Kanuni na taratibu za fedha.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano ya kina Bunge
liliazimia Serikali itekeleze yafuatayo:-

a) Kuhakikisha kuwa Mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato (TAUSI) unaanza kutumika katika Halmashauri zote za Serikali ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023 badala ya hali ilivyo sasa ambapo bado kuna Halmashauri zinazoendelea kutumia mfumo wa zamani (Local Government Revenue Collection Information System - LGRCIS) unaoruhusu marekebisho ya miamala kwa namna yenye kutia shaka ya wizi; na

b) Kuchukua hatua kali za kisheria kwa watendaji wote ambao wanakusanya mapato nje ya utaratibu wa kisheria na ambao hawapeleki makusanyo benki.

### *2.1.7 Matumizi yasiyofaa ya Fedha katika Akaunti za Amana*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Taarifa ya CAG na ilibaini kwamba katika Halmashauri mbalimbali fedha zilizomo katika akaunti za Amana zinatumika kwa shughuli ambazo hazikutarajiwa. Ripoti ya CAG ilibainisha matumizi mabaya ya

**Shilingi Bilioni 9.74** kutoka katika Akaunti za Amana kutokana na kutosimamiwa ipasavyo. Matumizi hayo yalibainika katika Halmashauri 81.
Kwa muktadha huo, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazowekwa katika Akaunti za Amana zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa kuliko hali ilivyo sasa ambapo Akaunti hizo zinaonekana kutumika kama maficho ya fedha ambazo baadaye hutumika kibadhirifu. Aidha, Maafisa Masuuli wote waliotumia fedha hizi kinyume na utaratibu, wachukulie hatua kali za kinidhamu.

### 2.1.8 Upotevu wa Mapato katika Mifumo ya Kieletroniki ya Kukusanya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua na kubaini kuwepo kwa uvujaji wa mapato kupitia katika mifumo ya kielekroniki katika Halmashauri zetu. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Halmashauri 27 zilifanya marekebisho ya miamala yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 1.6** kwenye mfumo bila uthibitisho wa ulazima na uhalali wa marekebisho hayo kufanyika.

Kutokana na dosari hizo, Bunge liliazimia kwamba, Serikali idhibiti mianya ya mapato katika mifumo hiyo na kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watumishi wote waliohusika na upotevu, mathalani watumishi walio katika Halmashauri ambazo miamala ya mapato ilibadilishwa au kufutwa bila ya uthibitisho wa ulazima wa kufanya hivyo.

### 2.1.9 Hasara ya Kifedha Kutokana na Vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibaini namna Mamlaka za Serikali za Mitaa zinavyoathiriwa kifedha kutokana na ushirikiano wake na Taasisi nyingine za Serikali kama vile NHIF, TEMESA, MSD na GPSA; athari hizo zinadidimiza kasi ya maendeleo katika Mamlaka hizo. Changamoto zilizobainika katika Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

#### i) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**Mheshimiwa Spika**, ilibainika kuwa jumla ya **Shilingi Bilioni 2.34** hazijalipwa katika Mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa nchini

kutokana na huduma za tiba zilizotolewa kwa wanufaika wa Mfuko huo. NHIF ilishindwa kulipa fedha hizo kwa maelezo kwamba fomu za wagonjwa zilijazwa vibaya kiasi cha kutoaminika.
Ili kulinda maslahi ya Mamlaka hizo, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ishughulikie mara moja suala la NHIF kutorejesha gharama za matibabu na vifaa tiba vinavyotolewa na Halmashauri kwa wanufaika wa Bima ya Afya chini ya Mfuko huo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

**ii) Bohari ya Dawa (MSD)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kwamba, Halmashauri nyingi zilikuwa zikilipa fedha kwenye Bohari ya Dawa (MSD) pasipo kupelekewa dawa na vifaa tiba kwa wakati. Hali hii imekuwa ni kero kubwa katika baadhi ya Halmashauri. Jumla ya dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya **Shilingi Bilioni 1.17** havikupelekwa na MSD katika Halmashauri kutokana na sababu mbalimbali zilizo nje na utendaji wa Halmashauri.
Hivyo, Bunge liliazimia kwamba, Serikali iisimamie ipasavyo MSD ili iwe inapeleka dawa na vifaa tiba katika Halmashauri kwa muda usiozidi mwezi mmoja na iwapo hawana dawa au vifaa tiba husika, iifahamishe
Halmashauri husika ndani ya saa Ishirini na Nne (24).

**iii) Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, Halmashauri mbalimbali zimekuwa zikiamrishwa kulipa fedha kabla ya kupata huduma au bidhaa husika, na kwa upande wa uagizaji na manunuzi magari, wameshindwa kufanya vizuri kwani wamekuwa na tabia ya kurudisha fedha kwa wateja pasipo kukamilisha manunuzi ya magari hayo kwa wakati uliopangwa.
Kutokana na changamoto zilizobainika, Bunge liliazimia kwamba, Serikali iisimamie GPSA ili itekeleze majukumu yake kwa weledi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za kazi zao ili hatimaye kuzisaidia Halmashauri katika utekelezaji wa mipango yao.

**iv) Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kutokana na Taarifa ya CAG ulibaini kuwa TEMESA imekuwa ikitumika kurudisha nyuma utendaji na uzalishaji katika baadhi ya Halmashauri nchini kwa sababu haitoi huduma ipasavyo kwa wateja wake. Aidha, kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwenye Halmashauri mbalimbali kuhusiana na udhaifu wa chombo hiki katika matengenezo na ukaguzi wa magari na mitambo.

Katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za Serikali, Bunge liliazimia kwamba, Serikali iimarishe TEMESA ili iweze kuzisaidia Halmashauri na Taasisi nyingine za Serikali ili kupunguza malalamiko ya udhaifu wake katika eneo la ukaguzi na utengenezaji wa magari na mitambo katika Halmashauri.

**2.1.10 Kuhusu Uteketezaji wa Dawa za Binadamu katika Hospitali na Vituo vya Afya**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya CAG ya Mwaka wa Fedha 2020/21 ilionesha kuwepo kwa wimbi kubwa la uteketezaji wa madawa ya binadamu yenye thamani kubwa sana ya fedha. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/19 Halmashauri 14 ziliteketeza dawa zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 7.3**, mwaka 2019/20 Halmashauri 31 (**Bilioni 1.5**) na Mwaka 2020/21 Halmashauri 46 (**Bilioni 3.5**). Sababu kubwa ya uteketezaji wa dawa hizi, ni kuisha kwa muda wa matumizi ya dawa hizo (expiry), hivyo Bunge liliazimia kwamba, Halmashauri zote nchini zihakikishe kuwa hazipokei dawa zilizobakiza muda wa matumizi unaopungua miezi sita.

***2.1.11 Mapungufu katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kutokana na Taarifa ya CAG ulibaini kuwa, baadhi ya Halmashauri hazina watumishi wenye utalaamu unaohitajika na kulazimika kutumia watumishi wasio na sifa kwa kazi zinazohitaji utalaamu. Kitendo hicho kilisababisha kufanyika kwa maamuzi yaliyosababisha hasara kubwa kwa Halmashauri. Hivyo basi, Bunge liliazimia kwamba, Serikali ipeleke katika kila Halmashauri wataalam wa kutosha wa sekta zote muhimu zinazohitajika katika utekeleaji wa miradi ya maendeleo na kuwatumia ipasavyo.

### *2.1.12 Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa*

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 08 Aprili, 2022, Taarifa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 ziliwekwa mezani. Katika Taarifa hiyo, CAG alitoa jumla ya **Mapendekezo 10,625** ambayo yalitakiwa kutekelezwa kikamilifu na Serikali. Katika kutekeleza jukumu lake la kuisimamia Serikali, Bunge liliazimia kwamba, Mapendekezo yote yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa na kubainishwa kwenye Taarifa zake zilizowekwa Mezani tarehe 08 Aprili, 2022 kuwa ni sehemu ya Maazimio hayo ya Bunge na kutakiwa kufanyiwa kazi na Serikali.

## 2.2 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KWA MUJIBU WA TAARIFA YA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge lako Tukufu kutoa maazimio yaliyoainishwa katika kipengele cha kwanza cha sehemu hii ya pili, Serikali imewasilisha Taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali kwakuwa, katika maeneo mengi, Serikali imetoa ufafanuzi tu badala ya kutekeleza kama ilivyoelekezwa na Bunge na Kamati haijaona nia ya dhati (commitment) na mkakati madhubuti wa kutekeleza maagizo hayo. Vile vile, majibu mengi yaliyotolewa na Serikali hayaendani na maazimio ya Bunge yaliyotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, majibu ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyowasilishwa na Serikali ni kama ifuatavyo:-

### *2.2.1 Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya akina Mama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu*

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, maelezo ya Serikali yanafafanua kuwa, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanya uchambuzi wa mwenendo wa utendaji wa Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika masuala mbalimbali ikiwemo

usimamizi wa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2021/22. Taarifa ya Wakurugenzi wote ambao wamebainika kuwa na utendaji usioridhisha imewasilishwa kwa Mamlaka ya Uteuzi kwa ajili ya hatua stahiki.

Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea na ufuatiliaji ambapo: Kati ya Halmashauri 155 zenye hoja ya kushindwa kukusanya **Shilingi Bilioni 47.01** zilizotolewa kwa vikundi mbalimbali, Halmashauri 126 zimeweza kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 16.17** sawa na Asilimia 34 ya mikopo iliyohojiwa. Aidha, Kati ya Halmashauri 83 zilizohojiwa kushindwa kuchangia **Shilingi Bilioni 6.68**, Halmashauri 37 zilichangia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 jumla ya **Shilingi Bilioni 2.12** sawa na asilimia 31 ya kiasi kilichohojiwa.

***2.2.2 Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa***

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa iliyowasilishwa na Serikali kuhusu hoja Tatu zilizotolewa katika azimio hili, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeeleza yafuatayo:-

i. Kuhusu kuzingatia matakwa ya Sheria, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuhakikisha kuwa zinazingatia Sheria ya Matumizi inayopitishwa na Bunge kila mwaka;

ii. Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikipokea fedha nyingi zaidi ikilinganishwa na Halmashauri nyingine kutokana na utaratibu uliowekwa kupitia Waraka wa Hazina Na.1 wa Utekelezaji wa Bajeti kwa kila mwaka ambao umeelekeza kwamba fedha za maendeleo kila mwaka lazima ziombwe. Hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango hutoa fedha kwenda Halmashauri baada ya kupokea maombi kutoka Halmashauri husika zikiwa zimeambatisha vielelezo vyote muhimu vya miradi husika kama vile mikataba, michanganuo ya gharama za miradi na vyeti vya malipo.

Aidha, kwa kuwa baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikisuasua kwenye utekelezaji wa maelekezo hayo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kuzielekeza Ofisi za Wakuu wa Mikoa kusimamia na kuratibu zoezi la maombi ya fedha kwa Halmashauri zote ndani ya Mkoa na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa wakati.

iii. Kuhusu Urejeshaji wa fedha ambazo hazijatumika kwenye Mfuko Mkuu mwishoni mwa mwaka wa fedha; Kamati imeelezwa kuwa zoezi hilo hufanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Bajeti Sura 439. Hata hivyo, marekebisho yaliyofanyika mwaka 2021 ya Kanuni ya 21 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti, yameruhusu fedha ambazo hazijatumika kuvuka mwaka unaofuatia baada ya kuomba na kuridhiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kabla au ifikapo tarehe 30 Juni ya mwaka husika. Hivyo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kuzisimamia Halmashauri kuhakikisha kuwa zinazingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti na Kanuni ya 21.

Aidha, kwa sasa Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika mapitio ya Sheria ya Bajeti Sura 439 na Kanuni zake ili kufanya maboresho ya vipengele mbalimbali vya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Wakati wa mapitio hayo, Bunge litapata nafasi ya kuona namna ya kufanya marekebisho kwenye Sheria hiyo hususan kwenye maeneo yenye shida.

**2.2.3 Uwekevu na Tija katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azimio lililotolewa katika eneo hili, Serikali imeeleza yafuatayo:-

i) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wengine, imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji na Ugharamiaji wa Miradi ya Kuzalisha Mapato (National Guideline for Developing and Financing Income Generating Infrastructure Projects). Mwongozo huu umeainisha hatua za uandaaji wa miradi kuanzia hatua ya kuibaini, kuandaa andiko, utekelezaji, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ili kuwezesha Halmashauri kufanya uwekezaji unaozingatia fursa za uwekevu na tija katika eneo la Halmashauri husika;

ii) Kuunda Timu ya Kitaifa ambayo imejumuisha baadhi ya Wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri ili kuzijengea uwezo na kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuibua miradi ya kimkakati na kuandaa maandiko; na

iii) Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa (Mipango na Uratibu) wamejengewa uwezo kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji na Ugharamiaji wa Miradi ya Kuzalisha Mapato (National Guideline for Developing and Financing Income Generating Infrastructure Projects).

**2.2.4 Manunuzi na Mikataba ya Upatikanaji wa Huduma na Bidhaa Mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

i) Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imefanya mafunzo kwa Maafisa Ununuzi na Ugavi pamoja na Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri zote 184 kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na Kanuni zake ili kuwajengea uwezo na kuwawezesha kutekeleza wajibu wao ipasavyo kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Manunuzi; ii) Muundo wa Sekretarieti za Mikoa umeimarishwa ambapo miongoni mwa maboresho yaliyofanyika ni kuanzishwa kwa Sehemu ya Menejimenti, Ukaguzi na Ufuatiliaji ambayo pamoja na majukumu mengine ina wajibu wa kufanya ukaguzi na ufuatiliaji kwenye Halmashauri kila robo mwaka kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ununuzi wa umma, ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa mali za Halmashauri, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na usimamizi wa rasilimali watu. Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24, Sekretarieti za Mikoa zimeongezewa jumla ya Shilingi bilioni 4.48 ili kuwezesha shughuli za ukaguzi na ufuatiliaji kwenye Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu uchukuaji wa hatua ni kwamba,

i) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa barua yenye Kumb.Na.CAG.26/322/01/31 ya tarehe 17 Mei, 2022,

iliwasilisha taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na kumwomba kufanya uchunguzi wa kina kwenye maeneo yenye viashiria vya udanganyifu na upotevu wa fedha za Umma na kuchukua hatua stahiki;

ii) Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Desemba, 2022, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanya tathmini ya utendaji wa Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi kwenye Halmashauri zote. Kufuatia matokeo ya tathmini hiyo, Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi wamechukuliwa hatua mbalimbali ikiwemo kuwaondoa Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi 23 katika nafasi zao na kuwapangia majukumu mengine kutokana na utendaji usioridhisha na kuwabadilishia vituo vya kazi Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi 68 kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuondoa utendaji kazi wa mazoea; na

iii) Kuna Wakurugenzi wa Halmashauri wameondolewa kwenye nafasi zao kutokana na uwepo wa dosari mbalimbali ikiwemo zinazohusiana na ununuzi wa umma. Wakurugenzi hao ni pamoja na waliokuwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya za Buchosa, Sengerema, Masasi, Muheza, Iramba, Ushetu, Buhigwe, Ludewa, Mvomero, Jiji la Mbeya na aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo.

### *2.2.5 Upatikanaji wa Stahili za Watumishi kwa Mujibu wa Sheria*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepata fursa ya kupitia majibu ya Serikali kuhusu eneo hili na imefafanua kuwa,

i) Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imelipa malimbikizo ya mishahara ya jumla ya **Shilingi Bilioni 78.22** kwa watumishi 66,233 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijumuisha watumishi waliostaafu 1,702 waliolipwa **Shilingi Bilioni 3.90** na watumishi wengine 64,531 walio katika orodha ya mishahara ambao wamelipwa **Shilingi bilioni 74.32**;

ii) Vile vile, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali imelipa jumla ya **Shilingi Bilioni 25.5** ikihusisha madai yasiyo ya mishahara kwa watumishi na wazabuni wa Mamlaka za Serikali za Mitaa; iii) Kutokana na uchambuzi uliofanyika kuhusu uwezo wa Halmashauri, imebainika kuwa kuna baadhi ya Halmashauri hazina uwezo wa kugharamia kwa asilimia 100 shughuli za uendeshaji pamoja na stahili za watumishi. Hivyo, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24 Serikali itawasilisha Bungeni ombi la stahili za Wakuu wa Idara na Vitengo katika Halmashauri zigharamiwe kwa ruzuku kutoka Serikali Kuu badala ya mapato ya ndani ya Halmashauri husika.

***2.2.6 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri***

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kuwa, hadi tarehe 31 Machi, 2023 mfumo wa TAUSI tayari umefungwa na unaendelea kutumika katika Halmashauri 169. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa Halmashauri 15 zilizosalia katika Mikoa ya Kigoma na Singida, zinafungiwa Mfumo wa TAUSI na kuanza kuutumia kabla ya tarehe 1 Julai, 2023 kama ilivyoazimiwa na Bunge.

Kuhusu Azimio la kuchukuliwa hatua kwa watendaji wote waliokusanya mapato nje ya utaratibu Serikali imeeleza kuwa imetekeleza yafuatayo:-

i) Wakurugenzi wa Halmashauri zenye kasoro mbalimbali ikiwemo usimamizi usioridhisha wa mapato ya ndani wamekuwa wakichukuliwa hatua stahiki ikiwemo kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi na kuwaondoa kwenye nafasi za ukurugenzi kama ilivyofanyika kwa waliokuwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Manispaa za Iringa, Singida na Halmashauri ya Wilaya ya Chato;

ii) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa barua yenye Kumb.Na.CAG.26/322/01/31 ya tarehe 17 Mei 2022, iliwasilisha kwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Taarifa ya Ukaguzi ya CAG ambayo imebainisha kasoro mbalimbali katika ukusanyaji wa mapato. Kwa barua hiyo, Mkurugenzi

Mkuu aliombwa kufanyia kazi maeneo yenye viashiria vya upotevu wa fedha za Umma ikiwemo fedha zitokanazo na makusanyo ya mapato ya ndani; na

iii) Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kwa barua yenye Kumb.Na.PCCB/08/3/Vol.LXXXII/120 ya tarehe 17 Januari, 2023 ametoa mrejesho kwamba, Taasisi hiyo inaendelea kufanyia kazi taarifa hiyo.

***2.2.7 Matumizi yasiyofaa ya Fedha katika Akaunti za Amana***

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyowasilishwa na Serikali katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

i) Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanya ufuatiliaji kwenye Halmashauri 81 zinazohusika na hoja hii na kubaini kuwa Halmashauri 17 zilizokuwa na hoja ya jumla ya **Shilingi Bilioni 1.38** sawa asilimia 19 ya fedha zote zilizohojiwa, zimetoa ufafanuzi na vielelezo vinavyojitosheleza vya uhalali wa matumizi ya fedha hizo na hivyo CAG amefunga hoja husika kwenye Halmashauri hizo;

ii) Halmashauri 31 zimerejesha fedha zilizoazimwa kutoka akaunti ya amana jumla ya **Shilingi bilioni 1.87**, sawa na asilimia 19 ya fedha zote zilizohojiwa na CAG; na

iii) Kwa kuwa Halmashauri 33 hazijarejesha kiasi chochote cha fedha zilizohojiwa, Wakurugenzi wa Halmashauri hizo wametakiwa kutoa maelezo ya sababu za uwepo wa kasoro hizo ili hatua stahiki za kinidhamu ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

***2.2.8 Upotevu wa Mapato katika Mifumo ya Kieletroniki ya kukusanya mapato***

**Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti mianya ya kufanyika kwa marekebisho ya miamala bila kuzingatia taratibu, Taarifa ya Serikali imefafanua kuwa, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeboresha zaidi mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya ndani (TAUSI) kwa kuuwekea udhibiti kama ifuatavyo:-

i) Kupitia mfumo huo, mwombaji wa marekebisho ya miamala analazimika kuambatisha vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa marekebisho yanayoombwa. Mfumo wa LGRCIS ulikuwa haumlazimishi mwombaji kuambatisha vielelezo hivyo;

ii) Mkurugenzi wa Halmashauri anapaswa kuingia kwenye mfumo wa TAUSI na kutoa idhini ya marekebisho ya miamala ya mapato. Katika mfumo wa LGRCIS, idhini ya Mkurugenzi ilikuwa inatolewa nje ya mfumo; na

iii) Mfumo wa TAUSI umewezeshwa kutoa taarifa ya marekebisho ya miamala ya mapato. Hivyo, ni rahisi Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Ofisi za Wakuu wa Mikoa kufanya ufuatiliaji kwa wakati kuhusu marekebisho hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kueleza kuwa, CAG amehakiki na kufunga hoja hii kwenye Halmashauri 10 baada ya kuridhishwa na ufafanuzi na vielelezo alivyopatiwa na Halmashauri hizo. Halmashauri hizo ni Halmashauri za Wilaya za Kisarawe, Rorya, Chamwino, Bagamoyo, Nyasa, Kiteto, Mbozi, Kaliua, Korogwe, na Mji wa Nzega; Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilimpelekea Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU taarifa ya CAG na kumwomba kufanya uchunguzi wa kina na kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa maeneo yote yenye viashiria vya udanganyifu na upotevu wa fedha za Umma.

***2.2.9 Hasara ya kifedha kutokana na Vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri***

**Mheshimiwa Spika**, katika hoja hii, Serikali imetoa ufafanuzi katika masuala yafuatayo:-

**i) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefuatilia na kupata ufafanuzi wa NHIF kwamba changamoto hii ilitokana na kasoro zifuatazo:-

a) Baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya hutoa huduma kwa wanufaika wa NHIF bila kuhakiki uhai/uhalali wa uanachama wao na hivyo kutoa huduma kwa wanachama wasio hai/halali;

b) Baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya hutoa huduma kwa wanachama wa NHIF bila kuzingatia wigo/kititа cha mafao ambacho mwanachama husika anastahili kupata kupitia NHIF na hivyo kutoa huduma zilizo nje ya makubaliano; na

c) Baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya kutojaza kwa usahihi fomu za madai ya Bima ya Afya.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto zilizofafanuliwa na Serikali hapo juu, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

a) Kwa kushirikiana na NHIF yamefanyika mafunzo kwa Watumishi kuhusu ujazaji wa fomu/folio ya wagonjwa kwa kufuata miongozo ya NHIF na mwongozo wa Taifa wa Matibabu (STG);

b) Baadhi ya Halmashauri zimeunda Timu za Wataalamu (Daktari, Mfamasia, Mtaalam wa Maabara pamoja na Mhasibu) kwa ajili kupitia fomu/folio za wagonjwa kabla ya kutumwa na pia kupokea taarifa za malipo ya vituo vyote ili kubaini changamoto zinazosababisha makato katika mwezi husika na kutoa taarifa kwa Mganga Mkuu wa Wilaya; na

c) Baadhi ya Halmashauri zimewachukulia hatua za kinidhamu watumishi waliofanya uzembe katika ujazaji wa fomu/folio za wagonjwa ikiwa ni pamoja na kuwawajibisha kulipa makato waliyosababisha.

Aidha, Halmashauri husika zimefanya ufuatiliaji ambapo kati ya **Shilingi Bilioni 2.35** zilizohojiwa, **Shilingi Milioni 788.97** zimerejeshwa.

**ii) Bohari ya Dawa (MSD)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekiri kupokea maazimio ya Bunge na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utendaji wa MSD, ikiwa ni pamoja na:-

a) Kufanya mabadiliko ya watendaji ndani ya MSD kwa lengo la kuongeza tija ya taasisi ambapo kwa sasa Menejimenti

yote imebadilishwa pamoja na kuteua bodi mpya. Aidha, muundo wa taasisi hii unafanyiwa mapitio ili kuboresha utendaji wake;

b) Serikali inaendelea kutoa fedha, ambapo **Shilingi Bilioni 74** zimetolewa katika robo ya kwanza mwaka 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya na usambazaji wake. Serikali katika kuimarisha uwezo wa MSD kiutendaji imeendelea kulipa deni lake kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni 57**. Yote ni kuhakikisha MSD wananunua bidhaa za afya;

c) Serikali imeisimamia Bohari ya Dawa katika kuhakikisha inaingia mikataba ya muda mrefu (Framework agreement) na wazalishaji wa bidhaa za afya ili kuweza kuharakisha upatikanaji wa dawa kulingana na mahitaji. Jumla ya mikataba 176 imeingiwa kwa ajili ya bidhaa aina 1,152 zikiwemo bidhaa za kipaumbele.

d) Bohari ya Dawa (MSD) imewekewa vigezo vya upimaji wa ufanisi katika mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya ambapo kiashiria cha uwepo wa bidhaa za afya kimeboreshwa kutoka bidhaa toshelevu za mwezi mmoja hadi miezi minne ili kupima kiwango cha chini cha bidhaa za afya 290 ashiria. Lengo ni kuhakikisha bidhaa za afya zinapatikana wakati wote.

**iii) Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kuwa, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanya ufuatiliaji na kupata ufafanuzi kwamba, ucheleweshaji wa ununuzi wa magari ya Serikali ulitokana na uhaba wa uzalishaji wa vifaa aina ya microchips na semiconductors vinavyotumika kwenye magari. Changamoto hiyo ilitokana na mlipuko wa UVIKO 19. Aidha, kwa sasa mnyororo wa ununuzi wa magari duniani umeanza kuimarika na Serikali imeanza kupata magari kwa haraka na hivyo kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Serikali kuendelea kama ilivyokusudiwa

**iv) Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kuwa imeandaa Mkakati wa Kuboresha Utendaji Kazi wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) kwa muda wa miaka kumi (10) ili kuboresha utendaji wake kwa kuangali pia uwezekano wa kushirikisha sekta binafsi. Aidha, katika kuboresha huduma ya uendeshaji wa karakana, Serikali imetekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa Karakana kama ifuatavyo:-

i) Imenunua na kusambaza vitendea kazi muhimu vya karakana kama vile diagnostic mashine, car lifter, 3D wheel alignment na mashine za kubadilishia magurudumu kwenye karakana kuu, karakana za Mikoa yote 26 na karakana tatu (3) za ngazi za Wilaya;

ii) Imefanya ukarabati wa majengo na miundombinu ya karakana kuu na karakana za Mikoa ya Singida, Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Songwe, Arusha, Njombe, Geita, Pwani na karakana za ngazi za Wilaya (Kahama na Ifakara); iii) Inaendelea na ujenzi wa karakana mpya ya kisasa katika Jiji la Dodoma eneo la Kizota (Mandatory Inspection Facility Centre);

iv) Imenunua karakana sita (6) zinazotembea na hivyo kuwa na jumla ya karakana kama hizo saba (7) kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa matengenezo ya magari kwa maeneo yasiyofikika kwa urahisi; na

iv) Imeandaa mpango wa mafunzo kwa mafundi wote wa TEMESA ili kuimarisha ubora wa utendaji na utoaji huduma. Mafunzo kwa makundi matatu ya mwanzo yatahusisha fani za magari, umeme, viyoyozi na vivuko.

***2.2.10 Kuhusu Uteketezaji wa Dawa za Binadamu katika Hospitali na Vituo vya Afya.***

**Mheshimiwa Spika,** taarifa iliyopokelewa kutoka Serikalini inafafanua kuwa, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imezielekeza Halmashauri zote Tanzania Bara kuhakikisha zinazingatia yafuatayo: Kutopokea dawa ambazo muda wake wa kuharibika ni chini ya miezi sita (6) hasa kwa bidhaa zenye matumizi

madogo (Slow Moving Items); na kwa bidhaa na vitendanishi vya maabara ambavyo muda wa matumizi (Shelf Life) ni miezi mitatu (3) hadi sita (6), kuhakikisha zinapokelewa zile tu zinazoweza kutumika bila kusababisha hasara ya kuharibika vituoni.

***2.2.11 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utekelezaji wa maazimio iliyowasilishwa na Serikali, imeeleza hatua mbalimbali zilizochukuliwa kama ifuatavyo:-

i) Kulingana na uwezo wa kibajeti, Serikali itaendelea kuajiri wataalam ili kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

ii) Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali iliajiri Wahandisi 260 ambapo Wahandisi 194 walipangwa kwenye Halmashauri, Wahandisi 52 Sekretarieti za Mikoa na Wahandisi 14 TARURA;

iii) Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa barua yenye Kumb.Na.FA.10/431/01'A'/76 ya tarehe 13 Februari, 2023 imetoa kibali kuajiri watumishi 250 wakiwemo Wahandisi 100, Wakadiriaji Majenzi 100 na Maafisa Ununuzi 50. Wataalamu hawa watapangwa kwenye Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri; na

iv) Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa barua yenye Kumb.Na.FA.10/431/01'A'/74 ya tarehe 13 Februari, 2023 imetoa kibali kujaza nafasi 4,596 za watumishi walioondoka kwenye Utumishi wa Umma kwa sababu mbalimbali.

***2.2.12 Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa***

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yote ya CAG, Serikali imefafanua yafuatayo:-

i) Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikiwemo ushughulikiaji wa hoja na mapendekezo ya CAG. Hatua hizo ni pamoja na kuidhinishwa kwa muundo mpya wa Sekretarieti za Mikoa ambapo miongoni mwa maboresho yaliyofanyika kupitia muundo huo, ni kuanzishwa kwa Sehemu ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Ukaguzi ambayo pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kufuatilia kwenye Halmashauri utekelezaji wa mapendekezo ya CAG na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC);

ii) Kumekuwa na mwenendo mzuri wa utekelezaji wa mapendekezo ya CAG. Mfano, idadi ya mapendekezo yaliyotekelezwa kwa asilimia 100 imeongezeka kutoka mapendekezo 2,217 mwaka 2018/19 hadi mapendekezo 3,511 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 58; na

iii) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa, imefanya ufuatiliaji kwenye Halmashauri na kupata taarifa kwamba, mpaka Februari, 2023 jumla ya hoja za ukaguzi **7,723** zimehakikiwa na kufungwa, ikiwa ni sawa na **asilimia 61** ya hoja zote **12,731**. Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kuhakikisha kuwa Halmashauri zote zinafanyia kazi hoja za ukaguzi zilizosalia.

**2.3 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE**

**Mheshimiwa Spika**, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alipokea majibu ya Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio Kumi na Mbili ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. CAG alihakiki majibu hayo kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa na Serikali na kuwasilisha Taarifa yake ya uhakiki katika Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, uhakiki uliofanywa na CAG katika majibu yaliyowasilishwa na Serikali katika kila kipengele cha azimio, ulijikita katika kujiridhisha iwapo maazimio yametekelezwa kikamilifu na vielelezo vilivyowasilishwa na Serikali vinakidhi matakwa ya kikaguzi. Kwa msingi huo, maoni ya Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge yanayowasilishwa katika Bunge lako Tukufu leo hii ni yale ambayo CAG amejiridhisha kuwa hayakutekelezwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na ambayo Serikali imeeleza katika taarifa yake kuwa yametekelezwa lakini imeshindwa kuwasilisha vielelezo muhimu kwa ajili ya uhakiki. Maoni hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo:-

### *2.3.1 Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya akina Mama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu*

**Mheshimiwa Spika**, katika azimio hili, CAG alifanya uhakiki katika maeneo mbalimbali. Aidha, hadi Kamati inapowasilisha taarifa hii, hakuna majibu ya Serikali kuhusu Halmashauri 11 kushindwa kuhamisha **Shilingi Bilioni 1.24** kutoka akaunti ya Amana kwenda akaunti za mifuko ya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu kama walivyotakiwa kufanya kwa mujibu wa kanuni za uendeshaji wa Mfuko.

Vile vile, Taarifa ya Serikali imeshindwa kuieleza Kamati kuhusu Halmashauri 17 zilizotoa mikopo ya **Shilingi Bilioni 3.26** kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu bila kuzingatia uwiano ulioainishwa. Pamoja na hayo, Serikali imeshindwa kuthibitisha na kuwasilisha kwa ajili ya uhakiki vielelezo vya kuchangia kiasi kilichosalia cha **Shillingi Bilioni 4.28** kinachohusu hoja ya Halmashauri 83 kutokuchangia jumla ya **Shilingi Bilioni 6.68** kwenye mfuko kutoka kwenye mapato yake ya ndani.

### 2.3.2 Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, Bunge liliazimia katika maeneo matatu ikiwa ni pamoja na Serikali kuzingatia matakwa ya Sheria ya Matumizi, Serikali kuweka angalau ukaribiano wa kiasi fulani cha ruzuku na Serikali kutorejesha Hazina fedha zinazokuwa zimepelekwa katika Halmashauri. Uhakiki uliofanywa na CAG katika majibu ya Serikali umeeleza kuwa:-

a) Majibu ya Serikali hayajibu moja kwa moja Azimio la Bunge kwa ukamilifu, badala yake yamelenga kutoa ufafanuzi jinsi inavyozisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuhakikisha

kuwa zinazingatia Sheria ya Matumizi zinazopitishwa na Bunge kila mwaka. Vile vile, suala la Hazina kupeleka fedha zaidi au pungufu ya bajeti kwenye baadhi ya Halmashauri haijajibiwa kama Azimio la Bunge lilivyoelekeza.

b) Katika hoja ya pili, majibu ya Serikali yamelenga kuelezea utaratibu unaotumika katika utoaji wa fedha za Maendeleo. Azimio la Bunge lilitaka kuwepo na uwiano wa utoaji wa fedha kwa Halmashauri katika kuondokana na suala zima la baadhi ya Halmashauri kupata fedha kuliko bajeti iliyopitishwa na Bunge na baadhi ya Halmashauri kupata fedha kidogo ikilinganishwa na Bajeti iliyopitishwa na Sheria ya Matumizi ya fedha za kila mwaka; na

c) Hoja ya mwisho katika azimio la Bunge lilikuwa na makusudi ya kuhakikisha fedha zikishatolewa kwa Halmashauri hazirejeshwi Hazina mwishoni mwa mwaka wa fedha. Ili Azimio hili liweze kutekelezwa, Serikali inatakiwa kurekebisha Kanuni iliyotajwa kwenye majibu ya Serikali kwa lengo la kutekeleza Azimio hilo.

**2.3.3 Uwekevu na Tija katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma**
**Mheshimiwa Spika**, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amejiridhisha kuwa, vielelezo vilivyowasilishwa na Serikali kuhusu kuandaliwa kwa mwongozo wa namna bora ya uwekezaji havijakidhi matakwa ya azimio kwakuwa Mwongozo uliowasilishwa uliandaliwa kabla ya Azimio hili (Julai, 2021), hata hivyo, mwongozo huo bado haujaondoa matatizo yaliyoibuliwa na Kamati. Vile vile, utendaji wa Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa (Mipango na Uratibu) kuhusiana na kuzijengea uwezo Halmashauri, haukuweza kuthibitika kutokana na kutokuwepo na ushahidi wa shughuli hiyo kufanyika.

***2.3.4 Manunuzi na Mikataba ya Upatikanaji wa Huduma na Bidhaa Mbalimbali***
**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukweli kwamba Azimio hili halijatekelezwa kikamilifu, CAG ameeleza kuwa, Serikali inaendelea kuchukua hatua stahiki kwa Maafisa Masuuli wote walioshindwa kusimamia ipasavyo manunuzi ya Umma kwa kufanya mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na watumishi

waliohusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu. Hata hivyo, hatua zilizooneshwa kuchukuliwa na Serikali ni za kipindi kilichopita na hakuna maelezo yanayohusu hatua zilizochukuliwa katika kipindi cha utekelezaji wa maazimio.

***2.3.5 Upatikanaji wa Stahili za Watumishi kwa Mujibu wa Sheria***

**Mheshimiwa Spika**, uhakiki wa CAG umebaini kuwa, Serikali imeanza utekelezaji kwa kipengele kimoja tu cha kuingiza katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 stahili za Wakuu wa Idara na Vitengo na kuacha eneo kubwa ambalo lilihojiwa na Kamati na kufanya azimio hilo kutotekelezwa kikamilifu kwakuwa:-

a) OR-TAMISEMI haijatoa vielelezo vinavyoonesha kuwa Serikali imelipa malimbikizo ya mishahara kiasi cha **Shilingi Bilioni** 78.22**;**

b) Serikali haijawasilisha vielelezo vinavyoonesha watumishi wastaafu 1,702 walilipwa kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.90** na watumishi waliolipwa kiasi cha **Shilingi Bilioni 74.32**; na

c) Serikali haijawasilisha nyaraka kuonesha ililipa madai ya watumishi na wazabuni kiasi cha **Shilingi Bilioni 25.5.**

***2.3.6 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri***

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa CAG amehakiki kuwa, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 mfumo wa TAUSI tayari umefungwa na unaendelea kutumika katika Halmashauri 169, bado kuna Halmashauri 15 ambazo matumizi ya mfumo huu haujaanza. Hata hivyo, uhakiki kuhusu utendaji wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa TAUSI utafanyika wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha za mwaka 2022/23. Vile vile, hatua za kisheria zimechukuliwa kwa watendaji wote ambao walikuwa wakikusanya mapato nje ya utaratibu wa kisheria.

***2.3.7 Matumizi yasiyofaa ya Fedha katika Akaunti za Amana***

**Mheshimiwa Spika**, uhakiki uliofanywa na CAG katika eneo hili umebaini utekelezaji wa Serikali usiokamilika katika baadhi ya maeneo ambayo ni kukosekana kwa uthibitisho kuwa ORTAMISEMI imewasiliana na Halmashauri/Makatibu Tawala wa Mikoa juu ya maelekezo kwa Halmashauri zote ya namna ya

kusimamia akaunti za amana na kuepuka mapungufu yaliyoonekana katika Halmashauri 81 pamoja na kukosekana kwa uthibitisho wa hatua stahiki zilizochukuliwa kwa wahusika wa Halmashauri 14 ambazo hazijarejesha kiasi chochote cha fedha zilizoazimwa kutoka Akaunti ya Amana.

***2.3.8 Upotevu wa Mapato katika Mifumo ya Kieletroniki ya kukusanya mapato***

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha kuwa changamoto hii imeondolewa kikamilifu, CAG atafanya ufuatiliaji wa utendaji na ufanisi wa mfumo mpya wa TAUSI wakati wa ukaguzi wa Taarifa za fedha za mwaka 2022/23.

**2.3.9 Hasara ya kifedha kutokana na Vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili, Bunge lako liliitaka Serikali kuondoa changamoto za kiutendaji katika baadhi ya Taasisi zake kama Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Bohari ya Dawa (MSD), Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ambazo kutotekeleza wajibu wake kikamiifu kunachangia kuzorotesha utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini pamoja na kusababisha hasara ya kifedha katika Mamlaka hizo. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amefanya uhakiki wa hatua zilizochukuliwa na Serikali katika maeneo hayo. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya maeneo ambayo Serikali haijatekeleza ikiwa ni pamoja na Serikali kutoonesha mpango mkakati wa kuimarisha utendaji wa GPSA.

**2.3.10 Kuhusu Uteketezaji wa Dawa za Binadamu katika Hospitali na Vituo vya Afya**

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha kuwa hakuna Halmashauri itakayoingia hasara itakayotokana na uteketezaji wa Dawa za binaadamu zilizokwisha muda wake, CAG atafanya uhakiki wa utekelezaji wa azimio hili katika kaguzi zijazo.

***2.3.11 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya jitihada mbalimbali katika kuajiri wataalamu katika sekta muhimu. Hata hivyo, Serikali

haijawasilisha uthibitisho wa mkakati wa kutekeleza azimio la Bunge kwa CAG kwa ajili ya uhakiki.

***2.3.12 Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa***

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa ya mwaka 2021/2022 imeonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 kulikuwa na jumla ya mapendekezo yasiyotekelezwa 10,625 kati ya mapendekezo hayo, mapendekezo 4,408 (42%) yametekelezwa; mapendekezo 3,349 (32%) yako kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo 960 (9%) hayajatekelezwa; mapendekezo 1,566 (15%) yamejirudia; na mapendekezo 342 (3%) yamepitwa na wakati.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA USHAURI 3.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Taarifa iliyowasilishwa na Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge kutokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Aidha, baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupokea majibu ya Serikali na kuyahakiki kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa na Serikali, Kamati imepata fursa ya kupitia na kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu utelelezaji wa maazimio hayo. Kwa kuzingatia uchambuzi wa taarifa hizo mbili zilizowasilishwa, Kamati ina maoni kama ifuatavyo:-

**3.2 Maoni ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati yanazingatia majukumu ya Kikatiba ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali ikiwemo eneo la usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa mantiki hiyo, maoni ya ujumla ni kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika,** Ushauri wa Kamati unatolewa kwa kuzingatia uhakiki uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye ndiye jicho la Bunge katika kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ushauri huu umejikita zaidi katika mapendekezo yote **Kumi na Mbili** (pamoja na vipengele vyake Kumi na Tatu) yaliyotolewa na Bunge lako Tukufu ili kuwe na utekelezaji wa haraka wa maazimio hayo kwa maslahi mapana ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa naomba kulijulisha Bunge lako kuwa, hakuna Azimio hata moja lililotekelezwa kwa ukamilifu. Hali hii imetokana na uzembe wa makusudi uliofanywa na baadhi ya Maafisa Masuuli katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kudharau maazimio yaliyotolewa na Bunge. Hata hivyo, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Taarifa zote mbili umebaini kuwa, mengi yaliyoelezwa na OR – TAMISEMI, ni ufafanuzi tu wa hoja wa namna ya kutekeleza maazimio hayo badala ya utekelezaji wenyewe. Vile vile, kwa kiasi kikubwa, maelezo yaliyotolewa hayaendani na maazimio yaliyotolewa na Bunge. Mchanganuo wa utekelezaji wa Maazimio hayo kwa mujibu wa Taarifa iliyowasilishwa na CAG ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Namba 1** hapa chini.

**Jedwali Na 1. Mchanganuo wa Utekelezaji wa Maazimio**

| S/N | AZIMIO | KIPENGELE CHA AZIMIO (HOJA) | KIWANGO CHA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya akina Mama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu | a. Halmashauri 155 kushindwa kukusanya **Shilingi Bilioni 47.01** | Limetekelezwa kwa Asilimia 34 |
| | | b. Halmashauri 11 kushindwa kuhamisha **Shilingi Bilioni 1.24** kutoka akaunti ya amana kwenda akaunti ya mifuko | Halijatekelezwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | c. Halmashauri 17 zilitoa mikopo ya **Shilingi Bilioni 3.26** kwa vikundi bila kuzingatia uwiano ulioanishwa | Halijatekelezwa |
| | | d. Halmashauri 83 kutokuchangia jumla ya **Shilingi Bilioni 6.68** kwenye mfuko kutoka kwenye mapato yake ya ndani | Limetekelezwa kwa Asilimia 36 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa | a. Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Matumizi zinazopitishwa na Bunge | Halijatekelezwa |
| | | b. Kuweka angalau ukaribiano wa kiasi fulani cha ruzuku | Halijatekelezwa |
| | | c. Kutorejesha HAZINA fedha zinazokuwa zimepelekwa katika Halmashauri | Halijatekelezwa |
| 3. | Uwekevu na Tija katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma | N/A | Halijatekelezwa |
| 4. | Manunuzi na Mikataba ya Upatikanaji wa Huduma na Bidhaa Mbalimbali | N/A | Halijatekelezwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | Upatikanaji wa Stahili za Watumishi kwa Mujibu wa Sheria | N/A | Halijatekelezwa |
| 6. | Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri | a. Kuhakikisha kuwa Mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato (TAUSI) unaanza kutumika katika Halmashauri zote | Limetekelezwa kwa Asilimia 92 |
| | | b. Kuchukua hatua kali za kisheria kwa watendaji wote ambao wanakusanya mapato nje ya utaratibu | Halijatekelezwa |
| 7. | Matumizi yasiyofaa ya Fedha katika Akaunti za Amana | N/A | Limetekelezwa kwa Asilimia 41 |
| 8. | Upotevu wa | N/A | Halijatekelezwa |
| | Mapato katika Mifumo ya Kieletroniki ya kukusanya mapato | | |
| 9. | Hasara ya kifedha kutokana na Vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri | a. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya | Limetekelezwa kwa Asiimia 33 |
| | | b. Bohari ya Dawa (MSD) | Halijatekelezwa |
| | | c. Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) | Halijatekelezwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | d. Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | Halijatekelezwa |
| 10. | Kuhusu Uteketezaji wa Dawa za Binadamu katika Hospitali na Vituo vya Afya | N/A | Utekelezaji Unaendelea |
| 11. | Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo | N/A | Halijatekelezwa |
| 12. | Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa | N/A | Limetekelezwa kwa Asilimia 42 |

**Mheshimiwa Spika**, tangu kuwasilishwa kwa Taarifa ya CAG Bungeni na kutolewa kwa maazimio haya, Serikali ilikuwa na muda wa kutosha wa kupitia hoja zote zilizotolewa pamoja na kuanza utekelezaji wake. Hali ya utekelezaji wa maazimio hayo ni wa kiwango kidogo kama ambavyo inaonekana katika Jedwali Namba 1 hapo juu. Ni mtazamo wa Kamati kuwa, Serikali (Mamlaka za Serikali za Mitaa) imeonesha viashiria vya kulidharau Bunge kwa kuacha kutekeleza maazimio yaliyotolewa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kutokuwepo kwa utaratibu maalumu kwa ajili ya kuratibu zoezi zima la utekelezaji wa maazimio ya Bunge baina ya Taasisi za Serikali. Hali hiyo imesababisha vielelezo muhimu kushindwa kufikishwa kwa CAG

kwa wakati kwa ajili ya uhakiki kinyume na Ibara ya 143 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na Kifungu cha 11 (a) na (b) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura ya 418.
Kamati ilipata nafasi ya kukutana na CAG tarehe 06 Juni, 2023 ambapo iliarifiwa kuwa, Serikali ilichelewa kupeleka majibu ya utekelezaji na vielelezo kwa ajili ya uhakiki. Aidha, Serikali iliwasilisha Taarifa ya utekelezaji tarehe 25 Mei, 2023 na siku nne baadaye tarehe 29 Mei, 2023 ndipo ilipowasilisha baadhi ya vielelezo, hali iliyopelekea CAG kushindwa kufanya jukumu lake la uhakiki wa majibu ya Serikali kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, limebainika tatizo la CAG kutopewa baadhi ya nyaraka na vielelezo muhimu kwa ajili ya kufanya uhakiki pale anapohitaji kufanya hivyo. Kwa kufanya hivyo, kunakwamisha na kuchelewesha utekelezaji wa majukumu ya jicho la Bunge pamoja na jitihada za Bunge za kuhakikisha tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Umma yanaondolewa na kunakuwa na ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufuatilia utekelezaji wa maazimio haya, Kamati imebaini changamoto ya kukosekana kwa mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali (Serikali kutozungumza) hali inayochangia kuchelewa kwa utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Hali ilivyo sasa, hapakuwa na utaratibu wowote wa Taasisi za Serikali kukutana ili kutekeleza Maazimio ya Bunge kwa pamoja. Majibu yaliyowasilishwa ni maelezo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI pekee badala ya Serikali kwa ujumla wake.
Kamati inaitaka Serikali kuandaa utaratibu maalumu utakaotumika kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maazimio yote yatakayokuwa yanatolewa na Bunge na kuwasilisha mapema vielelezo hivyo kwa CAG kwa ajii ya uhakiki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasikitishwa na vitendo vya baadhi ya Mamlaka za nidhamu za watumishi kutowajibika ipasavyo kwa kushindwa kuchukua hatua stahiki kwa watumishi waliobainika kufanya ubadhirifu na upotevu wa fedha za Umma kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 na Kanuni zake na

badala yake kuibebesha mzigo na kuitumia TAKUKURU kama kichaka cha kuchelewesha utekelezaji wa maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa na Serikali, Kamati imebaini utaratibu usioridhisha wa kuwahamisha Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo waliofanya kazi kinyume na matakwa ya Sheria za Nchi kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine badala ya kuwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria. Hali hii inasababisha mwendelezo wa matatizo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kusababisha mashaka kwa wananchi kuwa, upo uwezekano kwamba wakosaji wanashirikiana na wenye Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maoni hayo ya jumla, Kamati ina maoni kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kwa kila azimio lilitolewa na Bunge kama ifuatavyo:-

### *3.2.1 Mfuko wa Mikopo kwa vikundi vya akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu*

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa hoja hii, Kamati ilishindwa kupata majina ya Wakurugenzi waliobainika kuisababishia hasara Serikali kwa kushindwa kwa uzembe kusimamia utoaji wa mikopo hiyo na hatua zilizochukuliwa dhidi yao.

Aidha, uchambuzi wa Kamati katika azimio hili umebaini kuwa, katika Halmashauri 155 ambazo zilishindwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 47.01** zilizotolewa kwa vikundi mbalimbali, ni Halmashauri 129 pekee ndizo zilizoweza kukusanya **Shilingi Bilioni 16.17** ambayo ni sawa na **Asilimia 34** ya fedha zote zilizohojiwa na kiasi ambacho hakijakusanywa ni sawa **Asilimia 66** ya fedha zote. Katika Halmashauri 129 zilizokusanya fedha hizo, Halmashauri 31 zilitekeleza kikamilifu agizo la Bunge kwa kukusanya kiasi chote kilichohojiwa, Halmashauri 95 zilikusanya kiasi tu cha fedha kilichohojiwa na Wakurugenzi wa Halmashauri 29 waliamua kutotekeleza Agizo la Bunge kwa kutokusanya kiasi chochote cha fedha. Mchanganuo wa namna kila Halmashauri ilivyotekeleza agizo hili umefafanuliwa katika **kiambatisho Namba 1** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini ukiukwaji wa Kanuni za uendeshaji wa Mfuko kwa Halmashauri 11 ambazo zilishindwa kuhamisha **Shilingi Bilioni 1.24** kutoka Akaunti ya Amana kwenda akaunti za mifuko ya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. Mpaka kuwasilishwa kwa Taarifa hii ya Kamati, hakuna majibu ya Serikali kuhusu azimio hili, hali inayotia mashaka kuhusu matumizi sahihi ya fedha hizo. Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuhamisha kiasi hicho cha fedha ni **kiambatisho Namba 2** cha Taarifa hii.

Kuhusu hoja ya Halmashauri 17 zilizotoa mikopo ya **Shilingi Bilioni 3.26** kwa vikundi bila ya kuzingatia uwiano, Serikali imeshindwa kutoa majibu kuhusu hoja hii na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ili kufahamu iwapo fedha hizo zimewafikia walengwa au kuna dalili yoyote ya ubadhirifu wa fedha za Umma. Orodha ya Halmashauri zilizokiuka utaratibu ni **kiambatisho Namba 3** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, jumla ya Halmashauri 83 zilibainika kutochangia jumla ya **Shilingi Bilioni 6.68** kwenye mfuko kutoka kwenye mapato yake ya ndani ambapo hadi Kamati ilipokutana na CAG kiasi kilichokuwa kimechangiwa ni **Shilingi Bilioni 2.4** tu. Katika kiasi hicho kilichotolewa, Halmashauri 32 pekee ndizo zilizotekeleza kikamilifu agizo hilo kwa kuchangia kiasi chote cha fedha kilichohojiwa na Halmashauri 12 zilichangia sehemu ya kiasi cha fedha kilichohojiwa.

Aidha, Kamati imesikitishwa na utendaji wa Halmashauri 39 ambazo hazikuchangia kiasi chochote cha fedha kama ilivyoelekezwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, bado kuna kiasi cha **Shilingi Bilioni 4.45** sawa na **Asilimia 64** ambacho hakijapelekwa katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutoka katika mapato ya ndani ya Halmashauri zilizotajwa katika **Kiambatisho Namba 4** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, katika hoja hii ya mfuko wa mikopo kwa vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, dosari zote ziizoibuliwa

katika Halmashauri mbalimbali nchini za kushindwa kukusanya fedha zilizotolewa kwa vikundi, hasara kutokana na kukiuka Kanuni za uendeshaji wa Mfuko, kutoa mikopo bila kuzingatia uwiano pamoja na kushindwa kuchangia katika mfuko kutoka katika mapato ya ndani, kwa ujumla wake zimesababisha upotevu wa fedha za umma wa jumla ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 39.79** ambazo zingetumika katika uendeshaji wa mfuko huo.

Vile vile, zimebainika Halmashauri zenye matatizo sugu ambapo matatizo yake yamekuwa yakijirudia katika hoja nyingi zilizoibuliwa na CAG. Baadhi ya Halmashauri hizo ni H/Mji Geita, H/W Songwe, H/W Rungwe, H/Jiji Tanga, H/W Musoma na H/W Shinyanga

### 3.2.2 Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, Azimio la Bunge lililenga kuhakikisha kunakuwa na uzingatiaji wa Kifungu cha 50 (a-c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 inazozitaka Taasisi za Serikali kutumia kiasi cha fedha ambacho hakizidi kile kilichoidhinishwa na Bunge katika bajeti yake. Hata hivyo, majibu ya Serikali hayajalenga kujibu azimio hili la kupeleka fedha pungufu au zaidi ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Kwa upande mwingine, Azimio liliitaka Serikali kuhakikisha fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hazirejeshwi Hazina ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha husika. Hata hivyo, rejea iliyofanywa na Serikali, ya Kanuni ya 21 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti haiondoi tatizo lililopo katika Halmashauri jambo ambalo ni kiashiria cha dharau kwa maamuzi yaliyotolewa na Bunge.

### *3.2.3 Uwekevu na tija katika uwekezaji wa Mitaji ya Umma*

**Mheshimiwa Spika**, wajibu ya Bunge ni kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinatumika katika kuleta maendeleo kwa wananchi. Hata hivyo, kumekuwa na utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo haina tija wala faida kwa wananchi wa maeneo husika. Hali hii inasababishwa na baadhi ya wataalamu

wa Halmashauri wasio na uwezo katika kuandaa miradi yenye kuzalisha mapato na kuwanufaisha wananchi.

Uchambuzi umebaini kutotekelezwa kwa agizo hili kwakuwa, Taarifa ya Serikali haijaeleza mipango madhubuti ya kuondoa changamoto iliyoibuliwa katika Halmashauri zilizo nyingi nchini na badala yake imetoa Taarifa ya Mwongozo ulioandaliwa Mwezi Julai, 2021 kabla ya kutolewa kwa maazimio haya ambao kimsingi haujaondoa tatizo ambalo Kamati ilibainisha katika Taarifa yake ya Mwezi Novemba, 2022.

### 3.2.4 Manunuzi na Mikataba ya upatikanaji wa Huduma na Bidhaa mbalimbali

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Kanuni zake kwa baadhi ya Maafisa Masuuli katika Halmashauri mbalimbali nchini. Lengo la Azimio lilikuwa ni kuhakikisha watendaji wote waliohusika na upotevu wa fedha za Umma kulikosababishwa na kukiukwa kwa matakwa ya Sheria hiyo kuchukuliwa hatua stahiki.

Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali kwa kukiuka maazimio yaliyotolewa na Bunge kwa kuwaondoa katika nafasi zao Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi 23 waliobainika kuwa na utendaji usioridhisha na kusababisha hasara kwa kuwapangia majukumu mengine badala ya kuwawajibisha na kulipia hasara waliyoisababisha kama ilivyoainishwa na Kanuni ya 53 ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, kwakuwa kuwaondoa pekee ni kuzidi kuiongezea mzigo Serikali (wage bill) kwakuwa watalipwa mishahara yao kama ambavyo walivyokuwa katika nafasi zao za awali.

Katika hoja hiyo hiyo, Serikali imeeleza kuwabadilisha vituo vya kazi Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi 68 kinyume na Azimio la Bunge la kuwachukulia hatua kali za kisheria. Tafsiri ya haraka na maoni ya Kamati kuhusu hoja hii ni kuhamisha tatizo kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine ikiwa ni pamoja na kuwaaminisha watumishi hao kuwa, hakuna hatua zozote za

kisheria zitakazochukuliwa dhidi yao pindi watakapokiuka taratibu za kiutendaji.

**3.2.5 Upatikanaji wa Stahili za Watumishi kwa mujibu wa Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, hoja ya Kamati ilijikita katika watumishi **33,405** ambao wanadai malimbikizo ya muda mrefu ya mishahara yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 63.83** pamoja na madai mengine ya watumishi **71,670** yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 96.65**. Hata hivyo, katika hali isiyo ya kawaida, Serikali imetoa maelezo ya kulipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi **66,233** kiasi cha **Shilingi Bilioni 78.22** jibu ambalo ni tofauti na hoja iliyoibuliwa na Kamati. Aidha, CAG ambaye ndiye jicho la Bunge hajapelekewa vielelezo vya kuthibitisha kufanyika kwa malipo ya kiasi kilichotajwa katika Taarifa ya Serikali.

Taarifa ya Serikali imeeleza kuwalipa watumishi wengine 64,531 kiasi cha **Shilingi Bilioni 74.32** lakini hakuna vielelezo vilivyowasilishwa kwa CAG kuhusiana na malipo hayo. Vile vile, Serikali imeshindwa kuwasilisha kwa ajili ya uhakiki nyaraka zinazoonesha malipo ya **Shilingi Bilioni 25.5** kwa watumishi na wazabuni. Kwa muktadha wa huo, azimio hili halijatekelezwa.

***3.2.6 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri***

**Mheshimiwa Spika**, Azimio la Bunge liliitaka Serikali kuhakikisha hadi kufikia mwezi Juni, 2023, Halmashauri zote 184 zianze kutumia mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato wa TAUSI. Hata hivyo, hadi kuwasilishwa kwa Taarifa hii ya Kamati, bado kuna Halmashauri 15 zilizopo katika Mikoa ya Kigoma na Singida ambazo hazijaanza kutumia mfumo huu. Jambo hili ni kinyume na maelekezo ya Bunge na linatoa viashiria vya upotevu wa mapato yanayokusanywa katika Halmashauri hizo kwakuwa mfumo wa awali wa ukusanyaji wa mapato ulishaonesha udhaifu.

Kwa upande mwingine, Kamati haijajulishwa idadi ya Maafisa Masuuli ambao wamechukuliwa hatua kwa kukusanya mapato nje ya utaratibu wa kisheria na ambao hawapeleki fedha hizo benki kwakuwa, utaratibu huo ni kinyume na matakwa ya Kifungu cha 42 (2) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 ambacho kinaelekeza kuwa, stakabadhi zote zinazohusiana na

Mamlaka ya Serikali ya Mitaa zitalipwa katika akaunti ya benki au akaunti iliyothibitishwa na Mamlaka hiyo.

***3.2.7 Matumizi yasiyofaa ya Fedha katika Akaunti za Amana***

**Mheshimiwa Spika**, lengo la agizo hili lilikuwa ni kuhakikisha kunakuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha za Umma. Licha ya kwamba, Maafisa Masuuli wa Halmashauri zote nchini wanafahamu utaratibu wa kuingiza na kutoa fedha katika Akaunti ya Amana, bado kumekuwa na ukiukwaji wa matumizi ya fedha zilizowekwa katika akaunti hiyo kwa baadhi yao ambapo, ripoti ya CAG ilibainisha matumizi mabaya ya **Shilingi Bilioni 9.74** kutoka katika akaunti za amana za Halmashauri 81.

Hadi CAG anawasilisha taarifa yake ya uhakiki kwa Kamati, Halmashauri 19 zilizokuwa na hoja ya jumla ya **Shilingi Bilioni 1.43** zimewasilisha vielelezo na kuhakikiwa na CAG na jumla ya **Shilingi Bilioni 2.57** zilizohojiwa kutoka Halmashauri 35 zimerejeshwa. Hata hivyo, bado kuna Wakurugenzi wa Halmashauri 27 ambao hawajarejesha fedha zilizochukuliwa kutoka katika akaunti ya Amana zenye jumla ya kiasi **cha Shilingi Bilioni 5.74** kinyume na maelekezo ya Bunge.

***3.2.8 Upotevu wa Mapato katika Mifumo ya Kielektroniki ya kukusanya mapato***

**Mheshimiwa Spika**, upotevu wa mapato unaotokana na matumizi yasiyo sahihi ya mifumo, umekuwa ni tatizo sugu linalosababishwa na kutokuwepo kwa uwajibikaji. Katika hoja hii, Kamati haijaridhishwa na Taarifa iliyowasilishwa kwakuwa, Serikali haijatoa maelezo yoyote juu ya namna kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.6** kilichohojiwa kinaweza kurejeshwa. Aidha, uthibitisho wa vielelezo kuhusu ulazima wa kufanya marekebisho hayo kwenye mfumo kwa Halmashauri 17 kati ya 27 zilizohojiwa havijapatikana na havijawasilishwa kwa CAG kwa ajili ya uhakiki. Vile vile, Serikali haijatoa orodha ya Wakurugenzi waliohusika na hasara hiyo kwa kufuta na kubadilisha miamala ya mapato iliyopo katika mfumo bila ya uthibitisho wowote.

### 3.2.9 Hasara ya kifedha kutokana na vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri

**Mheshimiwa Spika**, katika azimio hili, Taasisi mbalimbali ambazo zinafanya kazi na Halmashauri zilihusika. Kwa upande wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) bado kuna kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.56** ambacho hakijalipwa kwa Halmashauri kutokana na huduma za tiba zilizotolewa kwa Wanufaika wa Mfuko huo.

Aidha, hadi kuwasilishwa kwa Taarifa hii, kiasi kilicholipwa kwa Halmashauri zinazodai ni **Shilingi Milioni 788.97** ambacho ni sawa na **Asilimia 33** tu ya kiasi chote cha **Shilingi Bilioni 2.5** kilichohojiwa.

Kuhusu Bohari ya Dawa (MSD), azimio la Bunge lilikuwa ni kuitaka Taasisi hiyo kupeleka dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya **Shilingi Bilioni 1.7** kwa Halmashauri ambazo zilishafanya malipo. Hata hivyo, majibu yaliyotolewa hayajalenga katika kujibu hoja ya msingi, na dawa na vifaa tiba hivyo havijapelekwa katika Halmashauri husika. Huku ni kuzorotesha juhudi za Serikali katika kuimarisha afya na ustawi wa wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika**, majibu yaliyotolewa kuhusu Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) kuchelewesha upatikanaji wa magari yanayoagizwa na Halmashauri yameonesha kutokuwepo kwa mpango mkakati wa kuimarisha utendaji wa GPSA ili kuondoa changamoto zilizoainishwa. Changamoto hii imebainika pia kwa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ambapo Taasisi hii imeshindwa kuzisaidia Halmashauri zetu katika eneo la ukaguzi na matengenezo ya magari na mitambo. Juhudi za makusudi za Serikali zinatakiwa ili kuimarisha utendaji wa Taasisi hizi.

### 3.2.10 Kuhusu Uteketezaji wa Dawa za Binaadamu katika Hospitali na Vituo vya Afya

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi katika eneo hili ambapo, katika Mwaka wa fedha 2018/19 Halmashauri 14 ziliteketeza dawa zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 7.3**, Mwaka

2019/20 Halmashauri 31 (**Bilioni 1.5**) na Mwaka 2020/21 Halmashauri 46 (**Bilioni 3.5**). Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kulichukua suala hili kwa uzito wake na kulitekeleza kama ilivyoeleza, kwakuwa fedha nyingi za Umma ambazo zingeweza kutumika katika kuwaletea maendeleo wananchi, zinatumika katika kuteketeza Dawa ambazo zimeisha muda wake wa matumizi.

### *3.2.11 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikipeleka fedha nyingi katika Halmashauri zetu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Hata hivyo, miradi mingi imekuwa haileti tija iliyokusudiwa kutokana na wataalamu walioaminiwa kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo kukosa taaluma zinazohusika kwa miradi husika. Hata hivyo, Serikali haijafafanua kwa kina kuhusu Ikama ya watumishi yenye upungufu na idadi ya wataalamu ambao wameshaajiriwa mpaka sasa kuona ukubwa wa tatizo lililopo na kushauri namna bora ya kukabiliana na changamoto hiyo. Mfano wa miradi yenye mapungufu ambayo haikusimamiwa vema kutokana na uhaba wa wataalamu umetolewa katika **kiambatisho Namba 5** cha
Taarifa hii.

### 3.2.12 Mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna changamoto kubwa ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwa Halmashauri mbalimbali nchini kwakuwa, tangu Ripoti ya CAG iwasilishwe Bungeni mwezi Aprili, 2022, ni **Asilimia 42** pekee ya mapendelezo yote ambayo yametekelezwa kikamilifu. Hali hii haitoi taswira nzuri kwa utendaji wa Halmashauri zetu kwakuwa, kutotekelezwa kwa mapendekezo hayo kunaashiria kujirudia kwa matatizo yaliyobainishwa na CAG katika kila mwaka wa fedha pamoja na kutothamini kazi kubwa inayofanywa na Jicho la Bunge katika kubainisha mapungufu mbalimbali yaliyopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati. Vile vile, kwa namna ya kipeeke, napenda kukushukuru na kukupongeza kwa kuhakikisha jukumu la Bunge la kuisimamia Serikali linatekelezwa kikamilifu na kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. Uchambuzi, maoni na ushauri wa wajumbe wote wa Kamati umewezesha kupatikana kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Halima James Mdee, Mb. - **Mwenyekiti**
2) Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb. - **M/M'kiti**
3) Mhe. Ally Mpembenwe Twaha, Mb. - Mjumbe
4) Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb. - Mjumbe
5) Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb. - Mjumbe
6) Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb. - Mjumbe
7) Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi, Mb. - Mjumbe
8) Mhe. Jesca J. Msambatavangu, Mb. - Mjumbe
9) Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb. - Mjumbe
10) Mhe. Lemburis Saputu Mollel, Mb. - Mjumbe
11) Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb. - Mjumbe
12) Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb. - Mjumbe
13) Mhe. Ally Juma Makoa, Mb. - Mjumbe
14) Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb. - Mjumbe
15) Mhe. Michael C. Mwakamo, Mb. - Mjumbe

16) Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb. - Mjumbe
17) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb. - Mjumbe
18) Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb. - Mjumbe
19) Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, Mb. - Mjumbe
20) Mhe. Abdul Yusuf Maalim, Mb. - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi, ndc. kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kusomwa kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho japo siyo kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere.

**4.2 Wasilisho**

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati yanalenga katika kuimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vile vile, Serikali itambue kwamba, ukaguzi unaotekelezwa na CAG ni kwa niaba ya Bunge na kwamba, Hoja zote za ukaguzi zinazotolewa na CAG ni Hoja za Bunge hivyo utekelezaji wake unatakiwa kufanyika kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya ufafanuzi huo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba Bunge lako Tukufu lipokee maoni ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokanayo na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, na kwamba Serikali ikatekeleze Maazimio yote ya Bunge ambayo utekelezaji wake haujakamilika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Halima James Mdee, Mb.
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**
27 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)*. Mheshimiwa Jerry William Silaa.

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuwasilisha Taarifa yenye Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Yaliyotolewa Wakati wa Kujadili Taarifa ya Kamati, Mwezi Novemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kufikia siku ya leo nimesimama hapa mbele kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati. Kutokana na ufinyu wa muda naomba taarifa hii yote kama inavyosomeka katika Kitabu cha Kamati iingie katika Kumbukubu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Masharti ya Fasili ya 1(a) na (b) ya Kifungu cha 11, Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma inalo jukumu la kufuatilia, kuchambua na kubaini iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma uliofanyika kwenye mashirika mbalimbali unafuata misingi na taratibu zilizopo na iwapo unaleta tija iliyokusudiwa. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa maelezo yako, kamati ilipata fursa ya kufuatilia utekelezaji wa Maazimio 13 ya Bunge ambayo yalitolewa wakati Bunge lilipokuwa likichambua na kujadili Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma inayohusu Utendaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne. Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili ina Maelezo ya Maazimio 13 kama yalivyopitishwa na Bunge lako Tukufu na vilevile inaeleza Utekelezaji wa Serikali pamoja na Maoni ya Msajili wa Hazina ya Utekelezaji huo. Sehemu ya Tatu inaelezea Maoni na Ushauri wa Kamati na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

Mheshimiwa Spika, Njia Zilizotumika na Kamati Kufanya Kazi ya Kutekeleza Jukumu Hili. Kamati ilitumia njia zifuatazo:-

(a) Kamati ilipata fursa ya kuyapitia tena Maazimio yote 13 ya Bunge.

(b) Kamati kupitia na kuchambua Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

(c) Kamati ilipitia na kuchambua uchambuzi na maoni ya Msajili wa Hazina kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

(d) Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji kwa kuzingatia maoni ya Msajili wa Hazina na hatimaye tuliandaa taarifa kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio. Kamati ilipokea maelekezo yako juu ya kushughulikia Taarifa ya Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa Katika Mkutano wa Tisa wa Bunge Wakati wa Kujadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(Public Investment Committee)* kwa Lengo la Kuleta Mrejesho kwa Bunge kwa Hatua za Utekelezaji wa Maazimio Hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilipitia Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa kwa kipindi hicho, kipengele cha maazimio na kujiridhisha kuwa Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio iliyowasilishwa na Serikali imezingatia maazimio yale yaliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Baada ya kujiridhisha Kamati ilianza kufanya uchambuzi wa utekelezaji wake

na kuoanisha utekelezaji wa Serikali pamoja na Maoni ya Msajili wa Hazina Juu ya Utekelezaji wa Taarifa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Rejea ya Maazimio ya Bunge. Kwa rejea na kwa lengo la kuweka kumbukumbu sawa Maazimio 13 yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma yameainishwa kwenye Taarifa ya Kamati hapo chini.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maazimio kwa Mujibu wa Taarifa ya Serikali Pamoja na Maoni ya Msajili wa Hazina. Katika kufanya ufuatiliaji wa maazimio haya Serikali iliwasilisha utekeleaji wa maazimio hayo. Sambamba na hilo Msajili wa Hazina aliwasilisha Taarifa yake iliyotokana na ufuatiliaji na uhakiki wa Taarifa ya Utekelezaji wa Serikali na Maoni yake Juu ya Utekelezaji Huo kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Lengo la taarifa hii ni kuleta mrejesho wa utekelezaji wa maazimio ambayo yalipitishwa na Bunge lako Tukufu wakati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kamati imepitia, kuchambua na kujadili maazimio yaliyotolewa, Taarifa ya Serikali Juu ya Utekelezaji wa Maazimio hayo pamoja na Maoni ya Msajili wa Hazina Kuhusiana na Utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imewasilisha hatua mbalimbali za utekelezaji wa Maazimio 13 yaliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa Tisa wa Bunge. Serikali imejitahidi kuzingatia na kutekeleza maagizo hayo ambapo katika Maazimio 13 Kamati imeridhika na hatua ya utekelezaji wa maazimio matano. Maeneo ambayo Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa Serikali yameainishwa kwenye taarifa hii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taasisi Kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa Muda Mrefu Kutokana na Kuchelewa Kuteuliwa kwa Wajumbe wa Bodi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bado kuna changamoto ama ucheleweshaji katika kupata Bodi

za Wakurugenzi za Mashirika ambapo Bunge lako Tukufu liliazimia kuwa Serikali itumie miezi mitatu kukamilisha uteuzi wa wajumbe wa bodi 12 kwenye Wizara tisa ambazo tayari zina wenyeviti, lakini hadi kufikia tarehe ya kikao cha kamati ni taasisi saba ndio zilikuwa zimekamilisha akidi na taasisi tano zilikuwa bado.

Mheshimiwa Spika, Bunge lilitoa miezi mitatu, lakini ni miezi saba sasa na jambo hili halijakamilika. Aidha, Bunge liliazimia kuwa Serikali itumie miezi sita kukamilisha uteuzi wa wajumbe wa bodi 23 kwenye Wizara 12 ambazo hazina bodi. Hadi kufikia tarehe ya kuwasilisha taarifa hii tayari taasisi 17 ndio zilikuwa zimepatiwa bodi na taasisi sita zilikuwa bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa kamati kuwa Serikali itafute utatuzi wa kudumu kwani utaratibu wa Msajili wa Hazina taasisi zote hutoa taarifa miezi tisa kabla. Ni maoni ya kamati kwamba, kama muda huu utatumika ipasavyo unatisha kabisa kukamilisha taratibu zote za taasisi kupata bodi. Kamati inapendekeza kama Wizara itakuwa makini kwa jambo hili ambalo hata Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alishalizungumzia wakati anapokea Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa serikali, tarehe 28 Machi, 2022 ufike wakati lisijirudie tena kwani taasisi kukosa bodi inapunguza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Hatua za Majadiliano Katika Mradi wa Mchuchuma na Liganga Kuchukua Muda Mrefu. Bunge lako Tukufu liliazimia kuwa Serikali ihakikishe kuwa mazungumzo yanayoendelea katika Kamati ya Majadiliano ya Serikali *(GNT)* yafikie mwisho ndani ya miezi mitatu au yapelekwe *NDC*. Kamati inatambua kwamba, kuna juhudi mbalimbali zinafanywa na Serikali katika kutekeleza azimio hili ikiwa ni pamoja na Serikali kutoa kiasi cha shilingi bilioni 15.4 ambayo imelipwa kama fidia kwa wanaopisha mradi na tayari wananchi wameshaanza kulipwa fidia. Ni hatua nzuri na inaonesha kuwa sasa eneo hili liwe tayari kwa ajili ya mradi kuanza. Kamati inasisitiza majadiliano hayo yaendelee kwa umakini na yafike mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Upungufu wa Mtaji wa Kampuni ya Ndege *(ATCL)* Unaosababishwa na Utaratibu wa Kukodisha

Ndege Kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali *(TGFA)*. Azimio la Bunge lilikuwa kuwa *TGFA* ikamilishe utaratibu na kurudisha umiliki wa ndege kwa *ATCL* kwani ukiondoa tatizo hili *ATCL* ina uwezo wa kujiendesha kwa faida. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Serikali iliunda Kamati ya Pamoja ya kushughulikia jambo hili ikiwemo masuala ya kiufundi, kisheria na kimkataba. Kazi hii imekamilika na kuwasilishwa ripoti kwa Baraza la Mawaziri. Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iweke muda maalum *(Time Frame)* wa mashauriano na utekelezaji wa jambo hili ili kuirudishia *ATCL* uwezo wa kujiendesha kwa faida.

Mheshimiwa Spika, Kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)*. Azimio la Bunge liliitaka Serikali itekeleze ahadi yake iliyoitoa kwa *TADB* ya kuiongezea mtaji kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa kila Mwaka wa Fedha lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na tija kwenye sekta ya kilimo. Uchambuzi wa kamati ulibaini kuwa azimio limetekelezwa, japo si kwa njia iliyokusudiwa ya awali ya kutoa bilioni 100 kila mwaka ambapo Serikali imeamua kutekeleza kwa kuiruhusu *TADB* kutafuta mikopo nafuu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha. Benki hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo. Kamati inasisitiza Serikali irejee kwenye ahadi yake ya kuipatia *TADB* shilingi bilioni 100 kila Mwaka wa Fedha ambapo kama ingekuwa imetekelezwa *TADB* ingekuwa na mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 760 kwa sasa na benki hii ingekuwa kwenye nafasi ya kuwahudumia wakulima wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kuathirika kwa Kilimo cha Pamba Kutokana na Maelekezo ya Serikali ya Mwaka 2019 ya Kuuza Pamba kwa Bei ya Juu Zaidi ya Bei la Soko la Dunia. Jambo hili lilisababisha deni la kiasi cha shilingi bilioni 21.8 kwa Serikali, limeathiri taswira ya Bodi ya Pamba kwa wakulima na limeongeza changamoto katika biashara ya kilimo cha pamba,

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu liliazimia kuwa Serikali iharakishe utekelezaji wa ahadi yake ya kulipa deni la pamba. Hatua hiyo itasidia kuongeza ufanisi wa sekta hiyo na kurudisha taswira Chanya ya Bodi ya Pamba. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa kuwa, Serikali ilikwishakamilisha uhakiki wa deni hili, msimu wa pamba umekwishazinduliwa na madeni ya watoa

huduma wa pamba kwenye benki yamesababisha benki nyingi kutokuwa tayari kuwakopesha, jambo lilisababisha ununuzi wa pamba kwa msimu huu kuanza kwa kusuasua. Malipo ya madeni haya yasipofanyika kwa haraka inaweza kusababisha kuwaathiri wakulima wa pamba ambao tayari wameshaanza uvunaji wa pamba. Kamati inasisitiza Serikali itimize ahadi yake ya kulipa deni hili mapema ndani ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na bajeti yake ionekane kwenye Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya TEHAMA Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* Ambapo *NHIF* Umeonesha Udhaifu Katika Utoaji wa Huduma Zake. Jambo hili limesababisha mfuko kupata hasara kunakosababishwa na kutokuwa na mfumo thabiti wa TEHAMA ambayo inatoa mianya ya kufanya udanganyifu kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa pamoja na Serikali kuripoti kuwa *NHIF* ina mifumo madhubuti ya TEHAMA, lakini bado kuna malalamiko makubwa ya watendaji wa shirika hili. Pamoja na kuwa wametoa majibu ya tehema, lakini majibu haya ni mepesi ukilinganisha na hali halisi iliyopo. Kamati inaona kuwa bado kuna malalamiko makubwa sana juu ya utendaji wa kazi wa shirika hili na kamati haioni umakini wa Menejimenti ya Shirika. Kamati inashauri Serikali iandae mkakati madhubuti wa kulisimamia shirika kwani, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kuwa kama shirika hili haliko katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Shukrani; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa namna unavyoliongoza Bunge letu Tukufu na kutoa fursa kamati kuweza kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Maazimio haya ya Bunge kuhakikisha Serikali inatekeleza kikamilifu. Ushauri na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Aidha, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika taasisi na mashirika ya umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa Taifa. Vilevile napenda kumshukuru Msajili wa Hazina Ndugu Nehemia Mchechu pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ushirikiano wa dhati walioutoa kwa Kamati wakati Kamati inatekeleza jukumu hili la kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo wa uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua wajumbe hao, majina yao ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. Kutokana na changamoto ya muda naomba nisiyasome, ila naomba yaingie kwenye Taarifa rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini sio kwa umuhimu. Nawashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa J. Mwihambi kwa uratibu wa shughuli za kamati na kutoa ushauri unaostahiki na kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wote kwa kusikiliza taarifa hii. Na sasa naomba Kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu Kukubali na Kupokea na Kujadili Maoni ya Kamati Juu ya Utekelezaji wa Maazimio 13 ya Bunge ambayo yalitolewa wakati wa Bunge lilipokuwa likichambua na kujadili Taarifa ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma inayohusu Utendaji wa Mashirika ya Umma.

**27 JUNI, 2023**

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YALIYOTOLEWA WAKATI WA KUJADILI TAARIFA YA KAMATI MWEZI NOVEMBA, 2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)

---

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kufikia siku ya leo nimesimama hapa mbele kuwasilisha taarifa hii ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 1 (a) na (b) ya Kifungu cha 11, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma inalo jukumu la kufuatilia, kuchambua na kubaini iwapo Uwekezaji wa Mitaji ya Umma uliofanyika kwenye mashirika mbalimbali unafuata misingi na taratibu zilizopo na iwapo unaleta tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa maelekezo yako Kamati ilipata fursa ya Kufuatilia utekelezaji wa Maazimio Kumi na tatu (13) ya Bunge ambayo yalitolewa wakati Bunge lilipokuwa likichambua na kujadili taarifa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) iliyohusu utendaji wa Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu **Nne**, Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili imegawanyika katika vipengele viwili ambapo kipengele cha kwanza kimeelezea rejea ya Maazimio yote kumi na tatu kama yalivyopitishwa na Bunge lako Tukufu na kipengee cha pili kimebainisha utekelezaji wa Serikali pamoja na maoni ya Msajili wa Hazina kuhusiana na utekelezaji huo. Sehemu ya Tatu inaelezea Maoni na ushauri wa Kamati na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

### 1.1 Njia zilizotumiwa na Kamati kufaya kazi

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilitumia njia zifuatazo:-

a) Kamati ilipata fursa ya kuyapitia tena maazimio yote kumi na tatu (13) ya Bunge kama yalivyotolewa Mwezi Novemba, 2022;

b) Kamati kupitia na kuchambua taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge;

c) Kamati ilipitia na kuchambua uchambuzi na maoni ya Msajili wa Hazina (TR) kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge; na

d) Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji kwa kuzingatia maoni ya Msajili wa Hazina na hatimaye tuliandaa taarifa kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge.

### 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea maelekezo yako juu ya kushughulikia taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge wakati wa kujadili taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa lengo la kuleta mrejesho kwa Bunge kwa hatua za utekelezaji wa maazimio hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilipitia taarifa ya Kamati iliyowasilishwa kwa kipindi hicho kipengele cha maazimio na kujiridhisha kuwa taarifa ya utekelezaji wa Maazimio inayowasilishwa na Serikali imezingatia maazimio yale yaliyohayopitishwa na Bunge lako tukufu. Baada ya kujiridhisha Kamati ilianza kufanya uchambuzi wa utekelezaji wake kwa kuoanisha utekelezaji wa Serikali pamoja na Maoni ya Msajili wa Hazina juu ya utekelezaji wa taarifa ya Serikali.

### 3.1 Rejea ya Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika**, kwa rejea na kwa lengo la kuweka kumbukumbu sawa maazimio kumi na tatu yaliyotokana na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni haya yafuatayo: -

#### *3.1.1 Taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kuteuliwa kwa wajumbe wa bodi;-*

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna Taasisi na Mashirika ya Umma 12 ambayo yana wenyeviti wa Bodi bila ya wajumbe na Taasisi na Mashirika ya Umma 23 hayana kabisa wenyeviti wala wajumbe wa Bodi, jambo ambalo ni ukiukwaji wa misingi ya utawala bora katika uwekezaji wa mitaji ya umma na kwamba ni jambo linalokwamisha upatikanaji wa tija ya uwekezaji unaofanywa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia mambo yafuatayo: -**

a) Serikali ikamilishe uteuzi wa wajumbe wa bodi 12 kwenye wizara 9 ambazo Rais ameshateua Wenyeviti ndani ya miezi 3;

b) Serikali ikamilishe uteuzi wa wajumbe wa bodi 23 kwenye wizara 12 ambazo hazina bodi ndani ya miezi 6;

c) Serikali ihakikishe inatimiza utaratibu wa kuanza maandalizi ya uteuzi wa Bodi mpya za Mashirika ya Umma au Taasisi zinazopaswa kuwa na Bodi ndani ya miezi tisa (9) kabla Wajumbe wa Bodi waliopo hawajamaliza muda wao.

#### 3.1.2 Uwezo wa SGR kuzidi uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam,

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Bandari ya Dar es salaam inauwezo mdogo wa kupokea mizigo ukilinganisha na uwezo wa SGR iliyoigharimu Serikali kwa uwekezaji mkubwa ilihali Bandari hiyo ni chanzo kikuu cha mizigo, jambo hii itachangia SGR isipate mzigo wa kutosha kwa ajili ya kusafirishwa pindi itakapo kamilika. Changamoto ya SGR kutokupata mzigo wa kutosha kusafirishwa

ni jambo litakalokwamisha kupatikana kwa tija ya uwekezaji uliofanyika na kwamba mkwamo huo utaweza kutatuliwa kwa kuongeza bandari ya Dar es Salaam na kujenga Bandari ya Bagamoyo.

**Mheshimiwa Spika, Bunge iliazimia kuwa: -**

a) Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo;

b) Serikali iharakishe zoezi la Kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaaam ikiwa ni pamoja na kuongeza Gati za kisasa katika Bandari ya Dar es Salaam na zoezi hilo likamilike kabla ya Ujenzi wa Reli ya SGR kukamilika.
   Hatua hii itasaidia SGR kupata mizigo ya kusafirisha hivyo kuleta tija iliyokusudiwa.

***3.1.3 Umuhimu wa Shirika la Taifa la Maendeleo – NDC,***

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mradi wa mchuchuma na liganga unachukua muda mrefu katika hatua za majadiliano ambayo kwa sasa yanayoratibiwa na Kamati ya Majadiliano ya Serikali – GNT. Kutokukamilika kwa majadiliano ambayo yanaendelea kwa muda mrefu ni jambo linalochelewesha upatikanaji wa manufaa ya mradi huo.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa,** Serikali ihakikishe kuwa mazungumzo yanayoendelea katika Kamati ya Majadiliano ya Serikali - GNT yafikie mwisho ndani ya miezi mitatu (3) au yapelekwe NDC lengo likiwa kuyamaliza na kupata tija iliyokusudiwa katika miradi hii kwa sababu Serikali imefanya mabadiliko katika taasisi hii ikiwemo kuipatia Bodi mpya ya wakurugenzi pamoja na Menejimenti.

***3.1.4 Mikopo Chechefu (Non-performing loans - NPLS),***

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Benki ya Maendeleo Tanzania – TIB na Benki ya Biashara Tanzania–TCB zinakabiliwa na changamoto ya kuwa na kiasi kikubwa cha mikopo chechefu (nonperforming loans – NPLS). Hali hiyo inaathiri mizania ya vitabu vya taasisi hizo, jambo ambalo ni hatari kwa misingi ya kibiashara na uendeshaji wa taasisi zinazotumia mitaji ya Umma.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa,**

a) Serikali ifanye tathimini ya madeni hayo na kuhakikisha wanayaondoa kwenye vitabu vya Benki hizo, bila kuathiri ulipaji wa mikopo inayolipika (performing loans). Hatua hiyo itasaidia benki hizo kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa; na

b) Serikali itengeneze mfumo fungamanishi kati ya bodi ya Uhasibu (NBAA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Taasisi za Fedha na Wafanyabiashara ili chanzo cha hesabu zote zinazotumiwa na wafanyabiashara kiwe kimoja. Hii itasaidia kukadiria kiwango halisi cha mkopo kinachoweza kulipika na mkopaji ili kupunguza mikopo chechefu.

***3.1.5 Upungufu wa Mtaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania – ATCL,***

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Kampuni ya Ndege Tanzania - ATCL inakabiliwa na changamoto ya mtaji hasi na changamoto ya uendeshaji wa biashara kutokana na utaratibu wa kukodisha ndege kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania – TGFA. Utaratibu ambao unaongeza madeni wanayodai (payables) katika vitabu vya TGFA.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa,** Wakala ya Ndege za Serikali Tanzania – TGFA ikamilishe taratibu za kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (alipokuwa anapokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 30 mwezi Machi, 2022) la kurudisha ndege kwa ATCL. Kwani ukiondoa tatizo hili ATCL inauwezo wa kujiendesha kwa faida.

***3.1.6 Kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya kilimo Tanzania – TADB,***

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa TADB ambayo ni Benki pekee inayohusika moja kwa moja na shughuli za kilimo lakini haijapatiwa mtaji wa kutosha wa kuendana na nia ya serikali ya kuongeza tija kwenye kilimo, kuleta mageuzi ya kilimo na kulisaidia taifa kufikia usalama wa chakula.

Pamoja na jitihada za Serikali za kuipatia TADB kiasi cha Bilioni 208 mwaka 2021, bado kuna ahadi ya serikali ambayo kama

ingetekelezwa Benki hii ingekuwa na mtaji wa jumla ya Sh. Bilioni 760. Kutofikiwa kwa mtaji huu kunaathiri ufanisi na tija katika sekta ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa,** Serikali itekeleze ahadi yake (commitment) waliyoitoa kwa TADB ya kuiongezea mtaji kiasi shilingi billioni 100 kwa kila mwaka wa fedha, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na tija katika Sekta ya Kilimo.

***3.1.7 Kuathirika kwa kilimo cha Pamba kutokana na maelekezo ya Serikali ya Mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya Soko la dunia*,**

Uchambuzi wa Kamati ilibaini kuwa, Serikali ilitoa agizo la zao la Pamba kununuliwa kwa bei ya juu zaidi ya bei ya soko la dunia, agizo hili limeathiri uwezo wa wanunuzi wa pamba kwa kiasi cha shilingi Bilioni 21.8 kiasi ambacho Serikali iliahidi kufidia deni hilo.
Deni hilo limeathiri taswira ya Bodi ya Pamba kwa wakulima na kuongeza changamoto katika biashara ya kilimo cha pamba.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa,** Serikali iharakishe utekelezaji wa ahadi yake ya kulipa deni la Pamba. Hatua hiyo itasaidia kuongeza ufanisi wa sekta hiyo na kurudisha taswira chanya ya Bodi ya Pamba.

***3.1.8 Mwingiliano wa majukumu kwa baadhi ya Taasisi za Umma, mfano ukiwa kwa taasisi ya TAA na TANROADS ambapo Mwaka 2017 Serikali iliamua majukumu ya TAA ya kujenga viwanja vya ndege yahamie TANROADS,***

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Mwaka 2017 Serikali iliamua majukumu ya TAA ya kujenga viwanja vya ndege yahamie TANROADS. Jambo hili ni kinyume cha viwango vya kimataifa na ni kinyume cha matakwa ya International Civil Aviation Organisation (ICAO) ambayo TAA ni mwanachama wake na ICAO inazitaka mamlaka za viwanja vya ndege kusimamia shughuli zote za viwanja vya ndege ikiwepo ujenzi wa viwanja vyao.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia,** Serikali itekeleze haraka agizo la kurejesha jukumu la Ujenzi wa Viwanja vya ndege kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – TAA pamoja na Rasilimali zake zote ikiwamo watumishi waliohama mwaka 2017, hii ni muhimu kwa ajili ya kukidhi vigezo vya Kimataifa katika uendeshaji wa viwanja vya ndege.

***3.1.9 Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA),***

Uchambuzi wa Kamati ilibaini kuwa Katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka 5, Serikali inaelekeza mageuzi ya kidigitali yanayojumuisha teknolojia ya TEHAMA kuwa nyenzo muhimu katika kuongeza ufanisi kwenye mifumo ya uzalishaji, huduma na utawala. Mashirika mengi ya umma hayazingatii matumizi sahihi ya TEHAMA hali inayopelekea upotevu wa mapato na udanganyifu katika utoaji wa huduma zake.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa: -**

a) Serikali ikamilishe mchakato wa Public Key Infrastructure (PKI);

b) Serikali iunde mfumo wa taarifa wa pamoja (centralized ledge) kuondoa udanganyifu wa mifumo ya taasisi; na

c) Serikali ihakikishe inasimamia kikamilifu taasisi na mashirika ya umma kuimarisha mifumo ya TEHAMA.
Hatua hizi itasaidia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma, ukusanyaji wa mapato, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kudhibiti udanganyifu kwa lengo la kupata tija iliyokusudiwa.

***3.1.10 Changamoto katika uendeshaji wa Kampuni ya Meli MSC,***

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Kampuni ya Meli (MSCL) iliyokuwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari kwa sasa imekuwa Kampuni huru inayojitegemea. Kitendo cha Mamlaka ya Bandari kuendelea kumiliki baadhi ya Mali za MSCL kunaathiri utendaji wa MSCL ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa mtaji wa umma uliowekwa MSCL;

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa,** Serikali ihakikishe kuwa, mali zote za MSCL zikiwemo cherezo, karakana na zinginezo zilizopo TPA, zinarejeshwa haraka kwa MSCL.

**3.1.11 Matumizi ya TEHAMA katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya – NHIF,**

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Taifa (NHIF) umeonyesha udhaifu katika utoaji wa huduma zake, jambo ambalo limepelekea Mfuko kupata hasara. Changamoto zilizojitokeza katika uendeshaji wa NHIF kwa kiasi kikubwa imetokana na kutokuwa na mfumo thabiti wa TEHAMA ambao inatoa mianya ya kufanya udanganyifu kwa urahisi.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa** Serikali ihakikishe NHIF inaandaa mfumo madhubuti wa TEHAMA na kuanza kuutumia haraka iwezekanavyo kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma wa mfuko na kuziba mianya ya udanganyifu.

**3.1.12 Matumizi Makubwa ya Gharama za Bima Za Ndege Kwa Shirika la Ndege la Taifa – ATCL,**

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Shirika la Ndege la Taifa ATCL linalazimika kununua Bima kutoka kwa Shirika la Bima la Taifa NIC, ambapo NIC ananunua Bima hizo kutoka kwa wakala wa nje ya nchi kwa mfumo wa moja kwa moja yaani Single Source. Changamoto zilizojitokeza ni kwa Shirika la ndege kujikuta linanunua Bima hizo kwa gharama kubwa hali inayopelekea kupunguza faida na tija ya Shirika.

**Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kuwa** Serikali iielekeze ATCL na NIC kufanya zabuni shindanishi ili kupata wakala mwenye bei nafuu, huduma bora na ambae atazingatia uwiano wa ndege shirika inazomiliki, hii italeta ufanisi, tija na kupunguzia shirika gharama za matumizi.

**3.1.13 Changamoto ya Kupata Vibali vya Kuajiri, Mheshimiwa Spika,**

Uchambuzi wa Kamati ilibaini kuwa Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara yanakabiliwa na changamoto ya

upungufu wa watumishi katika kujiendesha kwake kutokana na kutegemea mchakato wa ajira unaoendeshwa na Sekretarieti ya Ajira ya Utumishi wa Umma katika kupata watumishi. Changamoto hiyo inaathiri tija ya uwekezaji na manufaa yaliyotarajiwa kupatikana, kutokana na kukosa watumishi wanaostahili kwa wakati hata pale ambapo Shirika la Umma linapokuwa na uwezo wa mapato wa kuwalipa mishahara.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO KWA MUJIBU WA TAARIFA YA SERIKALI PAMOJA NA MAONI YA MSAJILI WA HAZINA

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya ufuatiliaji wa maazimio haya Serikali iliwasilisha utekelezaji wa maazimio hayo, sambamba na hilo Msajili wa Hazina aliwasilisha taarifa yake iliyotoka na ufuatiliaji na uhakiki wa taarifa ya Utekelezaji wa Serikali na maoni yake juu utekelezaji huo kama ifuatavyo;-

### *3.2.1 Taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kuteuliwa kwa wajumbe wa bodi;*

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imewasilisha utekelezaji wa azimio hili kuwa, hadi kufikia tarehe 27 Aprili 2023, kati ya Taasisi 248 zilizo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, Taasisi 212 zina Bodi hai, Taasisi 24 hazina Bodi kutokana na zilizokuwepo kumaliza muda wake na Taasisi 12 Bodi zake hazijatimiza akidi. Aidha, Ofisi imeendelea na utaratibu wa kukumbusha na kufuatilia mamlaka za uteuzi kukamilisha teuzi husika kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwafahamisha kuruhusu Bodi za Wakurugenzi zinazokaribia kumaliza muda ndani ya miezi 9 ila taratibu za uteuzi uanze kufanyika.

**Aidha,** uchambuzi wa Msajili wa Hazina ni kuwa Katika utekelezaji wa azimio la Bunge kuhusu ucheleweshwaji wa kuteuliwa kwa wajumbe wa Bodi, Serikali imeendelea kufanyiakazi changamoto hii na ufanisi umeendelea kuongezeka. Aidha, kuhusu Taasisi zilizobanishwa katika azimio hili, utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

- Kati ya Taasisi 23 ambazo hadi kufikia 31 Oktoba 2022 zilikuwa hazina Bodi, kufikia tarehe ya taarifa hii tayari Taasisi 17 zina Bodi ambayo ni asilimia 74% ya ufanisi;

- Kati ya Taasisi 12 ambazo hadi kufikia 31 Octoba 2022 zilikuwa hazina akidi, kufikia tarehe ya taarifa hii tayari Taasisi 7 zina akidi ambayo ni asilimia 58% ya ufanisi;

  Ili kuhakikisha kuwa wakati wote Taasisi, zinasimamiwa kwa mujibu wa Sheria, Ofisi itaendelea kukumbusha, na kufuatilia mamlaka husika kukamilisha mchakato wa uteuzi kwa wakati ili kuhakikisha kuwa Bodi za Wakurugenzi zinateuliwa kwa wakati.

***3.2.2 Uwezo wa SGR kuzidi uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam**,*
**Mheshimiwa Spika,** Serikali imejibu hoja hii kuwa

a) Serkali kupitia TPA imepanga kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo katika mwaka wa fedha 2023/24.

b) Serikali imekamilisha sehemu kubwa ya maboresho ya miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam. Tayari magati Na.0 hadi Na.7 yamekamilika na kazi za kuongeza Kina na Upana wa Lango la Kuingilia Meli na Eneo la Kugeuzia Meli imefikia asilimia 90 na itakamilika Agosti, 2023**.**

Magati yaliyokamilika yameendelea kutumika na ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam umeongezeka kutoka tani milioni 18.41 mwaka 2020/21 hadi tani milioni 20.43 mwaka 2021/22. Katika awamu ya pili ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam itakayoanza mwaka 2024/25, Serikali kupitia TPA itafanya maboresho na kujenga gati 12 hadi 15, gati jipya la kuhudumia shehena ya mafuta na ujenzi wa matenki ya kuhifadhia mafuta ili kuwa na uwezo wa kuhudumia meli kubwa. Kulingana na makadirio ya ukuaji wa shehena, Bandari ya Dar es Salaam inakadiriwa kuongezeka na kufikia tani milioni 47 kwa mwaka ifikapo mwaka 2045.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Msajili wa Hazina amewasilisha kuwa kuna juhudi zinazoendelea kufanyika kuhusu upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, pamoja na taratibu zinazoendelea

kuhusu ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo kuanzia mwaka wa fedha 2023/24, hoja ya SGR kuwa na uwezo mkubwa kuzidi uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam itakuwa imepatiwa ufumbuzi.

### *3.2.3 Hatua za majadiliano katika mradi wa Mchuchuma na Liganga kuchukua muda mrefu,*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali imeeleza kuwa, Wizara kupitia Kamati ya Majadiliano ipo katika hatua ya awali ya majadiliano ambapo NDC Ilikutana na Mwekezaji tarehe 12 Aprili, 2023 na kujadili kuhusu mstakabali wa mradi. Kikao kingine kitafuata mapema Mwezi Mei 2023, baada ya maandalizi kukamilika. Lengo kuu katika majadiliano haya ni kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na kama ni kuachana na mwekezaji wa sasa ifanyike pasipo kuleta hasara kwa Serikali na hatimaye kumpata mbia mwingine mwenye nia na uwezo wa kutekeleza mradi huo.

Aidha, Serikali tayari imetoa fedha za fidia Shilingi 15,424,364,900 kwa ajili kuwalipa wananchi watakaopisha mradi. Kutekelezwa kwa fidia kutawaondolea adha wananchi waliosubiri fidia hiyo kwa muda mrefu. Vile vile, kukamilisha ulipaji wa fidia kutaweka eneo la mradi tayari kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Ufuatiliaji na uchambuzi wa Msajili wa Hazina umefafanua kuwa Kikao cha Majadiliano kati ya NDC na Mwekezaji kilichopangwa kufanyika mwezi Mei, 2023 kitafanyika mwishoni mwa mwezi Juni, 2023.

Katika kuhakikisha kwamba Mradi wa Mchuchuma na Liganga unaanza bila kuchelewa zaidi, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliitisha Kikao cha pamoja na NDC tarehe 11 Mei, 2023 kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa mradi huu na miradi mingine ya Shirika ya Makaa ya Mawe. Katika Kikao hicho, pamoja na mambo mengine, NDC ilielekezwa kuhakikisha majadiliano yanayoendelea na mwekezaji SHG yanakamilishwa kwa haraka ili mradi uweze kuanza na kuingizia mapato NDC na Taifa kwa ujumla.

Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kufuatilia na kuisimamia NDC kwa ukaribu ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Mradi huu wa Kimkakati unaanza mapema iwezekanavyo na kuanza kuchangia katika pato la Taifa.

**3.2.4 Mikopo Chechefu (Non-performing loans - NPLS), kwa Benki ya Maendeleo Tanzania – TIB na Benki ya Biashara Tanzania–TCB,**

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Serikali imebainisha kuwa;-

a) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya tathmini ya mikopo chechefu iliyopo kwenye Benki ya TCB na TIB ambapo inaendelea kukamilisha mapendekezo kuhusu utaratibu bora utakaowezesha kuondoa mikopo chechefu katika vitabu vya Benki hizo na kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa shughuli za Benki hizo.

b) Bodi imeanza mchakato wa mabadiliko ya kanuni zinazoongoza tasnia ya uhasibu na ukaguzi nchini ambao utatoa muongozo na utaratibu wa uwasilishaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa kama hitaji la kisheria. Hata hivyo wakaguzi wote nchini watalazimika kuwasilisha hesabu zote walizokagua kabla ya kuziwasilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mchakato huu unategemewa kukamilika mwezi Juni, 2023.

Hata hivyo, Bodi imeanza kuunda mfumo wa kielektroniki utakaotumika katika uwasilishaji wa hesabu hizo na mfumo huo utaunganishwa na mifumo ya mamlaka nyingine za kiserikali kwa lengo la kurahisiha upatikanaji wa taarifa za hesabu zilizokaguliwa zitazotumika katika kufanya maamuzi mbalimbali. Mfumo huu unatajiwa kukamilika nakuanza matumizi mwezi juni 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Msajili wa Hazina kuhusu utekelezaji wa Kamati ni kuwa: -

a) Serikali imechukua hatua ya kuingiza kiasi cha Shilingi bilioni 30 katika Benki ya TCB mwezi Machi 2023, na inakamilisha utaratibu wa kutoa hati fungani maalum za Shilingi bilioni 101

ambayo itaenda kuiwezesha Benki ya TCB kuwa na ukwasi na mtaji toshelevu kujiendesha.

Kwa upande wa TIB, Serikali inaendelea na taratibu za ndani kuangalia namna bora ya kutatua changamoto za mtaji na ukwasi ili Benki iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

b) Kwa upande wa NBAA, Bodi inaendelea na taratibu za kukamilisha maboresho ya kanuni za tasnia ya uhasibu kuweka vifungu vitavyowalzaimu wakaguzi wote kuwasilisha Hesabu zilizokaguliwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Pia, kwa muktadha wa uandaaji wa Mfumo, Bodi pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, tayari ilishaanza kazi ya kuwa na mfumo fungamanishi ambao utarahisisha upatikanaji wa taarifa za Fedha za Taasisi na Mashirika ya Umma.

***3.2.5 Upungufu wa Mtaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania – ATCL, unaosababishwa na utaratibu wa kukodisha ndege kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania – TGFA;***

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya utekelezaji wa Serikali Serikali imeunda Kamati ya Wataalam ambayo inafanyia kazi suala hili ikiwemo masuala ya kiufundi, kisheria na kimkataba. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi Mei, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya Msajili wa Hazina ni kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina imewasiliana na Kamati husika na kutaarifiwa kuwa Kamati imemaliza kazi na kuandaa taarifa yake. Taarifa hiyo imewasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika mwezi Mei, 2023. Kwa sasa yanasubiriwa maelekezo ya Serikali juu ya hatua stahiki za kuchukua.

***3.2.6 Kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya kilimo Tanzania – TADB;***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali imefafanua kuwa Serikali imeendelea kuimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ili iwe na uwezo mkubwa zaidi wa kutoa mikopo na kutatua changamoto za mitaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi nchini. Hadi sasa Serikali imeshaweka kiasi cha Shilingi **Bilioni 322** kutoka Shilingi **Bilioni 60.0** zilizowekwa mwaka 2015 TADB ilipozinduliwa

rasmi. Aidha, Serikali imeiongezea benki ya TADB mtaji kwa kubadilisha mkopo wa shilingi **Bilioni 208** uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuwa mtaji.

Vilevile, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kutenga fedha za kuimarisha mitaji ya Taasisi na Mashirika ya Umma ambapo katika mwaka wa Fedha 2022/23 imetenga Shilingi **Bilioni 37** ya kuimarisha mitaji ya Taasisi na Mashirika ya Umma. Vile vile, TADB inaendelea kutekeleza mpango wa utafutaji wa fedha za gharama nafuu kwa ajili ya kuongeza uwezo wa utoaji wa mikopo kwa ushirikiano na Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, Maelezo ya Msajili wa Hazina kuwa Azimio linaendelea kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha kupitia bajeti ya Serikali kila mwaka. Aidha, hatua ya kutenga fedha kupitia Msajili wa Hazina kutarahisisha utekelezaji wa jukumu hilo.
Pamoja na jitihada hizi, Ofisi ya Msajili wa Hazina inakamilisha mchakato wa mabadiliko makubwa ya sheria yake ambayo pamoja na mambo mengine inawezesha Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa na Mfuko wa uwekezaji utakaosaidia kukwamua Mashirika yenye uhitaji wa mitaji kwa kufuata taratibu maalum zilizowekwa.

**3.2.7 Kuathirika kwa kilimo cha Pamba kutokana na maelekezo ya Serikali ya Mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya Soko la dunia, jambo lililosababisha deni la kiasi cha shilingi Bilioni 21.8 kwa Serikali, limeathiri taswira ya Bodi ya Pamba kwa wakulima na kuongeza changamoto katika biashara ya kilimo cha pamba;**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali inaelezea kuwa zoezi la uhakiki lilifanyika katika Ofisi ya Bodi ya Pamba Tanzania kuanzia tarehe 23 Februari, 2023 hadi 31 Marchi, 2023 ambapo madeni ya Shilingi **96,729,536,556.28** na USD **2,630,388.45** yaliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki, Aidha, madeni husika yalihusisha madeni ya Shilingi **74,451,737,309.71** na USD **2,630,388.45** wazabuni waliotoa huduma za pembajeo na Shilingi **22,277,799,246.57** hasara iliyotokana na ununuzi wa pamba msimu wa 2019/2020.

Kwa upande wa madeni ya wazabuni waliotoa huduma za pembejeo yaliyokidhi vigezo ni ya shilingi **71,678,099,163.40** na USD **2,630,388.45** na yasiyokidhi vigezo ni ya shilingi **2,764,638,146.31,** kwa upande wa madeni ya hasara iliyotokana na ununuzi wa pamba msimu wa 2019/2020 yaliyokidhi vigezo ni shilingi **21,410,877,476.80** na yasiyokidhi vigezo ni shilingi **866,921,769.77**.

Hivyo kwa ujumla madeni yaliyohakikiwa na kukidhi vigezo ni ya Shilingi **93,097,976,640.20** na USD **2,630,388.45** na madeni ambayo hayakukidhi vigezo kutokana na kukosekana kwa nyaraka, makosa katika ukokotozi na kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi ya bidhaa ni ya Shilingi **3,631,559,916.80**.

Taarifa husika yenye matokeo na mapendekezo kwa kina iliwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali tarehe 5 Aprili, 2023 kwa hatua zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Msajili wa Hazina unaelezwa kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kufuatilia madeni hayo yalipwe kama Serikali ilivyoahidi kulingana na upatikanaji wa fedha. Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imetenga Fedha mahsusi ya kulipa madeni kupitia Fungu 21 ikijumuisha madeni ya Bodi ya Pamba.

***3.2.8 Mwingiliano wa majukumu kwa baadhi ya Taasisi za Umma, mfano ukiwa kwa taasisi ya TAA na TANROADS ambapo Mwaka 2017 Serikali iliamua majukumu ya TAA ya kujenga viwanja vya ndege yahamie TANROADS;***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali inaeleza kuwa Serikali imeridhia kurejesha jukumu la ujenzi wa Viwanja vya Ndege kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwenda Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) kupitia barua ya Katibu Mkuu Kiongozi yenye Kumb. Na. SAB 20/558/01/C ya tarehe 30 Machi, 2023.

Taratibu za kurejesha jukumu la ujenzi wa Viwanja vya Ndege kutoka TANROADS kwenda TAA zinaendelea bila kuathiri

utekelezaji wa miradi inayoendelea kwa kuzingatia Maelekezo ya Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya Msajili wa Hazina ni kuwa, Baada ya Serikali kuridhia majukumu ya ujenzi wa viwanja vya ndege kutekelezwa na TAA badala ya TANROADS, Taasisi zinazohusika na mchakato huo zinaendelea na taratibu za utekelezaji.

**3.2.9 Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA), kama inavyoelekezwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka 5, kwa lengo la kuleta mageuzi ya kidigitali yanayojumuisha teknolojia ya TEHAMA kuwa nyenzo muhimu katika kuongeza ufanisi kwenye mifumo ya uzalishaji, huduma na utawala;**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali ni kuwa Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa kuna usimamizi sahihi kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma kwa kuhakikisha Taasisi na Mashirika ya Umma yanaimarisha na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kupitia mifumo ya uzalishaji na uendeshaji kwa kuzingatia matumizi sahihi ya TEHAMA

**Mheshimiwa Spika,** Msajili wa Hazina amewasilisha kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kushirikiana na Serikali katika kutekeleza suala hili.

**3.2.10 Changamoto katika uendeshaji wa Kampuni ya Meli MSC, inayosababishwa na baadhi ya Mali za MSCL kuendeles kumilikiwa na Mamlaka ya Bandari kitendo kinacho athiri utendaji wa MSCL ikiwa ni pamoja na kuathiri uendeshaji wa mtaji wa umma uliowekwa MSCL;**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali ni kuwa Kampuni ya Meli (MSCL) tayari imekabidhiwa chelezo, karakana na jengo la Ofisi eneo la Mwanza South Jijini Mwanza. Aidha, MSCL imekabidhiwa meli tatu (3) zilizokuwa zinamilikiwa na TPA katika Ziwa Nyasa, tarehe 07 Septemba, 2022.

Kuhusu mali nyingine, tayari timu ya pamoja ya wataalam kutoka MSCL na TPA imeainisha mali zote zinazotakiwa kurejeshwa MSCL. Hati ya makabidhiano (Deed of Hand Over) imeandaliwa na

kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa Upekuzi (vetting). Baada ya kukamilisha zoezi la upekuzi, Hati hiyo itasainiwa na pande zote mbili na hivyo kukamilisha mchakato wa urejeshaji wa mali zote zilizokuwa zinamilikiwa na TPA kwenda MSCL.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya msajili wa hazini kuhusu utekelezaji wa Serikali ni kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kufuatilia ukamilishaji wa Deed of hand over ili zoezi la uhamisho wa mali kutoka TPA kwenda MSCL liweze kukamilishwa.

**3.2.11 Matumizi ya TEHAMA katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya – NHIF, ambapo NHIF umeonyesha udhaifu katika utoaji wa huduma zake, jambo ambalo limepelekea Mfuko kupata hasara kunakosababishwa na kutokuwa na mfumo thabiti wa TEHAMA ambao inatoa mianya ya kufanya udanganyifu kwa urahisi;**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Serikali ni kuwa Mfuko wa NHIF umeendelea kujiimarisha katika matumizi ya TEHAMA ili kuimarisha utendaji wake na kuongeza ufanisi katika shughuli zake. Hadi sasa asilimia 90 ya shughuli za Mfuko zinatekelezwa kwa kutumia mifumo ya TEHAMA. Maeneo yanayotekelezwa kwa kutumia mifumo ya TEHAMA ni pamoja na;

a) Usajili wa Watoa huduma za Afya kwa njia ya kielekitroniki;

b) Uandikishaji wa wanachama na ukusanyaji wa michango kwa njia ya kielekitroniki iliyounganishwa na mifumo ya Taasisi nyingine ikiwemo GePG, NIDA, WCF na RITA;

c) Uhakiki wa wanachama kabla ya kupata huduma katika vituo vya afya kwa njia ya mtandao. Kwa sasa uhakiki wa uanachama unafanyika kwa njia ya alama ya vidole na uso (biometric identification) kwa wagonjwa wanachama wa Mfuko wanaopata huduma za kusafisha damu na wanafunzi;

d) Utoaji wa vibali katika vituo vya kutolea huduma kwa baadhi ya huduma kwa njia ya mtandao;

e) Uwasilishaji wa madai ya watoa huduma kwa njia ya mtandao (online claims submission); na

f) Mfumo wa kuchakata madai ya watoa huduma unaoweza kutambua viashiria vya udanganyifu na makossa yaliyomo katika madai.

Aidha, kwa kutambua umuhimu wa TEHAMA na kuongezeka kwa wigo wa wanachama na watoa huduma za afya, Mfuko utaendelea kuwekeza zaidi katika eneo la TEHAMA ili kuongeza ufanisi na tija katika shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Msajili wa Hazina kuwa Ofisi yake inaendelea kufuatilia utekelezaji wa matumizi ya TEHAMA kwa Mfuko sambamba na kupitia muundo wa matumizi ili kupunguza matumizi kwa NHIF.

**3.2.12 Matumizi makubwa ya Gharama za Bima Za Ndege Kwa Shirika la Ndege la Taifa – ATCL, ambapo ATCL inalazimika kununua Bima kutoka kwa Shirika la Bima la Taifa NIC, ambapo NIC ananunua Bima hizo kutoka kwa wakala wa nje ya nchi kwa mfumo wa moja kwa moja yaani Single Source;**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Serikali ni kuwa Serikali imepokea maelekezo kuhusu zabuni shindani katika kupata wakala wa bima mwenye bei nafuu na huduma bora kwa ATCL. Aidha, ili kuondoa migogoro kwa bima zilizokwishakatwa kupitia NIC, ATCL itasubiri hadi ifikapo tarehe 06 Julai, 2023 ambapo bima hizo zinafika kikomo. Baada ya hapo bima zote zitakazokatwa na ATCL zitakuwa shindanishi kama ilivyoelekezwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Msajili wa Hazina ni kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina inakubaliana na Azimio hili la Bunge kwamba bima zote zitakazokatwa na ATCL ziwe kwa njia ya ushindani ili kupunguza gharama za matumizi ya Shirika katika kukata bima.

Hivyo, baada ya bima zote kufikia ukomo tarehe 06 Julai, 2023, kuanzia mwaka ujao wa fedha (2023/24), ATCL isisitizwe kuwa inakata bima zake kwa njia ya ushindani.

### *3.2.13 Changamoto ya Kupata Vibali vya Kuajiri,*

**Mheshimiwa Spika,** Kabla ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, Ajira katika Utumishi wa umma zilikuwa zikishughulikiwa na Mamlaka za waajiri yakiwemo Mashirika ya Umma. Hata hivyo, katika ushughulikiaji huo kulikuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upendeleo, rushwa, kuajiri watu ambao hawana sifa na uwezo, kuajiri watu wa kutoka eneo moja, kushindwa kutimiza takwa la kisheria la kuajiri asilimia 21 ya watumishi kutoka Zanzibar (kwa Taasisi za Muungano) pamoja na ukiukwaji wa taratibu za usaili ikiwemo kutozingatia misingi ya ushindani na uwazi katika mchakato wa ajira kama inavyosisitizwa katika Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008. Hali hii ilisababisha kuwepo kwa malalamiko kutoka kwa wa waombaji kazi na wananchi kwa ujumla pamoja na kuanza kujengeka kwa matabaka makubwa katika Utumishi wa umma, hali iliyoanza kutishia mshikamano na umoja wa kitaifa.

Katika kukabiliana na changamoto hizo Serikali iliamua kujenga Mfumo rasmi wa Ajira kwa kuanzisha Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kama chombo huru cha kusimamia masuala ya ajira katika Utumishi wa Umma. Kuanzia wakati huo, ajira zimekuwa zikishughulikiwa kwa kuzingatia Kifungu 6A (2) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 kikisomwa kwa pamoja na Kanuni D (7) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la mwaka 2009. Uwepo wa Chombo hiki cha Ajira umeleta mafanikio ikiwa ni pamoja kuwawezesha Watanzania wote wenye sifa kuweza kupata ajira.

Pamoja na mafaniko yaliyopatikana baada ya kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma, kumekuwepo na changamoto ya ucheleweshaji wa mchakato wa ajira za Taasisi za Umma kutokana na Mifumo ya utendaji kazi iliyopitwa na wakati. Ili kutatua changamoto hizo, Serikali imechukua hatua kadhaa ikiwemo kujenga na kutumia Teknolojia ya Habari na

Mawasiliano (TEHAMA) ikiwemo matumizi ya Mfumo wa Wazi wa Maombi ya Kazi (Recruitment portal) ambao umeunganishwa na mifumo mingine inayotumiwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) katika kuendesha usaili. Hatua hii imesaidia kuboresha utendaji kazi, kurahisisha uhakiki wa taarifa za waombaji kazi na kuzuia waombaji kazi wasio na sifa kuweza kuomba Ajira Serikarini. Maboresho haya yamesaidia kupunguza siku za mchakato wa ajira. Hatua nyingine ni kuendesha saili kwa kutumia teknolojia ya video (video conference) kwa baadhi ya nafasi za ajira, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na kuwapunguzia gharama za usaili waombaji kazi Serikalini.

Katika kuzihudumia ipasavyo Taasisi na Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara, Serikali imechukua hatua ya kuanzisha Idara Maalum (Strategic Public Institutions Management Division) kwa minajiri ya kurahisisha na kuharakisha utoaji wa huduma kwa taasisi hizo. Idara hiyo itashughulikia maamuzi kwa haraka na kuzingatia wakati muafaka katika maeneo ya Ajira, kuidhisha miundo ya vibali vya ajira mpya, mafao. Uhamisho na uwezeshaji wa utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo kwa ujumla. Mchakato wa kuanzishwa kwa Idara hiyo umekwishaanza kwa kupata maoni kutoka menejimenti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hatua inayofuata ni kuwasilisha kwenye Kamati ya Rais ya Utekelezaji (Presidential Implementation Committee - PIC). Itakayomshauri Rais kuhusu kuanzishwa kwa Idara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuongeza ufanisi wa utendaji katika Taasisi zizojiendesha kibiashara zile za kimkakati kwa kuwa na utaratibu wa ajira mahsusi kwa Taasisi hizo, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaandaa utaratibu madhubuti wa ufuatiliaji, tathmini na udhibiti ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mfumo huo unaleta tija na ufanisi uliokusudiwa ili kufika malengo ya utendaji.

### *4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI*

**Mheshimiwa Spiaka,** Lengo la taarifa hii ni kuleta mrejesho wa utekelezaji wa maazimio ambayo yalipitishwa na Bunge lako

Tukufu wakati wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kamati imepitia, kuchambua na kujadili Maazimio yaliyotolewa, taarifa ya Serikali juu ya utekelezaji wa maazimio hayo pamoja na maoni ya Msajili wa Hazina kuhusiana na Utekelezaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imewasilisha hatua mbalimbali za utekelezaji wa maazimio Kumi na Tatu (13) yaliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa Tisa wa Bunge, Serikali imejitahidi kuzingatia na kutekeleza maagizo hayo ambapo katika maazimio kumi na tatu Kamati imeridhika na Hatua ya utekelezaji wa maazimio matano (5). Maeneo ambayo Kamati haijaridhwa na utekelezaji wa Serikali yomeainishwa kwenye taarifa hii kama ifuatavyo: -

**4.1 Taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kuteuliwa kwa wajumbe wa bodi**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bado kuna changamoto/ucheleweshaji katika kupata Bodi za Wakurugenzi za mashirika ambapo Bunge lako Tukufu liliazimia kuwa Serikali itumie miezi 3 kukamilisha uteuzi wa wajumbe wa bodi 12 kwenye wizara 9 ambazo tayari zina Wenyeviti, lakini hadi kufikia tarahe ya kikao cha Kamati ni Taasisi 7 ndio zilikuwa zimekamilisha akidi na taasisi 5 zilikuwa bado. Bunge lilitoa miezi mitatu (3) lakini ni miezi Saba (7) sasa na jambo hili halijakamilika,

**Aidha,** Bunge liliazimia kuwa Serikali itumie miezi 6 kukamilisha uteuzi wa wajumbe wa bodi 23 kwenye wizara 12 ambazo hazina, hadi kufikia tarehe ya kuwasilisha taarifa hii ni taarifa hii tayari Taasisi 17 ndio zilkuwa zimepatiwa Bodi na taasisi sita(6) zilikuwa bado.

**Mheshimiwa Spika,** Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali itafute utatuzi wa kudumu, kwani kwa utaratibu wa Msajili wa Hazina taasisi zote hutoa taarifa miezi tisa kabla, ni maoni ya Kamati kwamba kama muda huu utatumika ipasavyo unatosha kabisa kukamilisha taratibu zote za taasisi kupata bodi, Kamati inapendekeza kama taasisi itakuwa makini kwa jambo hili ambalo hata Mheshimiwa Rais wa JMT alishalizungumzia wakati

anapokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwezi Machi, 2021/22 lifike wakati lisijirudie tena kwani taasisi kukosa bodi inapunguza ufanisi.

***4.2 Hatua za majadiliano katika mradi wa mchuchuma na liganga kuchukua muda mrefu,***

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako tukufu liliazimia kuwa Serikali ihakikishe kuwa mazungumzo yanayoendelea katika Kamati ya Majadiliano ya Serikali - GNT yafikie mwisho ndani ya miezi mitatu au yapelekwe NDC. Kamati inatambua kwamba kuna juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kutekeleza azimio hili ikiwa ni pamoja na Serikali kutoa kiasi cha **Shilingi Bilioni 15.4** ambayo imelipwa kama fidia kwa waliopisha mradi na tayari wananchi wamekwisha anza lipwa fidia, ni hatua nzuri na inaonyesha kuwa sasa eneo hili liwe tayari kwa ajili ya mradi kuanza, Kamati inasisitiza majadiliano hayo yaendelee kwa umakini na yafike mwisho.

*4.3* ***Upungufu wa Mtaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania – ATCL, unaosababishwa na utaratibu wa kukodisha ndege kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania – TGFA;***

**Mheshimiwa Spika,** Azimio la Bunge lilikuwa kuwa TGFA ikamilishe taratibu la kurudisha ndege kwa ATCL. Kwani ukiondoa tatizo hili ATCL inauwezo wa kujiendesha kwa faida. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Serikali iliunda kamati ya pamoja ya kushughulikia jambo hili ikiwemo masuala ya kiufundi, kisheria na kimkataba, kazi hii imekamilika na kuwasilishwa ripoti kwa Baraza la Mawaziri. Ni Ushauri wa Kamati kuwa Serikali iweke muda maalum (Timeframe) ya mashauriano na utekelezaji wa jambo hili ili kuirudishia ATCL uwezo wa kujiendesha kwa faida.

*4.4* ***Kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya kilimo Tanzania – TADB;***

**Mheshimiwa Spika,** Azimio la Bunge liliitaka Serikali itekeleze ahadi yake (commitment) waliyoitoa kwa TADB ya kuiongezea mtaji kiasi shilingi billioni 100 kwa kila mwaka wa fedha, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na tija katika Sekta ya Kilimo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Azimio linatekelezwa japo sio kwa njia

iliyokusudiwa awali ya kutoa billioni 100 kila mwaka, ambapo Serikali imeamua kutekeleza kwa kuiruhusu TADB kutafuta mikopo nafuu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha. Benki hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Kilimo, Kamati inasisitiza Serikali irejee kwenye ahadi yake kuipatia TADB shiingi bilioni 100 kila mwaka wa fedha, ambapo kama ingekuwa imetekelezwa TADB ingekuwa na mtaji wa jumla ya Shilingi **Bilioni 760** kwa sasa na benki hii ingekuwa kwenye nafasi ya kuwahudumia wakulima wengi zaidi.

**4.5 Kuathirika kwa kilimo cha Pamba kutokana na maelekezo ya Serikali ya Mwaka 2019, ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya Soko la dunia, jambo lililosababisha deni la kiasi cha shilingi Bilioni 21.8 kwa Serikali, limeathiri taswira ya Bodi ya Pamba kwa wakulima na kuongeza changamoto katika biashara ya kilimo cha pamba;**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lako tukufu liliazimia kuwa Serikali iharakishe utekelezaji wa ahadi yake ya kulipa deni la Pamba. Hatua hiyo itasaidia kuongeza ufanisi wa sekta hiyo na kurudisha taswira chanya ya Bodi ya Pamba. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Kwa kuwa Serikali imekwishakamilisha uhakiki wa deni hili.

**Mheshimiwa Spika,** Msimu wa pamba umekwisha zinduliwa na madeni ya watoa huduma wa pamba kwenye mabenki yamepelekea mabenki mengi kutokuwa tayari kuwakopesha jambo lililisababisha uuzaji wa pamba kwa msimu huu kuanza kwa kusuasua, malipo ya madeni haya yasipofanyika kwa haraka inaweza pelekea kuwaathiri wakulima wa pamba ambao tayari wamekwisha anza uvunaji wa pamba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza Serikali itimize ahadi yake ya kulipa deni hili ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024, na bajeti yake inaokane kwenye Bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2023/2024.

**4.6 Matumizi ya TEHAMA katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya – NHIF, ambapo NHIF umeonyesha udhaifu katika utoaji wa huduma zake, jambo ambalo limepelekea Mfuko kupata hasara kunakosababishwa na kutokuwa na mfumo thabiti wa TEHAMA ambao inatoa mianya ya kufanya udanganyifu kwa urahisi;**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa pamoja na Serikali kuripoti kuwa NHIF ina mifumo madhubuti ya TEHAMA lakini bado kuna malalamiko makubwa ya utendaji wa Shirika hili, pamoja na kuwa wametoa majibu ya TEHAMA lakini majibu haya ni mepesi ukilinganisha a hali halisi iliyopo. Kamati inaona kuwa bado kuna malalamiko makubwa sana juu utendaji kazi wa Shirika hili na Kamati haioni umakini wa menejimenti wa Shirika, Kamati inaishauri Serikali iandae mkakati madhubuti wa kulisimamia Shirika kwani kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali ni kuwa kama Shirika hili haliko katika hali nzuri.

4.7 **Matumizi makubwa ya Gharama za Bima za Ndege kwa Kampuni ya Ndege Tanzania – ATCL, ambapo ATCL inalazimika kununua Bima kutoka kwa Shirika la Bima la Taifa NIC, ambapo NIC ananunua Bima hizo kutoka kwa wakala wa nje ya nchi kwa mfumo wa moja kwa moja yaani Single Source;**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia kuwa Serikali iielekeze ATCL na NIC kufanya zabuni shindanishi ili kupata wakala wa Bima mwenye bei nafuu, huduma bora na ambae atazingatia uwiano wa ndege shirika inazomiliki, hii italeta ufanisi, tija na kupunguzia shirika gharama za matumizi. Serikali imeeleza kuwa bima za ATCL zilizokwishakatwa kupitia NIC, zinafika kikomo ifikapo tarehe 06 Julai, 2023, baada ya hapo bima zote zitakazokatwa na ATCL zitakuwa shindanishi kama ilivyoelekezwa na Bunge. Kamati imeridhika na hatua hii, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali isimamie kwa ukamilifu utekelezaji wa suala hili, ili kupunguza gharama zinazotokana na utaratibu huu wa ununuzi wa Bima na kupunguza gharama za matumizi za ATCL.

***5.0 HITIMISHO 5.1 Shukurani***

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa namna unavyoliongoza Bunge letu tukufu na kwa kutoa fursa Kamati kuweza kufuatilia kwa ukaribu Utekelezaji wa Maazimio haya ya Bunge kuhakikisha Serikali inatekeleza kikamilifu. Ushauri na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Aidha, naomba nimshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa umakini mkubwa.

Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa Taifa.

Vile vile, napenda kumshukuru Msajili wa Hazina Ndugu Nehemia Mchechu pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ushirikiano wa dhati walioutoa kwa Kamati wakati Kamati inatekeleza jukumu hili la kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Jerry William Silaa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Augustine Vumma Hole,Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abbas Gulam Tarimba, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Aeshi Alfan Hillary, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Aida Joseph Kenani, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Bonah Ladislaus Kamoli, Mb - Mjumbe

9. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Charles Muguta Kajege, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb- Mjumbe
13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb- Mjumbe
14. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Francis Kumba Ndulane, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Fratey Gregory Massay Mb - Mjumbe
17. Mhe. George Natany Malima, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Haji Amour Haji , Mb - Mjumbe
19. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, ndc, kwa uratibu wa shughuli za Kamati na kutoa ushauri wa stahiki na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

***5.2 Kuwasilisha***

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru wabunge wote kwa kusikiliza taarifa hii, sasa naomba Bunge lako tukufu likubali kupokea maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Maazimio Kumi na tatu (13) ya Bunge ambayo yalitolewa wakati Bunge lilipokuwa likichambua na kujadili taarifa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) iliyohusu utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha

Jerry William Silaa, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**

27 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumeshazisikia Kamati zetu tatu, Kamati ya *PAC, LAAC* na *PIC* zikiwakilisha ama zikiwasilisha Maoni ya Kamati, lakini pia Taarifa ya Kamati Kuhusu Taarifa ya Serikali Inayoeleza Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ya Novemba, 2022.

Sasa mmewasikia hapa Wenyeviti wote wamewasilisha Taarifa na hawajatoa hoja. Kwa hiyo, Bunge halitahojiwa kuhusu Taarifa hizi na sababu ni kwamba, hili jambo ni jipya kwa hivyo, tunaendelea kutazama namna bora ya kuisimamia Serikali kwenye eneo la matumizi ya fedha. Kwa hivyo, mawazo yenu tutaendelea kuyapokea, ili tuendelee kufanya bora zaidi katika hilo eneo la kuisimamia Serikali. Sasa pengine, swali litakuwa hizi ni Taarifa za Bunge ama ni za Serikali?

Serikali imeleta Taarifa kwa Bunge na imekuwa ikifanya hivyo miaka yote, tofauti tu ni kwamba, zile taarifa zikishaletwa zinaishia kule kwenye Kamati, haziji hapa Bungeni. Sasa tumeamua zije hapa Bungeni kwanza, ili wananchi wafahamu taarifa zinazoletwa na *CAG* Mwezi Machi, Bunge huwa linazifanyia kazi, linaielekeza Serikali, Serikali inafanyia kazi na kisha Serikali inaleta tena taarifa Bungeni juu ya utekelezaji wa yale waliyoelekezwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni muhimu ili wananchi wafahamu na ninyi mtakumbuka kulikuwa na mjadala mkali sana baada ya Taarifa ya *CAG* ya Mwaka wa Fedha uliopita kuletwa hapa Bungeni Mwezi Aprili. Wako hata Wabunge ambao wanatamani tuahirishe shughuli za bajeti ili tuanze kujadili kwanza Taarifa hiyo ya *CAG* halafu ndio tuanze kujadili Bajeti ya Serikali.

Sasa hii Taarifa ya Kamati ama Taarifa hizi za Kamati zetu mbili zile za usimamizi, lakini pia hii moja ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma zinatuambia picha fulani. Picha gani?

Kwamba, Serikali inapopewa maazimio ya Bunge, inapopewa maelekezo na Bunge inayachukua kwa uzito na inayafanyia kazi. Hapa zimetajwa asilimia kadhaa, kila kamati imetaja asilimia kadhaa ambazo Serikali imeshafanya kazi na

imetaja asilimia kadhaa ambazo Serikali bado inafanyia kazi na imetaja asilimia kadhaa ambazo Serikali haijaanza kufanyia kazi na imetaja asilimia kadhaa ambazo mawazo hayo yamepitwa na wakati.

Sasa hapa mbele nilikuwa najaribu kufanya hesabu. Tangu tutoe maagizo hayo mwezi Novemba ni miezi saba hivi mpaka sasa na kwa upande wa *PAC* wamesema Maagizo ama Maazimio ya Bunge kwa asilimia 20, yale tuliyoyatoa Novemba, yameshatekelezwa. Kamati ya *PAC* inasema asilimia 60 yako kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji, asilimia 20 pekee ndio hayajaanza kuguswa.

Wakati huohuo Kamati ya *LAAC* inasema maelekezo tuliyotoa moja kwa moja kwa maana ya hapa Bungeni, yale Maazimio, lakini na yale tuliyosema kwamba, wakayatazame ya ujumla kwenye Taarifa ya *CAG* kwa ujumla wake *LAAC* inasema asilimia 42 yametekelezwa. Asilimia 32 yako kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji, asilimia tisa hayajaanza kabisa kutekelezwa, asilimia 15 yamejirudia kwa maana ya kwamba, ni ya siku nyingi yanaendelea na asilimia tatu yamepitwa na wakati.

*PIC* inasema katika Maazimio tuliyoyatoa asilimia 41 yameshatekelezwa na Serikali. maana yake ni nini? Ukipiga hesabu zile za wastani, wale ambao sijui hesabu zinaweza kuwa ziliishia darasa la tatu ama la ngapi, unapata picha kwamba, ni takribani asilimia 48 ya maagizo ambayo Bunge lilitoa mwezi wa 11, Serikali mpaka sasa imeshayafanyia kazi. Maana yake ni nini?

Katika kipindi hiki cha miezi saba Waheshimiwa Wabunge sisi wote tumemaliza. Jana tumepiga kura ya bajeti, Serikali wakati ikiendelea na utekelezaji wa yale ambayo sisi tumewaagiza pia, ilikuwa inaendelea na kutayarisha bajeti ambayo hapa Bungeni tumeweza kuijadili. Kwa hivyo, na sisi Wabunge lazima tutambue kwamba, Serikali inayafanyia kazi maelekezo tunayowapa. *(Makofi)*

Kwa sasa wamefika asilimia hizi katika miezi hiyo, tutarajie kwamba, tunakoenda huko mbele kufikia Novemba yale yaliyo

njiani yanayoendelea kutekelezwa pengine yatakuwa yamefika asilimia nyingi zaidi na tutasikia tena kutoka kwenye taarifa zetu hizi za Bunge kwa sababu, kamati zetu ziko hap ana sisi huu mchakato tunapoanza sasa kuelekea huko mbele kwa sababu ni jambo jipya, wenyeviti wa kamati zetu zile za kisekta ni kazi yao kufuatilia jambo gani linaangukia kwao maana sasa tusitarajie hizi kamati zitaanza kuruka kwenye kamati zetu kuanza kufuatilia utekelezaji. *(Makofi)*

Ni kazi yenu Wenyeviti kwenye Kamati zenu kuiuliza Serikali imefikia wapi juu ya maagizo ya Bunge yale ambayo tulishayatoa, yale ambayo yameshatekelezwa mnawapongeza, yale ambayo yanaendelea na utekelezaji mnawauliza mmefika wapi, ili na ninyi mtakapokuwa mnatoa taarifa zenu mwezi wa kwanza mwakani muweze kutoa taarifa juu ya haya. Kwa nini, ili Bunge lifanye kazi yake ya kuisimamia Serikali hasa katika yale maeneo ambayo tunafikiri uitendaji ukiboreshwa nchi yetu itapiga hatua sana.

Kwa hiyo, kwa upande mmoja tuipongeze Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo imezichukua katika kutekeleza maagizo ambayo imepewa na Bunge. Hiyo ni hatua moja, hatua ya pili, tuzipongeze sana kamati zetu kwa ufuatiliaji, tunawapongeza sana. Hatua ya tatu, tunamshukuru sana *CAG* kwa kuweka mkazo kwenye ufuatiliaji wa mambo haya na ameweza kutoa ushauri mzuri kwenye ngazi ya kamati mpaka tumeweza kufika hapa tulipofika leo. (Makofi)

Naamini huko mbele taarifa zetu hizi zitaisaidia zaidi Serikali kwa maana ya kupiga hatua nyingi zaidi, ili taarifa tutakapokuwa tunaisikia tuwe tunasikia hizi asilimia zikiwa zinapanda kila wakati tunapoletewa taarifa kama hizi. Kwa sababu, kwa upande wa taarifa iliyotolewa na *LAAC* nilikuwa nafuatilia hapa, halmashauri zimetajwa, kiasi ambacho pengine hakijapelekwa ama kiasi ambacho kimetumika vibaya, kila halmashauri imetajwa hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sisi wote ni Madiwani. Tupitie taarifa ile, halmashauri yako pale ilipotajwa kajitazame maana na

sisi Wabunge huwa wakati ule, eeh, halmashauri zetu zinapoleta hapa bajeti na sisi tunazisindikiza. Zinakwenda wapi kwenda kujieleza tunazisindikiza, halafu tunataka tukifika pale tuwe marafiki hivi. Kwa hiyo, na sisi wenyewe tukazitazame halmashauri zetu zifanye vizuri, ili matumizi ya fedha za umma yawanufaishe wananchi. *(Makofi)*

Naamini kwa ufafanuzi huo wananchi watakuwa wamepata picha kwamba, Wabunge wao wanafanya kazi ya kuisimamia Serikali na hatuachii njiani. Ndio maana tunaendelea kufuatilia hizi asilimia, ili tufike mahali ambapo tutakuwa tukipata taarifa hizi ambazo zina asilimia ndogo ambayo bado haijafanyiwa kazi na tutakuwa tunapiga hatua kwa namna hiyo.

Waheshimiwa Wabunge mawazo yenu yanaendelea kupokelewa kwenye jambo hili, ili tuendelee koboresha kwenye hili eneo la kuisimamia Serikali. kwenye eneo la kuishauri Serikali tuko vizuri sana na tunaamini kwamba, tutafanya vizuri zaidi tukiweza kusimamia vizuri Serikali kwenye eneo la matumizi ya fedha ambazo ni za umma.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, ninawatakia kila la heri na jioni njema. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.02 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 28 Juni, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*